بسم الله الرحمن الرحيم

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

Utangulizi WA KITABU CHA KHUTBA ZA IJUMAA

Utangulizi

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote. Rehema na amani zimshukie mwisho wa Manabii na Mitume: Muhammad na jamaa zake na Maswahaba zake na wenye kuwafuata wao kwa wema mpaka Siku ya Qiyama.

Baada ya hayo:

Uhutubiaji katika Uislamu, ulikuwepo na bado unaendelea kuwepo, ni msingi wa asili wa jengo la umma wa Kiislamu ulio mtukufu, ni taa yenye kuamsha nyoyo zilizoghafilika, kuziongoza nafsi zilizoduwaa na kuzinoa hima za juu. Hizo ni kipumbazi cha yule aliyeshikamana na Dini yake na zinampa uthabiti yule ambaye ana moyo ulio hai. Hii ndio mimbari ya mawaidha na wenye kuwaidhia na ni bendera ya ulinganizi na walinganiaji. Hizo ndizo ala za uelekezaji na ushauri mwema na ndio chombo cha uongozaji na upandaji. Kwenye hizo khutba, anajifunza asiyejua, anakumbuka aliyesahau na anapata majibu aliye na maswali yanayomshughulisha.

Mwenye kuhutubu huwa akizunguka kwenye mambo mbalimbali yanayokabili ummah wa Kiislamu, na anatatua matatizo yanayojitokeza, wakati mwingine kuwavutia watu kwenye kheri, kuwakhofisha wasifanye mabaya, kwa kuwasimulia visa, kuwapigia mifano, kuwapa ukweli wa mambo na kuwafanya wazingatie na kuhutubia akili zao, na pia hisia zao ili afikie lengo la kuijenga upya imani ya kila mtu na kukikamilisha kilichopungua kwa kuchakaa kwake hiyo imani, na ili kila aliyeasi na kuwa mbali atubie, na ili kila aliyepotea njia na kurandaranda arudie, na azinduke kila aliyeghafilika kutokana na ulevi wa kughafilika kwake, na ajikomboe kila aliyechukuliwa mateka na matamanio yake.

Hivyo basi nafsi zitakasike na nyoyo zikutane ziitetee Dini yake na zitangaze ulinganizi wa Mola wake, ili utukufu wa umma wa Kiislamu na enzi yake zirudi. Hilo ni jukumu kubwa lilioje, lau wao wanajua!

Daraja ya khutba ya Ijumaa:

Khutba ya Ijumaa katika Uislamu, iko mahali pa juu na daraja kubwa, ina lengo na risala ya kufikisha, ina kazi inayoitekeleza na athari inayoiacha. Miongoni mwayo ni:

1. Inatosha kuonesha umuhimu wake na utukufu wake kuwa mtu aliyeitekeleza vizuri zaidi ni bwana wa wanadamu, Nabii Muhammad, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie. Na baada yake, ilikuwa ndio kazi ya viongozi wa umma miongoni mwa wanazuoni watendaji na walinganizi wa Mwenyezi Mungu.

2. Kwamba khutba ni utangavu, kati ya tangavu za Uislamu, unaotekelezwa katika siku ambayo ni bora kuliko siku yoyote iliyotokewa na jua, nayo ni siku ya Idi ya Waislamu: siku ya Ijumaa, kwenye kiwanja kilichotakasika zaidi kuliko viwanja vyoe ardhini, ambavyo ni nyumba za Mwenyezi Mungu.
3. Kwamba ni njia ya ufikishaji na ni mimbari ya ulinganizi. Ndani yake mna kuamrisha mema na kukataza maovu, mbali ya kuwa ni chombo cha malezi na mafunzo na ni mapito ya kutengeza na kuweka sawa.
4. Kwamba ndiyo chimbuko la kuwahamasisha watu, kuharakisha hisia zao, kuzikinaisha akili zao na kuimarisha haki waliyonayo. Kwa nini isiwe hivyo? Na hali ya kuwa ni neno lenye kusikika, lenye joto la uhai, lenye hisia za kikweli na lenye kuathiri miili ya wenye kusikia, lina athari tendakazi zaidi na athari yake ni ya nguvu zaidi kuliko neno linalosomwa.
5. Kwamba ndiyo ngawira ya ulinganizi na walinganizi. Kwani kuhudhuria ili kutekeleza Swala ya Ijumaa na kusikiliza khutba mbili kabla yake ni jambo la lazima. Na juu ya hayo, inahudhuriwa na mkubwa na mdogo, msomi na asiyekuwa msomi, tajiri na masikini, kwa kuongezeka bila kupungua, kuendelea bila kukoma, na kukaririka kila wiki.
6. Kwamba hiyo khutba katika zama zetu hizi ndiyo njia ya kuwajulisha watu dini ya sawa, na kuzirudi tashwishi na hoja zisizo na misingi zinazotoka kwa watu wenye malengo maovu, wanaoendelea mchana na usiku kuiponda njia ya Bwana wa viumbe vyote na kuwazuia watu wasiifuate, kwa kutumia mbinu za kuvuta nyoyo za wenye kushuhudia na kuwaathiri wachache wa ufahamu, wajinga na wenye kudanganyika.

MAELEZO MAFUPI YANAYOFUNGAMANA NA HUKUMU ZA KHUTBA YA IJUMAA

Kwanza: Hukumu ya Khutba ya Ijumaa kwa Swala Ijumaa

Wanavyuoni wametofautiana kuhusu ulazima wa khutba ili Swala ya Ijumaa iwe sahihi katika kauliu mbili:

Ya kwanza: nayo ni kauli ya wanavyuoni wa Sharia walio wengi. Nayo ni kauli ya Mahanafi, wengi kati ya wanavyuoni wa madhehebu ya Malik, Shafii, Hambali. Kauli yenyewe ni kwamba khutba ndio sharti ya lazima ya kuswihi Swala ya Ijumaa.

Ya pili: Ni kwamba khutba imesuniwa tu.

Kauli yenye nguvu ni ile ya wanavyuoni wengi, kwa kuwa Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, alidumu nayo na kuwa vitendo vya Maswahaba vinathibitisha hilo na vinaenda kinyume na kauli inayotofautiana nay

Ni lazima kuwa na khutba mbili kwa Swala ya Ijumaa. Amepokewa ‘Abdullah bin ‘Umar, Mwenyezi Mungu Awaridhie wote wawili, akisema, “Nabii, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, alikuwa akihutubu khutba mbili, kisha akikaa baina ya hizo mbili.” (Aliyeipokea ni Bukhari katika Sahihi yake)

Pili: Masharti ya Khutba:

1. Kutia nia. Kwa kuwa Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, amesema: “Matendo yote yanazingatiwa kwa nia. Na hakika si lingine, kila mtu atapata kwa lile alilonuia.” (Aliyeipokea ni Bukhari katika Sahihi yake) na kwa kuwa khutba ya Ijumaa ni ibada, basi inalazimu nia kama ibada nyingine.
2. Khutba ni lazima ihudhuriwe na kundi la watu ambao kwao yatapatikana malengo ya khutba, nayo ni kuwaidhia na kukumbusha.
3. Iwe ni baada ya kuingia wakati wa Ijumaa.
4. Iwe ni yenye kutangulia Swala, kwa kufuata kitendo chake Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie.
5. Kuhutubu kwa kusimama iwapo mwenye kuhutubu anaweza kusimama.
6. Kuhutubu kwa sauti ya juu, kwa kuwa hiyo ndiyo njia ya kuitekeleza khutba na kufanya malengo yake yapatikane. Na kitu chochote ambacho wajibu hautimu isipokuwa kwacho, basi nacho huwa ni wajibu.
7. Iwe ni kwa lugha ya Kiarabu, iwapo wengi wa wenye kuhudhuria wanafahamu Kiarabu na wanaelewa maana yake kwa ujumla, ili kuhimiza kujifunza Kiarabu na kutoenda kinyume na maongozi ya Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie. Na iwapo wengi wa waliohudhuria Msikitini hawafahamu Kiarabu, basi si makosa kutoa khutba kwa lugha nyingine. Kwani la msingi katika khutba, ni kufunza na kuelekeza, sio kusoma peke yake. Hii ni pamoja na kuzisoma Aya kwa lugha ya Kiarabu na kuzifasiri.
8. Kufuatanisha baina ya sehemu za khutba, na pia baina ya khutba ya Ijumaa na Swala yake.

Tatu: Nguzo au Vikamilishaji Khutba ya Ijumaa:

Lililo na nguvu, ni kwamba khutba ya Ijumaa haina nguzo. Isipokuwa khutba huwa imepatikana kwa kile kinachoitwa khutba kulingana na ada. Lakini ukamilifu wa khutba unapatikana iwapo mwenye kuhutubu atayaleta yanayofuata:

1. Kumsifu Mwenyezi Mungu Aliyetukuka.
2. Kuleta shahada mbili (shahada ya kuwa hakuna anayepasa kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu, na shahada ya kuwa Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu).
3. Kumswalia Nabii, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie.
4. Kuleta mawaidha.
5. Kusoma kitu chochote katika Qur’ani.
6. Kuusia uchajimungu.

Nne: Suna za Khutba ya Ijumaa:

1. Ni kwamba, khutba itolewe juu ya mimbari, kwa kumfuata Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie. Na sunna ni kuwa mimbari iwe na daraja tatu, kwa kumfuata Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie.
2. Mwenye kuhutubu awasalimie walio pambizoni mwake anapoingia, na kabla hajapanda mimbari. Na haikupokewa kutoka kwa Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, kuwa alikuwa akiswali kabla ya Swala ya Ijumaa, kwa kuwa yeye alipokuwa akitoka nyumbani kwake alikuwa akiingia Msikitini, na anapoingia tu kunaadhiniwa na kuanza kuhutubu.
3. Na pia mwenye kuhutubu awasalimie watu anapopanda mimbari. Amepokewa Jabir bin Abdullah, Mwenyezi Mungu amridhie, akisema kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehema na amani zimshukie, alikuwa akipanda mimbari anatoa salamu.
4. Kukaa juu ya mimbari mpaka muadhini amalize kuadhini.
5. Iliyowekwa na Sharia ni adhana moja kwa Swala ya Ijumaa, pale anapokaa imamu juu ya mimbari, kama ilivyokuwa kipindi cha Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, Abubakar na 'Umar, Mwenyezi Mungu Awe radhi nao. Kwani uwezekano wa kujua kuingia wakati kwa sasa hivi upo kwa urahisi. Kwa hivyo ile sababu ya kuwapo kwa adhana ya 'Uthman, Mwenyezi Mungu Awe radhi naye, iliyokuwa ikiadhiniwa kwenye soko ya Madina ili watu wajue kuwa wakati umeingia haipo tena.
6. Imesuniwa kwa mwenye kuhutubu kuanza khutba yake kwa khutba ya haja na matamko yake ni:

   "Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu. Tunamtaka msaada na tunamtaka msamaha. Na tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu na shari za nafsi zetu na mabaya ya matendo yetu. Yoyote yule ambaye Mwenyezi Mungu Anamuongoza, hakuna mwenye kumpoteza; na yoyote yule ambaye Mwenyezi Mungu Anampoteza, hakuna mwenye kumuongoza. Ninashuhudia kwamba hakuna mola anayepasa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Peke Yake, Asiye na mshirika. Na ninashuhudia kwamba Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake."

   (Enyi mlioamini! Muogopeni Mwenyezi Mungu Anavyostahiki kuogopewa. Na msife isipokuwa na nyinyi mko katika hali ya Uislamu) (Enyi watu! Muogopeni Mola wenu Aliyewaumba kutokana na nafsi moja, na Akaumuumba kutokana na nafsi hiyo wapili wake, na Akaeneza kutokana na wawili hao, wanaume wengi na wanawake. Na muogopeni Mwenyezi Mungu Ambaye mnaombana kwa Jina Lake, na muogopeni vizazi. Hakika Mwenyezi Mungu kwenu nyinyi Anaona kila kitu) (Enyi mlioamini! Muogopeni Mwenyezi Mungu na mseme neno la sawa. Mkifanya hivyo, Atawatengezea matendo yenu na Awasamehe dhambi zenu. Na Mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, basi atafaulu kufaulu kukubwa.)

Baada ya hayo, ilivyo ni kwamba mazungumzo ya ukweli kabisa ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na uongofu mzuri kabisa ni uongofu wa Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, na mambo ya shari zaidi ni yale yaliyozushwa, na kila kizushi (katika Dini) ni bid'ah, na kila bid'ah ni upotevu, na kila upotevu ni Motoni."(1)

7. Mwenye kuhutubu aathirike kwa khutba yake. Katika muongozo wa Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, ulikuwa kwamba akihutubu macho yake yalikuwa mekundu, na huwa kama aliyeshikwa na hasira. Jabir bin Abdullah, Mwenyezi Mungu Awe radhi naye, alipokewa akisema kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu Alikuwa, anapohutubu, macho yake hubadilika kuwa mekundu na sauti yake ikiwa juu na huwa kama aliyeshikwa na hasira, kama kwamba anatoa tahadhari kwa jeshi kwa kusema, "Mnavamiwa asubuhi! Mnavamiwa jioni!" (Imepokewa na Muslim katika Sahihi yake)
8. Inapendekezwa kufupisha khutba na kurefusha Swala. Ammar bin Yasir, Mwenyezi Mungu Awe radhi naye, akisema, «Kwa hakika, urefu wa Swala ya mtu na ufupi wa khutba yake ni alama ya ufahamu wake. Basi refusheni Swala na mfupishe khutba. Na kwa kweli, kwenye maneno ya ufasaha pana kivutio.» (Imepokewa na Muslim katika Sahihi yake)
9. Kukaa baina ya khutba mbili kwa muda mchache. Nako kumewekwa na Sharia kwa kujipumzisha na kupambanua baina ya khutba mbili. Na hakuna mwenendo maalumu uliopokewa kwa Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, mahali hapa kuhusu dua ya kuombwa. Basi mwenye kutaka kuomba dua inafaa afanye hivyo, lakini bila kuleta tashwishi kwa waliohudhuria. Na wasiinuwe watu kwa wote pamoja mikono yao, lisije hilo kuwa ni mojawapo ya matendo ya ibada ya Ijumaa bila ya kuwa kuna muongozo wa Sunnah katika hilo.
10. Inafaa kwa mwenye kuhutubu kusema na baadhi ya waliohudhuria Msikitini kuswali, iwapo kuna maslahi ya kusema, kama vile kumtanabahisha aliyeingia punde na akakaa, ainuke aswali rakaa mbili. Hii ni kwa kauli ya Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, «Anapokuja mmoja wenu siku ya Ijumaa na imamu akiwa anahutubu, basi na aswali rakaa mbili na azifupishe.» (Imepokewa na Ibn Khuzaimah katika Sahihi yake).
11. Mwenye kuhutubu hainui mikono yake katika kuomba dua bali huinua kidole chake. Hii ni kwa Hadithi iliyopokewa na Muslim kutoka kwa Husain bin 'AbdurRahman akisema, "Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, haongezi zaidi ya kufanya kwa mkono wake hivi – na akaashiria kwa kidole chake cha shahada." Isipokuwa dua ni ya kuomba mvua inyeshe au kuomba mvua iache kunyesha au ipungue, hapo mikono miwili inainuliwa

(1) Khutbah al-Hajah. Nasir al Din al Albani, al-Maktab al-Islami, Beiruit, 1400 AH

SIFA ZA MHUTUBIAJI ALIYEFAULU NA UMAHIRI WA KUHUTUBU

Sifa ya kwanza: inayoambatana na yeye mwenyewe:

- Kumtakasia Mwenyezi Mungu Aliyetukuka. Hii ni kwa Neno lake Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, (Na hawakuamuriwa isipokuwa ni wamuabudu Mwenyezi Mungu hali ya kumtakasia Dini, hali ya kusimama kwenye njia ya haki na kujiepusha na njia za ubatilifu, na wasimamishe Swala na watoe Zaka. Na hiyo ndiyo Dini ya mila iliyolingana sawa) [al Bayyinah: 5]
- Kufuata muongozo wa Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, katika maneno yake na khutba zake: (Sema: Iwapo mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu Atawapenda na Atawasamehe dhambi zenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, ni Mwenye kurehemu.) [Aali 'Imran:31]
- Kujilazimisha tabia njema zote za Uislamu na kujiweka mbali na tabia mbaya na kila chenye kupelekea kwenye hizo tabia mbaya, kwa maneno na vitendo, mpaka awe ni mfano bora wa kuigwa na kielelezo cha kufuatwa. Bali awe ni kiongozi wa kuwaongoza walio pambizoni mwake na kuwaelekeza kwenye njia Yake iliyonyooka.
- Muumini anawazoea watu na wao wanamzoea. Na hatibu hodari na mlinganizi mwenye tabia njema anawapenda maratibu wake na wao wanampenda na anawatumikia, na wao wanapenda kukaa naye, ni mwenye hekima katika kuingiliana nao, ni mvumilivu kwao, ni muadilifu katika kuyazungumzia makosa yao.
- Kusadikisha maneno kwa vitendo pamoja na kutia maanani uwezekano wa kufunza kupitia utekelezaji kivitendo wa hukumu za Uislamu (Enyi watu! Kwa nini mnasema msiyoyafanya?)
- Kujiepusha na ubaguzi wa kikabila, ukoo, nchi, mkao, kundi au madhehebu. Na asijiunge isipokuwa na Qur'ani, Sunnah, Dini na mila ya Uislamu. (Shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu kwa pamoja na msipambanukane.)
- Kushiriki katika jamii yake anayoishi ndani yake kwenye mambo ya ufanisi na yenye nafuu, ili kuyafanya maisha yake kuwa ni tafsiri ya maana ya khutba zake anazowatolea. Na asijiepushe na watu na Waislamu, bali atangamane nao, awavumilie na awe ni mfano mzuri kwao.
- Kuwa mcheshi, kuwa na uso wa furaha na kuwa na tabia njema pamoja na wenye kuswali na wengineo. Kwani yeye ni kiigizo chema kwa Waislamu, anafanya kazi tukufu zaidi na anashika nafasi ya Mtume, rehema ya mwenyezi Mungu na amani zimshukie. Kwani kuzishika nyoyo za watu zinawafanya wao wamsikilize na wayakubali maelekezo yake na wayafanyie kazi yale aliyowafundisha.

Sifa ya pili: Inayofungamana na khutba yake:

- Aitayarishe khutba yake ifaavyo kwa juhudi anayoiweza, pamoja na kujishughulisha na mada zinazosaidia kumjenga Muislamu wa kikweli kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine kuzishughulikia kasoro zilizoko zinazomfanya kutozifuata Sheria za Uislamu kivitendo. Na kujitayarisha ni :
- Kujiandaa vizuri kwa analotaka kusema. Na lau ataiandika itakuwa bora zaidi.
- Kujiandaa kusoma khutba zaidi ya mara moja kabla ya wakati wa kuitoa ili azoee kutamka maneno magumu na ili lugha imwandame na kumfuata.
- Matamko mengine yanahitaji maandalizi kwa sauti atakayoitumia katika khutba. Kwani baadhi ya matamko na vifungu vya maneno vinahitaji kuinua sauti juu au kuifanya nene. Na baadhi ya matamko yanahitaji kuteremsha sauti chini au kuifanya nyembamba.
- Ufafanuzi wa lugha na kusalimika kwake na makosa. Mwenyezi Mungu Anasema: (Sisi tumeiteremsha ikiwa ni Qur›ani kwa lugha ya Kiarabu ili mpate kuielewa.) [Yusuf:2] Iwapo wanaohudhuria ni Waarabu itampasa awe fasaha wa lugha ya Kiarabu. Na iwapo wanaohudhuria si Waarabu, basi na awe na ufasaha wa ile lugha atakayoitumia katika khutba yake. Uwazi na kusalimika na makosa vinapatikana kwa:
    - uchungaji wa vikomo sahihi vinayobainisha maana na kuyafunua.
    - uwazi na usahihi wa maneno.
    - uwazi na usawa wa sauti
    - uwazi na usawa wa utekelezaji.
    - kujiepusha na uharaka wa kupita kiasi au upole unaochokesha.
- Ni vizuri kwa khutba ya Ijumaa iwe na maudhui mamoja yaliyo wazi, yasiyokuwa na pande mbalimbali wala yenye sehemu nyingi, yanayonasibiana na wakati unaokusudiwa kutolewa. Inapendekezwa khutba yake ya mwisho kabla ya kuingia mwezi wa Ramadhani iwe ni juu ya kuupokea mwezi wa Ramadhani na maelezo kuhusu hukumu zake; na kabla ya wakati wa Hija iwe ni kuhusu Hija na siku kumi za Mfungo Tatu. Na katika kila mnasaba aeleze mambo yanayonasibiana nao na yale yanayo washughulisha wenye kuswali.
- Vifungu vya mada ya khutba ni lazima vipangike, kimoja baada ya kingine, kwa msururu wa kimantiki unaokubalika. Pia kuyafanya yale maudhui makubwa yanayokusudiwa yawe wazi katika vituo vya utayarishaji na utoaji khutba, kwa namna ya kumfanya msikilizaji khutba ajue kile anachokitaka mhutubiaji na atoke Msikitini na hali kuwa mada iliyozungumzwa iko wazi kwenye akili yake.
- Kuwatazama waliohudhuria kuswali wote kwa namna ya usawa. Inapendekezwa awatazame walio mbele ya Msikiti na walioko nyuma yake, na walio kuliani na walio kushotoni kwa namna ya kawaida na haraka, inayomfanya aliyehudhuria ahisi mafungamano yaliyoko baina ya mtoaji khutba na waliohudhuria.

- Mwili na uso na sauti viende sambamba na maana yanayotolewa, kwa njia ya kawaida bila kujifanyisha na kujikalifisha. Jambo ambalo linafanya maana yanatolewa–pamoja na maneno yanayotamkwa–kulingana na umbo la mwenye kutoa sauti yake ilivyo na namna ya utoaji wake.
- Kufungamanisha uhusiano baina ya maana na sauti ya mtoaji khutba. Sauti yapasa itoe maana kwa vile inavyotolewa, kuoana kwake na maana na spidi yake. Na kwa hivyo, Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, alikuwa akihutubu, macho yake yanakuwa mekundu, na sauti yake inakuwa juu, na huwa kama aliyeshikwa na hasira, utadhania kama kwamba yeye ni mtoaji onyo la ushambulizi wa jeshi, yuwasema: litawavamia kipindi cha usubuhi! Litawavamia kipingi cha jioni!”.
- Kuwaondolea watu uchovu na kuwavuta wamsikilize kwa kugeuza sauti mara kwa mara katikati ya khutba, wakati mwingine aende haraka na wakati mwingine aende polepole, wakati mwingine ainue juu sauti yake na wakati mwingine aiteremshe chini. Na abadilishe mitindo ya sauti na ukali wake, na akariri baadhi ya vifungu vya maneno ili kuhakikisha kuwa maana yameorodheshwa kwa njia nzuri inayofahamika kwa urahisi na inayopendeza.
- Kutumia vikomo mahali pake pa sawa. Hakuna jambo baya kwa mtoaji khutba kama kutokuwa na vikomo vya kukomea, kwani kikomo, hata kama ni kifupi sana, kinamfanya mtu awe macho, kinavutia kusikiliza na kinasafisha akili. Kutangamanisha na kushikanisha baina ya kuhimiza mambo ya kheri na kuonya juu ya ufanyaji mabaya.
- Mtoaji khutba isiwe khutba yake ni kutisha, kuonya, kukataza na kuhadharisha peke yake. Vilevile isiwe tu ni kupa moyo, kutia tamaa, kuhimiza na kupa matarajio mema. Bali aende huku na kule baina ya mawili hayo na ayaoanishe kwa vipimo, kama alivyosema Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: (Wape habari waja wangu kwamba Mimi Ndiye Mimi Niliye Mwingi wa msamaha, Mwingi wa kurehemu, na kwamba adhabu Yangu ndio adhabu yenye uchungu).
- Kutumia visa na namna tofauti ya utumiaji huo. Kama alivyosema Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: (Watolee visa, huenda wao wakafikiria). Na miongoni mwazo ni visa vya Nabii Mpendwa, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, kwani yeye ndiye kiigizo na kielelezo (Hakika nyinyi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu mna kielelezo kizuri). Na visa vya Manabii, rehema za Mwenyezi Mungu na amani Yake ziwashukie, visa vya Maswahaba, Mwenyezi Mungu Awe radhi nao, na wale waliowafuata kwa wema. Bali pia kutumia visa vinavyotuka ambazo watu wanaishi navyo. Kwani visa vina athari ya ajabu.
- Kutumia hoja za kiakili inapolazimu na kuhakikisha kuwa zinaafikiana na Sharia, kama Alivyozitumia Mwenyezi Mungu katika Kitabu Chake, na pia kama alivyozitumia Mtume Wake.
- Kuzingatia utumiaji wa sifa za maneno zinazofaa, kwa mfano: kiwango cha spidi ya maneno, kurudia jambo muhimu mara kwa mara, kunyamaza kwa muda mchache kabla ya kuelezea jambo muhimu, kujiepusha na kimya

kirefu bila sababu yoyote, kuinua sauti wakati wa kutaja jambo muhumu na yasiyokuwa hayo.

- Kuzingatia usafi na umaridadi binafsi kama vile kuoga, kuwa na pambo zuri la nje, mavazi mazuri, manukato na harufu nzuri. Hii ni kwa kulingana na hadithi ya Abu Sa'id, aliyesema: Nashudia kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, alisema: ”Kuoga – kwa Swala ya Ijumaa – ni lazima kwa kila aliyebaleghe, na apige mswaki, na ajitie manukato akipata”. Na amesema tena Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie” ”Si makosa kwa mmoja wenu anapopata –au Hana makosa mmoja wenu mnapopata – aweke nguo mbili kwa siku ya Ijumaa, mbali ya nguo zake mbili za kazi.”

MAPENDEKEZO YA MKUTANO WA MISIKITI ULIOFANYIKA KWENYE MAKAO YA KIUNGANISHI CHA ULIMWENGU WA KIISLAMU KATIKA MJI MTUKUFU WA MAKKAH (1395 H) KUHUSU KHUTBA YA IJUMAA

Kwanza: Khutba ya Ijumaa inatakikana ilenge kufikia matakwa yafuatayo:

a. Kuwaidhia na kukumbusha kuhusu Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, hesabu Yake na malipo Yake huko Akhera, na kuhusu maana za uchaji Mungu ambazo kwazo nyoyo zinahuika, na kulingania kwenye kheri, kuamrisha mema na kukataza mabaya.

b. Kuwafahamisha na kuwafundisha Waislamu hakika za Dini yao kutoka kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu Aliyetukuka na mwenendo wa Mtume Wake, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, pamoja na kuzingatia kusalimika tabia na adabu kutokana na upitaji kiasi na kasoro.

c. Kusahihisha fikra za makosa kuhusu Uislamu, kuurudi udanganyifu na ubatilifu, unaoenezwa na watesi wake ili kushawishi akili, kwa njia ya hekima yenye kukinaisha, iliyo mbali na kutupiana maneno na matusi. Na kupambana na fikra za kuvunja na kupoteza kwa kuuorodhesha Uislamu sahihi kuwa ni njia ya umma ya kiasili ambayo Mwenyezi Mungu Amewachagulia na wao wenyewe wakajichagulia kuwa ni Dini yao, pamoja na kuzionesha wazi sifa zake za ueneaji, ukati na kati, undani na uhalisi.

d. Kuifungamanisha khutba na maisha na hali ya watu ilivyo, nako ni kutilia nguvu jambo la kutibu magonjwa ya jamii na kutatua matatizo yake kutoka kwenye Sheria nzuri ya Uislamu, pamoja na kuyapa umuhimu mambo ya mwanamke na nyumba ya Kiislamu kwa sababu ya fitna inayozushwa na maadui wa Uislamu juu yake.

e. Kutia maanani minasaba mbalimbali inayokaririka katika kipindi cha mwaka, kama vile Ramadhani, Hija na minasaba mingineyo, kwa kuzungumza mambo yanayoshughulisha fikra za wasikilizaji na kuwatia shauku ya kupata ujuzi utakaowang'arishia njia kuhusu minasaba hiyo.

f. Kuimarisha udugu wa Kiislamu na umoja mkubwa wa umma wake, kupambana na hisia za kibaguzi zilizojengwa juu ya misingi ya asili ya mtu, madhehebu yake, taifa lake na yasiyokuwa hayo katika mambo yanayofarakanisha umma mmoja, kuwa na hamu na kadhia zinazowahusu Waislamu ndani ya nchi za Kiislamu na nje yake, ili Muislamu asiwe amejitoa na kujiepusha, kimawazo na kihisia, na ndugu zake Waislamu kila mahali.

g. Kuipa uhai roho ya jihadi na nguvu katika nafsi za umma wa Kiislamu, na kuamsha hamasa kwa ajili ya kuhami sehemu takatifu za Kiislamu na miji yake, kuhifadhi damu za Waislamu, heshima zao na mali yao, kutetea Imani ya Uislamu na Sharia yake na kufanya kazi ya kuondoa waungu bandia wenye kuweka pingamizi ili ulinganizi wake usiendelee.

Pili: Khutba ya Ijumaa ni lazima iepushwe kufanywa kuwa ni chombo cha kumjenga mtu au chama au mfumo wa serikali, na iwe ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, Dini Yake na ufikishaji neno Lake. (Kwa hakika Misikiti ni ya Mwenyezi Mungu, basi msimlinganie yoyote pamoja na Mwenyezi Mungu).

Tatu: Ni lazima kwa mhutubiaji aiepushe khutba yake na kuingiliwa na kupelekwa na kiongozi wa nchi, akawa ataikariri kama mashine isiyokuwa na roho, na aachiwe uhuru wa kuchagua maudhui yake, kuyapanga na kuyatekeleza kwa njia ambayo akili yake na moyo wake zinairidhia, kuambatana na kile alichokisoma kutoka kwenye Kitabu cha Mola wake na mwenendo wa Mtume Wake, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie.

Nne: Ni juu ya wanavyuoni, walinganizi wenye ujuzi wa kutosha waweke mifano ya juu ya maudhui mbalimbali ya Kiislamu, yanayokusanya vifaa vya msingi vya namna ya kujenga khutba katika sura ya utoaji dalili na ushahidi kutoka kwenye Qur'ani, Sunna, sera ya Mtume, tarehe ya Uislamu, maneno yaliyopokewa na wanavyuoni wenye kuzingatiwa, mashairi yenye ufasaha. Vyote hivyo viwe mikononi mwa wahutubiaji katika maeneo yote ya Kiislamu, ili ajisaidiye navyo anayevihitajia katika kutayarisha khutba.

Tano: Ni lazima ategemee machimbuko ya ujuzi wa Kiislamu yanayoaminika katika utayarishaji khutba, na ajiepusha na hadithi dhaifu, zile za kuzuliwa, riwaya za Kiyahudi zilizopenyezwa, hikaya za urongo, maneno ya kuzidisha ya kutukanika na kila ambacho hakitiliwi nguvu na mapokezi yaliyo sahihi au akili iliyo wazi.

Sita: Khutba ya Ijumaa katika nchi za Kiarabu yapasa iwe kwa lugha ya Kiarabu fasaha iliyo rahisi kufahamika na iepushwe na utumiaji lahaja ya sehemu fulani, kujikalifisha utumiaji vina na vikomo na maneno yasiyozoeleka kusikiwa. Ama katika nchi zisizo za Kiarabu, basi inatosheleza kwa Utangulizi na nguzo za khutba kuwa kwa lugha ya Kiarabu, ama maudhui ya khutba, ni lazima iwe kwa lugha inayofahamika na wanaohudhuria.

Saba: Inatakikana kuwa utekelezaji khutba uwe ni wa kawaida. Kusiwe na kujiimbisha, kujikaza na kupiga kelele na kila namna ya kujikalifisha kunakochukiza.

Nane: Inatakikana kwa mwenye kuhutubu asirefushe kiasi cha kuwachokesha wasikilizaji na kuwafanya wachukiwe kusikiliza khutba. Na pia asifupishe sana mpaka akafikia hali ya kuharibu maudhui yake na kuyakata.

Tisa: Kila lilitotajwa kuhusu khutba ya Ijumaa litatumika katika khutba ya Idi, pamoja na kuzingatia mnasaba mahsusi wa kila Idi miongoni mwa Idi mbili za Kiislamu, na kuwa khutba yake ilenge ukumbushaji kijumla wa misingi ya Uislamu.

USHAURI KWA WENYE KUHUTUBU ILI WAFAIDIKE NA KITABU HIKI

1. Kitabu kinakusanya funguo za mwanzo tu za hatibu kuanza nazo, kwani eneo la mwenye kuhutubu linadhibitiwa na elimu yake na fikra zake. Hivyo basi, inapasa kwa mwenye kuhutubu aendelee kujifunza elimu ya Sharia inayotegemea Qur'ani na mwenendo wa Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie.
2. Kabla hajachagua khutba ya kuhutubu, inatakikana ahakikishe kuwa inanasibiana na wakati itakayotolewa. Khutba haicheleweshwi na wakati wake wala haisogezwi mbele ya wakati wake, bali inachaguliwa kwayo wakati unaonasibiana nayo. Kwa mfano: Khutba ya kukaribisha mwezi wa Ramadhani inatakiwa iwe ni khutba ya mwisho ya mwezi wa Shaabani au ya mwanzo wa mwezi wa Ramadhani, na haifai iwe kabla sana au baada ya hapo.
3. Inapendekezwa kwa mwenye kuhutubu asome kwenye maudhui ambayo atahutubu juu yake awe na ujuzi mwingi juu yake zaidi ya yale yaliyo ndani ya khutba yake, Kwani elimu ni utukufu wa duniani na Akhera, kama alivyosema Mtume, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie: "Ubora wa mwenye ujuzi juu ya mwenye kufanya ibada (bila ya ujuzi) ni kama utukufu wangu juu ya wa chini zaidi miongoni mwenu."
4. Mhutubiaji yampasa aonekane ameathirika na maudhui ya khutba yake. Hilo linatazamwa katika kuyafanyia kazi kwake yale anayoyasema na kuwa ndani ya hisia zake, na ajaribu kuyatenda na kuyatia kwenye hisia zake yale atakayosema kabla ya khutba. Na anapokuwa hatibu anayatenda anayoyasema na kuyatia kwenye hisia zake yale anayoyahadithia, huwa na athari kwa wasikilizaji. Kilio cha mama juu ya mwanawe si kama kilio cha anayejionesha kuwa ana huzuni. Kwa hivyo, matamko ya mwenye kuhutubu, uso wake, sauti yake na vile alivyo vinaonyesha ukweli wake, hamasa zake na ghera yake. Hii nayo inadhihirisha vile waliyokuja kuswali wanavyoathirika na yale anayoyasema.
5. Inamkinika kwa mwenye kuhutubu kuongeza juu ya hutuba yake mifano ya kweli na visa vilivyotokea kwenye eneo lake vinavyoambatana na jamii inayoswali naye, na kuvitia vyote hivyo kwenye khutba, ili kuwajulisha wenye kuswali kuwa khutba kwa hakika imeandaliwa kwao mahsusi., na kuwafanya wao waunganishe baina ya khutba ya Ijumaa na Dini, na baina ya maisha yao wanayoishi.
6. Tunapendekeza kwa mwenye kuhutubu asome khutba anayotaka kuihutubu kwa mara tatu hadi tano kabla ya kuhutubu. Na iwe kule kusoma ni kwa sauti kubwa na kwa kisomo cha utekelezaji kwa kuijaribu sauti yake, mahali pa kukoma, mahali pa kwenda haraka na namna ya kutamka kila kifungu katika khutba.

7. Baada ya matayarisho mazuri kabla ya utoaji khutba, tunapendekeza aitoe khutba kikawaida, zionekane sifa zote za nguvu kwa yule hatibu: katika sauti yake, haraka za mwili wake na vile alivyo. Kadhalika, ionekane athari ya matayarisho mazuri yaliyotangulia. Kwani tumekatazwa kujikalifisha, na watu wengi wao wanapenda ukawaida na wanawapenda wale wanaowahutubia bila ya kuangalia kwenye karatasi.
8. La mwisho ni kwamba ukweli wa nia na kumtakasia Mwenyezi Mungu Aliyetukuka ndio ufunguo wa kikweli wa kufaulu khutba. Basi inatakikana kulikumbuka hilo katika kipindi cha utayarishaji wote na wakati wa utoaji khutba na baada yake. Na kitambo, walisema baadhi ya watu wema waliotangulia: "Anayedodosa dodosa katika kuhutubu ni asiyekuwa na ikhlasi".

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

SEHEMU YA IMANI

Malengo Muhimu :

1. Kuweka wazi haki ya Mwenyezi Mungu juu ya waja wake
2. Kuzishikanisha nyoyo za waja na Mola wao Mtukufu
3. Kuweka wazi Ukubwa wa Mwenyezi Mungu aliyetakasika
4. Kudhihirisha athari ya Imani katika maisha ya watu.

Anuani ya Khutba katika Sehemu ya Imani:-

1. Fadhila za Mwenye kushikamana na Tawhid (Kumpwekesha Allah (Subhaanahu wa Taala) Katika Ibada)
2. Kuamini Majina ya Allah na Ufafanuzi wa baadhi ya Majina ya Allah (Subhaanahu wa Taala)
3. Alama za Kiyama
4. Kujihadhari na Uchawi na Uganga
5. Dalili ya Mwenyezi Mungu Katika Viumbe vyake
6. Kumtegemea Mwenyezi Mungu
7. Mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume
8. Kuamini Qadar (Mipango) ya Mwenyezi Mungu
9. Maisha ya ukweli ni Maisha ya Akhera (Siku ya malipo)
10. Miongoni mwa Athari ya Madhambi katika maisha ya Mja
11. Uchaji Mwenyezi Mungu na Athari yake katika maisha ya Muislamu
12. Kuogopa na Kutarajia
13. Kumtakasia Allah (Subhaanahu wa Taala)
14. Baadhi ya Raha za peponi na Adhabu ya Motoni
15. Baada ya Kifo.

[1] FADHILA YA KUDUMU KATIKA TAWHIDI (KUMPWEKESHA MWENYEZI MUNGU)

Lengo la Khutba:

1. Kubainisha umuhimu wa Tawhidi na Fadhila zake.
2. Kubainisha kwamba Tawhidi ni sababu ya kuokoka mwanadamu Siku ya Kiama na kupata msamaha wa dhambi.
3. Kubainisha kwamba Tawhidi ni sababu ya kuondosha balaa na fitna.
4. Kubainisha umuhimu wa kujifundisha Tawhidi, na Shirki kwa aina zake.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Shukrani za dhati ni kwa Mola Mkarimu. Rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad. Tutazungumzia katika khutba hii mambo yafuatayo:- kubainisha umuhimu wa Tawhidi na fadhila zake, kubainisha kwamba Tawhidi ni sababu ya kuokoka mwanadamu siku ya kiama na pia kubainisha kwamba Tawhidi ni sababu ya kuondoshewa balaa na fitna vile vile nibainishe umuhimu mkubwa wa kujifundisha Tawhidi na shirki kwa aina zake.

Ama baada ya haya, Tawhidi ni msingi mkubwa ambao Mwenyezi Mungu amewaumba majini na watu kwa ajili yake. Kwani Mwenyezi Mungu hakuwaumba majini na watu isipokuwa kwa kumuabudu yeye.

قال تعالى : ﴿وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾﴾ [الذاريات : ٥٦] .

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala) : {{Sikuwaumba majini na watu isipokuwa waniabudu}} [Addhariyati : 56].

Ndugu katika imani na wausia kumcha Mwenyezi Mungu kwa siri na kwa dhahiri na jueni ya kwamba moyo wa Muislamu hauwi mzuri isipokuwa kwa Tawhidi. Kwani Tawhidi ni jambo kubwa. Allah (Subhaanahu wa Taala) Amelibainisha katika kitabu chake na pia Mtume, rehma na amani zimfikie ameliweka wazi katika hadithi zake tukufu.Tawhidi ni jambo ambalo hawezi kuokoka mtu yoyote duniani na kesho Akhera ila alikamilishe jambo hilo la kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kutomshirikisha na chochote. Amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam): [Atakaye kufa na akijua ya kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu ataingia peponi].

Umuhimu wa Tawhidi

1. Tawhidi ni jambo bora sana, na kwa sababu hii Allah (Subhaanahu wa Taala) Ameshuhudia kwa nafsi yake vile vile Malaika wameshuhudia na pia waliopewa ilimu. Na hii ni kuonesha ubora wa jambo hili la Tawhidi. Jambo Amelishuhudilia Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), wakashuhudia Malaika watukufu na pia wanadamu watukufu na watu waliopewa ilimu.

قال تعالى : ﴿ شَهِدَ ٱللَّهُ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ وَأُو۟لُوا۟ ٱلْعِلْمِ قَآئِمًۢا بِٱلْقِسْطِ ۚ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ ﴿١٨﴾ ﴾ [ال عمران : ١٨].

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala): {{Ameshuhudia Mwenyezi Mungu ya kwamba hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye na Malaika na pia waliopewa ilimu,hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye Mwenye nguvu Mwenye hekima}} [Al-Imran : 18].

2. Miongoni mwa umuhimu wa Tawhidi ni kwamba Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) Alilingania Tawhidi kuanzia mwanzo wa ulinganizi wake hadi mwisho wa uhai wake, bali Mitume wote walilingania hivyo.
3. Pia tunapata katika sira ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) ya kwamba alipokuwa akituma maswahaba kwenda kulingania katika sehemu fulani huwausia kwanza kuwalingania Tawhidi.
4. Miongoni mwa umuhimu wa Tawhidi ni kwamba mwenye kushikamana na Tawhidi husamehewa dhambi zake na anaepushwa kukaa motoni.
5. Mwenye kushikamana na Tawhidi huwa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu na pia hupata amani kamili na uongofu hapa duniani na kesho akhera.

قال تعالى : ﴿ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَلَمْ يَلْبِسُوٓا۟ إِيمَٰنَهُم بِظُلْمٍ أُو۟لَٰٓئِكَ لَهُمُ ٱلْأَمْنُ وَهُم مُّهْتَدُونَ ﴿٨٢﴾ ﴾ [الأنعام : ٨٢]

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Wale walioamini na wasichangane imani zao na dhulma watapata amani na wataongoka}} [Al-Anaam : 82]. Kwa mujibu wa Aya hii ni kwamba Muislamu anayeshikamana na Tawhidi atakuwa na amani hababaiki hapa duniani yuwajua litakalompata hapa duniani ni kadari ya Mola (Subhaanahu wa Taala) na kuwa atapata amani kesho akhera.

Bila ya kusahau kuwa endapo waumini watashikamana na tauhudi wataondoshewa balaa na fitna kesho akhera. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Anayeshuhudia ya kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye asiyekuwa na mshirika na Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na kwamba Nabii Isa ni mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na neno lake alilolitia kwa Mariam na roho kutoka kwake na pepo ni haki na moto ni haki Mwenyezi Mungu atamwingiza peponi kulingana na amali].

Ni vyema niwatajie mifano ya ambao waliepushiwa balaa na fitna.Tutoe mfano katika Mitume walioepushiwa balaa na fitna ni Nabii Ibrahiim pale walipokuwa watu wake wanataka kumchoma Mwenyezi Mungu Alimwokoa kwa kuuambia moto: “Ewe moto kuwa baridi na salama kwa Ibrahim” na ikawa kama alivyotaka Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Na Mtume mwengine ni Nabii Lut pale Mwenyezi Mungu Alipowaangamiza watu wake na kumwokoa yeye na waliomwamini yeye na mifano ya walioepushiwa balaa na fitna ni mingi na sababu ya kuepushiwa balaa ni kwa sababu ya kushikamana kwao na Tawhidi. Enyi waumin! Napenda kutaja bali kufafanua japokuwa kwa uchache aina za Tawhidi.

Aina ya Tawhidi:

1. Tawhidi ya vitendo vya Mwenyezi Mungu nayo ni kumpwekesha Yeye katika uumbaji na uendeshaji wa mambo ya viumbe, na hashirikiani na yoyote katika hilo yoyote.

قال تعالى : ﴿ ٱللَّهُ ٱلَّذِى خَلَقَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ وَأَنزَلَ مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً فَأَخْرَجَ بِهِۦ مِنَ ٱلثَّمَرَٰتِ رِزْقًا لَّكُمْ ۖ وَسَخَّرَ لَكُمُ ٱلْفُلْكَ لِتَجْرِىَ فِى ٱلْبَحْرِ بِأَمْرِهِۦ ۖ وَسَخَّرَ لَكُمُ ٱلْأَنْهَٰرَ ﴿٣٢﴾ ﴾ [إبراهيم ٣٢].

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Mwenyezi Mungu ndiye aliyeumba mbingu na ardhi na ameteresha kutoka mawinguni maji akatoa kwa maji hayo mazao hali yakuwa ni riziki kweni nyinyi na akawadhalilishia majahazi ili yapite katika bahari kwa amri yake, na akawadhalilishia nyinyi mito ya maji} [Ibrahim: 32].

2. Tawhidi aina ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika ibada. Maana ya maneno haya ni kwamba Mwenyezi Mungu Ndiye Anayefaa kuabudiwa.

قال تعالى : ﴿ إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾ ﴾ [الفاتحة : ٥]

Asema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Ni wewe tu tunakuabudu na kwako wewe peke yako tunataka msaada}} [Al-Faatiha : 5].

3. Tawhidi ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika Sifa Zake na majina yake. Maana yake ni kwamba Mwenyezi Mungu hafanani na yoyote katika Sifa Zake na majina.Wala hafai yoyote kujifananisha wala kumfananisha yoyote na Mwenyezi Mungu katika sifa au majina yake kwani hana mfano wa yoyote.

قال تعالى : ﴿ قُلْ هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾ ٱللَّهُ ٱلصَّمَدُ ﴿٢﴾ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ﴿٣﴾ وَلَمْ يَكُن لَّهُۥ كُفُوًا أَحَدٌۢ ﴿٤﴾ ﴾ [الإخلاص : ١ – ٤].

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala): {{Sema; Mwenyezi Mungu ni mmoja Mwenyezi Mungu Ndiye Anayetakwa msaada, hakuzaa wala hakuzaliwa na Hana mfano Wake yoyote}} [Al-Ikhlas 1 - 4].

Aina zote za Tawhidi ni lazima kwa Muislamu azijue na azitumie katika maisha yake na hii ni kwa faida ya Muislamu. Na endapo mtu ataenda kinyume na aina hizi za Tawhidi basi ameshajitia matatizo duniani na kesho akhera, kwani Mwenyezi Mungu hamsamehe anayekufa katika shirki bila yakutubai.

قال تعالى : ﴿ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِۦ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَآءُ ۚ وَمَن يُشْرِكْ بِٱللَّهِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَٰلًۢا بَعِيدًا ﴿١١٦﴾ ﴾ [النساء : ١١٦].

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Hakika Mwenyezi Mungu hamsamehe anayemshirikisha na Anamsamehe isiyokuwa shirki kwa anayemtaka}} [An-Nisaa : 116].

Enyi ndugu katika imani!Napenda kuchukua fursa hii kutaja mambo ambayo yanakwenda kinyume na Tawhidi. Mambo ambayo anatakiwa Muislamu ayajue na ajiepushe nayo baada ya kuyajua. Mshairi amesema:»Nimeijua shari si kwa ajili ya kuifanya, lakini kwa ajili ya kuiepuka na asiyejua kheri kutokamana na shari ataingia katika shari hiyo.»

Mambo yanayo Haribu Tawhidi

Miongoni mwa mambo ambayo yanatakiwa ajitahadhari nayo yasije yakamtia katika matatizo dunaini na siku ya kiama. Miongoni mwa mambo hayo:-

- Ushirikina kwa aina zake zote. Kwani shirki kubwa inafutilia mbali imani. Na shirki ndogo ina punguza ukamilifu wa Tawhidi.Na mfano wa shirki ni kumuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu jambo ambalo hana uwezo nalo isipokuwa Mwenyezi Mungu. Na katika shirki kubwa ambayo tunayaona leo ni kufanya tawaf kunyenyekea makaburi, kwenda kwa waganga na wachawi bali kuyaamini yote wanayoyasema kwa kudai mambo yaliofichika, na uhakika ni kwamba hakuna anayejuwa yaliofichika isipokuwa Mwenyezi Mungu na hakuna anayeweza kuleta madhara kumpata mtu isipokuwa Mwenyezi Mungu na hakuna anayeweza kuzuia kheri Akitaka Mwenyezi Mungu kuleta kheri hiyo.

قال تعالى : ﴿وَإِن يَمْسَسْكَ ٱللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُۥٓ إِلَّا هُوَ ۖ وَإِن يَمْسَسْكَ بِخَيْرٍ فَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٧﴾﴾ [الأنعام : ١٧].

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Na Mwenyezi Mungu Akimpa mtu mtihani wa madhara (ugonjwa) hakuna Anayeweza kuuondoa isipokuwa yeye na akimpa neema (siha nzuri utajiri) hakuna awezaye kuiondosha kheri hiyo isipokuwa Mwenyezi Mungu}} [Al-Anaam : 17]. Kwa hivyo, tujue ya kwamba Mwenyezi Mungu Ndiye anayeleta manufaa na madhara, na kwa sababu hiyo yatakiwa Mwenyezi Mungu aogopewe haki ya kuogopewa.

- Na aina za shirki ni mtu kuomba dua kumuomba mtu jambo ambalo hakuna awezaye kulifanya isipokuwa Mwenyezi Mungu kama kuondoa ugonjwa. Huku tukijua ya kwamba dua ni ibada, kwa hivyo, ibada hiyo ya dua haifai kufanyiwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu.
- Aina nyingine ya shirki kubwa ni ushirikina katika nia na makusudio, hii ni mtu kunuwia au kufanya ibada kwa kutaka au kukusudia mambo ya kidunia au wamuone kwamba yuwafanya ibada au watu wamsikie au apate sifa kwa watu.

قال تعالى : ﴿مَن كَانَ يُرِيدُ ٱلْحَيَوٰةَ ٱلدُّنْيَا وَزِينَتَهَا نُوَفِّ إِلَيْهِمْ أَعْمَٰلَهُمْ فِيهَا وَهُمْ فِيهَا لَا يُبْخَسُونَ ﴿١٥﴾ أُو۟لَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ لَيْسَ لَهُمْ فِى ٱلْءَاخِرَةِ إِلَّا ٱلنَّارُ ۖ وَحَبِطَ مَا صَنَعُوا۟ فِيهَا وَبَٰطِلٌ مَّا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴿١٦﴾﴾ [هود : ١٥ – ١٦].

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Anayetaka uhai wa dunia na mapambo yake tutawapa malipo ya amali zao hapa duniani na hawatapunguziwa kitu, hao ni wale ambaye hawatakuwa na chochote kesho akhera isipokuwa moto na yatabatilishwa yote waliyoyafanya na ni batili yote ambayo walikuwa wakiyafanya}} [Huud : 15 - 16]. Haya ni malipo ya wanaofanya ibada kwa ajili ya kuonekana na watu na kwa ajili ya dunia.

- Aina nyingine ni shirki ya kutii viongozi wa dini kinyume na miongozo sahihi ya Uislamu katika kuhalalisha vilivyoharamishwa na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

قال تعالى : ﴿ٱتَّخَذُوٓا۟ أَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَٰنَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ ٱللَّهِ﴾ [التوبة : ٣١].

Amesema kuwatii wanaohalalisha vilivyoharamishwa: {{Wamewafanya

wanavyuoni wao na wafanya ibada ni miungu kinyume}} [Tawba : 31]. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) Alimfasiria Adiy bin Hatiim ibada yenu kwao ni kumtii katika kumuasi Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

KHUTBA YA PILI

Shukrani za dhati zote zamstahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote. Rehma na amani zimfikie Kipenzi chetu Mtume Muhammad. Ama baada ya haya, napenda kuendelea kuzitaja aina za shirki nazo ni:

Aina za Shirki:

- Aina nyingine ya shirki ni kumpenda mtu au kitu zaidi kuliko Mwenyezi Mungu tena katika hali ya kumtukuza au kukitukuza kitu kile na kukidhalilikia.Na pindi mapenzi haya yafanyiwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu basi ni shirki.

قال تعالى : ﴿وَمِنَ ٱلنَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ ٱللَّهِ أَندَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ ٱللَّهِ ۖ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ أَشَدُّ حُبًّا لِّلَّهِ ۗ﴾ [البقرة: ١٦٥].

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala): {{Na katika watu wanawafanya wasiokuwa Mwenyezi Mungu kuwa wanavyompenda Mwenyezi Mungu na hakika walioamini wanampenda zaidi Mwenyezi Mungu}} [Al-Baqara : 165].

Kueni ndugu katika imani kwamba ukubwa wa dhambi la shirki kwani Mwenyezi Mungu hamsamehe anayemshiriksha endapo atafariki na dhambi hizo bila kumtaka yeye msamaha kwa kuwa Mola (Subhaanahu wa Taala) haridhii isipokuwa Tawhidi na pia haisamehe shirki. Kwa hivyo, adhabu ya mshirikina ni kubwa na atapata udhalilifu hapa duniani kabla ya kuadhibiwa kesho akhera.

قال تعالى : ﴿إِنَّهُۥ مَن يُشْرِكْ بِٱللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ ٱللَّهُ عَلَيْهِ ٱلْجَنَّةَ وَمَأْوَىٰهُ ٱلنَّارُ ۖ وَمَا لِلظَّـٰلِمِينَ مِنْ أَنصَارٍ ﴿٧٢﴾﴾ [المائدة: ٧٢].

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Hakika mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu amemuharamisha pepo na makazi yake ni motoni na hawatapata madhalimu wenye kuwasaidia}} [Al-Maaidah : 72].

Napenda tujiuze maswali yafuatayo;

1. Ni nani katika sisi hataki usalama duniani na kesho akhera?
2. Ni nani kati yetu hataki kuingia peponi bila ya hesabu?
3. Ni nani kati yetu hataki kupata uhai mzuri duniani na kuokoka siku ambayo haitofaa mtu mali yake wala watoto isipokuwa atayenda kwa Mwenyezi Mungu kwa moyo uliyosalimika na madhambi?

Jawabu la maswali tuliyoyauliza kuitekeleza Tawhidi katika maisha yake yote. Kubwa linalotakiwa ni mtu kujifundisha mambo yanayofungamana na Tawhidi vizuri kuyatilia umuhimu mkubwa katika maisha yake kwa kusoma vitabu vya Tawhidi na kusikiliza darasa za wanavyuoni walioshikamana na Tawhidi na sunna, kwani kufanya hivyo ni nuru katika nyoyo. Na vile vile kuvisoma vitabu

vya Tawhidi ili kujua Tawhidi ni nini Tawhidi,sababu za shirki,hukmu za shirki na dalili za hukumu za shirki hizo, kuyajuwa hayo ni mwangaza ili mtu asibaki katika giza la shirki, na Tawhidi pia hutengeneza moyo wa mtu na jamii kwa jumla.

Enyi ndugu katika imani! Msihadaike na dunia na kuipuuza Tawhidi iliyokusanya kila kitu na kila mafanikio duniani na kesho akhera na kwa ajili ya Tawhidi wametumlizwa Mitume wote na kuumbwa pepo na moto. Nawausia ndugu zangu Waislamu mulipe suala hili la Tawhidi kipaumbele katika maisha yetu, na muikabili Tawhidi kwa nia njema na nia ya kweli. Na haifai kulipuuza kwa hali yoyote kwani atayelipuuza suala hili yuko katika hatari kubwa duniani na vile vile kesho akhera.

Mwisho

Twamshukuru Mungu tumegusia nukta muhimu kwa kubainisha umuhimu wa Tawhidi na kwamba Tawhidi ni sababu kubwa ya kuokoka mwanadamu siku ya kiama kupata msamaha pia tukabainisha kwamba Tawhidi ni sababu ya kuondoshewa balaa na fitna na mwisho tumebainisha umuhimu wa kujifundisha Tawhidi na shirki kwa aina zake.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Azitengeneze nia zetu katika vitendo vya kila siku na azitengeneze ibada zetu za kwa jumla, pia Aitengeneze Dini yetu na dunia yetu kwani yeye ni muweza wa kila kitu.

[2] MAJINA MAZURI YA MWENYEZI MUNGU NA UFAFANUZI WAKE

Lengo la Khutba:

1. Kuhimiza juu kuamini majina ya Mwenyezi Mungu.
2. Kufafanua baadhi ya majina ya Mwenyezi Mungu.
3. Kuhimiza kuomba dua kwa majina ya Mwenyezi Mungu.
4. Kubainisha majina ya Mwenyezi Mungu ni kwa mujibu wa Qur'an na Hadith za Mtume.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Shukran ni za Mola wa viumbe vyote.Rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad. Tutazungumzia katika khutba hii tukufu tutahimizana juu ya kuamini majina ya Mwenyezi Mungu pia tutafafanua maana ya baadhi ya majina ya Mwenyezi Mungu tutaendelea kuhimizana kuomba dua kwa majina ya Mungu vile vile tutaweka wazi ya kwamba majina ya Mwenyezi Mungu ni kulingana na Quran na hadithi za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam).

Ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumtakia rehma na amani Mtume Muhammad. Ni lazima kwa kila Muislamu aamini kuweko kwa Mwenyezi Mungu na kuamini kuwa Mwenyezi Mungu Ndie Aliyeumba kila kitu na yeye ndiye Anayeupeleka ulimwengu na anafanya atakalo. Pia ni wajibu kwa Muislamu kuamini kwamba Mwenyezi Mungu Ndiye anayestahiki kuabudiwa peke Yake kama ambavyo inatakiwa kwa Muislamu kuamini kwamba Mwenyezi Mungu hafanani na yoyote katika majina Yake na sifa Zake. Muislamu akiamini haya tuliyoyataja basi imani yake kwa Mwenyezi Mungu itakuwa imekamilika.

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu munaonisikiliza, Hakika ni katika kumuamini Mwenyezi Mungu kuamini majina Yake mazuri na sifa zake tukufu bila ya kufananisha wala kuzipuuza.

قال تعالى : ﴿وَلِلَّهِ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰ فَٱدۡعُوهُ بِهَاۖ﴾ [الأعراف : ١٨٠].

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Mwenyezi Mungu Ana majina mazuri, muombeni kwa majina hayo}} [Al-Araaf : 180]. Katika maneno haya tunapata faida kwamba haifai kwa yoyote kubadilisha jina lolote au sifa yoyote ya Mwenyezi Mungu kwa sababu yoyote ile na pia haifai kufananisha jina au sifa ya Mwenyezi Mungu na jina au sifa ya mtu yoyote. Kwani kufanya hivyo ni kumfanya sawa Mwenyezi Mungu na kiumbe wake, Vilevile haifai kabisa kusema kwamba jina ambalo Mwenyezi Mungu Amelithibitisha au Mtume wake (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) jina hilo au sifa hiyo. Ni vyema kwa Muislamu ayajue majina ya Mwenyezi Mungu na amuombe kwa majina hayo.

Misingi Muhimu ya Majina na Sifa za Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala)

Ndugu katika imani! Nafurahi kukutajia baadhi ya misingi inayohusiana na majina hiyo;

1. Majina ya Mwenyezi Mungu yote ni mazuri tena yamefikia kilele katika uzuri kwa kule kukusanya kwake sifa zilizokamilika zisizo na upungufu ndani yake kwa namna yoyote.

   قال تعالى : ﴿وَلِلَّهِ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰ فَٱدۡعُوهُ بِهَاۖ﴾ [الأعراف : ١٨٠].

   Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Mwenyezi Mungu Ana majina mazuri, muombeni kwa majina hayo}} [Al-Araaf : 180].

2. Majina ya Mwenyezi Mungu ni yale aliyojiita kwa majina hayo au aliyomwita yeye Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) na haifai kwa mtu yoyote kutunga jina na kumpa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Inavyotakiwa ni mtu kumwita Mwenyezi Mungu majina aliyojiita Mwenyewe katika kitabu chake na yale ambayo Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) katika hadithi zake tukufu, wala hafai mtu kuzungumza jambo bila ya ujuzi.

   قال تعالى : ﴿وَلَا تَقۡفُ مَا لَيۡسَ لَكَ بِهِۦ عِلۡمٌۚ﴾ [الإسراء : ٣٦].

   Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Asema: {{Wala usizungumze jambo ambalo huna ujuzi nalo, hakika masikio na macho na moyo kutaulizwa kuhusiana navyo}} [Al-Isra : 36].

3. Majina ya Mwenyezi Mungu hayana idadi maalumu. Muislamu atakiwa alijue hili vizuri kabisa, na hii ni kwa mujibu wa hadithi ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) aliposema: [Ewe Mwenyezi Mungu na kuomba kwa kila jina ambalo liko kwenye kitabu chako, au ulilomfundisha yoyote katika viumbe vyako, au ulilolificha katika elimu isiyojulikana na yoyote kwako]. Katika majina ambayo Mwenyezi Mungu hakuyataja wala hakuyafundisha viumbe nakuonesha kwamba majina yake hayana idadi maalumu.

   Baada ya kutaja misingi muhimu ambayo yatakiwa kwa Muislamu aifahamu vizuri ili imani yake kwa Mwenyezi Mungu hususan katika majina yake na sifa zake iwe imekamilika vyema.

Maana ya Majina ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala)

Nachukua tena nafasi nyengine kufafanua baadhi ya majina ya Mwenyezi Mungu. Na katika majina hayo ni:-

1. (ALLAH) ni muabudiwa wa haki kwa mapenzi yote katika ibada hiyo katika hali ya kumtukuza.
2. (MWINGI WA REHMA MWENYE KUREHEMU) ni Ambaye anawahurumia zaidi waja wake kuliko mzazi kumhurumia mwanawe, kwani neema yoyote inayopatikana ni kwa huruma ya Mwenyezi Mungu na hakuna dhara lolote lililomuepuka mwanadamu, pia ni kwa rehma ya Mwenyezi Mungu.

قال تعالى : ﴿ وَمَا بِكُم مِّن نِّعْمَةٍ فَمِنَ ٱللَّهِ ﴾ [النحل : ٥٣].

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Na hakuna neema yoyote isipokuwa yatoka kwa Mwenyezi Mungu}} [An-Nahal : 53].

3. (MFALME) Mwenye kumiliki ulimwengu wote juu yake na chini kiasi kwamba hakitikisiki chochote isipokuwa Anajua bali yeye Ndiye Aliyetaka kitikisike.

قال تعالى: ﴿ مَٰلِكِ يَوْمِ ٱلدِّينِ ﴿٤﴾ ﴾ [الفاتحة : ٣].

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Mfalme siku ya malipo}} [Al-Faatiha : 3].

4. (MTAKATIFU) ni aliyetakasika na upungufu waliyonao viumbe vyake, kwani Mwenyezi Mungu hapatwi na uchovu wala maafa yoyote kinyume na mwanadamu hupatwa na machovu na pia maafa.

قال تعالى : ﴿ وَلَقَدْ خَلَقْنَا ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا فِى سِتَّةِ أَيَّامٍ وَمَا مَسَّنَا مِن لُّغُوبٍ ﴿٣٨﴾ ﴾ [ق : ٣٨].

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Na hakika si lingine tumeziumba mbingu na ardhi zilizo kati yake na hatukupatwa na uchovu}} [Qaaf : 38].

5. (MWENYE NGUVU MTENDESHA NGUVU) hakuna kiumbe chochote isipokuwa kiko chini ya uwezo Wake pia kinamyenyekea Yeye.

قال تعالى : ﴿ مَا قَدَرُوا۟ ٱللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِۦٓ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ لَقَوِىٌّ عَزِيزٌ ﴿٧٤﴾ ﴾ [الحج : ٧٤].

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Na hawakumjua Mwenyezi Mungu haki ya kumjua hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Asiyeshindwa na yoyote}} [Al-Hajj : 74].

6. (MJUZI) ni Ambaye yuwajua siri na kilichodhihiri na anajua kilicho bara na baharini na anajua kila kitu Ametakasika Mwenyezi Mungu.
7. (MTUKUFU ALIYE JUU) Aliye juu kwa dhati Yake juu ya Arshi na pia ni Mtukufu kwa sifa zake.
8. (ANAFANYA ATAKALO) Mwenye uwezo wa hali ya juu wa kufanya lolote analolitaka.
9. (MWENYE KUSAMEHE) Anayesamehe makosa yote aliyotendewa na anayesitiri aibu hata zikiwa nyingi kiasi gani. Amesema Mola katika Hadithi Qudsi: [Ewe mwanadamu, hakika yako wewe utakachoniomba na ukatarajia basi nimekusamehe dhambi zote wala sijali].
10. (MWENYE HEKIMA) Anayeweka vitu pahali pake na anayekadiria vitu vizuri.
11. (MWENYE KUJITOSHELEZA) Anayejitosheleza mwenyewe asiyehitajia yoyote katika viumbe. Majina haya ndio nimeona niwafafanulie kwa uchache lakini majina mengine mengi ya Mwenyezi Mungu nimeyaacha kulingana na wakati

Enyi waumini, mnaonisikiliza! yamekuja mahimizo makubwa juu ya kuomba dua kwa majina ya Mwenyezi Mungu.

قال تعالى : ﴿وَلِلَّهِ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰ فَٱدۡعُوهُ بِهَاۖ﴾ [الأعراف : ١٨٠].

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Mwenyezi Mungu Ana majina mazuri, muombeni kwa majina hayo}} [Al-Araaf : 180]. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amebainisha namna gani tutamuomba Mwenyezi Mungu kupitia majina yake matukufu. Katika hadithi Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alimsikia mtu katika maswahaba akisema: [Ewe Mwenyezi Mungu, Nakuomba wewe kwani sifa na shukrani zote ni zako, hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Wewe peke yako. Huna mshirika, Mwenye kusimulia unalofanya, Muumba wa mbingu na ardhi, Mwenye utukufu, na ukarimu, Ewe ulio hai Mwenye kusimamia kila kitu. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akasema: “ Hakika umemuomba Mwenyezi Mungu aliyetukuka kwa jina lake tukufu ambalo akiombwa kwa jina hilo hujibu na Akiombwa hutoa]. Kwa hivyo, ni juu yako mja wa Mwenyezi Mungu kuomba kwa majina yake.

Amesema Sheikh Muhammad Swaleh Uthaimin Allah Amrehemu katika kubainisha maana ya Neno lake Mwenyezi Mungu: “Muombeni kwa majina yake”. Amesema Sheikh: ‘Ni kuyafanya ni njia ya kupata unachotaka katika maombi, kwa hivyo, utachagua jina linalonasibiana na matakwa yako, kwa mfano ikiwa unaomba msamaha basi utasema: “Ewe Mwenye kusamehe nisamehe”. Na hainasibiani kusema: “ Ewe Mwenyezi Mungu Mkali wa kuadhibu nisamehe, bali hii ni kama kumcheza Mwenyezi Mungu shere, na inatakiwa useme «Ewe Mwenyezi Mungu Mkali wa adhabu niepushie adhabu Yako’.

Ndugu Waislamu, kinachotakiwa kwetu ni kukitegemea zaidi kitabu cha Mwenyezi Mungu na hadithi za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) katika kuyajua majina ya Mwenyezi Mungu, kwani haifai kabisa kwa yoyote kumpa Mwenyezi Mungu jina ambalo hakujiita jina hilo wala hajamuita jina hilo Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

KHUTBA YA PILI.

Shukrani za dhati na sifa njema zote zinamstahiki Mwenyezi Mungu Mola wa mashariki na magharibi. Rehma na amani zimfikie Kipenzi chetu na kiongozi wetu Mtume Muhammad. Ama baada ya kumtukuza Mwenyezi Mungu na kumsifu kwa sifa zake Anazostahiki kusifiwa nazo na kumtakia rehema na amani Mtume wetu mkarimu.

Napenda kuchukua fursa nyingine katika khutba hii kuzitaja baadhi ya dua ambazo Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alizoomba kwa majina mazuri ya Mwenyezi Mungu. Mtume asema: [Ewe Mwenyezi Mungu wewe ni Mola wangu hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki ila wewe umeniumba na mimi ni mja wako na niko katika dhamana yako na ahadi yako niwezavyo, narudi kwako kwa neema zako kwangu, na nirudi kwako na dhambi zangu, basi nisamehe, kwani hasamehe dhambi isipokuwa wewe. Najilinda kwako kutokamana na shari ya kila nilichofanya]. Na akasema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Mwenye kusoma dua hii wakati wa usiku na akafa usiku huo, basi ataingia peponi].

Na Mtume alipokuwa akiswali alikuwa akisema: [Nimeuelekeza uso wangu kwa yule Aliyeumba mbingu na ardhi hali kujiepusha na shirki na hali ya kuwa mimi ni Muislamu na sikuwa katika washirikina. Hakika swala yangu na ibada zangu za kuchinja, na uhai wangu na kufa kwangu ni kwa Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, hana mshirika na kwa hili nimeamrishwa na mimi ni Muislamu wa kwanza. Ewe Mwenyezi Mungu, Wewe ni Mfalme hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa wewe, Wewe Mola wangu na mimi ni mja wako nimejidhulumu nafsi yangu, na nimezikubali dhambi zangu zote, kwani hakika hasamehe dhambi isipokuwa wewe. Niongoze katika tabia njema, kwani hakuna mwenye kuongoza katika tabia njema ila Wewe, na uniondoshee tabia mbaya kwani hakuna mwenye kuondosha tabia mbaya ila Wewe. Nakuitikia wewe, na utukufu ni wako na kheri zote ziko mikononi mwako na shari haitegemezwi kwako. Mimi niko kwako, umetukuka na umetakasika. Nakutaka msamaha na narudi kwako].

Na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alikuwa akisema wakati akirukuu: [Ewe Mwenyezi Mungu nimerukuu kwa ajili yako na nimekuamini Wewe na kwako Wewe nimjisalimisha na yamenyenyekea kwako masikio yangu, macho yangu, akili yangu, mifupa yangu na mishipa yangu]. Pia Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alikuwa akisema anapoinuka kutoka kwenye rukuu: [Mwenyezi Mungu Amemsikia Anayemsifu, Mola wetu, shukran ni zako wewe zilizomo mbinguni na ardhini na baina yake na katika kila kitu baada yake].

Vilevile Mtume alikuwa akisema katika sijida: [Ewe Mwenyezi Mungu, ni mesujudu kwa ajili yako na nimekuamini wewe na nimejisalimsha kwako, umesujudu uso wangu umsujudu Aliyeumba na Akautia sura na akapasua masikio yake na macho yake. Basi Ametakasika Mwenyezi Mungu Mbora wa kuumba]. Na akimaliza kuswali anasema: [Ewe Mwenyezi Mungu, Nisamehe mimi madhambi niliyoyatanguliza na niliyoyachelewesha na niliyoyafanya kwa siri na niliyofanya kwa dhahiri na niliyoyafanya kwa wingi na unayoyajua wewe zaidi kuliko mimi. Wewe ni Mwenye kumtanguliza umtakaye, na Mwenye kumweka nyuma umtakaye, hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila wewe].

Enyi waumini wa kweli! jiepusheni na kumuita Mwenyezi Mungu majina yasiyokuwa yake bila ya ujuzi, kwani kufanya hivyo ni kuzungumza juu ya Mwenyezi Mungu bila ya elimu.

قال تعالى : ﴿وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِۦ عِلْمٌ﴾ [الإسراء : ٣٦].

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Wala usizungumze jambo ambalo huna ujuzi nalo}} [Al-Isra : 36].

Mwisho napenda kukariri kwa kuhimiza kuyaamini majina ya Mwenyezi Mungu na kufanya vitendo ambavyo vinalingana na imani hiyo.

Enyi waumini mcheni Mwenyezi Mungu na mjue ya kwamba mnaelekea kwake, na shikamaneni na kitabu chake na mushikamane na sunna sahihi za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam), na mumuite Mwenyezi Mungu kwa majina yake Aliyejiita, na sifa zake alizojisifu nazo, na atakaye kwenda kinyume

na maamrisho yake, basi Mwenyezi Mungu Amemuahidi adhabu kali.

Mwisho

Kwa kweli tumezungumzia kuhusu kuhimizana juu ya kuamini majina ya Mungu pia tukafafanua maana za baadhi ya majina ya Mungu vile vile tukahimiza kuomba dua kwa majina ya Mungu kama ambavyo tumeweza ya kwamba majina ya Mungu ni kulingana na Quran na hadithi za Mtume rehma na amani zimfikie.

Mwisho kabisa tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaaliye tuwe miongoni mwa wenye kusikiliza yaliomema na tuwe ni wenye kuyafuata.Tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe imani iliyothibiti na aturuzuku matendo mazuri. Amin!

[3] ALAMA ZA KIAMA

Lengo la Khutba:

1. Kumuamini Mwenyezi Mungu kikweli na siku ya mwisho.
2. Kuhimiza vitendo vizuri na kutumia fursa hiyo.
3. Kuzindua watu kukaribia kiama.
4. Kuhadharisha watu nafitna na njia za kujiepusha.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Shukran zote ni za Muumba wa mbingu na ardhi Mola wa watu wote rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad.

Katika khutba hii ya leo tutazungumzia kwa kina kumwamini Mwenyezi Mungu kikweli na siku ya mwisho pia tutahimizana kufanya vitendo vizuri na tutazindushana kukaribia siku ya kiama, vile vile nitahadharishe kutokana na fitna na njia za kujiepusha, na nimalizie kuzitaja alama za siku ya kiama.

Ama baada ya kumsifu Mwenyezi Muungu na kumtakia rehma na amani Mtume Muhammad. Ni vyema Muislamu yoyote popote alipo ajue kuwa nguzo za imani ni lazima na kuzifanyia vitendo vizuri. Katika nguzo za imani kuna kuamini siku ya kiama ambayo ni siku ya mwisho siku ya malipo na kabla siku hii haijafika kuna alama za kuonesha kwamba imeshakaribia. Na sio siri kwani zimesha dhihiri baadhi ya alama zake na haya ndio mazungumzo katika khutba yetu ya leo.

Enyi Waislamu watukufu! mazungumzo yetu ya leo yatahusu alama za kiama. Kwa hivyo ni vyema watu wajiandae na siku hiyo.

قال تعالى : ﴿ فَهَلْ يَنظُرُونَ إِلَّا ٱلسَّاعَةَ أَن تَأْتِيَهُم بَغْتَةً ۖ فَقَدْ جَآءَ أَشْرَاطُهَا ۚ فَأَنَّىٰ لَهُمْ إِذَا جَآءَتْهُمْ ذِكْرَىٰهُمْ ﴿١٨﴾ ﴾ [محمد : ١٨]

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala): {{Kwani wanangoja lingine ila kiama kiwajie? basi alama zake zimekwisha kuja, kutawafaa nini wakati kitakapowajia}} [Muhammad : 18]. Ni lazima kwa kila muislamu kuamini siku ya mwisho alipe umuhimu mkubwa suala hili, kwani haikamiliki imani ya mtu mpaka aamini alama za kiama (kwani kuamini alama hizo ni katika kuamini siku ya kiama) ukizingatia kwamba Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alizitaja alama hizi na hakitasimama kiama mpaka zitokee alama hizi. Swahaba Hudhaifa ibn Asiid radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake amesema: [Tulikuwa tumekaa katika kivuli cha chumba cha Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) tukataja kiama na sauti zetu zikawa juu (mpaka Mtume akasikia) akasema : Hakitasimama au hakitakuwa kiama mpaka kupatikane kabla yake alama kumi].

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amebainisha ya kwamba siku ya kiama haijulikani ni wakati gani na wala hakuna anayejua isipokuwa yeye peke yake. Na hakumhusisha yoyote kukijuwa kiama si Malaika aliyekurubishwa wala Mtume aliyetumilizwa na Mwenyezi Mungu. Pia imebainishwa kwamba kiama kimekaribia wakati wake kama zilivyoeleza Aya za Quran Tukufu na hadithi za

Bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

قال تعالى : ﴿يَسْـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلسَّاعَةِ أَيَّانَ مُرْسَىٰهَا ۖ قُلْ إِنَّمَا عِلْمُهَا عِندَ رَبِّى ۖ لَا يُجَلِّيهَا لِوَقْتِهَآ إِلَّا هُوَ ۚ ثَقُلَتْ فِى ٱلسَّمَـٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۚ لَا تَأْتِيكُمْ إِلَّا بَغْتَةً ۗ يَسْـَٔلُونَكَ كَأَنَّكَ حَفِىٌّ عَنْهَا ۖ قُلْ إِنَّمَا عِلْمُهَا عِندَ ٱللَّهِ وَلَـٰكِنَّ أَكْثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٨٧﴾﴾ [الأعراف : ١٨٧].

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala): Amesema: {{Wanakuuliza kuhusu kiama kitakuja lini? sema: ilimu yake iko kwa Mola wangu tu hakuna wa kudhihirisha wakati wake ila yeye. Imekuwa nzito mbingu na ardhi, hakita kuja kiama ila ghafla}} [Al-Araaf : 187].

وقال : ﴿يَسْـَٔلُكَ ٱلنَّاسُ عَنِ ٱلسَّاعَةِ ۖ قُلْ إِنَّمَا عِلْمُهَا عِندَ ٱللَّهِ ۚ وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّ ٱلسَّاعَةَ تَكُونُ قَرِيبًا ﴿٦٣﴾﴾ [الأحزاب : ٦٣]

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Watu wanakuuliza kuhusu kiama kitakuja lini? sema: ilimu yake iko kwa Mola wangu tu. Na kipi kitakacho kujulisha lini kiama, pengine kiama kiko karibu}} [Al-Ahzab : 63]. Na pale Jibril alipomuuliza Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) kuhusu kiama Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akajibu: [hakuwa mwenye kuulizwa ni mjuzi kuliko anayeuliza» Aya na hadithi za Mtume rehma na amani zimfikie zinazoshiria kwamba hakuna anayejuwa wakati wa kutokea kiama isipokuwa Mwenyezi Mungu]. Vile vile mitume waliobakia hawajui wakati gani kiama kitasimama.

Kwa kweli Mwenyezi Mungu amebainisha wazi kwamba kiama kimekaribia na vile vile Mtume wetu Muhammad rehma na amani zimfikie ameweka wazi katika hadithi zake kwamba kiama kimekaribia sana.

قال تعالى : ﴿وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّ ٱلسَّاعَةَ تَكُونُ قَرِيبًا ﴿٦٣﴾﴾ [الأحزاب : ٦٣]

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema kwenye Qurani Tukufu: {{Na kipi kitakujulisha lini kiama pengine kiko karibu}} [Al-Ahzab : 63].

قال تعالى : ﴿ٱقْتَرَبَ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمْ وَهُمْ فِى غَفْلَةٍ مُّعْرِضُونَ ﴿١﴾﴾ [الأنبياء :١]

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{imekaribia watu hisabu yao (ya kiama) nao wamo katika kughafilika na wanalipuuza}} [Al-Anbiya : 1].

Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) asema: [Nimetumilizwa na kiama kama vidole viwili]. Akashiria vidole viwili cha kati na cha shahada.

Ndugu mnaonisikiliza napenda kuwabainishia vigawanyo vya alama za kiama. Kwa hakika alama za kiama zimegawanyika vigawanyo viwili.

1. Alama ndogo.
2. Alama kubwa.

Alama ndogo ni zinatangulia au zinazokuja kabla ya siku kiama kwa mda mrefu na zinazoeleka na zinaweza kudhihiri baadhi yake pamoja na alama kubwa au zikaja baada ya alama kubwa.

Ama alama kubwa ni mambo makubwa ambayo yatadhihiri karibu na kiama na huwa si ya kawaida kwa mfano kuja Dajjal na nyenginezo.

Na ukizingatia kudhihiri kwake zimegawanyika vigawanyo vitatu

1. Alama zilizodhihiri na kuweko
2. Alama zilizodhihiri na bado zinatokea

3. Alama ambazo hazijatokea mpaka sasa.

Alama Ndogo za Qiyama:-

Ndugu zangu Waislamu napenda kuzitaja alama ndogo za kiama nazo ni kama zifuatazo;

- Kutumilizwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Nimetumilizwa na kiama kama vidole viwili]. Akashiria vidole viwili cha kati na cha shahada.
- Kufa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) ni miongoni mwa alama ndogo za kiama, kwani ni ishara wazi ya kukatika wahyi kutoka mbinguni.
- Alama nyingine ya kiama ni kudhihiri fitna kubwa; itachanganyika haki na batili zitatikisika imani mpaka mtu ataamka asubuhi hali ya kuwa ni muislamu na atalala hali ya kuwa ni kafiri au atalala hali ya kuwa ni kafiri na ataamka hali ya kuwa ni muislamu.

Hii ni kuonesha kwamba mtu kuingia katika ukafiri ni wepesi kwa kule kuchanganyika haki na batili na ndio hali za zama zetu hizi, watu wamechanganyikiwa kiasi kwamba hawajui haki ni ipi na batili ni ipi. Na kila ikidhihiri fitna atasema haya ndio maangamivu yangu kisha itaondoka itakuja nyingine atasema muumini haya ndio maangamivu na na hazitawacha fitna kudhihiri kwa watu mpaka kiama kisimame. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Hakika kabla ya kiama kutakuwa na fitna kama kipande cha usiku wa giza mtu ataamka muislamu na atalala kafiri na atalala kafiri na ataamka muislamu na aliyekaa ni bora kuliko aliyesimama na aliyesimama ni bora kuliko aliyetembea na anayetembea ni bora ni kuliko anayekwenda mbio].

- Katika alama ndogo za kiama ni kudhihiri moto katika ardhi ya Hijazi na kupotea amana. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Hakitasimama kiama mpaka utoke moto katika ardhi ya Hijazi unatoa mwangaza moto huo kiasi utaona shingo za ngamia Basra]. Hakika moto huu umeshadhihiri katikati ya karne ya saba mwaka 654 hijria na ulikuwa mkubwa waliweza kuuona wanavyuoni wengi ambao waliokuwa zama hizo na waliokuja baada yao katika kuuelezea moto huo.
- Vilevile kupotea amana ni katika alama za kiama watu kutotekeleza majukumu waliopewa na kutowajibika inavyotakiwa, Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) asema: [Ikipotea amana ngojea kiama].
- Katika alama za ndogo za kiama ni kuenea zinaa kiasi kwamba litakuwa jambo la kawaida na asiyejihusisha na jambo hilo watu. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Naapa kwa ambae nafsi yangu iko mkononi mwake hautamalizika umma huu mpaka asimame mwanamume na mwanamke na amlaze njiani afanye nae zinaa aseme mbora wao siku hiyo lau mtazunguka nyuma ya ukuta (mufanyie huko)].
- Katika alama nyingine za kiama ni kuenea riba tukijua kuwa riba ni katika madhambi makubwa sana lakini namna itakavyoenea litakuwa jambo la

kawaida, lakini watu hawajali na watajaza matumbo yao haramu.

قال تعالى : ﴿وَأَحَلَّ ٱللَّهُ ٱلۡبَيۡعَ وَحَرَّمَ ٱلرِّبَوٰاْۚ﴾ [البقرة :٢٧٥]

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Na Mwenyezi Mungu amehalalisha biashara na ameharamisha riba}} [Al-Baqara : 275]. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [kabla ya kuja kiama kutadhhiri riba].

- Miongoni mwa alama za kiama ni kudhihiri na kuenea muziki kwa wingi na watu watahalalisha miziki hiyo, Mtume ameeleza haya katika hadithi zake nyingi suala hili kwa hivyo inatakiwa Waislamu wachunge mipaka ya Mwenyezi Mungu kwa kuomba msamaha kwake na kutubia, kwani hali za wanaadamu ni mbaya na za kusikitisha sana. Huku tusisahau kupeana nasaha kwa kuamrishana mema na kukatazana yalio mabaya.
- Miongoni mwa alama ndogo za kiama ni watu kujenga majumba makubwa na marefu tena kutoka kwa watu katika duni katika jamii kufikia kiwango cha utajiri na haya ni kwa mujibu wa maneno ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alipotaja baadhi ya alama za kiama: [Ni kuzaa mtumwa wa kike bwana wake na utaona watu wasiokuwa na viatu waliouchi, masikini, wachunga mbuzi wanashidana kurefusha majumba]. Na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Hakitasimama kiama mpaka watu wajifakhiri kwa kujenga Misikiti].
- Katika alama za kiama ni kukithiri uongo baina ya watu, watadanganyana kwa wingi huku tunajua kwamba uongo ni katika makosa makubwa Aliyoyakataza Mwenyezi Mungu katika Quran na vile vile Mtume rehma na amani zimfikie ameukataza uongo katia hadithi zake tukufu. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema katika hadithi yake: [Hakitasimama kiama mpaka zidhihiri fitna, kukithiri uongo na kukaribiana masoko].
- Vilevile hakitasimama kiama mpaka atamani aliye hai mauti kwa namna hali za watu zitakavyokuwa mbaya. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Hakitasimama kiama mpaka aende alie kaburini asimame aseme natamani mahali pako]. yaani atatamani alie hai afe yeye.
- Kukaribiana masoko ni miongoni mwa dalili za kiama. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Hakitasimama kiama mpaka kukithiri uongo na kukaribiana masoko]. Hizi ndio miongoni mwa alama chache za kiama na ni vyema kwa muislamu yoyote azijue vizuri kwani akiziona huenda akajiandaa na siku ya mwisho kabla hajafikiwa na mauti kwa kufanya vitendo vizuri na kujiepusha na vitendo vibaya.

KHUTBA YA PILI

Alama Kubwa za Kiama:-

Shukrani zote na sifa njema ni za Allah Mola wa viumbe na Mlezi wa viumbe vyote. Rehma na amani zimfikie Mwalimu wetu, Mtume wetu Muhammad.

Ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na vile vile kumtakia rehma na amani Mtume Mtukufu baada kutaja alama ndogo za kiama sasa katika khutba hii ya pili nitataja alama kubwa za kiama nazo ni kama zifuatazo:-

- Kutoka kwa Dajjal kiumbe wa ajabu ambaye atakaye wafitini sana watu na kuwapotosha sana na kuwatia katika ukafiri kwani atakuwa na pepo na moto, atakaye muamini yeye atamwingiza peponi na atakaye muasi atamtia motoni, ataendelea kufanya hivyo mpaka aje Nabii Isa aje apambane nae na kumuua.
- Miongoni mwa alama za kiama ni kutoka Yaajuj na Maajuj ambao watatokea Asia ya kati waliofungiwa kwa sababu ya uharibifu wao katika ardhi pale alipopita mfalme Dhul-Qarnain aliyewafungia na kuziba sehemu ambayo walitaka kutokea kupitia sehemu hiyo.

قال تعالى : ﴿ حَتَّىٰٓ إِذَا فُتِحَتۡ يَأۡجُوجُ وَمَأۡجُوجُ وَهُم مِّن كُلِّ حَدَبٖ يَنسِلُونَ ٩٦ ﴾ [الأنبياء : ٩٦]

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Hata watakapofunguliwa Yaajuj na Maajuj wakawa wanateremka kutoka kila mlima}} [Al-Anbiya : 96].

قال تعالى : ﴿ قَالُواْ يَٰذَا ٱلۡقَرۡنَيۡنِ إِنَّ يَأۡجُوجَ وَمَأۡجُوجَ مُفۡسِدُونَ فِي ٱلۡأَرۡضِ فَهَلۡ نَجۡعَلُ لَكَ خَرۡجًا عَلَىٰٓ أَن تَجۡعَلَ بَيۡنَنَا وَبَيۡنَهُمۡ سَدّٗا ٩٤ ﴾

[الكهف : ٩٤]

Na Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala): {{Wakasema: Ewe Dhul-Qarnain hakika Yaajuj na Maajuj wanafanya uharibifu katika ardhi, basi je tukupe ujira ili utie baina yetu na baina yao kizuizi}} [Al-Kahfi : 94].

- Katika alama za kiama ni kushuka Nabii Isa amani iwe juu yake atakuja kupambana na Dajjal ambaye alipotosha sana watu na Nabii Isa atamuuwa Dajjal.
- Miongoni mwa alama za kiama ni kuja Mahdy.
- Kuchomoza jua kutoka magharibi na wakati huo milango ya toba itafungwa na hatosamehewa mtu yoyote kuomba msamaha wala kurejea tena kwa Mwenyezi Mungu maneno haya yanatupa sisi changamoto ya kukimbilia kumuomba Mwenyezi Mungu na kurejea kwake, kwani mlango wa toba ukifungwa ufunguliwi na watu wataanza kuhesabiwa.
- Kudhihiri moshi duniani na kutoka mnyama anaezungumza na watu na kuwakumbusha mambo ya Mwenyezi Mungu.
- Kushikwa jua sehemu tatu; kushikwa jua mashariki, magharibi na bara arabu.
- Kutoka moto sehemu ya Aden katika nchi ya Yemen ulio wazi kabisa utakaokusanya watu katika ardhi ya watu kuhesabiwa vitendo vyake. Utalala moto huo watakapolala usiku na mchana pia utalala watakapo lala.

Kwa kweli alama hizi kubwa tena za kutisha hatuna ujanja wowote wa

kuzikwepa siku hii nzito na ya kuogopesha.

Enyi ndugu katika imani! Hizo tulizo zitaja ndizo alama za kuja siku ya mwisho ambayo ni siku ya hesabu watakapo hesabiwa watu wote, suala la kwamba je tumejiandaa kwa siku hii ni muhimu sana Je, tumefanya nini cha kutusaidia mbele ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala)? Kwanini basi tusimtake msamaha Mwenyezi Mungu na kurudi kwake?.

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu jueni ya kwamba kupatikana kwa alama ndogo za kiama kwa wingi ni dalili na ishara ya wazi ya kukaribia alama kubwa ambazo zitakapokaribia alama hizo kubwa ndio kuja kwa kiama chenyewe. Basi tumcheni Mwenyezi Mungu na tufanye amali nzuri na tujiandae vilivyo na siku hii ya mwisho. Na jueni ya kwamba kiama kitafika hakuna chembe cha shaka ndani yake.

Mwisho

Tunamshukuru Manani aliyetuwezesha kuwabainishia ndugu zangu Waislamu kumuamini Mungu na siku ya mwisho pia tumesisitiza vitendo vizuri na kutumia fursa vizuri kama ambavyo tumejitahidi kuwazindua waislamu kukaribia kiama, vile vile tumewatahadharisha waumini popote walipo kutokana na fitna na njia za kujiepusha tukamalizia kubainisha baadhi ya alama za kiama.

Mwisho tunamuomba Mwenyezi Mungu Atupe misimamo katika dini na kushikamana na dini mpaka mwisho wa pumzi zetu. Atujaalie miongoni mwa wanaofanya maandalizi mazuri ya kukutana naye siku ya kiama.

[4] KUTAHADHARI NA UCHAWI NA UGANGA

Lengo la Khutba:

1. Kufungamanisha nyoyo za Waislamu na Mola wao.
2. Kubainisha hukumu ya uchawi na uganga katika Uislamu.
3. Kutahadharisha watu kwenda kwa waganga, wachawi na wapiga ramli.
4. Kubainisha hatari za uganga na uchawi katika umma.
5. Kuhimiza kuchukua sababu za kisheria.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Shukrani ni za Allah (Subhaanahu wa Taala), Mola wa viumbe vyote. Tunamtakia rehema na amani Mtume Muhammad. Kwa uwezo wa Mungu tutazungumzia kuhusu kufungamanisha nyoyo za Waislamu na Mola wao. Vilevile tubainishe hukumu ya uchawi na uganga katika uislamu pia tutatoa tahadhari kwa watu kwenda kwa waganga na wapiga ramli na pia tuwabainishie hatari za waganga katika umma tutahimiza kuchukua sababu za kisheria.

Ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), na kumtakia rehma na amani Mtume Muhammad. Ni kweli usiofichika ya kwamba watu wanapitia mitihani mbali mbali, kwa mfano mitihani ya kiuchumi, ya kiafya na pia ya kijamii na mitihani mingineo. Kwa hivyo kukabiliana na mitihani hii ni lazima sheria ichungwe na sababu za kisheria zifuatwe katika kutatua matatizo yoyote yanayomkabili Muislamu popote alipo hafai kwenda kinyume na sheria.

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, hakika katika mitihani waliopewa watu leo, waume kwa wake, wakubwa kwa wadogo, isipokuwa walio rehemewa na Mwenyezi Mungu ni kwenda kwa waganga na watu wa ramli wanaokula mali za watu kwa batili. Unaweza kumuona kiongozi amefungamanishwa na mganga hafanyi jambo lolote isipokuwa kwa ushauri wake hata kama ushauri huo utaenda kinyume na dini ya kiislamu, na anahisi ndani ya moyo wake ya kwamba huyo mganga ndiye anayempa uongozi na anaweza kuuchukua uongozi huo.

قال تعالى : ﴿ قُلِ ٱللَّهُمَّ مَٰلِكَ ٱلۡمُلۡكِ تُؤۡتِي ٱلۡمُلۡكَ مَن تَشَآءُ وَتَنزِعُ ٱلۡمُلۡكَ مِمَّن تَشَآءُ وَتُعِزُّ مَن تَشَآءُ وَتُذِلُّ مَن تَشَآءُۖ بِيَدِكَ ٱلۡخَيۡرُۖ إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيۡءٖ قَدِيرٞ ﴿٢٦﴾ ﴾ [آل عمران:٢٦].

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Sema ewe Mwenyezi Mungu Mfalme wa wafalme Unampa ufalme unaye mtaka na unampokonya ufalme unayemtaka na unamtukuza unayemtaka na Unamdhalilisha unayemtaka katika mkono wako kuna kheri. Hakika yako wewe juu ya kila kitu ni muweza}}.

Utaona mfanyabiashara hanunui wala hauzi isipokuwa kwa ushauri wa mganga ambaye amefungamanisha moyo wake na mganga huyo na hufanya lolote atakaloambiwa na mganga namna litakavyokuwa jambo lile. Utapata mke anaetaka kumtawala mumewe kwa kiasi ambacho mume yule hatatamani mke mwengine isipokuwa yeye ataenda mke yule kwa mganga mchafu na atataka

usaidizi, akisahau kuwa Mwenyezi Mungu ndie ambaye amejaalia mapenzi ya dhati baina ya mume na mke hii ndio hali yetu waja wa Mwenyezi Mungu isipokuwa aliyerehemewa na Mwenyezi Mungu.

Ndugu katika imani ni vyema niwatajie Aya na hadithi za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Amebainisha Mola katika Qur’an tukufu kwamba kujifundisha uchawi ni ukafiri.

قال تعالى : ﴿وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّىٰ يَقُولَا إِنَّمَا نَحْنُ﴾ [البقرة: ١٠٢].

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Na hawamfundishi yoyote mpaka waseme hakika yetu sisi ni fitna usikufuru}}.

وقال تعالى : ﴿وَلَا يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَىٰ ﴿٦٩﴾﴾ [طه : ٦٩].

Vile vile Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Na hafaulu mchawi namna ajavyo}} [Twaha: 69]. Na amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Jiupusheni na mambo saba yanayoangamiza, wakasema maswahaba: Ni yapi, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): Kumshirikisha Mwenyezi Mungu, uchawi, kula mali ya yatima, kukimbia vitani na kuwasingizia kuwa wamezini wanawake waliojihifadhi walioghafilika tena waumini].

Asema Aisha: [Watu walimuuliza Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) kuhusu uganga akasema: Hao si chochote. Wakasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu hakika hao wanazungumzia mambo mara nyingine kisha yanatokea kweli. Akasema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): Hilo ni neno la haki analolichukua jinni kisha akalitia katika sikio la rafiki yake naye kwa upande wake akachanganya neno hilo na maneno mia ya uongo]. Na katika hadithi nyingine za kukataza uchawi na uganga. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Atakayeenda kwa mganga au mchawi akamuuliza na akamuamini kwa atakayosema basi amekufuru aliyoteremshiwa Mtume Muhammad rehma na amani zimfikie].

Hadithi hii tukufu inatufundisha kwamba mtu yoyote atakaye kwenda kwa mganga kumuuliza kitu na akamuamini kwa atakayomwambia basi ametoka kabisa katika dini ya Uislamu. Ama hukumu ambayo inatakiwa aichukue kiongozi kwa atakayepatikana anafanya uchawi ni kukatwa shingo yake na kuuwawa kama ilivyothibiti katika maneno ya Maswahaba Mwenyezi Mungu awawie radhi; Tahadhari tunayoitoa ni kwamba haifai kwa Muislamu kuchukua hatua mikononi mwake isije ikaleta balaa na fujo miongoni mwa watu.

Madhara ya Wachawi na Waganga katika Umma

Ninafuraha enyi Waislamu, kutaja baadhi ya madhara ya waganga na wachawi katika umma. Madhara hayo ni kama yafuatayo;

1. Kufutika imani za wanaokwenda kwa waganga na kuwaamini kwa watakayo ambiwa kama ilivyo katika hadithi ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) tuliyoitaja.

2. Kukithiri vifo na au kuona makaburi yanafukuliwa au kuona baadhi ya viungo vya wanadamu kwa hawa waganga baada ya kuwaamrisha wafuasi wao wawaletee.
3. Kuenea zina na machafu baina ya watu kwani ni wangapi katika waganga hufanya zina na wake za watu na wakaharibu ndoa za watu na wakafungua milango mikubwa ya shari.
4. Kula mali za watu kwa njia ya batili kinyume na haki, kwani kila anachochukua mganga ni kwa kazi yake mbovu na anakula uchafu. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amekataza kula thamani ya mbwa na mahari ya mzinifu na chumo la mganga.
5. Kuwapoteza watu na kuwafanya watu kuwa na tabia mbaya na kuwazuia wao kutekeleza maamrisho ya Dini, kwani kuna wengine huacha swala zote au baadhi yake na wengine huzuiliwa kuoga janaba na wengine huzuiliwa kufanya mema bali huamrishwa kufanya mabaya.
6. Kumkasirisha Mwenyezi Mungu na kusababisha adhabu yake. Alisema Zainab binti Jahshi kumwambia Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Je tunaweza kuangamizwa na kati yetu kuna watu wema? Akasema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): Ndio, ukikithiri uchafu]. Na je kuna wachafu zaidi kuliko waganga waovu?.
7. Kupata hasara duniani na kesho akhera.

وقال تعالى : ﴿وَلَا يُفۡلِحُ ٱلسَّاحِرُ حَيۡثُ أَتَىٰ ﴿٦٩﴾﴾ [طه : ٦٩].

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Na hafaulu mchawi namna ajavyo}} [Twaha: 69].

Sheikhul Islaam Ibn Taimia Mwenyezi Mungu Amrehemu amesema: «Hivi ndivyo ilivyo. Hakika ufuatiliaji unaonesha kwamba watu wakitegemea nyota hawafaulu. Si duniani bali vile vile kesho akhera.”

Hayo ndiyo baadhi ya madhara yanayopatikana kutoka kwa waganga waovu. Kwa hivyo, ni lazima ewe Muislamu kuelekea kwa Mwenyezi Mungu na watu wakumbushane kwamba jambo la kwenda kwa waganga na kuangaliliwa ni jambo baya na halifai. Jueni ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mfalme na Mwenye kumiliki kila kitu, hana wa kumzuwia anapo toa. Ametuamrisha Mola Wetu tutakapo kuwa na tatizo lolote tumuombe Yeye na tumtake Yeye msaada, na yafaa tumtegemee yeye katika kila kitu na tuchukue sababu za kisheria katika kufikia tunayoyakusudia na miongoni mwa sababu hizo ni kumuomba Mwenyezi Mungu dua. Kwa hivyo, atakaemuomba kwa nia njema hakika Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa amali ya anayeomba. Mwenyezi Mungu yuko karibu na hujibu maombi na yeye ndiye anayeruzuku ndege porini na samaki baharini.

قال تعالى : ﴿ٱللَّهُ ٱلَّذِي خَلَقَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضَ وَأَنزَلَ مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً فَأَخۡرَجَ بِهِۦ مِنَ ٱلثَّمَرَٰتِ رِزۡقًا لَّكُمۡۖ وَسَخَّرَ لَكُمُ ٱلۡفُلۡكَ لِتَجۡرِيَ فِي ٱلۡبَحۡرِ بِأَمۡرِهِۦۖ وَسَخَّرَ لَكُمُ ٱلۡأَنۡهَٰرَ ﴿٣٢﴾ وَسَخَّرَ لَكُمُ ٱلشَّمۡسَ وَٱلۡقَمَرَ دَآئِبَيۡنِۖ وَسَخَّرَ لَكُمُ ٱلَّيۡلَ وَٱلنَّهَارَ ﴿٣٣﴾﴾ [إبراهيم: ٣٢-٣٣].

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Mwenyezi Mungu ambaye ameumba mbingu na ardhi na ameteremsha maji kutoka mbinguni akatoa kutokana na maji hayo matunda hali ya kuwa ni riziki kwenu na Amewadhalilishia meli ili itembee baharini kwa amri Yake na Akawadhalilishia mito na akawadhalilishia jua na mwezi zinazotembea na akawadhalilishia usiku na mchana na akawapa kila mnachoomba na endapo mutazihesabu neema za Mwenyezi Mungu hamuwezi kuzidhibiti hakika mwanadamu ni dhalimu aliye mkufuru Mwenyezi Mungu}}.

KHUTBA YA PILI

Kufuata Sababu Pamoja na Kumtegemea Mwenyezi Mungu

Shukrani za dhati ni za Mola Mlezi wa viumbe vyote. Rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad. Ama baada ya kumshukuru Allah (Subhaanahu wa Taala) na kumtakia rehma na amani Mtume Wetu. Tumetaja katika KHUTBA YA KWANZA waliopewa mitihani ya matatizo, tukaweza kubainisha kwa kuzitaja Aya na hadithi zinazotoa tahadhari ya kwenda kwa waganga na wachawi pia tukaweza kutaja na kuweka wazi hatari na madhara ya waganga na wachawi katika jamii na mazingira tunayoishi tukaongezea kuwalingania watu kumuelekea Mwenyezi Mungu kwa kufuata sababu zinazoruhusiwa kisheria katika kukabiliana na matatizo mbali mbali.

Katika khutba hii ya pili napenda kurudia kwa kusisitiza sababu ambazo Ameziweka Allah (Subhaanahu wa Taala) kufuata ni dua, kumtegemea na kumtaka yeye pekee msaada. Kwani dua ni ibada na dua ni silaha ya Muislamu, Ametuamrisha Mwenyezi Mungu kumuomba yeye peke yake.

قال تعالى : ﴿وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۖ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ﴿١٨٦﴾﴾ [البقرة:١٨٦].

Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala): {{Na watakapoko uliza waja wangu kunihusu basi mimi niko karibu naitikia maombi ya anayeomba atakapoomba basi waniitikie mimi}}. Amesema mshairi kwamba Mwenyezi Mungu Anakasirika anapoombwa asiyekuwa yeye.

Ndugu Muislamu, Usiombe kabisa mwanadamu haja yoyote na muombe ambaye milango yake haifungwi. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Anakasirika ukiwacha kumuomba na ukimuomba mwanadamu anakasirika. Ewe unaye taka riziki, taka riziki kwa Mwenyezi Mungu.

قال تعالى : ﴿فَابْتَغُوا عِندَ اللَّهِ الرِّزْقَ وَاعْبُدُوهُ وَاشْكُرُوا لَهُ ۖ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿١٧﴾﴾ [العنكبوت:١٧]

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Takeni riziki kwa Mwenyezi Mungu na muabuduni na mshukuruni kwake yeye mtaregea}}.

Ewe unaetaka kuzaa, Je umesahau dua ya Nabii Zakariya pale alipomuomba dua Mola wake akasema:

دعاء زكريا عليه السلام حين دعا ربه فقال : ﴿رَبِّ هَبْ لِي مِن لَّدُنكَ ذُرِّيَّةً طَيِّبَةً ۖ إِنَّكَ سَمِيعُ الدُّعَاءِ ﴿٣٨﴾﴾ [آل عمران:٣٨].

{{Mola wangu, Nipe mimi kutoka kwako kizazi kizuri hakika yako unaitikia maombi}}. Ewe unaye taka ufalme au cheo au chochote kile, kitake kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Tunapenda kuwakumbusha viongozi popote walipo na wenye ghera katika dini kwa majukumu waliyonayo kuhusiana na hawa waganga na wachawi na mafasiki katika kusimamishiwa hukumu ya Mwenyezi Mungu na kuwakataza watu kwenda kwa waganga na kuwakodishia maduka yao.

قال تعالى : ﴿وَتَعَاوَنُواْ عَلَى ٱلۡبِرِّ وَٱلتَّقۡوَىٰۖ وَلَا تَعَاوَنُواْ عَلَى ٱلۡإِثۡمِ وَٱلۡعُدۡوَٰنِۚ﴾ [المائدة:٢].

Kwani Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Na saidianeni katika mema na uchaji Mungu wala musisaidiane katika madhambi na uadui}}. Amesema Sheikh Ibn Taimia Mwenyezi Mungu Amrehemu: "Na hakika imebainika katika tuliyoyataja kwa ujira unaochukuliwa kutoka kwa waganga, kuchukua hiba na karama ni haramu kwa anayetoa na anayechukua". Kwa hivyo inatakiwa watu wakatazane jambo hili, kwani wakiwacha ibada hii ya kuamrishana mema na kukatazana maovu watapata hasara kubwa. Kwa kweli maovu yanaenea kiasi kikubwa ni kama ugonjwa ambao hautibiwi kwa kutumia dawa huzidi na kumdhoofika zaidi mwenye ugonjwa.

Tahadharisho kwa ndugu zangu Waislamu tusiliwache jambo hili tukawa kama Banii Israil ambao walikuwa hawakatazani maovu waliokuwa wakiyafanya ikawa ni sababu ya wao kulaaniwa.

قَوْلُهُ تَعَالَى : ﴿كَانُواْ لَا يَتَنَاهَوۡنَ عَن مُّنكَرٍ فَعَلُوهُۚ﴾ [المائدة: ٧٩].

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Walikuwa hawakatazani maovu waliokuwa wakiyafanya}}. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Hakika watu watakapoona maovu na wasiliondoe inakaribia kujumuishwa na Allah kwenye adhabu yake].

Mwisho.

Nawausia ndugu zangu kumcha Mwenyezi Mungu na mtubie kwa Allah, mumtake msamaha na mtegemee yeye katika mambo yote pamoja na kufuata sababu za halali, wacheni kwenda kwa waganga na mujiepushe na jambo hilo hali ya kumtii Mungu na Mtume na kuhifadhi Dini yenu kwani leo ni kufanya vitendo bila kuhesabiwa na kesho ni hesabu bila kufanya vitendo.

Kwa ufupi katika khutba yetu hii tumezungumzia kufungamanisha nyoyo za Waislamu na Mola wao pia tumebainisha hukumu ya uchawi na uganga katika uislamu vile vile kutahadharisha watu kwenda kwa waganga na wapiga ramli, pia tumebainisha hatari za uganga katika umma na tumehimizana kufuata sababu za kisheria.

Mwisho tunamuomba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) atuhifadhi na kila balaa na Atuepushe na mitihani na matatizo. Atuongoze katika njia iliyonyooka, njia ya kukuelekeza katika dua na kufuata sababu za kisheria katika kutatua matatizo yetu..Ewe Mwenyezi Mungu itikia maombi yetu.

[5] KUWAKUMBUSHA WATU DALILI ZA MWENYEZI MUNGU KATIKA VIUMBE

Lengo la Khutba:

1. Kuwakumbusha watu baadhi ya alama za Mwenyezi Mungu katika viumbe.
2. Kubainisha ukubwa wa Allah na kwamba yeye Anastahiki kuabudiwa kinyume na mwingine.
3. Kulingania watu kumshukuru Allah aliyewadhalilishia viumbe hivyo.
4. Kulingania watu kutumia viumbe hivi katika kumuabudu Allah.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Tunamshukuru Allah (Subhaanahu wa Taala) Aliyetupa neema nyingi. Rehma na amani zimfikie Mtume wetu Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Nachukua fursa hii kuwakumbusha watu baadhi ya dalili na alama za kumjua Mungu kupitia viumbe vyake, pia nitabainisha ukubwa wa Mwenyezi Mungu na kwamba Anastahiki kuabudiwa. Vilevile nitagusia suala la watu kumshukuru Mwenyezi Mungu Aliyetudhalilishia viumbe hivyo, na tutakumbushana kuvitumia viumbe vya Mwenyezi Mungu katika kumuabudu yeye.

Ama baada ya kumtukuza na kumshukuru Allah na pia kumtakia rehma na amani Mtume wetu. Mwenyezi Mungu Ametuamrisha tuamini kwamba yeye yuko. Na Aya zinazozungumzia suala hili ni nyingi sana pia ameumba viumbe vinavyoonesha kwamba yeye yupo.Kwani kupatikana kwa viumbe ni kuonesha kuna aliyeumba.

Enyi ndugu katika imani ! Hakika katika kila kitu alivyoviumba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ni dalili ya kuonesha kwamba yeye ni mmoja, na ndiye anayestahiki kuabudiwa kwa haki kabisa na haifai kushirikishwa na yoyote wala chochote.

Napenda nizitaje baadhi ya Aya ambazo zimetuamrisha kuzingatia katika ulimwengu.

قال تعالى : ﴿ أَوَلَمْ يَنظُرُوا۟ فِى مَلَكُوتِ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَمَا خَلَقَ ٱللَّهُ مِن شَىْءٍ وَأَنْ عَسَىٰٓ أَن يَكُونَ قَدِ ٱقْتَرَبَ أَجَلُهُمْ ۖ فَبِأَىِّ حَدِيثٍۭ بَعْدَهُۥ يُؤْمِنُونَ ﴿١٨٥﴾ ﴾ [الأعراف : ١٨٥].

Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala): {{Je hawaangalii ufalme katika mbingu na ardhi na alivyoumba Mwenyezi Mungu katika vitu, na huenda ikiwa umekaribia muda wao wa kuondoka duniani kumalizika. Basi ni maneno gani baada ya Qur’an watayamini}} [Al-Araaf : 185].

وقال : ﴿ أَفَلَمْ يَنظُرُوٓا۟ إِلَى ٱلسَّمَآءِ فَوْقَهُمْ كَيْفَ بَنَيْنَٰهَا وَزَيَّنَّٰهَا وَمَا لَهَا مِن فُرُوجٍ ﴿٦﴾ وَٱلْأَرْضَ مَدَدْنَٰهَا وَأَلْقَيْنَا فِيهَا رَوَٰسِىَ وَأَنۢبَتْنَا فِيهَا مِن كُلِّ زَوْجٍۭ بَهِيجٍ ﴿٧﴾ تَبْصِرَةً وَذِكْرَىٰ لِكُلِّ عَبْدٍ مُّنِيبٍ ﴿٨﴾ ﴾ [ق : ٦ – ٨].

Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala): {{Je hawaangalii mbingu juu yao vipi tuliijenga na kuipamba na kuifanya kuwa haina nyufa. Na ardhi vipi tuliitandaza na kuiweka vigingi (isitikisike) na tukaotesha katika ardhi hiyo kila mimea mizuri

hali ya kuwa ni kifumbua macho kwa kila mtu muelekevu}} [Qaaf : 6 - 8].

وقال : ﴿أَفَلَا يَنظُرُونَ إِلَى ٱلۡإِبِلِ كَيۡفَ خُلِقَتۡ ﴿١٧﴾ وَإِلَى ٱلسَّمَآءِ كَيۡفَ رُفِعَتۡ ﴿١٨﴾ وَإِلَى ٱلۡجِبَالِ كَيۡفَ نُصِبَتۡ ﴿١٩﴾ وَإِلَى ٱلۡأَرۡضِ كَيۡفَ سُطِحَتۡ ﴿٢٠﴾﴾ [الغاشية ١٧ – ٢٠].

Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala): {{Je hamwangalii Ngamia vipi ameumbwa, na mbingu vipi zimeinuliwa, na milima vipi imekitwa na ardhi vipi imetandikwa}} [Al-Qaashiyah: 17- 20]. Hizi ni alama ambazo Mola anataka tuzingatie kuumbwa kwake.

Napenda sasa kutaja baadhi ya viumbe vingine vya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Navyo ni vinavyopatikana katika ardhi kama vile; Maji, Madini, Majabali, Mimea aina tofauti tofauti, kwani Mwenyezi Mungu ameidhalilisha ardhi hii kwa manufaa ya wanadamu na wanyama, wanadamu wanailima kwenye ardhi na kupanda mimea ili kujipatia chakula chao, wanatoa maji katika ardhi kwa matumizi yao na pia kuwanywesha wanyama wao. Mwenyezi Mungu amesema

قال تعالى ﴿وَفِي ٱلۡأَرۡضِ ءَايَٰتٞ لِّلۡمُوقِنِينَ ﴿٢٠﴾﴾ [الذاريات:٢٠].

Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala): {{Na katika ardhi kuna alama nyingi kwa wenye yakini}}. Tukiangalia mbinguni kuna nyota nyingi, jua, mwezi na sayari nyinginezo. Vilevile mbinguni kuna viumbe vya Mwenyezi Mungu ambao ni Malaika wanaotekeleza kazi alizowapa Mola aliyetukuka.

Na katika alama nyingine za kumjua Mwenyezi Mungu ni usiku na mchana. Mchana ni wakutafuta maisha na riziki na usiku ni kupumzika.

قال تعالى ﴿وَجَعَلۡنَا ٱلَّيۡلَ لِبَاسٗا ﴿١٠﴾ وَجَعَلۡنَا ٱلنَّهَارَ مَعَاشٗا ﴿١١﴾﴾ [النبأ:١٠:١١].

Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala): {{Na tumeufanya usiku ni nguo na tukaufanya mchana ni wa kutafuta maisha}}. Na katika alama hizi mbili za usiku na mchana amewafanyia watu mchana kwenda katika ardhi ya Allah na kutafuta fadhila zake na katika kutafuta fadhila hizo atazidi kubainikiwa mwanaadamu na kuzifahamu alama nyingine za Mwenyezi Mungu. Na katika usiku ni wakati wa kujipumzisha baada ya uchovu wa mchana katika hali ya kutafuta riziki na kutafuta maisha.

Tukigusia zaidi alama za Allah ni wanyama wengi wakubwa kwa wadogo na katika wadogo kuna wadogo zaidi, kuna wengine ametufanyia kuwatumia katika kazi zetu za kila siku, kama kubeba mizigo na kutupeleka sehemu nyingine Na dalili ya alama za Mwenyezi Mungu ni kuumbwa kwetu kwani kuna mazingatio makubwa sana.

قال تعالى ﴿وَفِيٓ أَنفُسِكُمۡۚ أَفَلَا تُبۡصِرُونَ ﴿٢١﴾﴾ [الذاريات:٢١].

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema:{{Na je katika nafsi zenu basi hamuoni}}. Aya hii inatueleza kuwa katika maumbile yetu wanadamu kuna mazingatio makubwa kumjua Mwenyezi Mungu. Lengo kuu la kumtambua ni kuzingatia katika viumbe vyako ni kumjua yeye ili kumthamini, kwani tukimthamini tutamuabudu haki ya kumuabudu na hilo ndio lengo kuu la kuumbwa majini na binadamu.

قال تعالى : ﴿وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾﴾ [الذاريات: ٥٦].

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Na sikuumba na majini na binaadamu isipokuwa waniabudu}}. Napenda kusema kwamba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ndiye aliyeumba ulimwengu wote na viumbe vyote bila usaidizi wa mtu yoyote na yeye ndiye anayeupeleka ulimwengu huu. Kwa hivyo, Yeye ndiye anayestahiki ibada kwa sababu hakuna yoyote aliyemsaidia katika uumbaji. Ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa kuumba na anaupeleka ulimwengu aliomba anavyotaka na wala haulizwi kwa analofanya bali viumbe ndio watakaoulizwa katika vitendo vyao.

Ndugu katika imani! Jueni ya kwamba viumbe vyote ambavyo vinapatikana ulimwenguni havijileti vyenyewe bali Mwenyezi Mungu aliyetukuka ndiye aliyeviumba viumbe hivyo.

قال تعالى : ﴿أَمْ خُلِقُوا۟ مِنْ غَيْرِ شَىْءٍ أَمْ هُمُ ٱلْخَٰلِقُونَ ﴿٣٥﴾ أَمْ خَلَقُوا۟ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ ۚ بَل لَّا يُوقِنُونَ ﴿٣٦﴾﴾ [الطور: ٣٥:٣٦].

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema kwenye Kitabu Chake: {{Au mumeumbwa kwa kisichokuwa kitu au nyinyi ndio waumbaji. Au nyinyi ndio mlioumba mbingu na ardhi bali wao hawana yakini}}. Kulingana na Aya hizi zinaonesha kwamba ulimwengu haukujiumba wenyewe na haukuwa kiumbe ambacho hakikumbwa wenyewe na kitu bali lazima tena kuna aliyeumba ulimwengu huu na akasimama kwa jambo lake (huo ulimwengu) naye si mwingine isipokuwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) hakuna Muumba asiyekuwa Yeye wala Mola asiyekuwa Yeye.

Enyi waumini! Lau mtaambiwa kuna jumba kubwa la ghorofa lililokamilika, halina kasoro yoyote, ya kwamba limejijenga lenyewe mtaamini? Bila shaka hili ni jambo lisilowezekana kabisa. Na lau inasemekana kuwa jumba kubwa la ghorofa limepatikana ghafla mtaamini? sina shaka kwamba mtasema haiwezekani. Kwa hivyo, huu ulimwengu ulio mpana uliokwenda juu na chini. Haiwezekani kabisa kujileta wenyewe na haiwezekani kabisa kujitokeza ghafla bali ni lazima kuna aliyeuleta ulimwengu huu ambaye ni Mjuzi Muweza naye ni Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

Tujue ya kwamba hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) katika kutudhalilishia ardhi na vilivyomo humo. Kwa hivyo, ni lazima kwa kila Muislamu kushukuru neema kubwa za Mwenyezi Mungu Alizotuneemesha Allah Mola wa viumbe vyote. Akipenda Mwenyezi Mungu tutabainisha suala la kuzishukuru neema za Mwenyezi Mungu katika KHUTBA YA PILI.

Enyi waumini! mcheni Allah (Subhaanahu wa Taala) na kumshukuru kwa uongofu aliotupa na aliyotufundisha yale ambayo tulikuwa hatujui katika mambo yaliyo na maslahi katika Dini yetu na kutujuza mambo yasiyofikiwa na akili zetu na ambayo haifungamani na na maslahi yetu hali ya kuwahurumia nyinyi na hamkupewa ilimu isipokuwa kidogo.

Mwenyezi Mungu Aliyetuelimisha vipi alianza kuumba huu ulimwenguni, na ilimu hii huwezi kuipata mpaka kupitia Mtume rehma na amani zimfikie. Na yoyote atakayetaja chochote kuhusu jinsi ya kuumbwa mbingu na ardhi, hakika ni wajibu tulinganishe na mafunzo walio kuja nayo Mitume ikiafikiana na vile walivyotufundisha Mitume, basi itakubaliwa, na ikienda kinyume na maelezo ya Mitume haikubaliwi na ikiwa Mitume hawakubainisha basi sisi itabidi tulinyamazie suala hilo wala haifai kabisa kutia ufundi wetu mpaka itubainikie kuwa ni haki au ni batili.

KHUTBA YA PILI

Kushukuru Neema za Mwenyezi Mungu

Tunamshukuru Mola aliyetukuka. Rehma na amani zimfikie Mtume wetu Muhammad. Ama baada ya kupeleka shukrani kwa Mwenyezi Mungu na kumtakia rehma na amani Mtume Muhammad. Tumegusia katika KHUTBA YA KWANZA yanayohusiana na dalili za kumjua Allah katika viumbe vyake, vile vile kubainisha ukubwa wa Mwenyezi Mungu na kustahiki kwake kuabudiwa peke yake, huku tukiangazia kudhalilishwa viumbe mbali mbali kwa maslahi ya wanadamu. Vilevile kulinganiwa watu kutumia viumbe hivi katika kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu na kumuabudu yeye peke yake. Katika khutba hii ya pili napenda kubainisha shukrani za wanadamu kwa Mwenyezi Mungu kwa neema tofauti tofauti.

Enyi ndugu katika uislamu! Shukrani ni kumsifu aliyekupa neema. Na shukrani kwa mtu inakusanya nguzo tatu muhimu, kiasi kwamba haiitwi shukrani kwa Mwenyezi Mungu mpaka zikamilike, nazo ni:

1. Mtu kuitambua neema katika moyo wake.
2. Kuizungumza neema ile kwa ulimi wake.
3. Kuitumia neema ile katika kumtii Mwenyezi Mungu. Kwa ufupi kabisa tunaweza kusema kuwa shukurani inafungamana na moyo, ulimi na viungo vya mwanadamu vilivyobakia. Kazi ya moyo ni kuitambua neema ile ya kwamba inatoka kwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) na kumpenda Mwenyezi Mungu.

Na kazi ya ulimi ni kuitaja neema ile na kumsifu Mwenyezi Mungu kwa neema hiyo na viungo vilivyosalia kazi yake ni kuvitumia katika kufanya maamrisho ya Mwenyezi Mungu. Tusisahau ya kwamba kuna faida anayoipata mwenye kumshukuru Mola na faida hiyo ni radhi zake Allah (Subhaanahu wa Taala).

قال تعالى : ﴿ وَٱللَّهُ أَخۡرَجَكُم مِّنۢ بُطُونِ أُمَّهَٰتِكُمۡ لَا تَعۡلَمُونَ شَيۡـٔٗا وَجَعَلَ لَكُمُ ٱلسَّمۡعَ وَٱلۡأَبۡصَٰرَ وَٱلۡأَفۡـِٔدَةَ لَعَلَّكُمۡ تَشۡكُرُونَ ٧٨ ﴾ [النحل:٧٨]

Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala): {{Mwenyezi Mungu Amewatoa katika matumbo ya mama zenu hali ya kuwa hamjui chochote akawajaalia masikio, macho na moyo ili mumshukuru yeye}}.

Mtume wetu Muhammad ni mfano mzuri katika kumshukuru Mola (Subhaanahu wa Taala) kwa neema nyingi alizomneemesha yeye na viumbe vyote. Alikuwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akiswali mpaka ikivimba miguu yake akaulizwa: Wewe pia wafanya hivi na umeshasamehewa dhambi zako zilizotangulia na zitakazaokuja?. Akasema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): Je, basi siwi mja mwenye kushukuru]. Na imethibiti kwamba Mu’adh bin Jabal alifundishwa na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie kukutaja na kukushukuru wewe na kufanya vizuri ibada yako].

Tunajua vyema kila wakati tukumbuke kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutudhalilishia neema nyingi na fadhila zake ili tupate kumuabudu yeye peke yake hana mshirika. Bado anasisitiza katika suala hili la kushukuru neema za Allah kwa kutaja neema za Allah kwa wingi. Anasema Hasan Al Baswariy: ‘ Tajeni neema hizi kwa kwa wingi kwani kufanya hivyo ndio kuzishukuru’. Kwa hakika Mola Amemuamrisha Mtume wake na pia sisi kuzizungumza na kuzitaja neema tulizopewa aliposema (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَأَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ ﴿١١﴾﴾ [الضحى : ١١]

{{Na ama neema za Mola wako zizungumze}} [Adhuhaa: 11]

Mwisho wa khutba hii, nawausia na kujiusia nafsi yangu kutumia neema za Mwenyezi Mungu vilivyo, kwani utumiaji wa neema vilivyo ni katika kushukuru neema hiyo. Kutumia macho inavyotakiwa ni kuishukuru neema hiyo kwani wako watu hawana neema hiyo ya macho,kutumia ulimi vizuri ni kushukuru neema hiyo ya ulimi. Neema ya mikono na miguu kuzishukuru neema hizi ni kuzitumia katika mambo ya kheri. Maneno haya tuliyoyataja yanatufundisha ya kwamba kila neema ina namna yake ya kuishukuru.Tukimalizia neema ya chakula.

يقول الله تعالى : ﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُلُوا مِن طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ وَاشْكُرُوا لِلَّهِ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿١٧٢﴾﴾ [البقرة : ١٧٢]

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Enyi mulioamini kuleni katika vizuri mulivyoruzukiwa na mumshukuru Allah ambaye mnamuabudu na kumtii}} [Al-Baqara : 172]. Pia Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Anasema:

وقال : ﴿فَكُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ حَلَالًا طَيِّبًا وَاشْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿١١٤﴾﴾ [النحل : ١١٤]

{{Kuleni katika alivyowaruzuku Allah vilivyo halali vizuri na mushukuru neema za Mwenyezi Mungu ikiwa kweli mnamuabudu}} [Al-Nahal : 144].

Mwisho

Tunamshukuru Mola Aliyetuwezesha kuyazungumza yanayohusiana na baadhi ya alama za kumjua Mungu kupitia viumbe vyake. Pia nimegusia kuhusu ukubwa wa Mungu na kwamba yeye Ndiye anayestahiki kuabudiwa. Vilevile ni kuweza kuchambua suala la watu kumshukuru Mungu aliyetudhalilishia viumbe vyake, na nimewakumbusha katika kutumia neema za Mungu alizotupa kwa kumuabudu yeye.

Mwisho kabisa tunamuomba Mwenyezi Mungu Atujaaliye miongoni mwa wenye kuzishukuru neema zake, na kupata radhi zake, na atujaaliye ni wenye kumcha na kumuabudu yeye mpaka mwisho wa uhai wetu na tuingie katika pepo yake. Na rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad.

[6] KUMTEGEMEA MWENYEZI MUNGU

(Subhaanahu wa Taala)

Lengo la Khutba:

1. Kubainisha uhakika wa kutegemea na umuhimu wake kwa Muislamu.
2. Kubainisha ya kwamba kutegemea ni katika ulazima wa Imani.
3. Kubainisha ya kwamba kuchukua sababu haikanushi kumtegemea Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala)
4. Kufunganisha nyoyo za Waislamu na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), na kubainisha ya kwamba waja wote wanamtegemea Mwenyezi Mungu.
5. Kutahadharisha Kumtegemea asiyekuwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Namshukuru Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Ambae wanamtegemea yeye wenye kumtegemea, Aliyesema mwenye kumtegemea yeye anamtosha. Sala na Salamu zimshukie Mtume Muhammad, Mtume wa mwisho na Jamaa zake na Sahaba zake wote..

Kutegemea imechukuliwa katika neno (wakala) kama kusema fulani amelitegemeza jambo lake kwa fulani na akamtegemea yeye. Kwa hivyo, kutegemea ni tafsiri ya kutegemea kwa mwenye kutegemewa, na wala hamtegemei mwanadamu mtu mwingine ila anaitakidi kwake kupata jambo.

Enyi wasikilizaji, kutafuta riziki ni maumbile ya kila mwanadamu. Utaona kukipambazuka mwanadamu anakwenda mbio, kwa sababu ya kutafuta riziki. Mkulima anajiandaa kwenda shambani. Mfanya biashara ajiandaa kwenda kwenye biashara yake. Kila mja hujiandaa kivyake. Na wote wanapata shida kwa sababu kila mmoja anataka kuhifadhi na kupata chakula cha yule anayemlazimu kumlisha; mke, watoto ama chakula cha familia yake.

Na hakika kuwa na himaya ya kutafuta cha kutosheleza au kutaka utajiri pamoja na kuwa njia yake ina vikwazo na safari ndefu. Yote hayo hupelekea lawama. Enyi Waja Dini ya kiislamu inakataa ya kwamba riziki inapatikana kwa njia ya udanganyifu. Na inakataza na kuchukia Muislamu kuitegemea njia hiyo ili apate riziki kutokana nayo. Na katika kuziba mlangu huu na njia hii. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Isiwepelekeeni nyinyi uzito wa kupata riziki mukaingia katika kumuasi Mwenyezi Mungu. Hazipatikani zilizoko kwa Mwenyezi Mungu ila kwa Twaa yake].

Kwa hivyo, ni yapi mapitio? Na nini suluhisho kutokana na maisha haya wanaoishi, watu wanatusiana, baadhi yao wanakula nguvu za wengine na baadhi yao kuwadhulumu baadhi. Na katika zama zetu hizi tunazoishi tunashuhudia hayo na kuna mifano mingi.

Enyi Waislam isikilizeni Hadithi hii inayotoka kwa Mtume wenu Muhammad, ikipokewa na ‘Umar Bin Khatwab Akisema: “Nimemsikia Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema: Lau hakika nyinyi mungalikuwa munamtegemea Mwenyezi Mungu haki ya kumtegemea, Angaliwaruzuku nyinyi kama anavyowaruzuku ndege, anatoka asubuhi akiwa na njaa, na anarudi jioni akiwa ameshiba”. Kutokana na hadithi hii tunajifunza ya kwamba tukimtegemea Mwenyezi Mungu kikweli basi Mwenyezi Mungu atatupa tunalolitaka.

Enyi Waislamu watukufu, zimekuja Aya nyingi na Hadithi nyingi zilizo sahihi kubainisha kumtegemea Mwenyezi Mungu kwa kila jambo letu na katika maisha yetu yote. Na hakika kumtegemea Mwenyezi Mungu ni jambo kubwa na ni amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu akiwaamrisha waja wake Waislamu. Amewaamrisha hilo kwa hali zote. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال تعالى : ﴿ وَلِلَّهِ غَيْبُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَإِلَيْهِ يُرْجَعُ ٱلْأَمْرُ كُلُّهُۥ فَٱعْبُدْهُ وَتَوَكَّلْ عَلَيْهِ ۚ وَمَا رَبُّكَ بِغَٰفِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٢٣﴾ ﴾ [هود : ١٢٣] .

{{Ni vya Mwenyezi Mungu vilivyofichika mbinguni na ardhini na mambo yote yanarejeshwa kwake na hakuwa Mola wako mwenye kughafilika na munayoyatenda}} [Huud : 123). Na Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال تعالى : ﴿ وَتَوَكَّلْ عَلَى ٱلْحَيِّ ٱلَّذِى لَا يَمُوتُ وَسَبِّحْ بِحَمْدِهِۦ ۚ وَكَفَىٰ بِهِۦ بِذُنُوبِ عِبَادِهِۦ خَبِيرًا ﴿٥٨﴾ ﴾ [الفرقان : ٨٥]

{{Mtegemeni Mwenyezi Mungu wa milele, Ambae hafi na mtukuze Mola wako naye anatosha kwa dhambi za waja wake anazijua}} [Al-Furqan : 58].

وقال تعالى : ﴿ وَتَوَكَّلْ عَلَى ٱلْعَزِيزِ ٱلرَّحِيمِ ﴿٢١٧﴾ ﴾ [الشعراء : ٢١٧]

{{Na umtegemee Mola wako mwenye nguvu mwenye rehema}} [Shuaraa : 217].

وقال : ﴿ وَتَوَكَّلْ عَلَى ٱللَّهِ ۚ وَكَفَىٰ بِٱللَّهِ وَكِيلًا ﴿٣﴾ ﴾ [الأحزاب : ٣].

{{Na umtegemee Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu atosha kuwa mlinzi}} [Ahzaab : 3].

Na katika Hadithi ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) inatuelezea kuhusu kumtegemea Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Imetokana na Abu Hurayra radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie Akipokea kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Wataingia peponi watu nyoyo zao ni mfano wa nyoyo za ndege] (Muslim). Maana yake wanaomtegemea Mwenyezi Mungu na kumesemwa nyoyo zao ni laini.

Enyi Ndugu, Hakika kutegemea ni kusadikisha kutegemea moyo kwa Mwenyezi Mungu katika kuleta mambo mema na kuondosha madhara. Vilevile kumtegemea Mwenyezi Mungu ni ukweli na imani na utulivu na kua na mafungamano baina ya mja na Mola wake.

Amesema Ibnul-Qayyim amrehemu yeye Mwenyezi Mungu: "Kutegemea ni nusu ya imani na ni nusu ya pili ya kurudi kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu amewaahidi wenye kumtegemea malipo makubwa na malipo mengi". Katika Hadithi iliyoko katika sahihi mbili hadithi ya watu sabini elfu wataingia peponi bila hisabu, nao ni wale ambao hawataki kuzunguliwa, wala hawajichomi, wala hawatabiri ndege wanamtegemea Mola wao".

Na hakukuwa kutegemea Mwenyezi Mungu kunakanusha kuchukua sababu za sheria zilizo halali. Mfano mtu akisema mimi sitafuti riziki wala siendei mbio, ikiwa imeandikwa kwangu niwe tajiri nitakuwa tajiri bila kutaabika wala shida, ikiwa SIkuandikiwa basi siwi hakuna haja nisumbuke wala nipate taabu. Kwahivyo, linalotakiwa ni kumtegemea Mwenyezi Mungu pamoja na kufuata sababu.

Na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amewasifu wenye kumtegemea Mwenyezi Mungu kwa sifa mbili:

1. Kwenda kutafuta riziki.
2. kutegemea sababu za kisheria.

Mwenye kukosa moja wa sifa mbili hizi hakika ameangukia patupu na amefanya shirki. Na mwenye kwenda kwa sababu zilizo halali na akamtegemea mola wake na akamshukuru mola kwa kila yanayopendeza na akasubiri hukumu ya Mwenyezi Mungu wakati anapopata msiba na machukivu amefaulu na amefadhilisha ukamilifu wote.

KHUTBA YA PILI

Enyi Waislamu hakika kutegemea ni kuusadikisha moyo juu ya kumtegemea Mwenyezi Mungu katika kuleta mambo mema na kujihami na madhara. Na kujua ya kuwa hapana yoyote anayeweza kukunufaisha na kitu chochote ila kile alicho kupangia Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Vile vile kutegemea ni ukweli na imani na utulivu na kuwa na uaminifu na Mwenyezi Mungu na matarajo yanayo shikamana na vitendo vizima ambavyo hauzimiki mwangaza wake japo yanapatikana matatizo.

Amesema Ibnul- Qayyim amrehemu yeye Mwenyezi Mungu: 'Kutegemea ni nusu ya imani na nusu ya pili ni kurudi kwa Mwenyezi Mungu'. Na haikuwa kutegemea inamzuia mwanadamu kutafuta sababu ya kisharia iliyo ya halali. Watu wema wanasema: Wakati unapo fanya bidii kutafuta riziki, na kumtegemea Mwenyezi Mungu utapata njia ya ya kila kheri. Na jambo kubwa linalo pelekea kumtegemea Mwenyezi Mungu, ni kumjua Mwenyezi Mungu kwa majina yake na sifa zake na kumpwekesha yeye Alie takasika.

Enyi Waislamu, Maajabu ni kwa yule anaye jua kuwa yeye ni muhitaji kwa Mola wake kwa kila hali zake kisha hamtegemei Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Hakika mwenye kumtegemea Mwenyezi Mungu anamtosha. Na mwenye kumtaka msaada Mwenyezi Mungu humtengenezea Dini yake na Dunia

yake. Na mwenye kujiona na nafsi yake na ukakatika moyo wake na Mola wake ameangamia na ameangukia patupu.

Na hakuna kufaulu wala kupata furaha ila kwa kumuabudu Mwenyezi Mungu na kuomba msaada kwake. Yeye ndie mwenye kuabudiwa kiukweli, na yeye anastahiki kuombwa msaada peke yake.

Mwisho

Mwenyezi Mungu atujaalie ni wenye kumtegemea yeye peke yake, na tusimshirikishe na chochote. Atujaaliye ni wenye kusikia pamoja na kufuata na Atuoneshe batili aturuzuku kuiepuka, Atupe mema ya ulimwenguni na akhera.

[7] MAPENZI YA MWENYEZI MUNGU (Subhaanahu wa Taala) NA MTUME WAKE (Swalla Llahu 'alayhi wasallam)

Lengo la Khutba:

1. Ni kubainisha kupasa mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume na kuwatanguliza kuliko kitu chochote.
2. Kuthibitisha mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake katika nyoyo.
3. Kubainisha alama ya mapenzi ya Mungu na Mtume wake.
4. Kutaja sababu zinazopelekea kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake.
5. Kutahadharisha kutanguliza mapenzi ya jamaa zako, mali yako na watoto juu ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma alie mmoja hana mshirika wake hakuzaa wala hakuzaliwa. Na rehma na amani zimshukie kipenzi chetu na mwalimu wetu Mtume Muhammad na Jamaa zake na Sahaba zake wote.

Nini mapenzi? Mapenzi ni jambo ambalo watu wana shindana katika kupenda kitu. Mapenzi huonyesha ukweli wa mwenye kupenda kitu. Na tukisema kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume ni vIpi? Ni kufuata kila walilo amrisha na kuacha kila walilo kataza, kama ilivyo kuja katika Qur'an.

قال تعالى : ﴿وَمَآ ءَاتَىٰكُمُ ٱلرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَىٰكُمۡ عَنۡهُ فَٱنتَهُواْۚ﴾ [الحشر: ٧].

Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala): {{Na anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho}} [Al-Hashri:7]. Ndugu Waislamu, mazungumzo yetu leo ni makubwa inahitajika kwa kila mmoja wetu sisi, bali kuhakikisha yanayolazimu imani, hakuna imani kwa yeyote ambae hatahakikisha hilo, nalo si lingine ni Mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wetu (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) na kuwa weka mbele kuliko yoyote. Hakika mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake ni katika imani. Hawi muumini yoyote ila atangulize mapenzi ya kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake kuliko chochote alichokimiliki mali, watoto, wazazi na watu wote. Kama alivyo toa khabari juu ya hilo Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿قُلۡ إِن كَانَ ءَابَآؤُكُمۡ وَأَبۡنَآؤُكُمۡ وَإِخۡوَٰنُكُمۡ وَأَزۡوَٰجُكُمۡ وَعَشِيرَتُكُمۡ وَأَمۡوَٰلٌ ٱقۡتَرَفۡتُمُوهَا وَتِجَٰرَةٞ تَخۡشَوۡنَ كَسَادَهَا وَمَسَٰكِنُ تَرۡضَوۡنَهَآ أَحَبَّ إِلَيۡكُم مِّنَ ٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ وَجِهَادٖ فِي سَبِيلِهِۦ فَتَرَبَّصُواْ حَتَّىٰ يَأۡتِيَ ٱللَّهُ بِأَمۡرِهِۦۗ وَٱللَّهُ لَا يَهۡدِي ٱلۡقَوۡمَ ٱلۡفَٰسِقِينَ ٢٤﴾ [التوبة : ٢٤].

{{Waambie Muhammad ikiwa wazazi wenu na watoto wenu na ndugu zenu na wake zenu na mali zenu mliyoyachuma na biashara zenu mnazoogopea kuharibika na majumba yenu mnavyoyapenda (ikiwa vitu hivi) ni vipendi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kupigania dini yake, basi ngojeni amri ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu maasi}} [Tawab :

24].

Amesema Kadhi ‘Iyadh: ‘ Inatosha Aya hii kuwa ni tanabahisho na ni dalili kubwa na ni huja juu ya ulazima wa mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na kuonyesha uwajibu wake na ni haki kumpenda Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Wakati Mwenyezi Mungu Alipotangaza yoyote atakaye kuwa mali yake, watoto wake, mke wake ni bora kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume, kisha akawaahidi adhabu kali, kwa kusema: “ Ngojeni amri ya Mwenyezi Mungu ije. Kisha Akakamilisha Aya kwa kuwaita maasi, na Mwenyezi Mungu na hawaongozi mafasiki.

وقال تعالى : ﴿إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ ٱللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ﴾ [آل عمران : ٣١]

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala): {{Waambie Ewe Muhammad, Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni mimi Mtume, hapo Mwenyezi Mungu atakupendeni na atawasamehe dhambi zenu}} [Al-Imran : 31].

وقال تعالى : ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تُقَدِّمُواْ بَيْنَ يَدَيِ ٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦۖ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَۚ إِنَّ ٱللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ۝١﴾ [الحجرات : ١].

Amesema tena Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala): {{Enyi mlioamini, Msitangulize kusema lenu mbele ya neno la Mwenyezi Mungu na Mtume wake; na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia na mwenye kujua}} [Al-Hujrat : 1].

Na kama ilivyo kuja katika Hadith. Imepokelewa na Anas Akisema: Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Hawi na imani mmoja wenu mpaka anipende zaidi mimi kuliko mzazi wake na mtoto wake na watu wote]. Amepokea Anas kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema: [Mambo matatu ukiwa nayo unapata utamu wa imani; Ni kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake zaidi kuliko wengine. Na asimpende mtu ila kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Na achukie kurudi katika ukafiri kama anavyo chukia kuingia motoni].

Na mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake yanao alama za kujulisha mapenzi yao. Wamezitaja na wakazibainisha Wanachuoni, zimetolewa katika Qur›an na sunnah na miongoni wa alama hizo:

Alama za kujulisha Mapenzi kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam)

1. Ni kufuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).
2. Ni kutekeleza Sunnah zake zote, kwa kumfuata Mtume na kufanya sunnah zake na kufuata maneno yake na vitendo vyake. Na kufuata maamrisho yake na kujiepusha na makatazo yake na kujipamba kwa adabu za Mtume katika uzito na wapesi. Amesema Qaadhi Iyadh: ‘Mwenye kupenda jambo huathirika na huathirika kwa kuliafiki. Asipokuwa hivyo, huwa si mkweli katika mapenzi yake.
3. Kuathirika na aliyoweka Mwenyezi Mungu na kujiepusha na mapenzi ya nafsi na kufuata matamanio.

KHUTBA YA PILI

Shukurani zote ni za Mwenyezi Mungu na mwisho mwema ni kwa wale wanao mcha Mwenyezi Mungu. Na hakuna anaye kiuka mipaka ya Allah isipokuwa ni dhalimu. Na kubali kwa moyo ni kutamka kwa ulimi ya kuwa hapana Mola Apasae kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu, Asiye na mshirika wake. Na kubali kwa moyo ni kutamka kwa ulimi ya kuwa Mtume Muhammad ni mja wa Mwenyezi Mungu na ni Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu msalie Mtume wetu Muhammad, kama ulivyo msalia Nabii Ibrahim wewe peke yako unastahiki kushukuriwa.

Mifano ya Mapenzi ya Mtume

1. Amri Bin Al-‘Asi radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie yeye, Amesema: ‘ Hakuwa yoyote anapendeza zaidi kwangu kuliko Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Wala hakuwa mtukufu katika macho yangu kuliko yeye. Na sikua na jaza jicho langu kwake yeye kwa sababu ya hishima yake. Na lau ningetakiwa ni msifu yeye nisingeweza, kwasababu jicho langu halitosheki naye’.
2. Aliulizwa Ali bin Abi Twalib radhi za Mwenyezi Mungu zimshukiye yeye Mlikuwa mkimpenda vipi Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam)? Akasema : [Na aapa kwa Mwenyezi Mungu, ilikua tuna mpenda zaidi kuliko mali yetu na watoto wetu na wazee wetu na mama zetu na kuliko maji baridi kwa mwenye kiu].
3. Imepokewa kwa Bilal na Hudhayfa Bin Yamani na Ammar Bin Yasir walikuwa wakisema yalipo wa hudhuriya wao kifo : ‘kesho tutakutana na Muhammad na kundi lake’. Na kama tunavyo jua kuna mambo ya kipatikana hukuepusha na mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wako nayo:

Mambo yanayo Haribu Mapenzi Ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake

1. Nikuzusha katika Dini yake
2. Nikuacha maamrisho ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Mwisho

Ndugu katika Imani, kukamilisha mapenzi ya Mtume ni kushikamana na mafundisho yake pamoja na mafundisho ya Masahaba zake. Kama alivyosema katika wasia wake juu ya kushikamana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na mafundisho yake sahihi.

Ewe Mwenyezi Mungu tujaalie ni wenye kumpenda Mtume, mapenzi ya uhakika wenye tushikamane na mafundisho yake, utujaaliye ni wenye kuingia peponi pamoja na Mtume bega kwa bega.

[8] KUAMINI KADARI

Lengo la Khutba:

1. Ni kubainisaha uhakika wa kuamini kadari na kwamba ni nguzo katika nguzo za imani.
2. Ni kubainisha ya kwamba kadari si hoja ya kufanya maasia.
3. Ni kubainisha wajibu wa mja anapofikiwa na kadari ambayo haipendi
4. Ni kubainisha matunda ya kuamini kadari
5. Kutahadharisha na makundi yaliyo potea katika kadari.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu aliyeumba kila kitu kwa kadari yake na na shahudia ya kwamba hapana Mola Apasae kuabudiwa kwa haki ila Yeye, hana mshirika katika uumbaji wake. Na nashuhudia ya kwamba Mtume Muhammad ni mja wake na ni Mtume wake. Swala na Salamu zimshukie Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) Ambaye alifikisha ujumbe na akatekeleza amana na akapigana katika njia ya Allah haki ya kupigana mpaka yakamfikia yeye mauti.

Ni lazima kwa kila Muislamu kuwa na itikadi ya kwamba kheri na shari ni kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na ujuzi wake na mapendeleo yake, lakini kufanya kheri na shari kwa mja ni kwa khiyari yake na uchungaji wa jambo na makatazo ni wajibu kwa mja haifai kumuasi yeye Mwenyezi Mungu kisha kusema Mungu amenikadiria.

Mazungumzo yetu leo ni makubwa yanatokana na nguzo moja katika nguzo za imani sita, ambayo mwenye kukanusha nguzo hiyo Mwenyezi Mungu hamkubalii yeye na haitimu imani ya mtu ila kwa kuamini kadari. Nguzo hii ni kubwa, mwenye kuwa nayo hupata utulivu na kujibu masuali mengi na mwenye kulemewa nayo huwa hapati kitu.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال جل و علا: ﴿إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَٰهُ بِقَدَرٍ ﴿٤٩﴾﴾ [القمر:٤٩]

{{Hakika kila kitu tumekiumba kwa kadari}} [Al-Qamar:49]. Na Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال سبحانه : ﴿سَبِّحِ ٱسْمَ رَبِّكَ ٱلْأَعْلَى ﴿١﴾ ٱلَّذِى خَلَقَ فَسَوَّىٰ ﴿٢﴾ وَٱلَّذِى قَدَّرَ فَهَدَىٰ ﴿٣﴾﴾ [الأعلى:١-٣]

{{Litukuze jina la Mola wako aliye mtukufu, aliyeumba akatengeneza na akakadiriya (kila jambo)} [Al-A'alaa : 1 - 3]. Na imethibiti katika sahihi ya kwamba Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alikuwa na masahaba zake, akamjia Jibril kwa sura ambazo si zake kwa sura za mtu katika watu akamuuliza kutokana na masuali ya Dini. Katika masuali hayo; "Akamuambia imani ni kuamini Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) na Malaika wake na Vitabu vyake na Mitume yake na Siku ya Mwisho na kuamini Kadari kheri yake na shari yake. Akasema Jibril: umesema kweli. Mwisho wa hadithi Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam)

Akawaambia waliokua naye: Je mnajua aliyekua akiuliza? Wakasema Mungu na Mtume wanajua zaidi, Akawaambia huyu ni Jibril amekuja kuwafundisha Dini yenu" (imepokewa na Muslim). Hadithi hii ina Tufundisha kujua nguzo sita za imani na yaliyokusanyika katika nguzo hizo nayo ni dini

Enyi Waislamu, Kadari ni ilimu ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) iliyotangulia vitu kabla ya kuandikwa, aliyo pambanuliwa kuwa yatakuwa. Hivyo basi ni kabla ya kuumbwa mbingu na ardhi kwa miaka khamsini elfu. Na uhakika wa kuamini kadari una dhamini mambo manne:

1. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ameumba kila kitu kwa kadari.
2. Kila kitu kimeandikwa kwenye (lawhul-mahfudh)
3. Ujuzi wa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) kujua kila kitu.
4. Kila kitu ni katika mapenzi ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

Kwa hivyo, kuamini kadari ni kuamini ujuzi wa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) wa kila kitu kabla ya kufanyika. Na halifanyiki jambo lolote nje ya ufalme wake. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) anayo ilimu ya kila kitu. Ni wajibu kwa kila Muislamu kuamini ya kuwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ameandika makadario ya viumbe vyote katika ubao uliohifadhiwa kabla ya kuumba mbingu na ardhi kwa miaka Khamsini elfu kama ilivyothibiti katika Hadithi iliyo sahihi, na kama alivyotoa khabari Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) katika kitabu chake:

وقوله: ﴿إِنَّ ذَٰلِكَ فِي كِتَٰبٍۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى ٱللَّهِ يَسِيرٞ ٧٠﴾ [الحج:٧٠]

{Hakika hilo liko kaitka kitabu na hakika hilo ni jepesi kwa Mwenyezi Mungu}. Kuamini kadari ni kuamini jambo lolote Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) akitaka linakua na mabalo halitaki liwe halitakua. Analolitaka liwe halina budi liwe na matakwa yote yako chini ya matakwa ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Na hamutaki jambo likawa ila atake Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), wala hamuwezi katika jambo asipotaka Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), Yeye ni mjuzi Mwenye hekima.

Jua Ewe Muislamu ya kwamba, itikadi ya Jabriya haina mahala katika Uislamu. Na katika akida ya Muislamu; Mwanadamu ni mwenye kuchaguzwa na hakua ni mwenye kwenda na maamrisho na makatazo bali anachagua ima achague njia ya kheri au njia ya shari.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

وقوله : ﴿وَهَدَيۡنَٰهُ ٱلنَّجۡدَيۡنِ ١٠﴾ [البلد:١٠]

{{Na tukambainishia zote njia mbili, ilio njema na ilio mbaya}} [Al-balad:10]. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) :

وقوله : ﴿قَدۡ أَفۡلَحَ مَن زَكَّىٰهَا ٩ وَقَدۡ خَابَ مَن دَسَّىٰهَا ١٠﴾ [الشمس:٩-١٠]

{{Hakika amefaulu mwenye kujitakasa nafsi yake na amepita patupu mwenye kuchafua nafsi yake}} [Ashamsu 9-10]. Na ilmu ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) iliyotangulia na maandishi yake hayakuwa ni yenye kuungwaungwa na

katika hilo ni kwasababu ya kusimamisha hoja juu ya waja na halipatikani jambo lolote ila Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) analijua kwa ukamilifu wa ilmu yake.

Na kama tunavyo jua baadhi ya watu wanafanya maasi kisha wanategemezea kadari. Haifai kutegemezea kadari pindi unapo fanya makosa. Si sawa mwanadamu kuchukua hoja kwa kadari juu ya kufanya maasia. Na kuna mengi sana kuhusu kuamini kadari lakini kwa sababu ya wakati tutakoma hapa. Mwenyezi Mungu atuafikie kila la kheri na atuepushe na kaila shari.

KHUTBA YA PILI

Shukurani zote ni za Mwenyezi Mungu Aliyetukuka Aliye mfalme wa mbingu na ardhi. Utakatifu ni wake Bwana wa walimwengu wote na rehma na amani zimshukie Mtume Muhammad alietumilizwa na rehma kwa viumbe. Na baada ya yote. Tutakugusia matunda ya mwenye kuamini kadari na kufuata sababu za kisheria katika kutekeleza maamrisho ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

Matunda ya kuamini kadari

Enyi waislam hakika matunda ya kuamini kadari kama ifuatvyo:-

1. Ni kumtegemea Mwenyezi Mungu Aliye Mtukufu. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ مَآ أَصَابَ مِن مُّصِيبَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ ٱللَّهِ ۗ وَمَن يُؤْمِنۢ بِٱللَّهِ يَهْدِ قَلْبَهُۥ ۚ وَٱللَّهُ بِكُلِّ شَىْءٍ عَلِيمٌ ﴿١١﴾ ﴾ [التغابن : ١١].

{{Haukufiki msiba ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na anaye muamini Mwenyezi Mungu huongoza moyo wake.Na Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa kila kitu}} [Taghabun : 11]. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال : ﴿ مَآ أَصَابَ مِن مُّصِيبَةٍ فِى ٱلْأَرْضِ وَلَا فِىٓ أَنفُسِكُمْ إِلَّا فِى كِتَٰبٍ مِّن قَبْلِ أَن نَّبْرَأَهَآ ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى ٱللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٢٢﴾ ﴾ [الحديد : ٢٢].

{{Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika kitabu kabla hatujaumba. Na hilo kwa Asema Mwenyezi Mungu ni lepesi}} [Al-Hadid : 22].

2. Ni kujua mja kila linalompata haliwi ni lenye kumkosa, madamu limekwisha andikwa lazima limfikie. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Jua lau watu wote watakusanyika ila wakuletee madhara hawatakudhuru ila kwa jambo alilo kuandikia Mwenyezi Mungu, na lau watu wote watakusanyika ili wakunufaishe hawatakunufaisha kwa jambo lolote ila kwa jambo alilokuandikia Mwenyezi Mungu].

3. Kupatikana utulivu wa moyo, kama ilivyokuja katika Aya. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال تعالى : ﴿ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَتَطْمَئِنُّ قُلُوبُهُم بِذِكْرِ ٱللَّهِ ۗ أَلَا بِذِكْرِ ٱللَّهِ تَطْمَئِنُّ ٱلْقُلُوبُ ﴿٢٨﴾ ﴾ [الرعد:٢٨].

{{Wale waliyo amini na zikatuliya nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Sikilizeni, kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu nyoyo hutulia}}.

Mwisho

Muogopeni Mwenyezi Mungu waja wa Mwenyezi Mungu. Na muamini kadari ya Mwenyezi Mungu, na mufuate mwito wa Allah (Subhaanahu wa Taala). Hio ni njia ya peke yake itakayo wafikisha kwa Allah (Subhaanahu wa Taala). Ndugu Waislamu tuombeni uongofu kotoka kwake, na tujue haifai kutoa hoja kwa kadari, mfano kufanya maasiya kisha ukategemeza kwa Mwenyezi Mungu, au kusema Mungu hakunijaaliya kufanya jambo Fulani. Haya ni katika madhambi makubwa kwa kumnasibishia Mwenyezi Mungu jambo uovu.

Ewe Mwenyezi Mungu tunakuomba katika kisimamo chetu hiki na katika kuongojea faradhi miongoni mwa faradhi zako ulizo faradhia juu yetu, utupendeze sisi imani na utengeneze katika nyoyo zetu, utuepusha nakila lenye kuharibu imani zetu. Ewe Bwana wa walimwengu wote tusamehe zambi zetu na utujaalie ni katika wenye kusikia mema pamoja na kuyafuata.

[9] MAISHA YA AKHERA

Lengo la Khutba:

1. Kuthibitisha imani ya kuamini siku ya mwisho.
2. Kuhimiza kuchukua zawadi za siku ya mwisho.
3. Kutahadharisha kufanya makao katika ulimwengu.
4. Kubainisha tafauti ya nyumba mbili; Nyumba ya Ulimwengu inayo malizika, na Nyumba ya Akhera ya kubakia milele.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Himidi zote ni za Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Na nashuhudia kwa moyo na kutamka kwa ulimi ya kwamba hapana apase kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah (Subhaanahu wa Taala) hana mshirika. Na nashuhudia kwa moyo na kutamka kwa ulimi ya kuwa Mtume Muhammad ni mja wake na ni Mtume wake. Na Sala na Salamu zimfikie Mtume Muhammad pamoja na Jamaa zake na Sahaba zake. Baada hayo, na wausia pamoja na kujiusia nafsi yangu kumuogopa Mwenyezi Mungu. Kwani kumuogopa Mwenyezi Mungu ndiyo sababu peke ya kutufanya sisi tuingie katika pepo ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

Ni ipi siku ya mwisho? Siku ya mwisho ni siku ambayo mwanadamu huacha dunia na kila kilicho chake na vitu vyote avipendavyo, na kuhamia nyumba ya mchanga, nyumba yenye giza nyumba ya wadudu iliyo na dhiki. Kukunjuliwa nyumba hiyo inategemea vitendo vyako. Kama ilivyo kuja kaburi ima inakua na bustani katika mabustani ya pepo au ni shimo katika mashimo ya motoni.

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, kila kilicho na uhai mwisho wake ni kufa. Na huu ni mwisho wa kila kiumbe sawa binadamu au mnyama, hakuna khiyari wala hakuna kuchagua upende usipende. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ ﴿٢٦﴾ وَيَبْقَىٰ وَجْهُ رَبِّكَ ذُو ٱلْجَلَٰلِ وَٱلْإِكْرَامِ ﴿٢٧﴾﴾ [الرحمن ٢٦ – ٢٧].

{{Kila kilicho juu ya ardhi na mbingu kitatoweka. Na itabaki dhati ya Mola wako Mwenye utukufu na hishima}} [Arrahmaan : 26-27]. Kwa hivyo, Mwanadamu ana nyumba mbili; nyumba ya mapito na kuondoka, na nyumba ya kubaki milele nayo ni nyumba ya akhera. Na nyumba ya akhera ndiyo nyumba ya utulivu na kubaki milele. Na ulimwengu namna utakao kua mrefu mwisho wake ni kumalizika. Kwa hivyo, mwenye akili ni yule ambae ameuangalia ulimwengu kisha akaupa mgongo, akaufanya ni mahali pa kupanda mbegu na akachukua zawadi za kumsaidia akhera. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ ٱعْلَمُوٓا۟ أَنَّمَا ٱلْحَيَوٰةُ ٱلدُّنْيَا لَعِبٌ وَلَهْوٌ وَزِينَةٌ وَتَفَاخُرٌۢ بَيْنَكُمْ وَتَكَاثُرٌ فِى ٱلْأَمْوَٰلِ وَٱلْأَوْلَـٰدِ ۖ كَمَثَلِ غَيْثٍ أَعْجَبَ ٱلْكُفَّارَ نَبَاتُهُۥ ثُمَّ يَهِيجُ فَتَرَىٰهُ مُصْفَرًّا ثُمَّ يَكُونُ حُطَـٰمًا ۖ وَفِى ٱلْـَٔاخِرَةِ عَذَابٌ شَدِيدٌ وَمَغْفِرَةٌ مِّنَ ٱللَّهِ وَرِضْوَٰنٌ ۚ وَمَا ٱلْحَيَوٰةُ ٱلدُّنْيَآ إِلَّا مَتَـٰعُ ٱلْغُرُورِ ﴿٢٠﴾ ﴾ [الحديد : ٢٠].

{{Jueni ya kwamba maisha ya kilimwengu ni mchezo na upuzi na mapambo na kujifakhirisha kwa mali na watoto. Ni kama mfano wa mvua iliyo mvutia mkulima mimea yake kisha ikabadilika rangi ya kawa rangi ya manjano kisha yakawa mabuwa. Na akhera kuna adhabu kali, na msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi zake. Na hayakuwa maisha ya kilimwengu ili na starehe ya kudanganya}} [Al- Hadid :20]. Tunaona ya kwamba maisha ya ulimwengu ni maisha ambayo yana malizika hayaendelei ni kama mfano wa mmea unanawiri kwa masiku machache baadaye yanabadilika, baada ya kuwa na nguvu na rangi mzuri ya kuvutia. Na. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال : ﴿ إِنَّمَا مَثَلُ ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا كَمَآءٍ أَنزَلْنَـٰهُ مِنَ ٱلسَّمَآءِ فَٱخْتَلَطَ بِهِۦ نَبَاتُ ٱلْأَرْضِ مِمَّا يَأْكُلُ ٱلنَّاسُ وَٱلْأَنْعَـٰمُ حَتَّىٰٓ إِذَآ أَخَذَتِ ٱلْأَرْضُ زُخْرُفَهَا وَٱزَّيَّنَتْ وَظَنَّ أَهْلُهَآ أَنَّهُمْ قَـٰدِرُونَ عَلَيْهَآ أَتَىٰهَآ أَمْرُنَا لَيْلًا أَوْ نَهَارًا فَجَعَلْنَـٰهَا حَصِيدًا كَأَن لَّمْ تَغْنَ بِٱلْأَمْسِ ۚ كَذَٰلِكَ نُفَصِّلُ ٱلْـَٔايَـٰتِ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٢٤﴾ ﴾ [يونس : ٢٤]

{{Hakika maisha ya ulimwengu ni kama mfano wa mvua inayo nyesha kutoka mawinguni ikaotesha mimea inayo toka aridhini vinavyo liwa na watu na wanyama ulipo kamilika uzuri wake, na ikapambika wakadhani wenye makulima hayo wanaweza juu yake, ikaja amri yetu mchana au usiku yakawa kama yaliyo vunwa kama kuwa hayakuwa jana. Hivi tunawafafanuliya alama zetu wakafahamu watu wanaofikiri}} [Yunus : 24]. Mwenyezi Mungu Atupigia mfano wa ulimwengu na mvua inayo nyesha ikaotesha mimea ikawa ni chakula cha watu na wanyama. vile vile Mwenyezi Mungu Akapiga mfano wa mmea hunawiri kawa muda fulani bada ya muda inabadilika.

Na katika kuonyesha udhaifu wa ulimwengu ni maneno yanayo fuatia.

Imetokana na Ali Bin Abi Twalb akisema : unaondoka ulimwengu ukipa mgongo na inaondoka akhera ikikulekea. Na kila mmoja ana watoto, kuweni watoto wa akhera, msiwe watoto wa ulimwengu. Hakika leo ni vitendo hakuna malipo na kesho ni malipo hakuna vitendo.

Hapa anatuonesha Swahaba Ali Bin Abi Twalib mfano wa dunia ni kama ulimwengu unaondoka kwa kukupa mgongo. Kwa maana ya kunaondoka ulimwengu ni kuuwacha ulimwengu, na akhera inakufuata kwa kukupa uso. Halafu tukabainishiwa vile vile, mtu ambae hamu yake itakuwa ni ulimwengu basi Mwenyezi Mungu Atajaalia umasikini mbele ya macho yake.

Imetokana na Zeydi Bin Thaabit radhi za Mwenyezi Mungu juu yake Amesema: Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Ambae ulimwengu utakuwa hamu yake Mwenyezi Mungu Atayakata mambo yake na atajalia ufukara mbele ya macho yake, na hatampatia ulimwengu ila kile alicho andikiwa. Na yule ambae akhera ndiyo lengo lake Mwenyezi Mungu atalikusanya jambo lake na atajalia utajiri katika moyo wake na atampa ulimwengu] (Ibnu Majah). Hadithi hii, Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) anatupa mafundisho bora nayo ni kutokuwa na hamu ya ulimwengu, tushughulike na akhera zaidi. Kwani ulimwengu ni kitu cha

kumalizika, lakini tushughulike na akhera zaidi ili tupate kufaulu ulimwenguni na akhera.

Enyi Waisilamu shindaneni kufanya vitendo vyema ili mupate kufaulu katika kuupata huo ulimwengu na akhera. Na watahadharisha na kuathirika na ulimwengu mtapata khasara ulimwenguni na akhera. Hakika ulimwengu ni mavuno ya akhera. Ambaye hakulima ulimwenguni hatovuna akhera.

Enyi Waislamu, hakika nyumba ya akhera ndiyo nyumba ya uhakika, ambayo mwanadamu atasema atakapo shuhudia uhakika wake: Natamani lau ningetanguliza maisha yangu ya dunia kuchuma maisha ya akhera. Kwasababu, maisha ya akhera ndiyo maisha bora mna kila kitu bora na watu hawatakufa wala hawatangonjeka, hakika hiyo ni nyumba ya amani nyumba isiyo na shida mna kila kinacho tamani nafsi.

Ubora wa Nyumba ya Akhera

Na katika ubora wa nyumba hiyo ni kama alivyo eleza Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam):

[Mahali pakuweka kibati peponi ni bora kuliko ulimwengu na vilivyoko ndani yake]. Ndiyo Amesema kweli Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Maisha ya akhera ni bora kuliko maisha ya ulimwengu, kulingamana na starehe zilizoko. Huko kuna wanawake wasio na aibu wameumbwa ni zawadi kwa wale watakao ingia peponi].

Na Akasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) katika kusifu pepo:

قال تعالى: ﴿فَأَمَّآ إِن كَانَ مِنَ ٱلْمُقَرَّبِينَ (٨٨) فَرَوْحٌ وَرَيْحَانٌ وَجَنَّتُ نَعِيمٍ (٨٩)﴾ [الواقعة: ٨٨ – ٨٩].

{{Ama wale walio kurubishwa na Mwenyezi Mungu ni raha na mabustani yaliyo jaa starehe}} [Al-Waqiah : 88 - 89]. Hivi ndivyo yatakavyo kuwa maisha ya akhera inayo takikana ni kusubiri. Na watu wa peponi watapewa watumishi wenye kuwatumikia hawataona jua wala baridi, watadhalilishwa matunda ya kila aina na vinywaji vya kila aina na vyombo watakavyo tumia ni dhahabu na fedha.

Enyi Waisilamu, shindaneni katika kufanya vitendo vya akhera ili mpate kwa hilo ulimwengu na akhera. Na watahadharisha na kuathirika na ulimwengu, mutakhasirika ulimwenguni na akhera. Hakika ulimwengu ni mapando ya akhera, ikiwa hukupanda katika ulimwengu kwa ajili ya akhera yako hakika umekhasirika akhera yako.

Enyi Waisilamu, hakika maisha ya nyumba ya akhera ndiyo maisha ya uhakika ambayo atasema mwanadamu atakapo shuhudia uhakika wake natamani ningetanguliza maisha yangu kwa ajili ya akhera. Hivyo basi ni kwamba maisha ya akhera ndiyo maisha watakaoishi watu hawatakufa. Watapata katika hiyo pepo kila wanacho kitaka macho yatafurahi hiyo ni nyumba ya amani iliyo salimika na kila upungufu na kila balaa hakuna magonjwa wala hakuna kufa wala hakuna kuzeeka.

Amesema Ibnu Rajabu katika kutafsiria hadithi ya Abdullahi Bin ‘Umar: «Kuwa katika ulimwengu ni kama mgeni:». Hadithi hii ni msingi wa kufupisha matarajio katika ulimwengu. Hakika Muisilamu hatakikani achukue ulimwengu ni mji na ni makao ya kutulia, lakini linalo takikana ni awe kama kwamba yuko safarini kwa maana ni mwenye kujiandaa na safari.

Mwenyezi Mungu atujalie ni wenye kuingiya peponi pamoja na Mitume na watu wema. Atupe mwisho mwema wakati wa kufa kwetu. Mwenyezi Mungu atujaalie ni wenye kushinda na katika kutafuta pepo. Atujaalie ni wenye kuingia katika pepo ya firdaus ya juu. Atujaalie ni katika wenye kuyasikia mema pamoja na kuyafuata. Atupe mema ya ulimwengu na akhera.

KHUTBA YA PILI

Himidi zote ni za Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma mwenye kuneemesha mwalimwengu wote kwa jumla katika dunia na swala na salamu zimshukie Mtume Muhammad na Jamaa zake na Swahaba zake wote.

Enyi watu, yalipokua maisha ya akhera ndio maisha ya uhakika ya milele. Watu wema waliopita waliyafanya maisha ya kidunia ni mashamba kwa ajili ya akhera.

Amesema ‘Umar Bin Abdulaziz katika khutuba yake: ‘hakika ulimwengu sio nyumba ya utulivu ameandika Mwenyezi Mungu juu yake kumalizika kwa wakazi. Ni wangapi wenye kuamrisha kwa kuamini kupata mazao na muda mdogo yanaharibika na ni wakaaji wangapi wamefungamana na pahali hapo na baada ya muda mdogo wanapewa mahali hapo, fanyeni vizuri safari yenu kwa usafiri mzuri na chukua zawadi hakika zawadi bora ni uchaji Mungu.

Na alikua Habib Bin Muhammad kila siku akiusia wasia wa mwenye kufikiwa na mauti kumuosha yeye na mfano wake na alikua kila akiamka akilia au akichwewa na jua, mkewe akamuuliza kuhusu kilio chake akamwambia anaogopa akichwewa na jua asiamke na akiamka asichwe na jua. Alikua Muhammad Bin akitaka kulala akiwaambia watu wake awape salamu nyinyi, Mwenyezi Mungu, huenda kifo changu nisiamke. Hivi ndivyo ilivyokua kawaida yake. Na akasema Abubakar Muzni akiweza mmoja wenu asilale ila wasia wake uko chini ya kichwa chake basi na afanye hajui huenda akalala akiwa ni watu wa dunia au akawa ni katika watu wa akhira. Na alikua Aweso akiambiwa: vipi zama juu yako? Akisema vipi zama kwa mtu akifikiwa na jioni anadhani ya kuwa hataamka na akiamka hadhaani atafikiwa na jioni, ni mwenye kubashiriwa pepo au moto.

Enyi Waislamu hakika zawadi bora ni uchaji Mungu na mjue ya kwamba Mwenyezi Mungu amewaandalia waumini wenye kwenda mbio kujenga maisha mazuri katika ulimwengu na akhira. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ مَنْ عَمِلَ صَٰلِحًا مِّن ذَكَرٍ أَوْ أُنثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهُۥ حَيَوٰةً طَيِّبَةً ۖ وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُم بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴿٩٧﴾ ﴾ [النحل : ٩٧].

{{Mwenye kufanya mema sawa akiwa mume au mke naye ana imani tutampa

maisha mazuri na tutawalipa thawabu zao kwa mema yao waliyoyafanya}} [Al-Nahal:97].

Mwisho

Mwisho, tujibidisheni kwa kutafuta maisha ya uhakika nayo sio mengine bali ya akhera. Tuishi maisha ya raha na tujiepushe na maisha ya ulimwengu tuweze kuvuna kesho akhera. Kama Alivyosema Mwenyezi Mungu: “Yoyote atakaye jiepusha nafsi yake na matamanio basi pepo ndio mashukio yake na marudio mema”. Mwenyezi Mungu Atujaalie ni wenye kukusanya zawadi njema zitufikishe kwake salama. Atupe mazuri ya ulimwenguni na ya akhera.

[10] ATHARI YA MADHAMBI NA MAASI KATIKA MAISHA YA MWANADAMU

Lengo la Khutba

1. Ni kubainisha hatari ya maasi kwa mwanadamu
2. Kutahadharisha kumuasi Mwenyezi Mungu
3. Kuthibitisha kumuogopa Mwenyezi Mungu katika nyoyo
4. Kuhimiza juu ya tawba iliyo ya kweli.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Himidi zote na shukurani zote ni za Mwenyezi Mungu alieumba Mbingu na Ardhi akaumba na binadamu kwa malengo ya kumuabudu yeye peke yake. Aliyeweka Twaa na Maasia, mwenye kumtii ataingia peponi na mwenye kumwasi ataingia motoni. Swala na Salamu zimshukie kipendi chetu Mtume Muhammad (Swalla Llahu 'alayhi wasallam), Yeye na Aali zake na Swahaba zake wote.

Waja wa Mwenyezi Mungu, na wausia pamoja na kujiusia mimi mwenyewe kumcha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Muogopeni Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), na Kufuata mwenendo wa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) na waja wema waliotangulia.

Waja wa Mwenyezi Mungu, hakika maasia yana athari mbaya kwa mtu mmoja bali kwa mujitamaa wote. Na wala hakuna shaka ya kwamba maasia wanayo fanya watu usiku na mchana athari ambayo inaangamiza mtu mmoja na jamii yote na maisha yote. Kwa hivyo, nguzo ya maisha na kutengenea kwa maisha ni katika twaa na kwa msimamo juu ya amri ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) na kufuata sharia ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) iliyo safi. Na kujiepusha na twaa na maamrisho ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ni kumfuata shetani.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ فَبِمَا نَقْضِهِم مِّيثَٰقَهُمْ لَعَنَّٰهُمْ وَجَعَلْنَا قُلُوبَهُمْ قَٰسِيَةً ۖ يُحَرِّفُونَ ٱلْكَلِمَ عَن مَّوَاضِعِهِۦ ۙ وَنَسُوا۟ حَظًّا مِّمَّا ذُكِّرُوا۟ بِهِۦ ۚ وَلَا تَزَالُ تَطَّلِعُ عَلَىٰ خَآئِنَةٍ مِّنْهُمْ إِلَّا قَلِيلًا مِّنْهُمْ ۖ فَٱعْفُ عَنْهُمْ وَٱصْفَحْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿١٣﴾ ﴾

[المائدة : ١٣].

{{Basi sababu ya kuvunja ahadi kwao tuliwalaani na tukazifanya nyoyo zao ngumu, wanabadilisha maneno ya Mwenyezi Mungu wameacha sehemu ya yale waliokumbushwa na utaendelea kupata habari zao basi wasamehe na waache hakika Mwenyezi Mungu anawapenda watu wema}} [Al-Maidah : 13].

Athari ya Maasia

- Nyoyo kuwa ngumu
- Kubadilisha maneno ya Allah (Subhaanahu wa Taala) bila ya kujali

- Raana ndani ya moyo nayo moyo kuwa mweusi. Kama alivyosema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala): (Si hivyo! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao kwa maovu waliyoyachuma). Inaonyesha ya kwamba maasia yana athari mbaya sana, nazo ni kuwa nyeusi nyoyo za watu wenye kuasi hapo huwa hazijui mema wala mabaya, haziamrishi mema wala hazikatazi mabaya.
- Kusahau kitabu cha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Na tunaposahau maagizo ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ni kuishi maisha mabaya. Kama Alivyosema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال : ﴿ وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِى فَإِنَّ لَهُۥ مَعِيشَةً ضَنكًا وَنَحْشُرُهُۥ يَوْمَ ٱلْقِيَـٰمَةِ أَعْمَىٰ ﴿١٢٤﴾ قَالَ رَبِّ لِمَ حَشَرْتَنِىٓ أَعْمَىٰ وَقَدْ كُنتُ بَصِيرًا ﴿١٢٥﴾ قَالَ كَذَٰلِكَ أَتَتْكَ ءَايَـٰتُنَا فَنَسِيتَهَا ۖ وَكَذَٰلِكَ ٱلْيَوْمَ تُنسَىٰ ﴿١٢٦﴾ وَكَذَٰلِكَ نَجْزِى مَنْ أَسْرَفَ وَلَمْ يُؤْمِنۢ بِـَٔايَـٰتِ رَبِّهِۦ ۚ وَلَعَذَابُ ٱلْـَٔاخِرَةِ أَشَدُّ وَأَبْقَىٰٓ ﴿١٢٧﴾ ﴾ [طه : ١٢٤ – ١٢٧].

{{Mwenye kupa mgongo utajo wangu hakika tutampa maisha ya dhiki na tutamfufua siku ya kiyama akiwa kipofu}}.

- Athari kubwa ya maasia na iliyo khatari ni ugomvi baina ya mja na Mola wake.
- kuwa mzito kumtii Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala)
- Kukosekana hifadhi ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala)
- Kusalitiwa na maadui na kuwa dhaifu mbele ya adui pamoja na kuondolewa utisho kutoka katika nyoyo za maadui
- Kudhihiri njaa na kuondoshwa baraka katika riziki.

KHUTBA YA PILI

Shukurani zote ni za Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) alie mwingi wa rehema ambae hakuzaa wala hakuzaliwa Mwenye nguvu na uwezo wa kila kitu anafanya analo litaka haulizwi analolifanya na nyinyi mtanaulizwa. Anafanya alitakalo kwa kusema kuwa lina kuwa.

Ewe Mwenyezi Mungu mpe rehema na amani kipenzi chako Mtume Muhammad kama ulivyo mrehemu Mtume Ibrahimu na umbariki Mtume Muhammad kama ulivyo mbariki Nabii Ibrahim kwa viumbe. Wewe ni Mwenye kushukuriwa .

Enyi waislamu, hakika anae taka amani ya ulimwenguni na akhera ni ajilazimishe na kumtii Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) na Mtume wake.

قال تعالى : ﴿وَمَن يُطِعِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٧١﴾ ﴾ [الأحزاب: ٧١].

{{Mwenye kumtwi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kwa hakika amefaulu kukubwa}}. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amefunganisha kufaulu kwa mwanadamu ni kushikamana na twaa yake, na kufeli kwa mwanadamu ni kumuasi Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Kwa hivyo, tushikamane na twaa ya Mwenyezi Mungu ili tupate kufaulu ulimwenguni na kesho siku ya kiyama. Kisha Mwenyezi Mungu Akaamrishwa kukimbilia kwake kwa kumuomba

msamaha wake.

قال تعالى : ﴿وَتُوبُوٓاْ إِلَى ٱللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهَ ٱلْمُؤْمِنُونَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ٣١﴾ [النور: ٣١].

{Rudini kwa Mwenyezi Mungu nyote ni waisilamu huenda mukafaulu}. katika Aya hii Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Anatuonesha ya kwamba tufanye haraka kurudi kwake, tupate mafanikio ya ulimwenguni na akhera.

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, jueni ya kwamba kitakacho waokowa nyinyi na adhabu ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ni kuamrisha mema na kukataza mabaya kama alivyo elezea kipenzi chetu Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Imepokewa na Hudhayfa mtoto wa Yamani (Radhiya Llahu ‘anhu), Akipokea kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Naapa kwa Mwenyezi Mungu ambae nafsi yangu iko mikononi mwake mtaamrishana mema na mtakatazana mabaya au tutawaletea nyinyi adhabu kali, kisha mtamuomba Mwenyezi Mungu, na hatawajibu]. Imetolewa na Tirrmidhi. Hadithi hii inatuonyesha ya kuwa kufaulu kwetu inatokana na kuamrisha mema na kukatazana mabaya la sivyo, basi hatuna kufaulu hata maombi yetu hayatakubaliwa.

Masharti ya Kurudi kwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala)

Kurudi kwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) kuna masharti yake. Wanavyuoni wametaja masharti hayo, nayo ni kama ifuatavyo:

1. Ni kujuta kwa uliyo ya fanya yote
2. Kuweka nia kuto rudiya madhambi uliyo yafanya katika baki ya umri wako
3. Kuacha maasiya yote.
4. Kurudi kwa Mwenyezi Mungu kwa wakati wake. yaani kabla juwa halijatoka upande wa kuchwa.

Mwisho

Enyi Waisilamu rudi kwa Mwenyezi Mungu mupate mafanikio mema ya ulimwenguni na akhera na muepukane na kumuasi Mwenyezi Mungu. Kwani hakupatikani mafanikio bora pamoja na kumuasi Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, tushikamane na twaa ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) na kufuata njia na mafundisho ya Mtume Muhammed (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

Mwenyezi Mungu atujaalie ni wenye kushikamana na twaa yake na atupe mafaniko bora ya ulimwenguni na akhera atupe mwisho mwema tukutane na Mwenyezi Mungu kwa salama atujaalie ni wenye kusikia mema pamoja na kuyafuata.

[11] UCHAJI MUNGU NA ATHARI ZAKE KATIKA MAISHA YA MUISLAMU

Lengo La Khutba

1. Kubainisha umuhimu wa uchaji Mungu na fadhila zake
2. Maana ya uchaji na uhakika wake.
3. Fadhila za wachaji Mungu na waliyoandaliwa na Mwenyezi Mungu kutokana na malipo mema.
4. Kubainisha sifa za wa chaji Mungu.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Himidi zote ni za Mwenyezi Mungu tunamshukuru Yeye na tunaomba msaada kwake na tunaomba msamaha kwake. Tunajilinda kwake na shari za nafsi zetu na vitendo vyetu vibaya. Na Rehma na Amani zimshukie Mtume wetu Muhammad na Jamaa zake na Maswahaba wake wote.

Nini uchaji mungu?. Ni kujiepusha na kila ambalo Mwenyezi Mungu halitaki na kutekeleza kila jambo ambalo Mwenyezi Mungu analipenda. Vile vile, uchaji Mungu ni kujilinda na adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa kufanya vitendo vizuri, na kuogopa kwa siri na kwa dhahiri. Na kuogopa. Ni kama alivyosema Ali Bin Abi Twalib: ‘ Ni kumuogopa Mola, na kutumia Qur’an, na kuridhika na kidogo, na kujianda kwa siku ya safari’. Imekuja ya kwamba ‘Umar Bin Khatwab radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie alimuuliza Ubayyah Bin Ka’ab: Taqwa ni nini? Akamwambia: Je umefuata njia ya miba? Akamwambia kwa nini? Hukujua? Akasema nilitembea kwa hadhari kuogopea miba kunidunga. Akasema hiyo ndiyo taqwa’.

Enyi Waislamu: na wausieni pamoja na kujiusia nafsi yangu kumuogopa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Kumuogopa Mwenyezi Mungu ni mkusanyiko wa kheri na mambo mengi yametajwa katika Qur’an tukufu. Hakuna kheri yoyote ya dunia na akhera wala ya ndani na nje ila Taqwa imeshikanishwa nazo. Na hakuna shari yoyote ya dunia na akhera wala ya ndani na nje ila Taqwa imekuwa mbali nayo. Na katika kheri za Taqwa ni kufunguliwa milango ya kheri, na kwa Taqwa hufunzwa usioyajua.

Jueni Enyi waja wa Mwenyezi Mungu; Taqwa ni wasia wa watu wa mwanzo na wa mwisho. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿وَلَقَدْ وَصَّيْنَا ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْكِتَـٰبَ مِن قَبْلِكُمْ وَإِيَّاكُمْ أَنِ ٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ۚ﴾ [النساء:١٣١].

{{Na kwa hakika tuliwausia waliopewa kitabu kabla yenu, na nyinyi pia, kwamba mumche Mwenyezi Mungu}} [Nisaa : 131]. Na Taqwa ni Mwito wa Mitume na alama ya waja wema. Kila Mtume alikuwa akiwaambia watu wake:

قال تعالى ﴿أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٠٦﴾﴾ [الشعراء:١٠٦].

{{Je hamumuogopi Mungu}} [Ashuraa :106]. Taqwa asli yake ni kinga baina

ya mja na lile analoliogopa na kujitahadhari nalo. Na Mola wetu mtukufu ndiye Anaye stahiki kuogopewa nayeye pekee ndiye Anayetukuzwa. Kama Alivyosema Ali Radhi za Mwenyezi Mungu juu yake ‹Taqwa ni kumuogopa Mwenyezi Mungu na kutumia kitabuchake (Qur'an) na kutosheka na kichache na kujiandalia siku ya safari›.

Sifa za Wachaji Mungu.

Na inatulazimu sisi Enyi Waislamu tusimame na sifa za wanaomuogopa Mwenyezi Mungu. Katika sifa za wanaomuogopa Mungu (Subhaanahu wa Taala):

1. Kuamini mambo ya siri (ghaib)
2. Kusimamisha Swala kwa wakati wake.
3. Kutoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.
4. Kuamini Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).
5. Kuwa na yakini na Siku ya Akhera. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿الٓمٓ ﴿١﴾ ذَٰلِكَ ٱلۡكِتَٰبُ لَا رَيۡبَۛ فِيهِۛ هُدٗى لِّلۡمُتَّقِينَ ﴿٢﴾ ٱلَّذِينَ يُؤۡمِنُونَ بِٱلۡغَيۡبِ وَيُقِيمُونَ ٱلصَّلَوٰةَ وَمِمَّا رَزَقۡنَٰهُمۡ يُنفِقُونَ ﴿٣﴾ وَٱلَّذِينَ
يُؤۡمِنُونَ بِمَآ أُنزِلَ إِلَيۡكَ وَمَآ أُنزِلَ مِن قَبۡلِكَ وَبِٱلۡأٓخِرَةِ هُمۡ يُوقِنُونَ ﴿٤﴾ أُوْلَٰٓئِكَ عَلَىٰ هُدٗى مِّن رَّبِّهِمۡۖ وَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ ﴿٥﴾﴾ [البقرة : ١ - ٥].

{{Hiki ni kitabu hakina shaka ndani yake ni ongofu kwa wanaomcha Mwenyezi Mungu. Ambao huyaamini yasioonekana na husimamisha swala na hutoa zile tulizowapa. Na ambao wanaamini yaliyo teremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako na wanaamini Akhera. Hao wako juu ya ongofu utokao kwa Mola wao na hao ndio waongufu}} [Al-Baqara : 1 - 5]

6. Kutekeleza ahadi na kusubiri wakati wa raha au shida. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَلَٰكِنَّ ٱلۡبِرَّ مَنۡ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِ وَٱلۡمَلَٰٓئِكَةِ وَٱلۡكِتَٰبِ وَٱلنَّبِيِّـۧنَ وَءَاتَى ٱلۡمَالَ عَلَىٰ حُبِّهِۦ
ذَوِي ٱلۡقُرۡبَىٰ وَٱلۡيَتَٰمَىٰ وَٱلۡمَسَٰكِينَ وَٱبۡنَ ٱلسَّبِيلِ وَٱلسَّآئِلِينَ وَفِي ٱلرِّقَابِ وَأَقَامَ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَى ٱلزَّكَوٰةَ وَٱلۡمُوفُونَ
بِعَهۡدِهِمۡ إِذَا عَٰهَدُواْۖ وَٱلصَّٰبِرِينَ فِي ٱلۡبَأۡسَآءِ وَٱلضَّرَّآءِ وَحِينَ ٱلۡبَأۡسِۗ أُوْلَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ صَدَقُواْۖ وَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُتَّقُونَ ﴿١٧٧﴾﴾ [البقرة
: ١٧٧].

{{Bali wema ni wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Mitume na wanawapa mali – juu ya kuwa wanayapenda- jamaa na mayatima na maskini na wasafiri na waombao na kuwakomboa watumwa na wanasimamisha swala na kutoa zaka, na watekelezao ahadi zao wanapoahidi, na wavumiliao katika shida na raha na wakati wa vita}} [AL-Baqarah : 177].

7. Kuomba msamaha kwa madhambi yao. Kama Alivyosema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَٱلَّذِينَ إِذَا فَعَلُواْ فَٰحِشَةً أَوۡ ظَلَمُوٓاْ أَنفُسَهُمۡ ذَكَرُواْ ٱللَّهَ فَٱسۡتَغۡفَرُواْ لِذُنُوبِهِمۡ وَمَن يَغۡفِرُ ٱلذُّنُوبَ
إِلَّا ٱللَّهُ وَلَمۡ يُصِرُّواْ عَلَىٰ مَا فَعَلُواْ وَهُمۡ يَعۡلَمُونَ ﴿١٣٥﴾﴾ [آل عمران : ١٣٥].

{{Na wale ambao wanapofanya uchafu au kudhulumu nafsi zao hukumbuka Mwenyezi Mungu na kuomba msamaha kwa dhambi zao}} [Al-Imraan : 135].

Fadhila Za Taqwa:-

- Taqwa hufungua moyo. Kama Alivyosema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَاتَّقُوا اللَّهَ ۖ وَيُعَلِّمُكُمُ اللَّهُ﴾ [البقرة : ٢٨٢].

{{Muogopeni Mwenyezi Mungu atawafundisha nyinyi}} [Al-Baqarah : 282]. Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن تَتَّقُوا اللَّهَ يَجْعَل لَّكُمْ فُرْقَانًا وَيُكَفِّرْ عَنكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٢٩﴾﴾ [الأنفال : ٢٩].

{{Enyi mlioamini mkimuogopa Mwenyezi Mungu atawapa ufafanuzi kufafanua baina ya haki na batili na atakufutieni makosa yenu,na kukusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kubwa kabisa}} [Anfal : 29]..

- Kupata kabuli. Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala):

- وقال تعالى: ﴿ وَيُنَجِّي اللَّهُ الَّذِينَ اتَّقَوْا بِمَفَازَتِهِمْ لَا يَمَسُّهُمُ السُّوءُ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦١﴾﴾ [الزمر:٦١].

{{Na Mwenyezi Mungu Atawaokowa wale wamchao kwa ajili ya kufaulu kwao hawataguswa na ubaya na wala hatahuzunika}} [Azumar : 61].

- Kuokoka na moto na kufaulu kwa nyumba ya furaha. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

وقال تعالى: ﴿ تِلْكَ الْجَنَّةُ الَّتِي نُورِثُ مِنْ عِبَادِنَا مَن كَانَ تَقِيًّا ﴿٦٣﴾﴾ [مريم:٦٣]

{{Hiyo nidiyo pepo tutakayowarithisha katika waja Wetu wale ambao ni wachaji Mungu}} [Maryam : 63]. Mwenyezi Mungu Atujaalie katika wale wanao muogopa Mwenyezi Mungu nakupata msamaha wake Allah. Muombeni msamaha Yeye peke yake. Hakika Yeye ndie Mwenye kusamehe waja wake wote.

KHUTBA YA PILI

Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu peke yake. Na nashuhudia hakuna anaye pasa kuabudiwa kwa haki ila Yeye, na nashuhudia ya kuwa Muhammad ni mja wake na ni Mume wake. Na Rehma na Amani zimfikie Mtume aliefikisha ujumbe na Akatekeleza Amana na Jamaa zake na Sahaba zake wote

Thawabu za Wanaomcha Mwenyezi Mungu.

- Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wale wanaomcha. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ إِنَّ اللَّهَ مَعَ الَّذِينَ اتَّقَوا وَّالَّذِينَ هُم مُّحْسِنُونَ ﴿١٢٨﴾﴾ [النحل:١٢٨]

{{Kwahakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wanaomcha na wale wafanyao wema}}.

- Kufunguliwa Baraka zitokazo mbinguni. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال : ﴿وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْقُرَىٰ آمَنُوا وَاتَّقَوْا لَفَتَحْنَا عَلَيْهِم بَرَكَاتٍ مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ وَلَٰكِن كَذَّبُوا فَأَخَذْنَاهُم بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٩٦﴾﴾ [الأعراف : ٩٦].

{{Na lau kama watu wa miji wangaliamini na kuogopa, kwa yakini tungaliwafungulia baraka za mbinguni na radhi. Lakini walikadhibisha tukawapatiliza kwa sababu ya yale waliokuwa wakiyachuma}} [Al-A’raaf : 96]. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال : ﴿وَمَن يَتَّقِ ٱللَّهَ يَجْعَل لَّهُۥ مَخْرَجًا ۝٢﴾ [الطلاق:٢].

{{Na yoyote anaemcha Mungu, Humjaalia matokeo na kumtengenezea njia ya kuokoka na balaa}}.

Ndugu Waislamu na wausia kumcha Mungu ambae ndie anaekuokoa wewe katika siri yako na anakuchunga wewe katika dhahiri yako. Mjaalie Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) moyoni mwako na kwa kila hali; mchana na usiku. Enyi watukufu Waislamu chukueni zawadi za uchaji Mung, bora ya zawadi ni kumcha mungu. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال : ﴿وَتَزَوَّدُوا۟ فَإِنَّ خَيْرَ ٱلزَّادِ ٱلتَّقْوَىٰ ۚ﴾ [البقرة: ١٩٧].

{{Chukueni zawadi hakika zawadi bora ni kumcha Mungu}} [Al-Baqarah : 196].

Enyi mlioamini mcheni Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala): na iyangalie nafsi imetanguliza nini. Na muogopeni Mungu hakika Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ni mjuzi kwa mnayoyatenda. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

وقال : ﴿وَلَا تَكُونُوا۟ كَٱلَّذِينَ نَسُوا۟ ٱللَّهَ فَأَنسَىٰهُمْ أَنفُسَهُمْ ۚ أُو۟لَـٰٓئِكَ هُمُ ٱلْفَـٰسِقُونَ ۝١٩﴾ [الحشر: ١٩].

{{Na wala msiwe kama wale waliomsahau Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu akawasahaulisha nafsi zao. Hao ndio maasi wakubwa}} [Al-Hashr : 19].

Mwisho:

Ndugu Waislamu na wausia kumcha Mungu Ambae ndie Anaye kuokoa wewe katika siri yako na anakuchunga wewe katika dhahiri yako. Mjaalie Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) moyoni mwako kwa kila hali; mchana na usiku. kumesemwa: Enyi watukufu Waislamu chukueni zawadi za uchaji Mungu na bora wa zawadi ni kumcha mungu. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Atujaalie katika wanaomcha yeye, Atuhifadhi na machafu, Atupe mwisho mwema tukiondoka duniani.

[12] KUOGOPA NA KUTARAJI

Lengo la Khutba:-

1. Ni kubainisha hakika ya kuogopa na kutaraji.
2. Umuhimu wa kuogopa na kutaraji.
3. Fadhila za kuogopa na kutaraji.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Himidi zote niza Mwenyezi Mungu Anaefaa kuogopewa na kutarajiwa, hakuna wa kuogopewa na kutarajiwa ila yeye peke yake. Na Swala na Salamu zimshukie Mtume wetu Muhammad (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) pamoja na Jama zake na Swahaba zake wote walio mfuata yeye na kuigiza mwenendo wake.

Nini kuogopa? Na nini kutaraji?

Kuogopa ni tafsiri ya kuuma moyo na kuchomeka kwa sababu ya kuingia katika jambo la karaha, la kuchukiza. Mfano; mtu akafanya kosa mbele ya mfalme kisha likamchukia moyoni kwake kwa kuogopa kufa na ikawa anajua kuwa inafaa kusamehewa na muogopaji zaidi ni yule anayeiogopa nafsi yake. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) Amesema: "Mimi namjua zaidi Mwenyezi Mungu na nina mwogopa zaidi kuliko nyinyi". Kuogopa na kutaraji ni mbawa mbili wanarukia wenye kujikuribisha na kila jambo nzuri na ni kipando wanakaa kwa hizo njia mbili.

Ewe waja wa Mwenyezi Mungu hakika vitendo vya moyo ni katika jambo kubwa na katika matukufu. Thawabu zake ni tukufu na ni kubwa na adhabu yake ni kubwa na vitendo vya viungo vinafuata vitendo vya moyo na vinajengwa juu yake. Kwa hivyo, ndiyo kukasemwa: Moyo ni mfalme wa viungo na baki ya viungo ni vijakazi wake.

Imepokewa na Anas radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie, akipokea kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) Amesema: [Hawi na msimamo mja mpaka awe na msimamo na moyo wake] (Imepokewa na Ahmad). Maana ya msimamo wa moyo ni kumpwekesha Mwenyezi Mungu, kumtukuza, kumpenda, kumuogopa, kumtaraji, kupenda twaa yake na kuchukia maasi yake.

Amepokea Muslim kutoka kwa Abu Hurayra Amesema; Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Hakika Mwenyezi Mungu haangalii sura zenu na mali yenu. Lakini ataangalia ndani ya nyoyo zenu na vitendo vyenu].

Amesema Al-Hassan kumuambia mtu: 'Ufanyie dawa moyo wako, hakika haja ya Mwenyezi Mungu kwa waja ni kutengea nyoyo zao. Na hakika vitendo vya nyoyo ambazo zinapelekea vitendo vizuri na huvutia nyumba ya akhera, na hukemea vitendo vibaya na hupa mgongo ulimwengu na huchukia nafsi mbaya illiyoaswi ni kuogopa na kutaraji.

Na makusudio ya kuogopa ni kupiga moyo na kubabaika na kuogopa adhabu ya Mwenyezi Mungu. Kwa kutofanya mambo ya haramu au kuacha jambo la wajibu au kuwa na kasoro katika mambo mazuri. Vilevile, ni katika kuogopa kuwa na hamu ya kutokubali Mwenyezi Mungu vitendo vyako, ikatetemeka nafsi na mambo ya haramu na kukimbilia mambo ya kheri. Amesema Ibnul-Qayyim Mwenyezi Mungu amrehemu : 'Kuogopa ni kwa Waislamu wote na kicho ni kwa wanavyuoni wanaojua '.

Enyi Waja wa Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu Amemuahidi mwenye kumuogopa yeye, kumzuia yeye na matamanio na kumsaidia katika Twaa na kumlipa malipo bora. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿وَلِمَنۡ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِۦ جَنَّتَانِ ﴿٤٦﴾ فَبِأَيِّ ءَالَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٤٧﴾ ذَوَاتَآ أَفۡنَانٖ ﴿٤٨﴾﴾ [الرحمن:٤٦-٤٨]

{{Yule anaemuogopa mola wake atapata mabustani mawili. Ni yapi katika neema za Mwenyezi Mungu munakanusha? mabustani yenye miti yenye matawi mengi}} [Arahmaan : 46 - 48].

Tuangalie watu wema namna walivyokua wakimuogopa Mwenyezi Mungu na kumtarajia. Ilikua kuogopa kwao ni hali ya juu wakifanya vitendo vizuri na kutaraji rehma ya Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, kuogopa iliwatengeneza na wakasafisha vitendo vyao na yakawa mazuri maregeo yao. Amesema Abu Hafsi: 'Kuogopa ni kibati cha Mwenyezi Mungu huwanyosha waliokimbia mlango wake'. Na akasema : 'kuogopa ni taa katika moyo'.

Nakumuogopa Mwenyezi Mungu inapelekea kufanya mambo ya akhera na ni ngome ya kila jambo. Inamsukuma mja kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu na malipo yake. Inapelekea kuwa na hima ya juu kufanya vitendo vizuri.

Kumuogopa Mwenyezi Mungu huzuia nafsi na shahwa zake na huikemea na upotevu na inamuhami kumpelekea kwa kila jambo zuri na kufaulu. Na kumuogopa Mwenyezi Mungu ni sehemu katika sehemu za kumpwekesha Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, inafaa iwe kuogopa kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu ni sehemu katika sehemu ya shirki kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Na ameamrisha Mwenyezi Mungu kumuogopa yeye katika Aya nyingi na akakataza kumuogopa asiyekuwa yeye. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala)::

فقال تعالى: ﴿إِنَّمَا ذَٰلِكُمُ ٱلشَّيۡطَٰنُ يُخَوِّفُ أَوۡلِيَآءَهُۥ فَلَا تَخَافُوهُمۡ وَخَافُونِ إِن كُنتُم مُّؤۡمِنِينَ ﴿١٧٥﴾﴾ [آل عمران : ١٧٥]

{{Hakika huyo shetani ambaye anawafanya uwoga marafiki wa Mwenyezi Mungu musimuogopeni yeye niogopeni mimi ikwa nyinyi ni waumini wa kweli, mukiwa Waislamu wa kweli}} [Al-Imran : 175].

Na katika Hadithi za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). Imepokewa na Anas radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie Amesema: Alikuja Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) Akasema: " Lau mgejua ninayo yajua mgalicheka kidogo na mkalia kwa wingi". Masahaba wakajifunika nyuso zao wakatoa koromo za kilio". (imepokewa na Bukhari na Muslim).

KHUTBA YA PILI

Himidi na sifa njema zisizo kifani zisizo na shaka ni za Mwenyezi Mungu Ambaye hakuzaa wala hakuzaliwa, Anayefaa kuogopwa na kutarajiwa Yeye pekee. Na Swala na Salamu zimshukie Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

Maudhui ni kubainisha uhakika wa kutaraji nao; ni kuwa na tamaa katika kupata malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na kuogopa inayopendeza ni ile inayo kuvutia kufanya vitendo vyema na ina kuzuiya kufanya ya haramu. Na pindi uoga unapopita kiasi unapelekea kukata tamaa na rehma ya Mwenyezi Mungu na hilo ni katika madhambi makubwa.

Amesema Ibnu Rajab Amrehemu yeye Mwenyezi Mungu: ‘Kiasi kinacho faa kutokana na kuogopa ni iliyo msaidia mtu kutekeleza jambo la lazima na kujiepusha na mambo ya haramu. na ikiwa juu hapo; nao ni kupelekea nafsi kufanya bidii kufanya Twaa ya ziada na kujizuia na yenye kuchukiza na kukunjua itakuwa ni yenye kupendeza. Na ikizidi juu ya hapo linarithisha magonjwa au kufa kwa moyo. Na kusababisha nafsi kukataa kukimbilia vitendo vizuri na hili si jambo lakupendeza.

Baada ya hapo tuangalie kutaraji nayo ni kuwa na tama kwa malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu juu ya kufanya vitendo vyema. Na sharti ya kutaraji ni kutanguliza vitendo vizuri na kujizuia na mambo ya haramu. Ama kuacha ya wajibu na kufuata matamanio na kutamani malipo kwa Mwenyezi Mungu na kumtarajia yeye, hapo itakua ni kutaka amani na adhabu ya Mwenyezi Mungu na wala si kutaraji. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿فَلَا يَأْمَنُ مَكْرَ ٱللَّهِ إِلَّا ٱلْقَوْمُ ٱلْخَٰسِرُونَ ﴿٩٩﴾﴾ [الأعراف:٩٩].

{{Hawaaminishi adhabu ya Mwenyezi Mungu ila watu waliopata hasara}} [Al-Araaf:99]. Enyi Waislamu: Jueni ya kwamba kutaraji bila vitendo ni kujidanganya. Na Mwenyezi Mungu amekataza Hilo. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّ وَعْدَ ٱللَّهِ حَقٌّ ۖ فَلَا تَغُرَّنَّكُمُ ٱلْحَيَوٰةُ ٱلدُّنْيَا ۖ وَلَا يَغُرَّنَّكُم بِٱللَّهِ ٱلْغَرُورُ ﴿٥﴾﴾ [فاطر : ٥]

{{Enyi watu hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli, basi yasiwadanganye maisha ya kilimwengu wala Yule mdanganyaji mkubwa (Iblis) na sikudanganyeni juu ya Mwenyezi Mungu}} [Fatir: 5].

Mwisho

Ndugu Waislamu tumuogope Mwenyezi Mungu na tutarajie kheri kutoka kwake. Natuogope adhabu yake ili tupate malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu malipo ya akhera na dunia. Mwenyezi Mungu atujalie ni wenye kumuogopa yeye na kumtarajia yeye, na atupe kheri ya dunia na akhera atujalie ni katika wenye kusikia mema na kuyafuata, na mabaya tuyaepuke.

[13] IKHLAS (KUMTAKASIA NIA MWENYEZI MUNGU)

Lengo la Khutba:-

1. Kupasa Ikhlas katika kumuabudu Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala)
2. Kubainisha ya kwamba Ikhlas ni katika nguzo ya kukubaliwa ibada
3. Kubainisha umuhimu wa Ikhlas, na hatari yake katika kumuabudu Allah (Subhaanahu wa Taala)
4. Kutahadharisha yanayo batilisha na kuharibu Ikhlas
5. Kubainisha matunda ya Ikhlas na faida zake

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Aliyetujaalia sisi ni katika umma bora, umma wa Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Na hapana apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye peke yake, hana mshirika katika ibada, hakuzaa wala hakuzaliwa. Sala na Salamu zimfikie Mtume wake Aliye tumilizwa kuwa ni rehma na amani kwa viumbe vyote. Sala na Salamu ziwafikie Jamaa zake na Sahaba zake wote.

Kabla ya kuingia katika maudhui, tunataka tueleze Nini Ikhlasi? Ikhlasi ina maana nyingi; Kuna wanao sema: Ikhlasi ni kuwa sawa ndani ya mwanaadamu na nje yake. Wengine wasema: Ikhlasi n ikufanya vitendo bila yakujionesha. Na mtu yoyote anayefanya vitendo vyoyote bila ya kujitakasa, vitendo vyake havikubaliwi. Kwasababu Ikhlasi ni nguzo muhimu ya kukubaliwa vitendo.

Enyi Waja wa Mwenyezi Mungu, hakika Ikhlas ni jambo ambalo havikubaliki vitendo vya mtu inapokosekana. Na kwa sababu ya Ikhlas huzidishiwa daraja mtu.

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu Ikhlas ni jambo kubwa, nayo ni katika nguzo za kukubaliwa vitendo. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) hakubali vitendo ila viwe ni vyema vimefanywa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Mwenye kufanya vitendo na akamshirikisha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) kwa kumkusudia mtu mwengine asiyekuwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) hakubali amali yake, hata amali hiyo iwe nyingi kiasi gani. Dalili katika hayo ni maneno yake Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Aliposema:

قال تعالى : ﴿ إِنَّآ أَنزَلْنَآ إِلَيْكَ ٱلْكِتَٰبَ بِٱلْحَقِّ فَٱعْبُدِ ٱللَّهَ مُخْلِصًا لَّهُ ٱلدِّينَ ۝٢ أَلَا لِلَّهِ ٱلدِّينُ ٱلْخَالِصُ ﴾

[الزمر : ٢ – ٣].

{{Hakika sisi tumekuteremshia Kitabu hiki kwa haki, basi muabudu Mwenyezi Mungu, kwa kumfanya Mola yeye tu Wakuitakidiwa Mola ni Mwenyezi Mungu pekeyake}} [Az-zumar 2-3].

Enyi Waislamu jueni ya kuwa vitendo vyote lazima viwe na (Ikhlas) kujitakasa. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال : ﴿ قُلْ أَمَرَ رَبِّى بِٱلْقِسْطِ ۖ وَأَقِيمُوا۟ وُجُوهَكُمْ عِندَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَٱدْعُوهُ مُخْلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ ۚ كَمَا بَدَأَكُمْ تَعُودُونَ

﴿٢٩﴾ [الأعراف : ٢٩].

{{Sema: Mola wangu ameniamrisha uadilifu, na elekezeni nyuso zenu kwake wakati wa kila sala na muabuduni yeye tu kwa utii khalisi kama alivyo kuumbeni kwanza}} [A- Araf : 29].

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال : ﴿وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلَّا لِيَعۡبُدُواْ ٱللَّهَ مُخۡلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ حُنَفَآءَ وَيُقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤۡتُواْ ٱلزَّكَوٰةَۚ وَذَٰلِكَ دِينُ ٱلۡقَيِّمَةِ ﴿٥﴾﴾ [البينة : ٥].

{{Na wala hawakuamrishwa ila kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia dini, waache dini za upotofu}} [.Bayyina: 5].

Sifa na vitendo vyote vilivyo mbali na ikhlasi havikubaliwi na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Ewe mja wa Mwenyezi Mungu ni kukusudia vitendo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu peke yake wala usimshirikishe na chochote ndio utapata malipo kutoka kwa Allah.

Zingatia Ewe Muislamu ni vipi Qur'an ina muombea mwenye kuisoma, pamoja na kuwa Qura'n ni maombezi siku ya kiyama lakini hapa haikumuombea kwa sababu ya kukosa ikhlas. Ni hivyo hivyo mali hayamuombei mwenye mali kwa kufanyia watu wema kuunga kizazi kwa sababu ya kukosa ikhlas. Na vile vile aliyepigana vita lakini kupigana kwake hakukumsaidia Allah. Kwa sababu alikuwa mbali na ikhlas. Je mimi na wewe tuko wapi? Ole wetu tukihalifu ikhlas ambayo ni nguzo kubwa ya kukubaliwa vitendo.

Mambo yanayo haribu Ikhlas:

a. Kumshirikisha Mwenyezi Mungu sawa kwa shiriki ndogo au kubwa. (1) Shirki kubwa : Ni kuthibitisha mshirika wa Mwenyezi Mungu kwa kukusudiwa mwingine. Na Shirki hii inamtoa mtu kwenye dini, na kwasababu ya shirki ataingia motoni na atabaki humo milele na shirki kubwa hubatilisha na kuharibu vitendo yote. (2) Shirki ndogo: nayo ni kila neno au kitendo kilicho kusudiwa kuonyesha watu. Shirki haimtoi mtu katika dini kama kujionesha kutaka sifa. Na hio ni mbaya kwa muumin, kwasabau inakanusha ikhlas na inabatilisha vitendo ambavyo vimepatikana kwa kujionesha sio kwa ajli ya Allah. Imepokewa na Mahmuod Ibnu Labidi ya kwamba Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) Amesema: [Ni nalo waaogopea juu yenu ni shirki ndogo wakasema ni ipi shirki ndogo?. Akasema: ni Riya. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) atawaambia wao siku ya kiyama atakapo walipa watu kwa vitendo vyao: Nendeni kwa wale mliyo kuwa mkijionesha katika dunia muangalie mtapata malipo kwao] (Imetolewa na Ahmad).

b. Kukusudia ulimwengu kupitia vitendo vya akhera. Nayo nikufanya baadhi ya vitendo vya akhera kwa ajili ya kupata starehe za ulimwengu. Mfano anae pigana kwa ajili ya kupata mali ya makafiri, au kufundisha ilimu ya sheria kwa sababu ya kupata cheti au kupata kazi. Na hayo kuna hali mbili : (1) Ikiwa kutaka ulimwengu kwa kitendo cha akhera ni chenye kukusudiwa kwa ajili ya ulimwengu, au kikawa ni sawa sawa na kusidio ya akhera. Kufanya hivyo,

inapelekea kuharibu ikhlasi, bali inapelekea kupata dhambi, na kubatilisha vitendo vyote. Imetokana na Ubayyu Ibnu Kaab akisema; Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Wape bishara umma huu kumakinika katika miji na kunusurika na kutukuza dini. Mwenye kufanya katika wao kitendo cha akhera kwa ajili ya ulimwengu, hana fungu siku ya akhera]

Ewe Mwenyezi Mungu takasa vitendo vyetu na shirki, utujaalie kuwa na ikhlasi utujaalie ni katika wenye kusikia mema pamoja na kufuata. Na utuepushe na maovu, na utukubalie vitendo vyetu vyote

KHUTUBA YAPILI

Shukurani zetu za dhati tuna mshukuru Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) alie mtumiliza Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) ni rehema kwetu sisi alie na huruma mwingi wa sikitiko. Na sala na Salamu zimshukie Mtume wa mwisho wa Mitume. Na Sahaba zake na kila alie wafuata wao kwa wema mpaka siku ya kiyama.

Maudhui yetu ni kukamilisha khutuba ya kwanza nayo ni kujitakasa. Kama tunavyo jua kila mti una mtunda yake. Je matunda ya kujitakasa ni yapi?

Matunda ya Kuvitakasa Vitendo kwa Ajili ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala)

1. Ni kuthibitisha tawhidi na Akida ya Muislamu, pamoja na kusalimika na unafiki.
2. Kuingia Peponi na kuepukana na moto. Na Muisilamu anapo ingia motoni ni kuwa hana uhakika wa imani.
3. Kukubaliwa vitendo na kuongezewa malipo.
4. Kusamehewa madhambi
5. Kuonja utamu wa ibada na daraja zake.
6. Kufaulu kupata uombezi wa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) siku ya akhera.
7. Kupata amani kwa ukamilifu, na uongofu duniani na ahkera.
8. Kutambua kufaulu na kuufungamanisha moyo na tawfiki.
9. Kuhifadhiwa na fitna na vitimbi vya shetani.
10. Kumkomboa mja na ibada ya Shetani
11. Kufurahiwa na watu na kupendwa.
12. Kuepushwa moyo wake na uchafu wa kujiona kibri na hasadi.
13. Kupata nusra ya Mwenyezi Mungu. Na alikuwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) Akijilinda kwa Mwenyezi Mungu kuingia katika shirki kwa sababu ya kukosa ikhlasi.

Anasema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Shirki imefichika kama ubawa wa chungu mweusi nitakujulisha jambo ukilifanya itakuwa kando na wewe shirki ndogo na kubwa. Sema: Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi najilinda kwako na kukushirikisha hali najuwa, naomba msamaha kwako kwa nisilo lijuwa]. Ewe Mwenyezi Mungu turuzuku ikhlasi katika maneno na vitendo.

Mwisho

Enyi Waislamu hakuna katika sisi asiye taka kufaulu. Basi tunapo taka kufaulu tushikamaneni na ikhlasi, kwani ikhlasi ni katika nguzo za kukubaliwa vitendo vyetu. Kama ilivyopokewa kutoka kwa maneno ya wanavyuoni sharuti zakukubaliwa matendo ni mbili: (1) Ikhlasi (2) Kumfuata Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam).

Tunakuomba Mwenyezi Mungu uturuzuku ikhlasi na utuepushe na kujonyesha katika vitendo vyetu. Ewe Mwenyezi Mungu tuhifadhi na shirki zote aina mbili; kubwa na ndogo.

[14] NEEMA YA PEPO NA ADHABU YA MOTO

Lengo la Khutba:

1. Kuwavuta watu kupenda pepo na kuwatahadharisha na moto
2. Kuwafunza watu kufanya mambo mema
3. Kuwatahadharisha na vitendo vibaya
4. Kubainisha sifa za watu wa pepo
5. Kubainisha sifa za watu wa motoni.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Mwenye kurehemu wema na wabaya ulimwenguni, Mwenye kurehemu wema watupu kesho akhera. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Ambaye Ameumba pepo na moto. Mwenye kufanya wema atamlipa pepo, na Mwenye kufanya mabaya atamlipa moto. Na Swala na Salamu zimuende Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam), na Maswahaba wake na Jamaa zake wote.

Nini neema? kila linalo takiwa na kupendeza huitwa neema. Lakini neema ya uhakika ni kufaulu Akhera na kuingia peponi. Pepo ni nyumba ilyo andaliwa watu wema ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), ndani kuna majumba na mashamba yaliyo na miti tofauti, na mito aina mbali mbali.

Enyi Waislamu leo tutazungumzia juu ya bidhaa iliyo ghali haipati bidhaa hiyo ila aliye rehemewa na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Wanaikimbilia biashara hiyo kila mmoja wetu sawa akiwa mume au mke, ni bidhaa iliyo na thamani kubwa inatafutwa na kila mtu. walienda mbio waliopita katika Waislamu na mpaka Waislamu wa sasa kwa lengo la kupata bidhaa hiyo. Na bidhaa hiyo si nyingine bali ni Pepo, iliyo andaliwa wale wote wenye vitendo vyema. Kama pepo ilivyo andaliwa kwa watu wema, vile vile Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) akauandaa moto kwa makafiri na wanafiki na kila anayemuasi Mwenyezi Mungu. Na pepo ni ya wanaomcha Mwenyezi Mungu, na moto ni ya wanaomuasi Mwenyezi Mungu. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ وَسَارِعُوٓاْ إِلَىٰ مَغۡفِرَةٖ مِّن رَّبِّكُمۡ وَجَنَّةٍ عَرۡضُهَا ٱلسَّمَٰوَٰتُ وَٱلۡأَرۡضُ أُعِدَّتۡ لِلۡمُتَّقِينَ ١٣٣ ﴾ [آل عمران : ١٣٣].

{{Kimbilieni msamaha wa Mwenyezi Mungu na pepo upana wake ni mbingu na ardhi wameandaliwa wamchao Mwenyezi Mungu}} [Al-Imran:133].

Na Akasema tena Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ فَإِن لَّمۡ تَفۡعَلُواْ وَلَن تَفۡعَلُواْ فَٱتَّقُواْ ٱلنَّارَ ٱلَّتِي وَقُودُهَا ٱلنَّاسُ وَٱلۡحِجَارَةُۖ أُعِدَّتۡ لِلۡكَٰفِرِينَ ٢٤ ﴾ [البقرة : ٢٤].

{{Na msipo fanya sasa na wala hamtofanya mbelini, ogopeni moto ambao kuni zake ni watu na binidamu umeandaliwa makafiri}} [Al-Baqarah : 24].

Enyi Mlioamini, Hakika pepo ni nyumba ya wachaji Mungu. Nyumba iliyo

neemeshwa imeandaliwa watu wema miongoni mwa Mitume na wa kweli na mashahidi pepo inayo pita chini yake mito, na nyumba ambazo kuta zake ni dhahabu na fedha, ndani yake mna wake wema walio wazuri, ndani yake watu wanakula wala hawaendi haja, kunao ndani ya pepo walio neemeshwa wana furaha siku zote wala hawapati huzuni wanacheka na wala hawalii watakuwa hai siku zote na wala hawatokufa. Nyuso zao zina furaha, ndani yake mna Hurul-'Ain. Bali watu wa peponi wana neema zaidi na zaidi kwenye pepo mna mambo jicho halijaona wala sikio halijasikia. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) :

قال تعالى : ﴿ فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَّآ أُخْفِيَ لَهُم مِّن قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَآءًۢ بِمَا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴿١٧﴾ ﴾ [السجدة : ١٧].

{{Haijui nafsi yaliyo fichwa katika hayo yanayo furahisha macho yao. Hayo ni malipo yale waliyo yafanya}} [Assajdah : 17].

Neema za Peponi katika Hadithi za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam)

Na Hadithi nyingi za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) zimebainisha hayo. Imepokewa na Abi Hurayra, Akipokea kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) Anasema: [Mwenyezi Mungu (alie mshindi na mwenye nguvu: Nime waandalia waja wangu neema ambao jicho halijaona na wala sikio halijasikia na wala haipiti fikra katika moyo wa mwanadamu]. Vile vile imekuja katika Hadithi za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) Ameipokea Abu Hurayra Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Hakika kundi la kwanza Litakaloingia peponi litaingia kama mwezi wa kumi na nne na wanaofuatia ni kama nyota iliyo mbinguni kwa muangaza wake hawakojoi wala hawaendi haja kubwa pafumu yao ni miski wake zao ni Hurul-'Ain umbile lao ni moja kwa sura ya baba yao Adam dhiraa sitini kwenda juu]. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Anayeingia peponi atastarehe wala hangonjeki, wala nguo yake hairaruki wala hawi mzee] (Muslim).

Vilevile katika kuonesha neema za peponi ni Hadithi ya Abu-Said Al-Khudhriyi na Abu Hurayrah wakipokea kwa Mume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) Amesema: [Atalingania mwenye kulingania Aseme: Hakika uzima ni wenu na hamtakuwa wagonjwa kabisa, na hakika ni wenu nyinyi uhai hamtokufa kabisa, na hakika ni wenu nyinyi ubarobaro hamtakuwa wazee kabisa, na hakika ni zenu nyinyi starehe hamtakuwa na shida kabisa]. [Na wataitwa waambiwe hiyo ndiyo pepo mlio ridhishwa ni malipo yale mliyoyafanya].

Baada ya kuzungumzia watu wa peponi na starehe zao. Kidogo tuizungumzie hali ya watu wa motoni na sifa zao na hali ya moto, ndani ya moto mna vinywaji vikali. Hakika moto ni nyumba ya watu wabaya, na ni nyumba ya adhabu kama Alivyosema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿لَهُمْ شَرَابٌ مِّنْ حَمِيمٍ وَعَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٧٠﴾﴾ [الأنعام : ٧٠]

{{Ni za watu wa motoni vinywaji vya maji ya moto na adhabu yenye kuumiza kwa sababu ya kukanusha kwao}} [An-Aam : 70].

Na Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) :

وقال تعالى أيضا : ﴿وَالَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ شَرَابٌ مِّنْ حَمِيمٍ وَعَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٤﴾﴾ [يونس : ٤].

{{Na wale waliyo kufuru ni vyao wao vinywaji vikali na adhabu yenye kuumiza kwa walivyokuwa wamekufuru}} [Yuunus : 4].

Kwa hivyo, Moto ni mahali pa watu wabaya wanaokosea amri ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Kama Alivyosema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿هَٰذَا ۚ وَإِنَّ لِلطَّاغِينَ لَشَرَّ مَآبٍ ﴿٥٥﴾ جَهَنَّمَ يَصْلَوْنَهَا فَبِئْسَ الْمِهَادُ ﴿٥٦﴾﴾ [ص : ٥٥ – ٥٦].

{{Hivi basi hakika wapotevu wana mashukio mabaya, wataingia moto wa jahanamu na ubaya wa marudio ni kurudia motoni}} [Saad : 55—65].

Na katika kukamilisha kuizungumzia habari ya moto na sifa zake ni Hadithi Shaqiq. Imetokana na shaqiq amepokea kwa ‘Abdillahi Akisema: Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) : [Utaletwa moto siku hiyo umefungwa vifungo sabini elfu na kila kifungo kimoja kina vutwa na Malaika sabini elfu, wanauburuza] Tunamuomba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Atuepushe na moto wa Jahannam Atujaalie ni katika wenye kusikia mema pamoja na kuyafuata.

KHUTUBA YAPILI

Shukurani zote ni za Mwenyezi Mungu Aliye umba mbingu na ardhi pasina nguzo Aliye takasika na shirki na rehma na amani zimshukie Mtume Muhammad na Sahaba zake pamoja na Jamaa zake walio wema. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَىٰ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُم بِأَنَّ لَهُمُ الْجَنَّةَ ۚ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ ۖ وَعْدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّوْرَاةِ وَالْإِنجِيلِ وَالْقُرْآنِ ۚ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِ مِنَ اللَّهِ ۚ فَاسْتَبْشِرُوا بِبَيْعِكُمُ الَّذِي بَايَعْتُم بِهِ ۚ وَذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١١١﴾﴾ [التوبة ١١١].

{{Hakika Mwenyezi Mungu Amenunuwa kwa waumini nafsi zao na mali yao kwa pepo. Wana pigana katika njia ya Mwenyezi Mungu wanauwa na wanauawa}} [Tawba : 111].

Sababu za kupata pepo :-

1. Imani kamili iliyo kita ndani ya moyo
2. Kutenda vitendo vyema.

3. Kufunga kwa ajili ya Mwenyezi Mungu
4. Kupigana Jihadi kwa ajili ya kutetea Dini ya Allah
5. Kutoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.
6. Kuwafanyia wema wazazi wawili.

Na ushahidi wa yote ni Hadith za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). Imepokewa na Jarir Bin Abdillahi: tulikuwa na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam), na ulikuwa mwezi wa kumi na nne, Mtume akawaambia: [Hakika yenu mtamuona Mola wenu kama mnavyo uona mwezi kwa wazi hamtochoka. Mkiweza msishinde na kusali kabla ya kutoka juwa na kabla ya kuchwa]. Kwa maana isiwapite nyinyi Swala ya Asubuhi na Al-asri. Na neno lake Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Enyi watu peaneni salamu na mulishe chakula na muunge kizazi na mswali usiku na watu wamelala, mtaingia peponi kwa amani].

Kama ambavyo sababu hizi hukupelekea peponi hatuna budi kukuelezea sababu za kupelekea watu motoni.

Sababu za kukupelekea motoni nazo ni:-

1. Kumkufuru Mwenyezi Mungu
2. Utesi na wazazi wawili.
3. Kusengenya.
4. Kutia fitina.

Mwisho

Enyi wa Waislamu fanyeni haraka kurudi kwa Mwenyezi Mungu, na kufanya vitendo vyema. Mwenyezi Mungu Atuepushe na moto na adhabu yake na Atuingize peponi na Atujaalie ni katika wenye kusikia mema tuyafuate na Atuoneshe batili tuweze kuiepuka.

[15] BAADA YA KUFA

Lengo la Khutba:

1. Kubainisha yatakayo tokea baada ya kufa kutokana na hali ya Siku ya Kiama
2. Kuhimiza juu ya kufanya vitendo vizuri, na kuhadharisha vitendo vibaya.
3. Kufanya haraka kutubia toba ya uhakika kabla ya kupitwa na wakati.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Baada ya kumshukuru na kumhimidi Mwenyezi Mungu na kumswalia Mtume wetu Muhammad. Nawausia pamoja na kujiusia nafsi yangu juu ya kumcha Mwenyezi Mungu na kufuata nyayo za Mtume Muhammad na mwendo wa Masahaba zake na Watu wema.

Nini kufa? Kufa ni kuepukana roho na kiwiliwili, au kufa ni kukatika matumizi ya roho kwa kiwiliwili na kukosa kiwiliwili ala yake na kumuepusha mtu na amali yake na watoto wake na mke wake. Kufa inakata utamu wa maisha ya kilimwengu na kwenda ulimwengu mwengine. Mtu ambae alikuwa akifurahia maisha ya ulimwengu amepata khasara baada ya kufa. Na yule ambae alikuwa akifurahi kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu basi atapata neema kubwa na ina kamilika kufaulu kwake.

Watu wengi hudhania ya kwamba Mtu anapo kufa na akazikwa amemaliza kila kitu na amepumzika na ulimwengu, wala halimjii yeye jambo lolote. Kudhania hivyo ni kosa kubwa bali hakika Mwanadamu baada ya kufa kwake anaingia katika maisha mapya, maisha ya barzakh na kutoka maisha ya barzakh huenda kwenye maisha ya Akhera ambayo ndiyo maisha ya mwisho na ya milele.

Njooni Waja wa Mwenyezi Mungu tuangalieni kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) zina semaje kujibu suala; Ni nini baada ya kufa ?

Hakika Qu’rani imebainisha wazi na Hadithi za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) yatakayo tokea baada ya kufa. Wakati anapokufa Mwanadamu na akazikwa, jambo la kwanza linalompata ni fitina ya kaburi.

Imepokewa katika sahihi mbili ya Bukhari na Muslim kutoka kwa Anas Bin Malik Akipokea kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Hakika mja anapo wekwa katika kaburi lake na wakaondoka watu wake, Anasikia mlio wa viatu vyao. Akasema wanamjia Malaika wawili wakamkalisha wakamuambia unasemaje juu ya mtu huyu. Akasema: Ama Muislamu atasema: Nilikuwa nikishuhudia ya kwamba ni mja wa Mwenyezi Mungu na ni Mtume wake. Akasema: Ataambiwa angalia makao yako motoni umebadilishiwa pepo. Akasema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) Atayaona makao mawili. Amesema Qatada tumeelezwa: hukunjuliwa kaburi lake dhiraa sabiini na atajaziwa kila aina ya chakula. Ama aliye kufuru na mnafiki ataulizwa unajua nini juu ya Mtu

huyu atasema sijui nilikuwa nikisema walivyokuwa wakisema watu ataambiwa hukujuwa na wala hukusoma atapigwa nyundo ya chuma moja moja, watasikia watu wote wasiokuwa viumbe aina mbili (wanadamu na majini)].

Na imepokewa na Abu Ayyub radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie Amesema : [Alitoka Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) na jua limetoka, Akasikia sauti ya Yahudi ana adhibiwa katika kaburi lake’ (Bukhari na Muslim). Kwa hivyo, Alikuwa Mtume haswali swala yeyote ila alikuwa akijilinda na adhabu ya kaburi. Na akaamrisha hivyo watu wake].

Kisha ataadhibiwa kafiri na mnafiki. Na Mu’mini atastarehe. Basi tujiulize nafsi zetu, je tumeandaa jawabu ya masuali ya kaburini. Ewe mja wa Mwenyezi Mungu, hakika hiko ni kiyama kitakuja hakina shaka. Na baada yayote atawafufuwa Mwenyezi Mungu walioko kwenye makaburi. Na dalili ni Aya tukufu:

قال تعالى : ﴿أَوَلَمْ يَرَ ٱلْإِنسَٰنُ أَنَّا خَلَقْنَٰهُ مِن نُّطْفَةٍ فَإِذَا هُوَ خَصِيمٌ مُّبِينٌ ﴿٧٧﴾ وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا وَنَسِىَ خَلْقَهُۥ ۖ قَالَ مَن يُحْىِ ٱلْعِظَٰمَ وَهِىَ رَمِيمٌ ﴿٧٨﴾ قُلْ يُحْيِيهَا ٱلَّذِىٓ أَنشَأَهَآ أَوَّلَ مَرَّةٍ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٧٩﴾﴾ [يس : ٧٧ – ٧٩].

{{Je hatambui Mwanadamu ya kwamba tumemuumba kwa tone la manii? mara amekuwa hasimu yetu aliye dhahiri. Na akatupigia sisi mfano, na akasahau kuumbwa kwake. Akasema ni nani atakayeihuisha mifupa na hali imesagika?. Sema Ewe Muhammad; Ataihuisha Yule aliyeiumba mara ya kwanza na yeye ni mjuzi wa kila namna ya kuumba}} [Yaasin : 77 – 79]. Halafu atawakusanya watu wote kwa ajili ya hisabu. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال : ﴿وَنَحْشُرُهُمْ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ عُمْيًا وَبُكْمًا وَصُمًّا ۖ مَّأْوَىٰهُمْ جَهَنَّمُ ۖ كُلَّمَا خَبَتْ زِدْنَٰهُمْ سَعِيرًا ﴿٩٧﴾﴾ [الإسراء : ٩٧].

{{Na tuwakusanya siku ya kiama hali kuwa wanakokotwa juu ya nyuso zao na hali ya kuwa ni mapofu na mabubu na viziwi. Makazo yao ni Jahannamu. Kila ukifanya kusinzia kidogo tutawazidishia mwako}} [Israai : 97].

Haya ndiyo matukio ya kuogopesha utawaona wabaya na madhalimu na wana fiki wameinamisha vichwa vyao, hawarudishi macho yao, wala hasemi siku hiyo ila aliye pewa ruhusa na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Na nyoyo siku hiyo zimefika kooni wamekasirika na madhalimu hawana muombezi wala rafiki mwenye kutiiwa. Na siku hii kiasi chake ni miaka khamsini alfu.

Waja wa Mwenyezi Mungu, wakati huo watu watasimama mbele ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), hakuna pa kufichika. Siku hiyo watu watatoka makaburini vikundi vikundi kwa ajili ya kuona vitendo vyao. Na itaanza hisabu. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Ataletwa kafiri siku ya kiama aambiwe waonaje lau ungekuwa na mjazo wa ardhi dhahabu ungalijikomboa? atasema ndiyo. Ataambiwa umeulizwa ambalo ni sahali kuliko hilo]. Na katika mapokezi mengine: [Nimekuuliza ambalo ni sahali kuliko hili na wewe uko katika mgongo wa Adam usimshirikishe Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ukakataa na ukanishirikisha na viumbe vingine].

Enyi waisilamu haya ni baadhi ya yale yatakayo tokea siku ya kiama, mbali na yale tuliyo ghafilika nayo. Na kila mmoja katika sisi atakuwa juu ya yale aliyo yafanya katika maasi. Ewe hakimu, Ewe rais, utatubiya lini? rudi kwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Utamwambia nini Mola wako. Je hukumbuki neno la Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) : [Hakuna mchungaji yoyote aliye pewa uchungaji na Mwenyezi Mungu, atakufa siku atakayo kufa na yeye ni mdanganyifu ila ataingiya motoni].

Enyi mawaziri na manaibu hamuogopi Mwenyezi Mungu kwa mliyoyabeba juu ya mabega yenu. Je mume jiandaa vipi na hali hii ya utisho miongoni mwa fitina ya kaburi na adhabu yake kukusanywa kwa ajili ya hisabu. Nini mume jianda na siku hiyo. Ewe Mwenye kufanya khiyana, Je utawacha lini khiyana zako, utasimamisha lini swala. Rudi kwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Na wewe mwizi utaaacha lini wizi wako kwa hakika huna budi lazima upitie njia hii ngumu. Na wewe barobaro umejiandaa vipi na siku hii. Je umejiandaa na siku ya kufa. Na wewe msichana wadhani ya kwamba kifo hakitakuja kwako?

Na baada ya hapo zifunguliwe vitabu. Na wenye kupewa vitabu ni aina mbili; ni mwenye kupokea kitabu kwa mkono wa kulia, na mwenye kupewa kitabu kwa mkono wa kushoto. Kisha iwekwe mizani kwa uadilifu siku ya kiama. Baada ya hayo itakuja sirat na kila mmoja atapitia njiya hiyo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) atuafikie tuweze kufaulu katika siku hii nzito.

KHUTUBA YA PILI

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) na kumsalia Mtume Muhammad na Sahaba zake. Maudhui ni kubainisha hakika nyumba za akhera ni mbili; ima ni pepo au ni moto. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَكَذَٰلِكَ أَوْحَيْنَآ إِلَيْكَ قُرْءَانًا عَرَبِيًّا لِّتُنذِرَ أُمَّ ٱلْقُرَىٰ وَمَنْ حَوْلَهَا وَتُنذِرَ يَوْمَ ٱلْجَمْعِ لَا رَيْبَ فِيهِ ۚ فَرِيقٌ فِى ٱلْجَنَّةِ وَفَرِيقٌ فِى ٱلسَّعِيرِ ﴿٧﴾﴾ [الشورى : ٧].

{{Na namna hivi tuliwafunulia Qur'an kwa lugha kiarabu ili uwaonye watu wa Makka na walio katika vijiji na uwakhofishe siku ya mkusanyiko ambayo haina shaka na kundi moja litaingia peponi na kundi moja motoni}} [Ashuraa : 7].

وقال : ﴿إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَءَايَةً لِّمَنْ خَافَ عَذَابَ ٱلْءَاخِرَةِ ۚ ذَٰلِكَ يَوْمٌ مَّجْمُوعٌ لَّهُ ٱلنَّاسُ وَذَٰلِكَ يَوْمٌ مَّشْهُودٌ ﴿١٠٣﴾﴾ [هود : ١٠٣].

{{Hakika katika hilo kuna mazingatio kwa Yule anayeogopa adhabu ya Akhera. Hiyo ndio siku itakayokusanywa watu na hiyo ni siku itakayoshuhudiwa}} [Huud :103]. Na Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال : ﴿وَسِيقَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوٓا۟ إِلَىٰ جَهَنَّمَ زُمَرًا ۖ حَتَّىٰٓ إِذَا جَآءُوهَا فُتِحَتْ أَبْوَٰبُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَآ أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنكُمْ يَتْلُونَ عَلَيْكُمْ ءَايَٰتِ رَبِّكُمْ وَيُنذِرُونَكُمْ لِقَآءَ يَوْمِكُمْ هَٰذَا ۚ قَالُوا۟ بَلَىٰ وَلَٰكِنْ حَقَّتْ كَلِمَةُ ٱلْعَذَابِ عَلَى ٱلْكَٰفِرِينَ ﴿٧١﴾ قِيلَ ٱدْخُلُوٓا۟ أَبْوَٰبَ جَهَنَّمَ خَٰلِدِينَ فِيهَا ۖ فَبِئْسَ مَثْوَى ٱلْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٧٢﴾ وَسِيقَ ٱلَّذِينَ ٱتَّقَوْا۟ رَبَّهُمْ إِلَى ٱلْجَنَّةِ زُمَرًا ۖ حَتَّىٰٓ إِذَا جَآءُوهَا وَفُتِحَتْ أَبْوَٰبُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَا سَلَٰمٌ عَلَيْكُمْ طِبْتُمْ فَٱدْخُلُوهَا خَٰلِدِينَ ﴿٧٣﴾﴾ [الزمر ٧١ – ٧٣].

{{Na waliyo kufuru watapelekwa katika moto makundi makundi, mpaka watakapoifikia itafunguliwa milango yake}} [Azzumar : 71].

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, fanyeni haraka kurudi kwa Mwenyezi Mungu na mufanye vitendo vizuri kwa kuchukua zawadi za Akhera. Muogopeni Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) waja wa Mwenyezi Mungu, na mjue ya kwamba mtukufu wenu ni amchae Mungu. Na ambae amemcheleweshа na vitendo vyake hakimsaidii kizazi chake na hakika hayo ni vitendo vyenu mlivyo vichuma. Atakaye pata kheri na amshukuru Mwenyezi Mungu, na mwenye kupata kinyume ya hayo na asilaumu isipokuwa nafsi yake.

Mwisho

Tumuogopeni Mwenyezi Mungu na tujiandae na kifo, na yatakayotokea baada ya kufa. Kwani hakuna budi kila kinacho ishi ulimwenguni kitakumbana na kifo hakuna mnyama wala binadamu, wote watakumbana na kifo na baadae kukutana na Mola wao na kulipwa kila moja kwa aliyofanya.

Mwenyezi Mungu Atujaalie ni katika wenye kujiandaa na kifo na atupe mwisho mwema katika vifo vyetu. Atujaaliye ni katika wenye kusikia mema pamoja na kuyafuata, na kujiepusha na mabaya.

(2) SEHEMU YA IBADA

Malengo Muhimu :

1. Kutia nguvu uhusiano wa mwanadamu na Mola wake
2. Kujua daraja ya Ibada na umuhimu wake katika maisha ya mwanadamu
3. Kujua hukumu za Mwenyezi Mungu katika aliyoamrishwa mtu katika Ibada.

Anuani ya Khutba katika Sehemu ya Ibada:-

1. Umuhimu wa Swala na Hukumu zake katika Sheria
2. Siku ya Ijumaa na Hukumu zake
3. Umuhimu wa Dua na Sharti zake
4. Kumi la Mwisho katika Mwezi wa Ramadhani
5. Zaka za Fitri na Sala ya Iddi
6. Kumtaja Mwenyezi Mungu
7. Kuupokea Mwezi wa Ramadhani
8. Zaka na Hukumu zake
9. Maana ya Ibada katika Uislamu
10. Kujilazimisha na Sunna ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam)
11. Kutahadhari na Uzushi katika Dini
12. Fadhila za Siku kumi za Mwezi wa Mfungo Tatu
13. Kusoma Qur’an na Adabu zake
14. Maana ya Hija
15. Utwahara wa Mgonjwa.

[1] UMUHIMU WA SWALA NA HEKIMA YA KUFANYA KUWA SHERIA

Lengo la Khutba:

1. Wajibu wa kuhifadhi swala tano na namna ya kuswali.
2. Umuhimu wa swala, na daraja lake katika Uislamu.
3. Swala ndio mafungamano kati ya mja na mola wake.
4. Athari ya swala katika moyo na viungo.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Dini ya kiislamu ambayo Mwenyezi Mungu ameitukuza na kuridhia nayo, na ameweka malipo makubwa kwa vile vinavyotamani nafsi na uislamu umejengwa na misingi na hatosalimika anaekeuka misingi hayo na adhabu iumizayo, na atakae fuata misingi hayo atapata utukufu na heshima hapa duniani na kesho akhera, na miongoni mwa misingi hayo ni swala, swala ambao ni msingi wa dini na nguzo ya pili baada ya kutamka shahada mbili, na swala ni fadhila kubwa ambapo Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Swala ni bora, na atakae weza kuzidisha basi na azidishe].

Swala ni nguzo ya pili katika uislamu. Imepokewa na Anas akisema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) : [Nimependekezwa na wanawake mafuta mazuri na nikajaaliwa kuwa swala ndio kitulizo cha macho yangu]. Na ni ibada ya kwanza aliyofaradhisha Mwenyezi Mungu, na mwanzo atakayohisabiwa mwanadamu, na ndio wasia wa mwisho ambao Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) ameusia umma wake akisema: [Swala, swala na watumwa wenu]. Na ndio mwanzo itakayopotea na ikipotea imepotea dini.

Na kuonyesha umuhimu wa swala kufaradhishwa katika mbingu ya saba, na ndio inaowekwa mafungamano kati ya mja na mola wake, na inakataza maovu. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ تَنْهَىٰ عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ﴾ [العنكبوت: ٤٥].

{{Hakika Swala humzuilia huyo mwenye kusali na mambo machafu na maovu}}

Wengi miongoni mwa watu wanaswali swala ya ghurabu (kudonoa), hawana utulivu, wala hawamtaji Mwenyezi Mungu ila kwa uchache, kugeuka katika swala kujikuna, mfanya biashara kufikiria mali yake anaposwali.

Hadithi iliopokewa kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akimuambia mtu ambae hakua na utulivu katika swala “Rejea ukaswali kwani hujaswali”

Mambo Ambayo Husababisha kuhudhurisha Moyo unapokuwa katika Swala

Mambo ambayo husababisha kuhudhurisha moyo ni kujua unacho kizungumza au unachokifanya, mfano;

- Unapotoa Takbir na kuinua mikono miwili hii inamaanisha kumtukuza Mwenyezi Mungu.
- Na ukiweka mkono wa kulia juu ya kushoto ni kujidhalilisha mbele ya Mwenyezi Mungu.
- Na ukirukuu inamaanisha kumuadhimisha Mwenyezi Mungu.
- Na ukisujudu ni kunyenyekea kwa Mwenyezi Mungu.
- Anaposema: "Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu" anaitikia Mwenyezi Mungu amenishukuru mja wangu, na anaposema " Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na neema ndogo ndogo" anasema Mwenyezi Mungu: amenisifu mja wangu, na anaposema mwenye kumiliki siku ya mwisho, anasema Mwenyezi Mungu: amenitukuza mja wangu., anaposema kwako wewe nakuabudu na kwako wewe nataka msaada, anasema Mwenyezi Mungu: haya ni kati yangu na mja wangu.
- Anaposema ametakasika Mola wangu aliekua mkubwa, na ukisema ametakasika mola wangu alie juu, Mwenyezi Mungu anasikia hata kama ni kwa sauti ya chini, anasikia kila neno unalolisema na hata kama ni kwa sauti ya chini.
- Kumuomba Mwenyezi Mungu usaidizi wa kufanya amali nzuri, imepokewa na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akisema: [Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie katika kukutaja na kukushukuru, na kufafanya uzuri ibada yako].
- Kujua kuwa unyenyekevu ni roho ya swala, Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ٱلَّذِينَ هُمۡ فِي صَلَاتِهِمۡ خَٰشِعُونَ ٢﴾ [المؤمنون:٢].

{{Ambao katika Sala zao huwa ni wanyenyekevu}}.

Wito wa kuhifadhi Swala

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿حَٰفِظُواْ عَلَى ٱلصَّلَوَٰتِ وَٱلصَّلَوٰةِ ٱلۡوُسۡطَىٰ﴾ [البقرة: ٢٣٨].

{{Angalieni sana Sala – zote kuzisali kwa jamaa- Na khasa ile Sala ya kati na kati}}.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿قَدۡ أَفۡلَحَ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ١ ٱلَّذِينَ هُمۡ فِي صَلَاتِهِمۡ خَٰشِعُونَ ٢﴾ [المؤمنون:١:٢]

{{Kwa hakika wamefaulu waumini. Ambao katika Sala zao huwa ni wanyenyekevu}}.

Na akasema tena Mwenyezi Mungu(Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ وَٱلَّذِينَ هُمۡ عَلَىٰ صَلَوَٰتِهِمۡ يُحَافِظُونَ ﴿٩﴾ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡوَٰرِثُونَ ﴿١٠﴾ ٱلَّذِينَ يَرِثُونَ ٱلۡفِرۡدَوۡسَ هُمۡ فِيهَا خَٰلِدُونَ ﴿١١﴾ ﴾ [المؤمنون: ٩:١١]

{{Na ambao Sala zao wanahifadhi. Hao ndio warithi. Ambao watarithi pepo; wakae humo milele}}.

HUTBA YA PILI

Ndugu Waislamu, Hakika Sala ni nguzo muhimu katika dini ya kiislamu. Bali Uislamu wa mtu haukamiliki bila ya Sala. Na Nguzo hii ndio ya kutafautisha baina ya Muislamu na kafiri. Amepokea Jabir hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema: “Kati ya Muislamu na kafiri ni kuwacha swala” na akasema tena Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Tofauti kati yetu na wao ni kuacha swala, atakae wacha swala ni amekufuru]. amepokea ‘Abdillah bin Shakik Ukeili, amesema maswahaba yake Mtume walikuwa hawaoni ukafiri isipokua ni kuacha swala.

Umuhimu wa kuswali Swala ya Jamaa.

Ndugu katika imani, Sala ya jamaa ni wajibu kwa wanaume. Hadithi za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) zimeweka wazi jambo hili. Amepokea Ibn Abbas hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema: [Mwenye kusikia adhana na asijibu basi hana swala isipokua mwenye udhuru]. Amepokea Abu-Hureira amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) : [nimeazimia kuamrisha pote la watu wanileteе kuni, kasha niwaendee waja wasiokuja kuswali swala kwa jamaa nichome nyuma zao].

Kuwahimiza Watoto kuswali na kuwalea kwa Mfumo huo

Watoto ni neema ya Allah (Subhaanahu wa Taala) kwa waja wake. Na neema ikiwa ni ya Allah ni lazima ichungwe kulingana na matakwa yake Allah. Mwenyezi Mungu Alipotupatia neema hii, Hakutuacha tuitumie neema hii kama tunavyotaka sisi, bali Yeye Mwenyewe Alichukua jukumu la kutufundisha namna ya kuitunza neema hii kupitia kwa mafundisho ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Na miongoni mwa mafundisho hayo, ni kuwafundisha watoto Sala wakiwa wadogo kuanzia miaka saba. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Waamrisheni watoto wenu kuswali wakiwa na miaka saba, na wapigeni wakiwa na miaka kumi].

Na Mwenyezi Mungu Akututahadharisha tusiwe ni wenye kupuuza jukumu hilo.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ قُوٓاْ أَنفُسَكُمۡ وَأَهۡلِيكُمۡ نَارٗا ﴾ [التحريم: ٦]

{{Enyi mlioamini, Jiokoeni nafsi zenu, na watu wenu, na moto ambao kuni zake ni watu na mawe}}. Na ameseme Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال تعالى : ﴿ وَأۡمُرۡ أَهۡلَكَ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱصۡطَبِرۡ عَلَيۡهَاۖ ﴾ [طه: ١٣٢]

{{Na waamrishe watu wako kusali, na uendelee mwenyewe kwa hayo}}.

Mwisho

Ndugu katika imani, Sala ni jambo kubwa lina uzito mkubwa katika Dini yetu. Muislamu akiacha kusali basi ajuwe yuko katika hali mbaya, ikiwa ataendelea na hali hiyo mpaka afikiwe na mauti basi mwisho wake ni mabaya. Kwa hivyo, tufanyeni bidii kuhifadhi Sala kwa wakati wake. Na miongoni mwa kuhifadhi sala ni kuisoma na kuifahamu kama alivyofundisha Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam), ili uweze kuitekeleza kama alivyo kuwa akitekeleza Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Tunamuomba Allah Atupe tawfiq ya kuweza kutekeleza sala kwa wakati wake. Na tuweze kusali kama alivyo kuwa akisali Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

[2] SIKU YA IJUMAA NA HUKUMU ZAKE

Lengo la Khutba:

1. Kubainisha fadhila za Mwenyezi Mungu juu ya baadhi ya viumbe vyake.
2. Kubainisha fadhila za siku ya Ijumaa, na uongofu wake kwa Umma wa Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).
3. Kubainisha hukumu za swala ya Ijumaa na adabu zake.
4. Kubainisha madhambi ya mwenye kuacha swala ya Ijumaa

KHUTBA YA KWANZA.

Utangulizi

Enyi watu, Mcheni Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Na mjuwe ya kuwa hakika Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) huumba atakavyo na huchagua atakavyo. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿وَرَبُّكَ يَخْلُقُ مَا يَشَآءُ وَيَخْتَارُ مَا كَانَ لَهُمُ ٱلْخِيَرَةُ﴾ [القصص: ٦٨]

{{Na Mola wako huumba atakavyo na huchagua atakavyo, hawana viumbe hiari}}.. Na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ndie anaye jua hekima kwa kila kitu anacho kichagua miongoni mwa viumbe vyake. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) huchagua Mitume miongoni mwa Malaika na watu. Na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ameufadhilsha Mji wa Makka kushinda sehemu nyingine. Na akauchagua Mji wa Madina kuwa ni mji aliohamia Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) na Masahaba. Kisha akauchagua Baytul Maqdis akajalia ni sehemu ya Mitume wengi ambayo Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ametuelezea habari zao katika Qur’an Tukufu. Na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) amefadhilisha baadhi ya Miezi kuliko mingine na Usiku na Mchana. Akachagua Miezi mine Mitukufu (Dhul-qa’ada, Dhul-hijja, Muharam na Rajab). Na bora wa masiku ni siku ya Ijumaa. Kwa hivyo, mtukuzeni Allah (Subhaanahu wa Taala) na kumsifu na kumsalia Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

Hukumu ya Swala ya Ijumaa

Swala ya Ijumaa ni miongoni mwa swala muhimu za faradhi. Na sharia imetia mkazo zaidi na kusisitiza kutekelezwa swala ya ijumaa kwa jamaa. Na malipo yake ni makubwa zaidi.

Fadhila za siku ya Ijumaa:

1- Kupata Thawabu na Malipo kwa kila hatua ya kwenda Msikitini sawa na Mtu aliyesimama kuswali na kufunga Mwaka mzima. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) : [Mwenye kuoga na kujisafisha, kisha akaenda Msikitini na mapema na akamkurubia Khatibu na akasikiliza kwa utulivu. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) atamlipa kwa kila hatua malipo sawa na Mtu aliyesimama kuswali na kufunga Mwaka mzima] (Imepokewa

na Ahmed).

2- Kusamehewa Madhambi yake ya wiki mzima pamoja na siku tatu za ziada. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) : [Mwenye kutawadha vizuri, kisha akaja Msikitini na akamsikiliza Khatibu na kunyamaza. Anasemehewa Madhambi yake ya wiki mzima pamoja na siku tatu]. Imepokewa na Muslim.

3- Kukubaliwa dua katika siku hii tukufu. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) : [Hakika katika Siku ya Ijumaa kuna wakati, haafikiwi Muislamu na wakati huo hali akiwa anamuomba Allah, ila Mwenyezi Mungi humkubalia Dua yake].

Adabu na Sunna za Siku ya Ijumaa:

- Kuoga na kujisafisha na kupaka manukato mazuri pamoja na kuondosha harufu mbaya mwilini.. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) : [Mwenye kuoga siku ya Ijumaa, kisha akaenda Msikitini na mapema. Mfano wake ni kama mtu aliyetowa sadaka ya Ngamia].
- Kwenda Msikitini mapema na kumkurubia khatibu. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) : [Nedeni mkasali sala ya Ijumaa, na mkae karibu na khatibu].
- Kujishughulisha kwa Kumtaja Allah, kusoma Qur'an, kuomba msamaha, kuomba dua kwa wingi na kumsalia Mtume Muhammad (Swalla Llahu 'alayhi wasallam).
- Kumsilikiza Khatibu kwa utulivu, bila ya kujishughulisha na mambo mengine. Asema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) : [Mwenye kutawadha vizuri, kisha akaja Msikitini na akamsikiliza Khatibu na kunyamaza. Anasemehewa Madhambi yake ya wiki mzima pamoja na siku tatu]. Imepokewa na Muslim.

Mambo yalio katazwa katika swala ya Ijumaa:

- Kuja Msikitini kuchelewa na kukata safu kwa kuruka watu, kwa lengo la kutaka kukaa safu ya mbele. Siku moja Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alimuona mtu akikata safu na kuruka watu; Akamuambia kaa chini kwa hakika umewaudhi watu na umefanya maasi makubwa.
- Kuwashawishi waja wa Mwenyezi Mungu, kwa kusoma Qur'an kwa sauti kubwa, au kufanya Dhikri kwa sauti ya juu. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) aliwakataza Masahaba kusoma kwa sauti ya juu, na akawambia; Asisome mmoja wenu Qura'n kwa sauti ya juu kuliko mwingine.
- Kuzungumza wakati wa Khatibu anatoa khutbah ya Ijumaa. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) : [Ukimuambia mwenzako nyamaza na Khatibu akiwa anazungumza, kwa hakika umeharibu swala ya Ijumaa].

Khatari ya kuacha kuswali swala ya Ijumaa

Mtume Muhammad amesisitiza na kutilia mkazo juu la suala la kutekeleza swala ya Ijumaa. Na akawatahadharisha Waislamu wanaoacha kutekeleza swala hii. Adhabu kubwa watakayo pata watu hao hapa duniani ni nyoyo zao kuwa ngumu na kupigwa muhuri wa kughafilika. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Hawataendelea watu kuacha swala ya Ijumaa, mpaka Mwenyezi Mungu apige muhuri nyoyo zao, kisha watakuwa niwenye kuishi katika mughafala].

Ndugu Waislamu, tujihadhari sana na kuacha swala ya Ijumaa, kwasababu adhabu yake ni nzito sana. Moyo ukiwa mgumu, basi mwanadamu anakuwa sawa na myama, hajali lolote wala chochote. Utamuona hamuogopi Mwenyezi Mungu, kwa kufanya maasi usiku na mchana.

Tunamuomba Allah (Subhaanahu wa Taala) athibitishe nyoyo zetu juu ya twaa yake, na atulinde na machafu yote.

KHUTBA YA PILI

Ndugu Waislamu, katika Mafundisho ya Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) ni kuitukuza siku hii ya Ijumaa, kwani hii ni siku tukufu ilio chaguliwa na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) na kupatiwa Umma huu wa mwisho.

Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alikhusisha baadhi ya vitendo katika siku ya Ijumaa:

- Kusoma Surat Sijdah na Surat Insaan katika swala ya Al-Fajiri. Imepokewa na Abu Hureirah – Radhi za Allah ziwe juu yake- {Alikuwa Mtume akisoma katika swala ya Al-Fajri siku ya Ijumaa (Surat Sijdah) katika rakaa ya kwanza. Na katika rakaa ya pili (Surat Insaan)} Muslim.
- Kusoma Surat Al-Kahfi. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): {Mwenye kusoma Surat Al-Kahfi siku ya Ijumaa, Mwenyezi Mungu anampa mwangaza baina ya Ijumaa mpaka Ijumaa nyingine}. Al-Bayhaqi na Haakim.
- Kuzidisha kwa wingi kumsalia Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Amesema Ibnu-Qayyim: “Mtume wa Mwenyezi Mungu ni Bwana wa viumbe vyote, na siku ya Ijumaa ni bwana wa siku zote. Kumswalia Mtume siku hii ina malipo mengi kushinda siku nyingine”.
- Kuzidisha kumuomba Allah (Subhaanahu wa Taala) katika siku hii. Kwasababu kuna wakati wa kukubaliwa dua ya Muislamu. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) : [Hakika katika Siku ya Ijumaa kuna wakati, haafikiwi Muislamu na wakati huo hali akiwa anamuomba Allah, ila Mwenyezi Mungu humkubalia Dua yake].

Mwisho

Ndugu katika Imani, kama tulivyo sikia umuhimu wa siku ya Ijumaa, na namna sheria ilivyo tilia mkazo siku hii. Na vilivile malipo na thawaabu nyingi kwa Yule atakae tekeleza ibada kwa masharti yake na nguzo zake. Ni jukumu letu kufanya bidii kwa kufanya ibada mbali mabali kama alivyo tufundisha Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam), ili tuweze kupata malipo na thawabu nyingi kutoka kwa Allah (Subhaanahu wa Taala). Enyi Waislamu, Tushindaneni kufuata Sunna na Mafundisho ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) katika siku hii kuu.

Mwenyezi Mungu atujaalie miongoni mwa waja wake wema na atupe uwezo wa kufuata Sunna za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Tunamuomba Allah atukubalie ibada zetu na atupe mwisho mwema tukiondoka duniani.

[3] UMUHIMU WA DUA NA MASHARTI YAKE

Lengo la Khutba:

1. Kubainisha ukweli wa kuomba Dua na haja ya viumbe katika kuomba Dua
2. Kubainisha Hukmu zake, Sharti zake na Adabu zake
3. Kutahadhrisha ufahamu mbaya wa kuomba Dua.

KHUTBA YA KWANZA.

Utangulizi

Enyi Waja wa Allah, viumbe vyote vinamuhitaji Mola wao katika kupata manufaa yao au kuzuia madhara yasiwafikie, kwa lengo la maisha yao hapa Duniani na kesho siku ya mwisho. Na kila mja anapojikurubisha kwa Allah, basi Allah anamuinua daraja na kumfanya mtukufu mbele ya viumbe vyake. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Anawapa mitihani viumbe vyake kwa misukosuko mbalimbali ili waweze kurudi kwa Mola wao na kuomba msaada kwake katika kupambana na mitihani hiyo.

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) anapenda kuombwa msaada na waja wake na anapenda waja wake kurudi kwake pindi wanapofikwa na shida na misukosuko ya ulimwengu. Kufanya hivyo, ndio msingi wa ibada. Na makusudio makubwa ya sharia kuamrisha na kunyeyekea kwa Allah na kutaraji pamoja na kumtegemea Yeye peke yake kwa mambo yote. Imepokewa na Abi Dharri katika hadithi Qudsi: [Amesema Mwenyezi Mungu: Enyi waja wangu nyinyi wote ni wapotevu ila Yule niliye muongoza, basi niombeni uongofu wangu].

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amepanga kila kitu, na Akaweka sababu ya kila kitu. Ameweka sababu za kufaulu Mwanadamu na sababu za kufeli Mwanadamu. Ameumba sababu zote na athari ya hizo sababu, na hakuna kitu kitakua bila ya kutaka Allah (Subhaanahu wa Taala). Na lau angetaka Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) kuumba kitu bila sababu angefanya. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالى: ﴿فَعَّالٌ لِّمَا يُرِيدُ ﴿١٦﴾﴾ [البروج: ١٦]

{{Mwingi wa kutenda Alipendalo}}. Na Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال تعالى: ﴿أَلَا لَهُ ٱلْخَلْقُ وَٱلْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ ٱللَّهُ رَبُّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٥٤﴾﴾ [الأعراف: ٥٤]

{{Fahamuni, kuumba ni kwake tu Mwenyezi Mungu, na amri zote ni zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote}}.

Hukumu ya Kuamrishwa kuomba Dua

Dua ni ibada bora mbele ya Mwenyezi Mungu. Ameamrisha kwa lengo la la kupata kheri na kuzuia shari. Dua ni sababu kubwa ya kupata kheri na Baraka za Mwenyezi Mungu. Na ni sababu kubwa ya kukinga madhara na shari zote. Na hakika Mwenyezi Mungu ameamrisha waja wake kumuomba Dua katika Aya

nyingi. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالى: ﴿وَقَالَ رَبُّكُمُ ٱدۡعُونِيٓ أَسۡتَجِبۡ لَكُمۡۚ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَسۡتَكۡبِرُونَ عَنۡ عِبَادَتِي سَيَدۡخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ٦٠﴾ [غافر: ٦٠]

{{Na Mola wenu anasema; Niombeni nitakujibuni. Kwa hakika wale wajivunao kufanya ibada yangu, bila shaka wataingia Jahannam wadhalilike}}.

Uhakika wa kuomba Dua

- Kutukuza mapenzi ya mja kwa mola wake katika kuomba msaada wakutatuliwa matatizo ya ulimwenguni na matatizo ya Akhera.
- Kuhakikisha ukweli wa kumuabudu Mola wa walimwengu wote. Kufanya hivyo, ni kufungamanisha moyo wa mja na Mola wake na kumtakasia ibada zote Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), na kutotegemea mtu au kitu kingine pamoja na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).
- Kuwa na yakini kamili yakuwa Allah ndie Mweza wa kila kitu, hakuna kitu kinacho mshinda, Mjuzi wa kila kitu, hakuna kitu kilicho fichika mbele ya Allah (Subhaanahu wa Taala).
- Kudhihirisha mja unyonge wake mbele ya Muumba wake. Na kumhitaji Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) katika mambo yake yote. Na huu ndio Ukweli wa kumuabudu Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

Fadhila za Dua:

1. Dua ni Ibada. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Dua ni Ibada] (Abu-Daaud). Dua ni ubongo wa ibada, kwa sababu Dua imekusanya ibada zote; kunyenyekea, kutegemea, kutarajia, kuogopa, kuomba msaada, n.k.
2. Dua ni Ibada tukufu kushinda ibada zote. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Hakuna ibada tukufu mbele ya Allah kushinda Dua] (Atirmidhi).
3. Kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu kwa ulinzi wake na hifadhi yake. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) katika hadithi Qudsi: [Mola Asema: Mimi niko pamoja na mja wangu pindi anapoelekea kwangu kwa maombi yake] (Bukhari na Muslim).

Nyakati za kukubaliwa Dua.

a. Wakati wa kusujudu. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Mja anakuwa karibu zaidi na Mola wake wakati akiwa katika sijida. Kwa hivyo, ombeni Dua wa wingi] (Muslim).
b. Baada ya Adhana. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Dua hairejeshwi baina ya Adhana na Iqaama] (At-Tirmidhi).

c. Thuluthi ya mwisho wa usiku. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Mola wetu anateremka kila usiku mpaka katika uwingu wa dunia wakati wa thuluthu ya mwisho wa usiku. Na Anasema: Nani mwenye kuniomba nimkubalie dua yake] (Bukhari).

d. Siku ya Ijumaa. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Katika siku ya Ijumaa kuna Saa, atakaye omba Dua. Mwenyezi Mungu hukubali dua yake] (Bukhari na Muslim).

KHUTBA YA PILI

Ndugu Waislamu, kukubaliwa Dua na Allah ni lazima yapatikane masharti yake. Na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) Ametufundisha masharti ya kimsingi ya kukubaliwa Dua.

Masharti ya kukubaliwa Dua:-

1. Kumtakasia Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) na kumpwekesha Allah katika kuomba Dua. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala) :

   قال الله تعالى: ﴿فَٱدۡعُواْ ٱللَّهَ مُخۡلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ وَلَوۡ كَرِهَ ٱلۡكَٰفِرُونَ ١٤﴾ [غافر:١٤]

   {{Basi muombeni Mwenyezi Mungu yeye tu ibada yenu, ingawa makafiri watachukia}}.

2. Kujiepusha na haramu; Kula, kunywa na kuvaa mavazi ya haramu. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Enyi watu, hakika Mwenyezi Mungu ni mzuri, na hakubali ila kitu kizuri. Kisha akataja mfano wa mtu anayesafiri safari ndefu hali akiwa amechoka, nywele zake zimejaa vumbi, anainuwa mikono yake kuelekeza mbinguni huku akisema: Ewe Mola wangu, Ewe Mola wangu, na hali kwamba chakula chake ni cha haramu, Kinywaji chake cha haramu na mavazi yake ni ya haramu. Vipi Allah ataikubali Dua yake].

3. Kuhudhurisha moyo wakati wa kuomba Dua, na kuwa na matarajio ya ukweli kwa Allah (Subhaanahu wa Taala). Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Muombeni Allah hali mkiwa na hakika ya kukubaliwa Dua yenu. Na mjuwe Allah hakubali Dua ya moyo ulioghafilika] (At-Tirmidhy).

Adabu za Kuomba Dua:

a. Usafi wa mwili. Kwa sababu Dua ni Ibada, na Ibada haikubaliki bila ya usafi

b. Kuinua mikono juu wakati wa kuomba Dua. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) : “Hakika Mola wenu ana sifa ya haya na ukarimu. Anaona haya kumrejesha mja wake anapoinua mikono yake kumuomba Dua”

c. Kuomba Dua zilizothibiti katika Qur’an na Sunna ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

Mwisho

Ndugu Waislamu, kwa hakika Dua ni silaha ya Muislamu. Muislamu anaweza kutumia silaha hii kwa ajili ya kupambana na adui yoyote, sawa katika binadamu au katika majini. Vilevile, Dua ni kinga ya Muislamu, ikiwa Muislamu ataitumia kinga hio kujilinda nayo. Ndugu Waislamu, tusisahau masharti ya kukubaliwa dua zetu, ni muhimu sana. Bila ya kukamilisha masharti hayo dau zetu hazikubaliwi na Allah (Subhaanahu wa Taala). Tunamuomba Allah Atukubalie dua zetu, na Atuepushe na haramu. Atupe uwezo wakutafuta halali. Na Atujaalie mwisho mwema, tukutane naye hali Akiwa radhi na sisi.

[4] KUMI LA MWISHO LA MWEZI MTUKUFU WA RAMADHANI

Lengo la Khutba:

1. 1. Kuwakumbusha watu fadhila za siku kumi za mwisho wa Mwezi wa Ramadhani
2. Kubainisha mafundisho ya Mtume katika siku hizi
3. Kuimarisha mafungamano ya mja na Mola wake, na kufanya bidii na kujikurubisha kwa Allah

KHUTBA YA KWANZA.

Utangulizi

Enyi Waislamu, Siku za mwezi mtukufu wa Ramadhani zinaendelea kuisha. Na hivi karibuni tutaanza kumi la mwisho. Je ndugu yangu Muislamu umejiuliza suala moja; Je nimefaidika kiasi gani na siku zilizopita? Kuwa mkweli na nafsi yako na ujifanyie hisabu ya vitendo vyako kabla hujafika siku ya kufanyiwa hisabu. Ndugu Muislamu, bado wakati upo, na fursa ya kufanya mambo ya kheri bado inaendelea.

Je umejiandaa kiasi gani na umejipangia mikakati gani katika kumi la mwisho? Kwa hakika ni siku muhimu katika umri wa mwanadamu, ndani yake kuna usiku mtukufu. Mwenye kuafikiwa usiku huo basi amepata kheri ya dunia na akhera. Na mwenye kukosa usiku huo basi amekosa kheri ya dunia na akhera. Ni khasara ilioje mtu kuishi duniani miaka mingi kisha aondoke duniani patupu bila ya kupata kheri ya dunia wala kheri ya akhera. Ndugu Muislamu tafakari na uzingatie, hujui kama utafika mwakani ili uweze kufunga Mwezi wa Ramadhani.

Watu wema walikuwa wakimuomba Allah mwaka mzima awaafikie kuweza kuzifikia siku hizi za kheri. Na wakififikiwa na siku hizi huwa na furaha nyingi, kwa kupata bahati ya kuishi mpaka kuweza kufunga Mwezi wa Ramadhani. Ndugu Muislamu Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) Ametufundisha mambo mengi na ibada nyingi ambazo Muislamu anaweza kuzifanya kwa ajili ya kujikurubisha kwa Allah (Subhaanahu wa Taala). Katika Ibada hizo ni kama ifuatavyo:-

Sunna za Kumi la Mwisho:

1. Kufanya bidii kusali swala ya usiku, na kuwahimiza watu wako nyumbani kuamka kusali pamoja na wewe. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Mwenye kusimama usiku katika mwezi wa Ramadhani kwa Ikhlasi na kutarajia malipo kwa Allah. Atasamehewa madhambi yake yaliyo tangulia]. Imepokewa katika Sunna ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) likifikia kumi la mwisho alikuwa akigura matandiko yake na akijitahidi kusimama usiku na kuamsha wake zake na familia yake.
2. Kuzidisha juhudi kutafuta Usiku wa cheo. Usiku huu ni bora kuliko miezi elfu moja, bali ni bora kushinda vitu vyote vilivyomo duniani. Mwenye kuafikiwa

kupata usiku huu basi kwahakika amefaulu na kupata kheri ya dunia na akhera. Katiak mafundisho ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) kuhusu usiku mtukufu; Ni sunna kuzidisha kusoma Qur’an kwa wingi, kumsifu Allah na kumtukuza na kumsalia Mtume, kutoa sadaka. Na ni sunna kuomba dua kwa wingi. Bibi Aisha Alimuuliza Mtume: Je niombe dua gani katika usiku huu? Akamuambia sema: [Ewe Mola hakika yako wewe ni mwenye kusamehe waja wako na unapenda kusamehe. Nakuomba unisamehe].

3. Kufanya ibada ya I’tikaaf, nayo ni kutia nia kukaa Msikitini kwa lengo la kujitenga na watu na kukusudia kufanya ibada katika siku hizi. Alikuwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) linapofika kumi la mwisho, akijitenga na familia yake na kuingia Msikitini kwa ajili ya kumuabudu Allah (Subhaanahu wa Taala). Na masahaba waliendelea kutekeleza Sunna hii bada ya Mtume kuondoka duniani.
4. Kusoma Qur’an kwa wingi na ikiwezekana kuhitimisha Msahafu katika siku hizi tukufu. Imepokewa kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam), ilikuwa ni kawaida yake katika siku za mwezi wa Ramadhani kukutana na Malaika Jibril kwa ajili ya kusoma Qur’an, na Jibril anamsikiliza.

Ndugu Muislamu, Siku kumi katika kumi la mwisho ni chaguo lake Allah (Subhaanahu wa Taala) kwa Umma huu. Na kwa rehma zake Ametujalia sisi kuweza kuzifikia siku hizi tukufu. Kwa hivyo, ni jukumu letu kufanya bidii kumuiga Mtume katika ibada zake zote, na kushindana katika kutafuta Usiku wa cheo (Laylatul Qadri). Tunamuomba Allah Atuajalie miongoni mwa waliochaguliwa kupata Lailatul Qadri (Usiku wa cheo).

KHUTBA YA PILI

Ndugu Waislamu, Allah (Subhaanahu wa Taala) Anatupenda sana, na kwa mapenzi yake juu yetu ni kutujalia malipo na thawabu nyingi kwa kutekeleza ibada ndogo. Mfano Usiku wa cheo ni usiku moja, lakini thawabu zake ni nyingi kushinda thawabu za ibada katika miezi elfu moja. Angalia ndugu Muislamu, utukufu na rehma ya Allah juu yetu, lakini wengi katika Waislamu hawana khabari na neema kama hizi. Wakati unapita, siku zinapita na sisi tumeghafilika, mpaka tutakapofikwa na mauti ndio tutazinduka na hali ya kuwa muda umekwisha.

Ndugu Katika Imani, Khasara kubwa zaidi watapata wale waliofanya bidii kufunga mwezi huu na kufanya ibada mwanzo wa Mwezi wa Ramadhani, lakini wanapofikiwa na kumi la mwisho wanarudi nyuma, na kuacha kutekelza ibada na sunna za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Ni khasara ilioje kwa mtu aliyefanya bidii kuchuma mazuri, kisha akashindwa kuendelea na msimamo huo, na kushindwa kukamilisha kumi la mwisho.

Hukumu ya Ibada ya I’tikaafu:

Ibada ya I’tikafu ni Suuna. Muislamu anaweza kutekeleza ibada hiyo wakati wowote akitaka. Lakini ni Sunna iliotiliwa mkazo katika Kumi la mwisho la Mwezi wa Ramadhani. Amesema Mama ‘Aisha: Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) hakuacha katika maisha yake kufanya I’tikaaf katika kumi la mwisho la Mwezi wa Ramadhani.

Mambo yanayo lazimu kufanywa katika I’tikaaf:-

a. Kutia Nia kukaa Msikitini kwa ajili ya kufanya Ibada kwa lengo la kujikurubisha kwa Allah.

b. Kuchagua sehemu ya kukaa katika Msikiti, na kujilazimisha kubaki hapo ila kwa dharura ya kisheria, unaruhusiwa kutoka.

c. Kujiepusha na tendo la ndoa au njia za kupelekea kufanya tendo hilo.

d. Kufanya bidii kuzidisha kusoma Qur’an kwa wingi, na kuomba dua kwa wingi. Kufanya hivyo, itakusaidia kupata usiku wa cheo na kusamehewa madhambi yako.

e. Kujitahidi kufuata mafundisho ya Mtume katika kutekeleza lbada hii.

Mwisho

Ndugu katika imani, Umri wetu ni mfupi sana, na mwanadamu hajui kama ataweza kupata nafasi tena kufikia mwezi wa Ramadhani mwakani. Jambo la msingi ni kufanya bidii na juhudi kubwa kutafuta Usiku wa cheo ili tupate kheri ya usiku huu. Yule atakaye bahatika kupata usiku huu, kwa hakika huyo amefaulu hapa duniani na kesho akhera.

Tunamuomba Allah kwa majina yake matukufu na sifa zake njema atujaalie miongoni mwa waja wake Aliowachagua kupata kheri ya Usiku wa cheo. Tunamuomba Allah Atuwafikie kwa kufanya Ibada mbalimbali ambazo anazozipenda na anazoridhia. Tunamuomba Allah Atuwezeshe kufuata mafundisho ya Mtume Muhammad katika maisha yetu na atuingize pamoja na yeye katika Jannatul Firdaws.

[5] ZAKA ZA FITRI NA SWALA YA IDDI

Lengo la Khutba:

1. Kubainisha Mambo Yanayompasa Muislamu Kufanya Baada ya Ramadhani.
2. Kubainisha Namna ya Jamii Kusaidiana Katika Uislamu.
3. Kubainisha Hukumu za Swala ya Iddi na Hikma Zake.

KHUTBA YA KWANZA.

Utangulizi

Allah (Subhaanahu wa Taala) ametuwekea zaka za fitri kwa hikma ya kuwa ni kafara pindi unapopatikana upungufu katika saumu ya Muislamu katika Mwezi wa Ramadhani. Na hakika hakuna binadamu mkamilifu. Na Iddi imewekwa ili kuonyesha kuwa Uislamu unazingatia maumbile ya binadamu, kwani binadamu huwa anapenda kuwa na wakati wa kusherehekea, kwa ajili hiyo ndio ikawekwa Iddi mbili ili ziwe sherehe zetu zimefungamana na ibada.

Kubainisha Maana ya Zaka za Fitri na Hukumu yake.

Ni nini maana ya zaka za fitri? Kabla ya kueleza hilo, napenda kuwakumbusha waja wa Allah ya kuwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni mgeni mtukufu aliyetujilia na amekurubia kuondoka. Inatakikana tupatilize siku zillizobakia kwa wingi wa toba na amali njema huenda Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) akaziunganisha amali zetu.

Enyi waja wa Allah, Mwisho wa mwezi huu mtukufu kuna amali tukufu zenye kuzidisha imani na kukamilisha ibada zetu, na amali hizo ni; zakatul fitri, takbira na swala ya iddi. Na zakatul fitri ni sadaka ambayo inapasa kwa sababu ya kufungua mwezi wa Ramadhani, na hakika imetambuliwa zaka za fitri kuwa ni swadaka ya wajibu, kwa hivyo ndio tunaiita zaka za fitri sadakatul fitri. Sasa twende katika kueleza hukumu ya zaka za fitri na dalili ya kuwekwa ibada hii.

Wanazuoni wa fiq'hi wameafikiana ya kuwa zaka za fitri inampasa kila Muislamu mwenye uwezo. Na dalili ni hadithi iliyopokewa na Ibnu 'Umar asema katika mafhuum ya maneno yake: Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amefaradhishia watu inapomalizika Ramadhani kutoa pishi ya tende au pishi ya ngano, na hilo ni kwa kila Muislamu, awe muungwana au mtumwa, mume au mke". Amepokea hadithi hii Bukhari.

Hikma ya kuwekwa Zaka za Fitri

Ni muhimu Muislamu kujua hikma ya zaka za fitri, hikma ya zaka za fitri ni mambo mawili :-

Hikma ya kwanza ni kuwa inatwahirisha saumu ya mwenye kufunga. Kwani binadamu kwa ubinadamu wake anaweza kufanya mambo ya kumpunguzia thawabu, basi hapo ndipo inapokuja nafasi ya zaka za fitri. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) ametuambia katika hadithi iliyopokewa na Ibnu 'Abbas katika maana ya hadithi: [Zaka za fitri ni twahara ya mwenye kufunga kutokana na upuuzi na maneno machafu, na ni chakula kuwalisha maskini]. Imepokewa na Abu Daud.

Hikma ya pili ni kuwakunjua mafukara na maskini na kuingiza furaha nyoyoni mwao.

Masharti ya kutoa Zaka za Fitri

Zaka za Fitri ina masharti yake :-

Sharti ya kwanza ni kuwa Muislamu. Kafiri si wajibu juu yake hata kama ana jamaa zake Waislamu ambao ni wajibu kwake kuwalisha.

Sharti ya pili ni mtu kuwa huru sio mtumwa. Kwani Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) ametuambia: " Watekelezeeni (zakatul fitri) kila huru na watumwa mnaowalisha".

Sharti ya tatu ni uwezo wa kimali nao ni kuwa na chakula cha siku moja na usiku wake.

Sharti ya nne ni kuingia wakati, nao ni kutwa jua la siku ya Iddi mwisho wa mwezi wa Ramadhani. Na mwisho wa wakati wake ni baada ya kuswali iddi. Na mtu inafaa aanze kujitolea yeye mwenyewe kwanza kisha amtolee anayepaswa kumlisha. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). ametuambia katika maana ya Hadithi : [Jianzie na nafsi yako kisha unayemlisha].

Kiwango cha Zaka za Fitri na Vipimo vya Kisasa

Kiwango cha zaka za fitri ni pishi moja ya ngano au wimbi au zabibu au chakula chochote ambacho ni chenye kutumika sana mjini. Na pishi kwa kipimo cha kisasa ni kilo 2 na gramu 176. Ibnu 'Umar amepokea hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam), ya kuwa alifaradhisha zaka za fitri pishi ya mtama.

Na wanazuoni wa fiq'hi wa madhehebu ya hanafi waliporuhusu kutoa thamani ya kiwango cha chakula kinachopasa kutolewa ni kwa kuzingatia makusudio yaliyokusudiwa katika kufaradhishwa zaka, nayo ni kuwakidhia maskini haja zao katika siku hiyo ya iddi. Mu'adh amekubali kutoa thamani kwani ndio maslahi ya mafukara. Na Ibnu Taimiyya amesema hakuna ubaya wa kutoa thamani.

KHUTBA YA PILI

Iddi katika Uislamu yakusanya Maana na Manufaa Makubwa

Kuna akida ambayo ni safi na ni kupiga takbira na dua na kunyenyekea bila ya kumshirikisha Mola, kama alivyosema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), katika maana ya Aya:

قال تعالى: ﴿وَأَنَّ ٱلْمَسَٰجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا۟ مَعَ ٱللَّهِ أَحَدًا ﴿١٨﴾﴾ [الجن:١٨].

{{Hakika Misikiti yote ni ya Mwenyezi Mungu, basi msiabudu yoyote asiyekuwa Mwenyezi Mungu}}.

Na iddi, kuna kubainisha hukmu za Mwenyezi Mungu kwa kudhihirisha Alama za kiislamu. Na katika khutba kuna kufafanua hukumu za kiislamu kama vile kusubiri, kusamehe na kuondosha chuki katika nyoyo, na kuonyesha uhusiano mwema baina ya Waislamu. Kama alivyosema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) katika maana ya hadithi: [Watoshelezeni katika siku hii ya leo (yaani mafukara)]. Imepokewa na Daaraqutni kutoka kwa Ibnu Umar.

Baadhi ya Hukmu zinazopatikana katika Siku ya Iddi

kumtukuza Mola wakati tukikamilisha hesabu. Allah (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

فقال تعالى: ﴿وَلِتُكْمِلُوا۟ ٱلْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُوا۟ ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَىٰكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٨٥﴾﴾ [البقرة:١٨٥].

{{Ili mkamilishe hisabu na mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa kuwaongoza, na hakika mutamshukuru}}. Na kumeamrishwa hata wanawali na wenye hedhi watoke wapate kushirikiana na Waumuni wenzao katika dua. Kama hadithi iliyopokewa na Ummu 'Atia.

Ni sunna kula tende au chochote katika iddil fitri kabla ya kwenda kuswali. Kama alivyoeleza Anas sunna hii ya Mtume. Na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ametuambia, katika maana ya Aya:

قال الله عز وجل: ﴿لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِى رَسُولِ ٱللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا۟ ٱللَّهَ وَٱلْيَوْمَ ٱلْءَاخِرَ وَذَكَرَ ٱللَّهَ كَثِيرًا ﴿٢١﴾﴾ [الأحزاب:٢١].

{{Hakika mna kielezo chema kwa Mtume wa Allah kwa mwenye kumtarajia Allah na siku ya mwisho na akamtaja Mwenyezi Mungu sana}}.

Mwisho

Tumeona kama ilivyo tangulia ya kuwa idd ni kuchunga maumbile ya binadamu, na zaka ni kuchunga maslahi ya mafukara na wasiojiweza na pia kurekebisha makosa madogo madogo ambayo huenda binadamu asiye weza kuepukana nayo.

[6] KUMTAJA MWENYEZI MUNGU (Subhaanahu wa Taala)

Lengo la Khutba:

1. Kubainisha Ukubwa wa Kumtaja Mwenyezi Mungu Katika Maisha ya Muislamu
2. Kuhimiza Kumtaja Mwenyezi Mungu Katika Hali Zote
3. Kuimarisha Uhusiano wa Mja na Mola Wake
4. Kutahadharisha na Wenye Kughafilika na Kusahau

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Baada ya kumshukuru Allah (Subhaanahu wa Taala) na kumtakia rehema bwana Mtume Muhammad (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). Mola Mtakatifu kwa rehema yake Amewawekea waja wake kila njia za kusahilisha kufikia kwake. Mojawapo wa njia hizo ni dhikri. Dini ya Kislamu imewahimiza wafuasi wake kufanya bidii Kumtaja Mweyezi Mungu kwa kila hali. Kwasababu, Dhikri ni mawasiliano baina ya mja na Mola wake popote alipo, na ni silaha ya Muislamu wakati wakupambana na madui. Na vile vile, Dhikri ni kinga ya kumuhifadhi Muislamu na madui wote.

Kumtaja Allah ni Uhai wa Moyo na kusafishika kwake

Nawausia enyi watu na kujiusia nafsi yangu kumcha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) kwa siri na kwa dhahiri, mumche, mumuabudu, mumsujudie na mfanye kheri kwa hakika mutafaulu.

Hakika nyoyo za binadamu wote ni kama viumbe vingine vyote, hayawani, mimea, na visivyokuwa na roho. Hayawani anahitajia vyakula, mimea inahitajia maji na hata chuma. Sheikhul-Islam Ibnu Taimiyya - Mungu Amrehemu- amesema: 'Utajo wa Mungu kwa moyo ni kama maji kwa samaki, je huaje akitolewa majini?'

Uhusiano wa mja na mola wake ukiwa ni wakati wa asubuhi au jioni tu, basi mja huyo anafanya ghushi, lakini uhisiano wa maana wa mtu kuwa nao na mola wake ni kushikamana na maamrisho na kuepukana na makatazo. Na dhikri iwe ni yenye kumsaidia katika shida zake.

Fadhila za Dhikri na namna Uislamu ulivyohimiza

Dini ya kiislamu imehimiza sana uhusiano wa Muislamu na mola wake uwe imara. Na kuna dalili nyingi kuhusu jambo hilo. Miongoni mwa dalili hizo ni pale Allah (Subhaanahu wa Taala) aliposema katika mana ya Aya:

قال عز وجل : ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ ذِكۡرٗا كَثِيرٗا ﴿٤١﴾ وَسَبِّحُوهُ بُكۡرَةٗ وَأَصِيلًا ﴿٤٢﴾﴾ [الأحزاب:٤١-٤٢].

{{Enyi mlioamini mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi na mumtakase asubuhi na jioni}}.

Na pale Aliposema katika maana ya Aya:

وقال سبحانه : ﴿وَالذَّاكِرِينَ اللَّهَ كَثِيرًا وَالذَّاكِرَاتِ أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ مَغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴿٣٥﴾﴾ [الأحزاب:٣٥].

{{Wenye kumtaja Mwenyezi Mungu sana waume na wake, Allah Amewaandalia msamaha na malipo makubwa}}.

Na aliposema katika maana ya Aya:

وقال تعالى : ﴿فَاذْكُرُونِي أَذْكُرْكُمْ﴾ [البقرة:١٥٢]. وقال سبحانه: ﴿وَلَذِكْرُ اللَّهِ أَكْبَرُ﴾ [العنكبوت:٤٥].

{{Nikumbukeni (kwa twaa na ibada), Nami nitawakumbuka (kwa rehema na msamaha)}. Na amesema katika maana ya Aya: {{Na hakika utajo wa Mwenyezi Mungu (dhikri Allah) ni mkubwa}}.

Na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alitilia mkazo jambo hili kwa kusema katika maana ya hadithi: [Maneno mawili yanayopendekeza kwa Mola, mepesi katika ulimi, mazito katika mizani, nayo ni subhanaallah wabihamdihi, subhanaallahul adhiim]. Imepokewa na Bukhari na Muslim.

Na akasema katika maana ya hadithi: [Je siwapi habari za amali zenu bora na iliyotakasika zaidi mbele ya mfalme wenu na yenye kuinua daraja zenu zaidi na ni bora kwenu nyinyi kuliko dhahabu na pesa na bora kwenu nyinyi kuliko kupambana na adui na mkakata shingo na wakawakata. Wakasema: ni lipi hilo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: ni kumtaja Allah (Subhaanahu wa Taala)]. Imepokewa na Ahmad.

Na akasema katika maana ya hadithi: [Mwenye kusema, subhanallah wabihamdihi, hupandiwa mti wa mtende katika pepo]. Imepokewa na Haakim na Tirmidhi aliyehukumu kuwa ni hadithi hasan swahiih.

Enyi waja wa Allah kumtaja Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) huondosha shida na balaa na hupamba ndimi za mwenye kumtaja kama yanavyo pambwa macho ya mwenye kuangalia kwa nuru. Ndimi zilizoghafilika ni kama jicho pofu, sikio ziwi na mkono ulio poza. Hasan al Basri amesema: 'tafuteni utamu katika mambo matatu, katika swala na dhikri na kusoma Qur'an mkipata ni sawa na msipo pata basi mjue mlango umefungwa.

Kazi ya Dhikri katika kumsaidia Muumini kupambana na Shetani

Pindi binadamu anapofanya madhambi huwa si jambo jengine ila ni kughafilika na kumtaja Allah (Subhaanahu wa Taala), ndio mola akatuambia katika maana ya Aya:

قال تعالى : ﴿وَمَن يَعْشُ عَن ذِكْرِ الرَّحْمَٰنِ نُقَيِّضْ لَهُ شَيْطَانًا فَهُوَ لَهُ قَرِينٌ ﴿٣٦﴾﴾ [الزخرف:٣٦].

{{Mwenye kughafilika na utajo wa Mwenyezi Mungu, tunamfanya shetani kuwa ndiye rafiki yake}}.

Na Allah (Subhaanahu wa Taala) Amesema katika maana ya Aya:

وقال تعالى : ﴿وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنكًا وَنَحْشُرُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَعْمَىٰ ﴿١٢٤﴾﴾ [طه:١٢٤].

{{Na Mwenye kuupa mgongo utajo wangu hakika mtu huyo atakuwa na maisha ya dhiki na tutamfufua hali ya kuwa ni kipofu}}. Na Ibnul-Qayyim - Allah Amrehemu - alipokea kutoka kwa baadhi ya watu wema waliotangulia walisema:

‘Ukimakinika utajo wa Allah katika moyo wa binadamu, shetwani akimkaribia husongwa kama anavyosongwa binadamu na sheitwani, basi sheitani huyo aliosongwa hukusanyikiwa na mashetani wenzake na huku wakimuuliza “Ana nini huyu? Huwa kunajibiwa: “ Hakika shetani huyu amerogwa na binadamu.

Enyi Waislamu hii ndio kazi ya dhikri ambayo ni silaha ya Muumin ya kuweza kupambana na adui mkubwa wa binadamu.

Dhikri ni usaidizi wa Muumini katika mambo yake yote

Enyi waja wa Allah, kitu kitukufu zaidi chenye kupita akilini mwa binadamu, na twahara zaidi chenye kutamkwa na midomo ni dhikri ya Allah (Subhaanahu wa Taala). Na binaadamu wote kwa jumla huwa wana babaiko na maisha yao na hakuna jambo lolote lenye kuondosha babaiko ila dhikri ya Allah, ndio akatuamuru Allah na ndiye Mkweli kama ilivyo katika Aya ambayo mana yake:

قال تعالى : ﴿ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَتَطۡمَئِنُّ قُلُوبُهُم بِذِكۡرِ ٱللَّهِۗ أَلَا بِذِكۡرِ ٱللَّهِ تَطۡمَئِنُّ ٱلۡقُلُوبُ ٢٨﴾ [الرعد: ٢٨].

{{Walioamini nyoyo zao hutulia kwa utajo wa Mwenyezi Mungu, jueni na mtanabahi kwamba utajo wa Mwenyezi Mungu hutuliza nyoyo}}. licha ya hivyo hata kazi zako za kawaida, nyumbani, ofisini, sokoni huwa nyepesi kwa kumtaja Allah kwa dalili ya maneno ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alipolalamikiwa na Sahaba Ali na binti yake Fatma kuhusu uzito anaopata Fatma katika kazi za nyumbani na huku wakitaraji bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) atawawekea mfanyakazi nyumbani, lakini Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akawaambia katika maana ya hadithi yake: [Je, niwaonyesheni jambo bora zaidi kuliko kuweka mfanyakazi nyumbani? mkifika kitandani mseme: “Subhanallah mara thalathini na tatu, Alhamdulillah mara thalathini na tatu, na Allahu Akbar mara thalathini na tatu hizi ni mia kwenye ulimi lakini ni elfu katika mizani].

Shida inayo wapata Watu Wenye kughafilika na Dhikri

Enyi waja wa Allah, tukipeleleza vyema tutaona kuwa wengi wanaokumbwa na shida za kila aina, magonjwa, kurogwa, na kukosa raha ya maisha utapata yote haya husababishwa na kuwa mbali na dhikri. Na huenda tukajiuliza kwanini watu hawaingii katika hifadhi ya Mola wao naye atawakinga kutokana na balaa zote? Kwani binadamu hajui kuwa kulala, kuamka na harakati zote ziko na dhikri, hata kulala na mkewe? ndio siri ya Allah (Subhaanahu wa Taala) kusema katika maana ya Aya:

قال تعالى : ﴿وَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ كَثِيرٗا لَّعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ ١٠﴾ [الجمعة: ١٠].

{{Na mumtaje Mwenyezi Mungu sana hakika mtafaulu}}.

Na binadamu yoyote namna atakavyo kuwa na nguvu, basi yeye ni dhaifu mbele ya mitihani ya Mungu, na huwa anamuhitaji Mola wake kama anavyohitaji maji na hewa.

HUTBA YA PILI

Kumtaja Mwenyezi Mungu kwa Mazingatio

Ukiwa unamtaja Mungu kwa ulimi na unazingatia kwa moyo basi ni dalili ya mtu kuwa na imani. Neno la Allahu Akbar ndio kichwa cha kila nguzo na ndio jambo la kwanza alilokalifishwa nalo Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) pale alipoamrishwa kuwaonya watu, Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلْمُدَّثِّرُ ۝١ قُمْ فَأَنذِرْ ۝٢ وَرَبَّكَ فَكَبِّرْ ۝٣﴾ [المدّثر: ١-٣].

{{Ewe uliyejifunika, inuka ukhofishe, na Mola wako umtukuze}]. Hakika (Allahu Akbar) ndio neno la kwanza ambalo huhuisha ardhi iliyokufa, na sauti yake inashinda ngurumo ya bahari iliyochafuka. Kwa hivyo, inapasa sauti yake isikilizwe katika sikio la kila mwenye kufikiria kufanya maovu.

Enyi Waislamu, mkumbukeni Allah kwa wingi hakika mtafaulu mkifanya hivyo. Ewe mwenye kughafilika, ukiona moyo wako hauko ujue kwamba kwa kumtaja Allah utahuika na utaimarika.

Kwa nini kuwe kumtaja Mungu ni Ibada yenye manufaa zaidi kuliko Ibada nyingine pamoja na wepesi wake iwapo Moyo wako haukughafilika?

Utakapouliza swali hilo, jawabu ni kwamba ibada zote zimewekewa kiwango na wakati isipokuwa dhikri haina kiwango wala wakati. Allah (Subhaanahu wa Taala) anatuambia:

قال تعالى : ﴿وَٱذْكُر رَّبَّكَ فِى نَفْسِكَ تَضَرُّعًا وَخِيفَةً وَدُونَ ٱلْجَهْرِ مِنَ ٱلْقَوْلِ بِٱلْغُدُوِّ وَٱلْءَاصَالِ وَلَا تَكُن مِّنَ ٱلْغَٰفِلِينَ ۝٢٠٥﴾ [الأعراف: ٢٠٥].

{{Mkumbuke mola katika nafsi yako kwa kunyenyekea pasina kudhihirisha neno, asubuhi na jioni, wala usiwe miongoni mwa wenye kughafilika}}.

Na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) ametujulisha silaha ya kujikinga na moto nayo ni [Al-Baaqiyaatu Swalihaatu (Visalio vyema) Subhanallah, Walhamdulillah, Wala Ilaaha Illa llah Allah Akbar]. Na kwa sababu ya kuwa mara nyingi moyo huamrisha maovu inatakikana kwa binadamu awe mara zote anamfikiria Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

Tahadhari na Vikao vya Watu Walioghafilika

Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) ametahadharisha watu kuondoka katika kikao bila ya kumtaja Allah (Subhaanahu wa Taala) katika kikao hicho kwa neno lake: [Hakuna watu wowote watakaoinuka katika kikao wakawa hawakumtaja Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) katika kikao hicho ila ni kama waliokalia mzoga wa punda, na watakuwa wamepata hasara]. Kwa ajili hiyo Mtume amevipinga vikao vya watu walioghafilika, na amekataza vikao vyote ambavyo havimtaji Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Na vile vikao ambavyo vinawasahaulisha watu kumtaja Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) na vinavyowafanya watu kutumia muda mrefu katika mambo ya kipuuzi, hivi vyote ni vikao vya uvundo havina faida. Na ili mtu akikaa asipate hasara katika vikao vya aina hii, ni aseme anapoondoka katika vikao hivi, kwa kulingana

na mafundisho ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) aliposema: “Yoyote atakaye kaa kwenye kikao, maneno ya kipuuuzi yakawa mengi, basi naye akasema kabla hajainuka katika kikao hicho, [Subhaanak Allahumma Wabihamdika Ash-hadu An-lailaaha illa Anta, Astagh-firuka wa Atubu ilaika], ila Mwenyezi Mungu humfutia makosa yaliyotokea katika kikao hicho”. Na Allah (Subhaanahu wa Taala) anatuambia :

قال تعالى : ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تُلۡهِكُمۡ أَمۡوَٰلُكُمۡ وَلَآ أَوۡلَٰدُكُمۡ عَن ذِكۡرِ ٱللَّهِۚ وَمَن يَفۡعَلۡ ذَٰلِكَ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡخَٰسِرُونَ ٩﴾ [المنافقون:٩].

{{Enyi mlioamini yasiwapumbaze mali yenu na watoto wenu yakawafanya msikumkumbuke Mwenyezi Mungu, na mwenye kufanya hivyo atakuwa ni miongoni mwa waliopata hasara}}.

Mwisho

Tumeona namna ya Allah (Subhaanahu wa Taala) na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) wanavyotuhimiza kuleta dhikri na kuonyesha ya kuwa dhikri ndio njia ya kuondosha hamu na ghamu za binadamu, sio kutizama vipindi vya TV na sinema au kukaa vibarazani. Ndugu Waislamu, Tufanyeni bidii kumtaja Allah kama alivyo tufundisha Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

[7] KUUPOKEA MWEZI WA RAMADHANI

Lengo La Khutba

1. Kuwahimiza watu kujiandaa kiroho kwa kuja mwezi wa Ramadhani.
2. Kuwahimiza watu kupatiliza masiku ya Ramadhanii yaliyo bora.
3. Kubainisha fadhila, hukumu na faida za kufunga.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Ametuwekea misimu mbali mbali na kwa minaajili ya kuipatiliza misimu hiyo kwa kurudi kwa Mwenyezi Mungu kwa kukufanya ibada, miongoni mwa misimu hiyo ni mwezi wa Ramadhani.

Kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa Misimu ya Twaa na Kuipaliza

Baada ya kumshukuru Allah. Mwenyezi Mungu mtakatifu ametuambia:

قال الله عز وجل: ﴿شَهۡرُ رَمَضَانَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ فِيهِ ٱلۡقُرۡءَانُ هُدٗى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَٰتٖ مِّنَ ٱلۡهُدَىٰ وَٱلۡفُرۡقَانِۚ فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ ٱلشَّهۡرَ فَلۡيَصُمۡهُۖ وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوۡ عَلَىٰ سَفَرٖ فَعِدَّةٞ مِّنۡ أَيَّامٍ أُخَرَۗ يُرِيدُ ٱللَّهُ بِكُمُ ٱلۡيُسۡرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ ٱلۡعُسۡرَ وَلِتُكۡمِلُواْ ٱلۡعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُواْ ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَىٰكُمۡ وَلَعَلَّكُمۡ تَشۡكُرُونَ ١٨٥﴾ [البقرة:١٨٥].

{{Mwezi wa Ramadhani ambao umeteremshwa Qur'an ndani yake ambayo ni ubainifu na uongofu kwa watu na upambanuzi. Mwenye kuushuhudia Mwezi wa Ramadhani miongoni mwenu na afunge na atakayekuwa mgonjwa ama akawa safarini (na akala katika mwezi wa Ramadhani) basi ni juu yake kufunga katika siku nyengine, Mwenyezi Mungu awatakia wepesi na wala hawatakii uzito na ili mukamilishe hesabu ya masiku na mumtukuze Mweyezi Mungu, hakika mukifanya hivyo mutakuwa ni wenye shukrani}}.

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, mwezi mtukufu wa Ramadhani umetukabili inatupasa tuupokee kwa kumcha Mwenyezi Mungu na kufanya twaa na ibada kwa wingi na kukaa mbali na maovu kama tunavyo jua ya kuwa malipo ya amali njema huongezeka na vile vile malipo ya amali mbaya. Na mwezi huu mtukufu mwanzo ni kumi la rehma na kumi la maghfira na mwisho ni kuachwa huru na moto. Kufunga mchana ni wajibu na kusimama kwa ibada usiku ni sunna yenye kukamilisha faradhi. Ukifunga kwa imani na kutarajia malipo utasamehewa madhambi yaliyotanguliia. Ukifanya 'umra ni kama uliye hijji. Milango ya pepo hufunguliwa na ya moto hufungwa. Na saumu ni ibada ya pekee ambayo Mola amejihusishia mwenyewe kama alivyosema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) katika hadithi ya Bukhari aliyoipokea kutoka kwa Abu Huraira kuwa Mwenyezi Mungu amesema [Amali zote za binaadamu ni zake ila saumu. Hakika ya saumu ni yangu na ni Mimi ndiye nitakaye ilipa na saumu ni kinga, ikiwa ni siku ya mmoja wenu kufunga basi asifanye machafu, wala asiseme maovu, basi atakapo tukanwa na yoyote au akataka kupigana naye basi amwambie mimi nimefunga. Naapa kwa Yule ambaye nafsi ya Muhammad iko mikononi mwake harufu ya kinywa cha mmoja wenu ni nzuri zaidi kuliko harufu ya miski, na

mwenye kufunga ana furaha mbili, moja huipata akifungua saumu, na ya pili ni wakati akikutana na Mola wake].

Wakati wa kufunga Mwezi wa Ramadhani

Fungeni kwa kuuona mwezi na fungueni kwa kuuona mwezi, kwani Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amekataza kutangulia kufunga Ramadhani kwa siku moja ama mbili ila ikiwa mtu ana ada ya funga yake kama vile jumatatu na Alkhamisi, na haifai kufunga siku ya shaka, Amesema Ammar bin Yaasir “Mwenye kufunga siku ya shaka basi amemuasi Abal Qaasim, yaani Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

Na amepokea Bukhari kutoka kwa Ibnu ‘Umar ya kuwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema katika maana ya Aya: [Msifunge mpaka muuone mwezi wala msifunguwe mpaka muuone mwezi, na iwapo mtafinikwa na mawingu kamilisheni hesabu ya thalathini]. Na atakaye uona mwezi kwa yaqini na amjulishe kiongozi aliyewakilishwa wala asifiche.

Na utakapotangazwa mwezi katika vyombo vya habari, kuingia kwa Ramadhani fungeni na kutoka kwa Ramadhani fungueni, kwani kutangaza kwa kiongozi aliyewakilishwa ndio hukumu.

Kufunga Mwezi wa Ramadhani ni nguzo moja katika uislamu na mwenye kupinga huwa kafiri.

Kufunga ni nguzo iliothibiti katika Qur-ani na mwenye kupinga huwa amemkanusha Mungu na Mtume na maelewano ya Waislamu wote Allah atwambia:

قال الله تعالى : ﴿ يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُتِبَ عَلَيْكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٨٣﴾ ﴾ [البقرة: ١٨٣].

{{Enyi mlio amini mmefaradhiwa swaumu kama walivyofaradhiwa waliotangulia}}. Na saumu ni wajibu kwa kila muislamu alio baleghe na akawa na akili na uwezo wa kufunga, na mwanamke asiyekuwa na hedhi. Kafiri si wajibu kufunga, lakini ataulizwa siku ya kiyama na akisilimu halazimishwi kulipa zilizopita ila akisilimu katikati ya huo mchana wa Ramadhani atalazimika akamilishe siku na mtoto mdogo si wajibu kufunga mpaka abaleghe lakini yafaa tuwafundishe kufunga kama walivyokuwa masahaba. Na kubaleghe kwa mtoto hujulikana kwa moja katika mambo matatu: Jambo la kwanza; ni kufikia miaka kumi na mitano. Jambo la pili; ni kutokwa na manii kwa kuota, ama jambo jingine. Jambo la tatu; ni kutokwa na nywele za kinena. Na mtoto wa kike huzidisha Jambo la nne nalo nikupatwa na hedhi. Mtoto akipatwa na mambo haya tuliyoyataja, humlazimu faradhi zote za Mwenyezi Mungu ikiwa ana akili.

Na mwendawazimu si wajibu kufunga wala faradhi yoyote nyingine. Na wala mwenye kushindwa kufunga kwa sababu ya utu zima ama ugonjwa ambao hautarajiwi kupona, itakuwa si lazima kufunga lakini atalisha maskini kila siku alioacha atalisha maskini mmoja, kila maskini robo ya pishi kwa pishi za Mtume na ni bora kumuongezea kitoweo.

Ni nini Hukumu ya Wenye Udhuru katika kufunga ?

Mgonjwa anayetarajiwa kupona, ikiwa saumu haimsumbui wala kumdhuru, haifai kula kama mtu huyo hana udhuru wowote. Na ikwa saumu inamsumbua lakini haimdhuru na inafaa afungue na ni karaha kufunga na ikiwa saumu itamdhuru ni haramu kufunga na popote atakapopoa itamlazimu ailipe saumu na akifa kabla ya kupona hana madhambi.

Na mwanamke mwenye mimba akiwa ni dhaifu ama mimba itamletea uzito akashindwa kufunga mwanamke huyo anaruhusiwa asifunge lakini akihisi ya kuwa na uwezo wa kufunga, atafunga hata ikiwa ni kabla ya kujifungua na itakapokuwa haiwezekani atasubiri baada ya kujifungua na kutwahirika na nifasi. Na mwanamke mwenye kunyonyesha akiogopea kupunguka maziwa atakula kisha atalipa.

Na msafiri akikusudia kukimbia saumu haifai ni lazima afunge. Na ikiwa hakukusudia kukimbia kufunga basi ana hiari ya kufunga na kutofunga. Na ikiwa kufunga na kutofunga ni sawa basi ni bora afunge.

Na ikiwa safari itamsumbua ni karaha kufunga iwapo mashaka yatazidi na ni haramu kufunga. Kwani Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alitoka kwenda Makka mwaka wa fat-hi na huku amefunga akaambiwa kuna watu wameshindwa kufunga na wanakusubiri wewe utakavyofanya. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akaitisha maji akanywa na watu wanamwangalia kisha na watu wakanywa, kisha akaambiwa kuna watu hawakufungua akasema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) : [Hayo ni maasi].

Na safari ni ya aina yoyote ile, kama madereva wa malori wakati wowote wanapoacha miji yao wanaruhusiwa kufungua kama vile wanavyoruhusiwa kupunguza swala za rakaa nne na kuzikusanya swala mbili mbili ikiwa mtu amesafiri katikati ya mchana ni vizuri akamilishe saumu ya siku ile ya kwanza ya safari.

Na haifai kufunga kwa mwenye hedhi na nifasi na wala haiswihi. Wakati wakitwahirika na hedhi ni lazima wafunge hata kama hawajaoga kisha watalipa siku walizokula.

Kuhimiza kusimama Usiku wa Ramadhani na kuwanasihi Maimamu kuwa na makini katika Swala bila kuangalia wingi au uchache wa Rakaa

Enyi Waislamu, Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amehimiza kusimama kufanya ibada katika masiku ya Ramadhanii. Na mtu akiendelea na imamu kuswali mpaka akamaliza huandikiwa thawabu za mtu aliyesimama usiku kucha.

Na ni juu ya maimamu kumcha Mwenyezi Mungu katika kuswalisha tarawehe. Inafaa awachunge wanaomfuata asiwaendeshe mbio bila ya utulivu katika kusimama, kurukuu na kusujudu. Kwani Mwenyezi Mungu Amesema (Subhaanahu wa Taala) katika mafhum ya Aya:

قال الله تعالى : ﴿لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا﴾ [هود:٧]

{{Ili apate kuwaonja walio na amali nzuri zaidi (sio walio na amali za haraka zaidi)}}. Na Mtume alikuwa ni mwenye kupenda kheri zaidi na ni kielelezo chema lakini hakuzidisha zaidi ya rakaa kumi na moja sio katika Ramadhanii wala masiku mengine. Na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) aliswali na jamaa katika Ramadhani kisha akaacha kwa kuogopea isifaradhishwe.

Na iliyo swahihi kutoka kwa Amirul muuminiina 'Umar ibnul Khatwb ni kuwa alimuamrisha 'Ubai ibn Ka'ab na Tamimi Daar waswalishe watu kwa rakaa kumi na moja na hii ndio idadi aliodumu nayo Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) na akafuata khalifa muongofu 'Umar Ibnul khatwab ndio bora zaidi, na ikiwa mtu atazidisha kwa mapenzi yake sio kufuata sunna hapingwi lakini asifanye haraka kama wanavyofanya maimamu wabaya.

Mungu atuafikie kupaliza nyakati za twaa na atuhifadhi na maovu na atuongoze njia iliyonyooka na atuepushe na njia ya motoni na atufanye wenye kufunga Ramadhani na wenye kusimama usiku kwa ibada kwa imani na kutarajia malipo na thawabu za Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyyezi Mungu ni Mpaji na ni Mkarimu.

Namaliza maneno yangu kwa kumuomba Mwenyezi Mungu msamaha na kuwaombea Waislamu wote msamaha kutokana na madhambi yote.

Faida za Kufunga:

Miongoni mwa faida ni kuivunja nafsi, kwani shibe ya maji na chakula na kuvaana na wanawake inapelekea kughafilika.

Faida nyingine ni moyo kukaa faragha kwa kumfikiria Mwenyezi Mungu na kuleta dhikri, kwani tumbo likiwa tupu husababisha moyo kunawirika.

Na faida nyingine ni kwa mtu tajiri hujua neema ya Mola juu yake. Kwa sababu ya kujinyima kwa muda fulani na hupelekea kumkumbuka ndugu yake aliyenyimwa neema ile moja kwa moja humsikitikia mwenzake maskini.

Na saumu hufanya mapitio ya damu kuwa membamba ambayo ndio mapitio ya shetani, kwani shetani anatembea katika mwili kama inavyotembea damu basi Mtume amesema "Fungeni mapito ya shetani kwa njaa."

Saumu ya Mja haiwezi kutimia ila akiepuka yaliyo haramishwa katika hali zote.

Kwani Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) Amesema [Ambaye haachi maneno ya uongo na kutumia uongo, Mwenyezi Mungu hana haja aache chakula chake na kinywaji chake]. Na watu wema ilikuwa wakifunga hukaa Msikitini ili kuepukana na kusengenya.

KHUTBA YA PILI

Makundi ya Wenye kufunga

Kuna makundi mawili ya wenye kufunga:

1. Wanaofunga kutarajia pepo.
2. Wanaofunga kuacha dunia na kuelekea kwa Allah (Subhanahu wa Taala).

Imepokewa kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). katika swahihi mbili akisema [Hakika katika pepo kuna mlango unaoitwa Rayyan, haingii yoyote isipokuwa wenye kufunga]. Na katika riwaya nyingine: [wakiingia utafungwa]. Hiyo ndiyo tabaka la kwanza, ambao wanatarajia pepo, huyu amefanya na Mola atamlipa. Ama tabaka la pili ni ambao wanafunga na wanaepukana na dunia, huhifadhi kichwa na kilochokusanya (macho, masikio, na mdomo) na huhifadhi tumbo, na hukumbuka mauti na kuoza baada ya kufa. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema :

قال الله تعالى : ﴿مَن كَانَ يَرْجُواْ لِقَآءَ ٱللَّهِ فَإِنَّ أَجَلَ ٱللَّهِ لَأَاتٍ﴾ [العنكبوت: ٥]

{{Mwenye kutarajia kukutana na Mwenyezi Mungu, hakika ajali ya Mungu inakuja}}.

Na Mwenyezi Mungu amesema katika maana ya Hadithi al-Qudsi: [Saumu ni yangu na mimi ndiye mwenye kuilipa].

Ubora wa Mwezi wa Ramadhani

Allah (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

قال الله تعالى: ﴿شَهْرُ رَمَضَانَ ٱلَّذِىٓ أُنزِلَ فِيهِ ٱلْقُرْءَانُ﴾ [البقرة:١٨٥]

{{Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa Qur-ani ndani yake}}. Na Ibnu 'Abbas (Radhiya Llahu 'anhu) amesema Qur-ani iliteremshwa kwa mara moja kutoka Lauhul mahfuudh mpaka Baitul 'izza katika usiku wa cheo. Na ushahidi ni kuwa Allah (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

قوله تعالى: ﴿إِنَّآ أَنزَلْنَٰهُ فِى لَيْلَةِ ٱلْقَدْرِ ١﴾ [القدر:١].

{{Hakika yetu sisi tumeiteremsha Qur'an katika usiku wa cheo}}. Na maswahaba walikuwa wakisimama usiku mpaka karibia na alfajiri. Na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) ulikuwa ukarimu wake ukizidi katika mwezi wa Ramadhani na hiyo ni sababu ya kukaa sana na Jibril kwa kumsomea Qur-ani na kumhimiza katika tabia njema.

Faida za kuwa Mkarimu katika Mwezi wa Ramadhani.

- Ya kwanza ni utukufu wa zile zama na kuongezeka malipo ya amali
- Ya pili ni kuwasaidia wenye kufunga na wenye kufanya ibada katika ibada zao.
- Ya tatu ni kuwa katika Ramadhani Allah anawakirimu waja wake kwa rehema na maghfira kuwaacha huru na moto haswa katika Lailatul Qadri kwa Allah anawarehemu waja wake wenye sikitiko zaidi.
- Ya nne, kuchanganya baina ya saumu na sadaka ni katika mambo yenye kumtia mtu peponi.
- Ya tano, kufunga pamoja na kutoa sadaka ni mambo yanayofuta madhambi zaidi na kuepushwa na moto wa jahanamu. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Saumu ni kinga].
- Ya sita hakika ya saumu hakuna budi kutapatikana kasoro au upungufu, basi sadaka itaziba kasoro hiyo au upungufu huo na ndio ikawajibishwa kutoa Zakatul fitri.
- Ya saba, Imam Shafi amesema inapendeza zaidi kwa mtu kufanya wingi wa kutoa katika mwezi wa Ramadhani ili kumwiga Mtume na watu kuhitajia maslahi yao na watu kushughulika na ibada na kuwacha kufanya kazi. Ewe Mola tukubalie funga yetu na kisimamo chetu. Ewe Mola msamehe aliyekufa na aliye hai kati yetu na mdogo wetu na mkubwa wetu na mume na mke na aliyeko na asiyekuweko miongoni mwetu.

Mwisho

Enyi ndugu Waislamu, tujipinde katika mwezi wa Ramadhani kwani tusipo fanya hivyo tutakuwa mbali na rehma za Allah (Subhaanahu wa Taala) na kama tulivyobainisha ya kuwa twaewza tukafunga njaa iwapo hatutaepukana na makatazo ya Allah katika hali ya kufunga.

[8] ZAKA NA HIKMA ZAKE NA HUKUMU ZAKE

Lengo La Khutba

1. Kubainisha zaka na daraja yake katika Uislamu.
2. Kubainisha hikma zilizomo katika kufaradhiwa
3. Kubainisha hukumu zinazofungamana na mali za zaka
4. Kubainisha matumizi yake na kufanya bidii katika kuichukua na kuitoa.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Allah (Subhaanahu wa Taala) kwa hikma yake amewakunjulia baadhi ya waja riziki na wengine akawabania, na sio dalili ya kupendwa na Mwenyezi Mungu ukiwa umekunjuliwa riziki wala sio kuchukiwa ikiwa umebaniwa riziki. Kwani siku ya kiyama atakayenufaika ni atakayekuwa na moyo uliosalimika na maovu na ukiwa umeneemeshwa na Mola kwa kupewa mali, basi Allah amekupa mtihani kwa kukulazimisha utoe zaka ili kukuangalia utashukuru kwa kutekeleza amri yake ama utafanya ubakhili wa kutotoa zaka.

Kubainisha namna ya Mwenyezi Mungu Alivyotofautisha Waja wake katika Riziki

Enyi watu mcheni Mungu haki ya kumcha. Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, miongoni mwa hikma za Mungu ni vile alivyo tofautisha tabia za watu na riziki zao. Amewakunjulia watu wengine na amewabania watu wengine na yote hayo ni kwa hikma yake Allah. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala) katika Qur'an Tukufu:

قال الله تعالى : ﴿فَأَمَّا ٱلۡإِنسَٰنُ إِذَا مَا ٱبۡتَلَىٰهُ رَبُّهُۥ فَأَكۡرَمَهُۥ وَنَعَّمَهُۥ فَيَقُولُ رَبِّيٓ أَكۡرَمَنِ ۝١٥ وَأَمَّآ إِذَا مَا ٱبۡتَلَىٰهُ فَقَدَرَ عَلَيۡهِ رِزۡقَهُۥ فَيَقُولُ رَبِّيٓ أَهَٰنَنِ ۝١٦﴾ [الفجر:١٥-١٧]

{{Pindi binaadam anapoonjwa na Mola wake na akamtukuza na akampa neema zake basi husema binaadam, Mola wangu amenitukuza, na pindi anapo muonja Mola wake na kumbania riziki yake basi husema, Mola wangu amenitweza. Sivyo hivyo}} [fajri 15-17].

Yaani sio kila aliyepewa ndio amependwa na wala sio kila aliyenyimwa huwa amechukiwa, bali hapa duniani, Mungu humpa amtakaye na humnyima amtakaye kwa hikma anayo ijua yeye mwenyewe ili kuangalia shukrani ya tajiri na subira ya maskini, kwani mali ni balaa kwa wengine na ni neema kwa wengine. Mwenye kujua ya kuwa kuna haki ya Mwenyezi Mungu katika mali yake, basi kwa mtu huyo mali kwake huwa ni neema, na ukisahau na mali ikawa ni sababu ya kupotea, basi mali itakuwa ni balaa kwako na mali itakuwa ni sababu ya kuadhibiwa kwa mtu huyo. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala) katika Qur'an Tukufu:

قال الله تعالى : ﴿فَلَا تُعۡجِبۡكَ أَمۡوَٰلُهُمۡ وَلَآ أَوۡلَٰدُهُمۡۚ إِنَّمَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيُعَذِّبَهُم بِهَا فِي ٱلۡحَيَوٰةِ ٱلدُّنۡيَا وَتَزۡهَقَ أَنفُسُهُمۡ وَهُمۡ كَٰفِرُونَ ۝٥٥﴾ [التوبة:٥٥]

{{Yasikushangaze mali na watoto wao, hakika si jingine ila anataka kuwaadhibu kwa mali hayo katika uhai wa duniani na iwatoe roho zao hali ya kuwa ni makafiri}}.

Na Allah anatuambia kuhusu nabii wake Suleiman alipo muelimisha aliyo muelimisha na akaona neema ya Mungu juu yake. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala) katika Qur'an Tukufu:

قال الله تعالى : ﴿هَٰذَا مِن فَضْلِ رَبِّي لِيَبْلُوَنِي ءَأَشْكُرُ أَمْ أَكْفُرُ﴾ [النمل:٤٠].

{{Hii ni fadhila ya Mola wangu ili apate kunifanyia mtihani kama nitashukuru ama nitakufuru}}. kinyume na aliyeghurika na akasema:

وقال: ﴿إِنَّمَآ أُوتِيتُهُۥ عَلَىٰ عِلْمٍ عِندِيٓ﴾ [القصص:٧٨].

{{Hakika si jingine, nimepewa kwa ajili ya elimu niliyonayo}}

Uwajibu wa Zaka na kuwa ni Nguzo katika Uislamu.

Ewe Muislamu Allah amewajibisha matajiri haki katika mali zao kuwapa maskini {Na wale katika mali zao kuna haki inayojulikana kwa wenye kuomba na wale walionyimwa}

Ili matajiri wawakunjulie ndugu zao maskini, na Allah Akafanya zaka ni nguzo ya tatu katika nguzo za Uislamu, kama alivyotuambia Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano, kushuhudia ya kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na Muhammad (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) ni Mtume wake, na kusimamisha swala, na kutoa zaka, na kufunga mwezi wa Ramadhani na kwenda kuhiji]. Amepokea hadithi hii Bukhari kutoka kwa Ibnu 'Umar. Na katika swahihi mbili kutoka kwa Ibnu 'Abbas radhi za Mungu ziwe juu yao amepokea neno la Mtume kumwambia Mu'adhi : [Wajulishe ya kuwa Allah (Subhaanahu wa Taala) Amewafaradhia Sadaka juu yao na inachukuliwa kutoka kwa matajiri wao na kurudiswa kwa maskini wao]. Na dalili nyingi zimeeleza kuhusu zaka na umuhimu wake.

Ni nini Hikima ya Kufaradhishwa Zaka?.

Katika kufaradhishwa kwa zaka kuna hikma nyingi ambazo Allah (Subhaanahu wa Taala) Ameweka ndani yake. Kwanza ni kuusafisha moyo kutokana na ubakhili na kusafisha mali kutokana na uchafu kisha kutia baraka katika mali. Na kutoa zaka ni kuvunja nguvu za shetani kwani ukitoa zaka hutia nguvu imani kwa sababu huwa umeshinda hawaa yako na matamanio yako na wasiwasi wa shetani. Kwa sababu Allah (Subhaanahu wa Taala) Atwambia:

قال الله تعالى : ﴿ٱلشَّيْطَٰنُ يَعِدُكُمُ ٱلْفَقْرَ وَيَأْمُرُكُم بِٱلْفَحْشَآءِ ۖ وَٱللَّهُ يَعِدُكُم مَّغْفِرَةً مِّنْهُ وَفَضْلًا ۗ وَٱللَّهُ وَٰسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٦٨﴾﴾ [البقرة:٢٦٨].

{{Shetani anawaagiza ufukara na anawaamrisha maovu na Mwenyezi Mungu anawaagiza msamaha kutoka kwake na fadhila na Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu wa ilimu}}.

Na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) anatuambia: [Na Sadaka haipunguzi mali].

Ewe ndugu yangu Muislamu, toa zaka kwa kupenda na kuamini ya kuwa ni wajibu wako na kumtii Mola wako, usipofanya hivo siku ya qiyama ni siku ambayo hayakufai mali wala watoto ila mwenye kuja kwa Mungu (Subhaanahu wa Taala) hali ya kuwa na moyo uliyosalimika.

Ewe ndugu yangu Muislamu toa zaka na huku watia nia kwani nia ndiyo yenye kuzingatiwa katika amali zote na ukitoa zaka kwa nia ya hiyo zaka, basi pokea bishara ya kheri na baraka kutoka kwa Mungu na malipo makubwa siku ya kupambana na Mola wako.

Sampuli ya Vitu ambavyo yapasa kutolewa Zaka.

Kitu cha kwanza unacho wajibika kutoa ni kinachotoka Ardhini, mbegu na matunda, Allah (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

قال الله تعالى : ﴿وَءَاتُواْ حَقَّهُۥ يَوۡمَ حَصَادِهِۦ﴾ [الأنعام: ١٤١].

{{Toeni haki yake siku ya kuvuna}}. Na sharti zake ni kufikia vikapu vitano kwa sasa ni 900kg. Na ikiwa imenoshezwa kwa gharama itakuwa kiwango cha kutoa ni nusu ya fungu la kumi. Ama ikiwa haikuwa na gharama itakuwa ni fungu la kumi. Ama mboga na vinginevyo ambavyo havikai muda mrefu havina wajibu wa kutolewa zaka.

Zaka za Wanyama na Hukumu yake.

Wanyama wanaopaswa kutolewa zaka ni Ngamia, N’gombe na Mbuzi. Wanyama hawa wakiwa wanalisha wenyewe katika mimea ya Ardhini na uchache wa kiwango cha Ngamia kinachopaswa kutolewa zaka ni Ngamia watano na kiwango cha N’gombe ni thelathini na cha Mbuzi ni arubaini. Ama wanyama wanao lishwa kwa kununuliwa chakula hawatolewi zaka ila kuwa mwenyewe ataka kuwafanyia biashara atatoa zaka za biashara.

Zaka ya Mali ya Biashara na Hukumu yake.

Mali ya biashara ni kila kitu ambacho Muislamu amekiandaa kuuza au kununua kutokana na bidhaa tofauti tofauti; kama chakula au mavazi au kipando au chochote chingine kikifika mwisho wa mwaka tutatoa robo ya fungu la kumi ni sawa umepata faida ama hasara. Mfano thamani ya kitu iwe ni shilingi laki moja, lakini baada ya kupitiwa na mwaka ikawa ni laki tano basi zaka zake ni hisabu ya hizo elfu mia tano, na ikiwa kimepunguwa kima cha mali yako elfu mia moja, mali yatahisabiwa vile yalivyo pungua.

Zaka za Naqdain (Dhahabu na Fedha)

Dhahabu na fedha ni wajibu kuzitolea zaka, Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

قال تعالى: ﴿وَالَّذِينَ يَكْنِزُونَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلَا يُنفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَبَشِّرْهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٣٤﴾
يَوْمَ يُحْمَىٰ عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فَتُكْوَىٰ بِهَا جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ وَظُهُورُهُمْ ۖ هَٰذَا مَا كَنَزْتُمْ لِأَنفُسِكُمْ فَذُوقُوا مَا كُنتُمْ
تَكْنِزُونَ ﴿٣٥﴾﴾ [التوبة:٣٤:٣٥].

{{Na wale ambao wanaziweka dhahabu na fedha kwenye hazina kisha wasizitolee zaka kwa ajili ya njia ya Mwenyezi Mungu basi wape bishara ya adhabu kali siku ambayo zitachomwa hizo dhahabu na fedha katika moto wa jahannam kisha wapigwe nazo pasi katika nyuso zao na mbavu zao, kisha waambiwe, hizi ndizo mlizozihifadhi kwa nafsi zenu, basi onjeni mlivyokuwa mkivihifadhi}}. Kwa hivyo, dhahbu na fedha hutolewa zaka na hizi pesa pia hutolewa zaka kwani hutumika badala ya dhahabu na fedha na huchukua hukumu ya dhahabu na fedha na hutolewa robo ya fungu la kumi.

Zaka ya Hisa za Kampuni

Na hisa za kampuni mbali mbali huwa zinagawanyika mara mbili:-

1. Ni hisa ambazo zinabadilishiana, Muislamu akiwa na hisa hizo huwa anataka faida na huzificha wakati mwengine, hisa hizo zinalazimu kutolewa zaka kama vile dhahabu na fedha.
2. Ni hisa ambazo huwekwa kama akiba, haziuzwi wala kununuliwa isipokuwa mwenyewe huwa anatumia faida yake, basi ile faida akikaa nayo mpaka ukapita mwaka basi itamlazimu kuitolea zaka.

Je, Majumba na Viwanja vya kukodisha vina Zaka?

Zaka za majumba na viwanja vya kukodisha inategemea yale makubaliano ya kukodishiana, ikiwa malipo watachukuwa mwisho wa mwaka basi itakuwa ni wajibu kutoa zaka, lakini kama watapokea malipo ya nyumba kila baada ya miezi sita, basi itakuwa si wajibu kutoa zaka ikiwa malipo hayo watayatumia, lakini ikiwa watakusanya na ikafika mwisho wa mwaka na hujayatumia, utawajibika utoe zaka.

Ama nyumba unayoikaa na gari unalolitumia kwa kulipanda wewe mwenyewe vitu hivi havitolewi zaka.

KHUTBA YA PILI.

Wenye kufaa kupewa Zaka.

Ewe ndugu muislamu, Allah (Subhaanahu wa Taala) hakumuachia Mtume yeyote wala Malaika kueleza wanaofaa kupewa zaka, Ewe muislamu, muogope Mwenyezi Mungu katika kutoa zaka zako na ujuwe ya kuwa umepewa amana kwa hivyo fikisha amana kwa wahusika {hakika Mwenyezi Mungu anawaamrisha kutekeleza amana kwa wenyewe} maana ya Aya.

Na kuna sampuli ya watu wanaostahiki kupewa zaka nao ni:-

Maskini na fukara ambao hawana kitu au wanacho lakini hakiwatoshi, basi ni wajibu tuwape zaka za kuwatosha mwaka mzima na anaye hitaji kuoa katika wao, kwani hayo ndio mahitaji muhimu sana. Ama mtu akiwa ana uwezo inafaa umnasihi na umtahadharishe kwani Mume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alijiliwa na watu wawili wakamuomba sadaka, Mtume akawaangalia vizuri akawaona ni watu barabara, kisha Mtume akasema [Mukitaka nitawapa na tajiri hana haki katika zaka wala mwenye nguvu anayefanya kazi]. Maana ya hadithi, imepokea hadithi hii na Ahmad na Abu Daud na Annasai kutoka kwa ‘Ubaydullah ibn Adiyyi.

Na sampuli nyingine ni mwenye madeni ni sawa ikiwa deni ni la nafsi yake kisha akashindwa kulipa lakini isiwe ndio kawaida yake ya kukopesha kisha kushindwa kulipa. Na yafaa kumpaa zaka mtu aliyeingia madeni kwa sababu ya kusaidia umma.

Na wengine wenye kufaa kupewa zaka ni wenye kupigana jihadi na waliokatikiwa na safari.

Kutahadharisha Wasiostahiki Zaka wasiombe.

Ewe Mja wa Allah, Ewe Muislamu ukiwa ni tajiri tahadhari na kuchukua zaka, ukichukua ni haramu unayokula, na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wassalam) Amesema katika maana ya hadithi: [Mwenye kuomba watu kwa ajili ya kufanya wingi (mali yake) hakika si lingine ila anaomba kaa la moto, basi ni apunguze au afanye wingi]. Na katika musnad ya Imam ahmad ibn Hambali amepokea kutoka kwa Abu Hurayra.

Ndugu yangu Muislamu, ni watu wangapi wanaoomba zaka na hali ya kuwa hawana haki ya kupewa. Kwa hivyo ndugu yangu Muislamu, tahadhari kuchukua zaka ikiwa huna haki nayo.

Na wewe mwenzangu mwenye kutoa zaka, uangalie sana ni nani wanao stahiki kupewa zaka. Kuna watu ambao (wamejihifadhi ambao hawaombi watu kwa kuwahimiza, na wasiowajua wanaowadhania kuwa ni matajiri kwa sababu ya kujihifadhi). Jaribu kupeleleza kwani unaweza ukamuona mtu ni tajiri mbele za watu, kumbe ni maskini na anayejua hali yake ni Allah peke yake.

Na miongoni mwa mambo muhimu ni kuwa Allah ameifanya zaka ni sababu ya jamii kuzoeana na kushirikiana na kushikamana na kuhurumiana Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Warehemuni walioko Ardhini, atawarehemu

aliyeko mbinguni]. Imepokewa ma Ahmad na Abu Dawuud na At-Tirmidhi.

Na lau matajiri wangalitoa zaka za mali yao, maskini wangalitosheka na wangehifadhi nyuso zao na wangehifadhika na uhalifu na wangekuwa mbali na mambo yasiokuwa na kheri.

Basi fanyeni pupa kwa kutoa zaka za mali yenu na kwa wanaostahiki na ni uzuri kuhusisha jamaa zako, kwani ukifanya hivyo utapata mambo mawili, thawabu ya kutoa zaka na thawabu ya kuunga kizazi na utafute majirani zako. Vile vile yafaa tusaidiane kutafuta mafukara wanaostahiki kupewa zaka.

Tumuombe Allah atukubalie mema yetu, Yeye ndiye muweza wa kila kitu na mjue ya kuwa hakika maneno mazuri zaidi ni kitabu cha Mwenyezi Mungu na uongofu bora ni uongofu wa Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wassalam)

Mwisho

Nawausia ndugu zangu Waislamu waliowajibika kutoa zaka wazifikishe zaka hizo kwa wenye kustahiki na inapobidi kuficha zaka zenu wakati mnapotoa mfanye hivyo. Kwani baadhi ya mafukara hawataki kujulikana hali zao, na jaribu kuhusisha zaka zako kwa jamaa zako waliokuwa mafukara, kwani huwa ni sadaka na kuunga kizazi, tumuombe Mwenyezi Mungu atuafikie kila la kheri kwani yeye ndiye muweza wa kila jambo.

[9] MAFHUMU (Mtazamo) YA IBADA KATIKA UISLAMU

Lengo la Khutba

1. Lengo la kuumbwa viumbe
2. Kueleza sampuli za ibada katika uislamu
3. Kufafanua ya kuwa ukitaka malipo katika mambo ya kawaida huandikiwa thawabu.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Kumuabudu Mwenyezi Mungu ndio hikma kubwa ya kuumbwa kwa binaadamu. Na ibada ni kuelekea kwa Mungu katika hali zako zote hata ukiwa unafanya mambo ya kawaida na huku watarajia thawabu utalipwa na Allah.

Hikma ya kuumbwa kwa Binaadamu na Majini.

Enyi waja kuumbwa kwa binaadam sio kwa mchezo, bali ni kwa hikma kubwa ndio Allah akawa anatueleza katika Aya nyingi kuhusu kuumbwa kwa binaadamu akatuambia:

وقال جلّ جلاله: ﴿وَمَا خَلَقْنَا ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا لَٰعِبِينَ ﴿٣٨﴾ مَا خَلَقْنَٰهُمَآ إِلَّا بِٱلْحَقِّ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٩﴾﴾ [الدخان: ٣٨:٣٩].

{{Hatukuumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake kwa mchezo}}.

وقال: ﴿وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾﴾ [الذاريات: ٥٦].

{{Sikuumba majini na binaadamu ila ni kwa hikma ya kuniabudu}}. Yote haya ni kueleza hikma ya kuumbwa kwa binaadamu.

Mafhuum ya Ibada

Hakika ya ibada ni kila jambo la kheri katika mambo ya dini na mambo ya dunia na inakusanya maneno na vitendo vyenye kumridhisha Allah. Na utukufu wa Muislamu ni kuwa mnyenyekevu na kwenda mbio kuhakikisha kuwa mja wa Mwenyezi Mungu kisawa sawa kwa kufuata maamrisho na kuepukana na makatazo.

Sampuli za Ibada

Kwa fadhila zake Mwenyezi Mungu ameweka ibada nyingi tofauti tofauti, kuna ibada ya moyo kama ikhlas na ibada za mwili kama vile swala tano na kuna ibada za mali kama kutoa zaka. Kutoa mali hali ya kuwa na imani na radhi kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu. Kuna ibada ambazo zinakusanya baina ya mali na mwili kama hija na jihadi. Kisha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ametutukuza kwa kutuwekea sunna za swala na Sadaka na swaumu na hajj na ‘umra ili zipate kutuinua daraja.

Sharti za kukubaliwa Ibada.

Ibada haikubaliwi ila kwa masharti mawili:-

1. Amali iwe ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na haina riyaa.
2. Ifanyike kulingana na alivyoiweka Mwenyezi Mungu na kuelezewa na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

Kwani dini imekamilika haitaki kuzidishwa wala kupunguzwa kwani Allah anatuambia:

قال تعالى: ﴿ٱلۡيَوۡمَ أَكۡمَلۡتُ لَكُمۡ دِينَكُمۡ﴾ [المائدة: ٣].

{{Leo nimewekamilishia dini yenu}}. Na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) ameifikisha kama ilivyo na hakuna mtu mpotevu kuliko mwenye kufuata hawaa yake.

Ukitaka malipo kwa mambo ya kawaida huwa ni ibada yenye kukukurubisha.

Ewe Muislamu vitendo vyako vyote, ukikusudia kupata radhi za Mola utapata.

Kuwatii wazazi wako ni ibada. Alikuja mtu kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akitaka ruhusa kwenda jihadi. Akaulizwa: [Je wazazi wako hai? Akasema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): nenda ukapigane jihadi kwa kuwatii]. Utakuta kuwatendea wema wazazi ni kama kwenda katika uwanja wa jihadi. Kuunga kizazi ni kutekeleza wajibu.

Kama vile alivyosema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ ٱلَّذِي تَسَآءَلُونَ بِهِۦ وَٱلۡأَرۡحَامَۚ﴾ [النساء: ١].

{{Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana na (muwatazame) jamaa}}.

Ndugu Muislamu hata chakula unacholisha watoto wako unapata thawabu. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) Amemwambia Sa’ad: [Hata unacho kiweka katika kinywa cha mke wako]. Yaani utapata thawabu. Imepokewa na Bukhari na Muslim.

Kuwalea watoto wako pia ni ibada, Allah anatuambia:

قال تعالى: ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ قُوٓاْ أَنفُسَكُمۡ وَأَهۡلِيكُمۡ نَارٗا﴾ [التحريم: ٦]

{{Ziokoeni nafsi zenu na ahli zenu kutokana na moto}}. Biashara zako, kuoa kwako kwa ajili ya kujihifadhi ni ibada, kila jambo unalolifanya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu unaandikiwa thawabu. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) ametuambia: [Hakuna Muislamu yoyote atakayepanda mmea, au atakayelima kisha akala mmea huo binaadamu au ndege ila yule aliyeupanda mti ule mara ya kwanza hupata malipo].

Kuondosha udhia katika barabara ni Sadaka na ni ibada, hata ilimu yoyote anayojifundisha mja huwa anapata thawabu iwapo atataka kunufaisha umma atapata thawabu kwa Mungu kwani amali zote huzingatiwa nia.

Namna ya kuitengeneza Ibada na kuifanya kwa yakini.

Ewe Muislamu, kuwa na msimamo na udumu katika ibada na usichoke kwani Allah (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

قال تعالى: ﴿ وَٱعْبُدْ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأْتِيَكَ ٱلْيَقِينُ ﴿٩٩﴾ ﴾ [الحجر:٩٩].

{{Muabudu Mola wako mpaka yakufikie mauti}}. Isiwe hamu yako ni kumaliza ibada au kumalizika, bali hamu iwe ni kuifanya ibada. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alikuwa akimwambia Bilali: [Tupumzishe kwa swalah]. Imepokewa na Ahmad. Na alikuwa akisema: [Kutulia jicho langu ni katika swala}. imepokewa na An-Nasai kutoka kwa Anas. Hata kumuingilia mke wako ni ibada, hii ni neema ya Mola kwa waja wake.

Kukatazwa kutia uzito na kuvuka mipaka katika Ibada.

Kwani ukiwa na mikazo utashindwa mwishowe, Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). alipofikiwa na khabari ya 'Abdullah bin 'Umar ya kuwa usiku anasimama kuswali na mchana anafunga, mkewe akamshitaki. Amesema Mtume (Subhaanahu wa Taala): [Hakika Mola wako ana haki juu yako, na Nafsi yako ina haki juu yako, na hakika ahli yako ana haki juu yako, ewe 'Abdullahi, funga kila mwezi siku tatu, akakataa akasema naweza zaidi ya hizo, akakazana naye Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) mpaka akamfanya kuwa akifunga siku moja na anafungua siku moja, hivi hivi ndio akamueleza kuswali usiku na kusoma Qur-aani].

Na vile vile, kuongeza mambo katika dini ni mja kujisumbua na wala hafikii lengo, kwani amali ndogo yenye kudumu ni bora kuliko amali nyingi ambayo utaifanya siku na siku nyingine utaacha, na Muislamu kuwa na ibada tofauti tofauti ni bora kwani hufanya uhusiano wake na Mola wake uwe na nguvu. Na Mungu atuafikie kila jambo la kheri.

Kumnyenyekea Mwenyezi Mungu ni Sharafu na Utukufu.

Kwa utukufu wa kunyenyekea kwa Allah ndio Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akawa ni mtukufu zaidi wa viumbe wa Mwenyezi Mungu na akalingania mlinganio mtukufu nao ni kuwa mja wa Mungu mwenye kunyenyekea. Allah amesema:

قال سبحانه وتعالى: ﴿سُبْحَٰنَ ٱلَّذِىٓ أَسْرَىٰ بِعَبْدِهِۦ لَيْلًا مِّنَ ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ إِلَى ٱلْمَسْجِدِ ٱلْأَقْصَا﴾ [الإسراء: ١].

{{Utakatifu ni wa Allah ambaye alimpeleka mja wake israai}}.

Na Akasema tena:

وقال تعالى: ﴿تَبَارَكَ ٱلَّذِى نَزَّلَ ٱلْفُرْقَانَ عَلَىٰ عَبْدِهِۦ لِيَكُونَ لِلْعَٰلَمِينَ نَذِيرًا ﴿١﴾﴾ [الفرقان: ١].

{{Ametukuka ambaye kwamba amemteremshia Qur-aani mja wake ili apate kuwakhofisha walimwengu}}. Na ndio alama kubwa ambayo inatakikana ili apate utukufu wa kuwa mja wa Allah mwenye kunyenyekea. Kwa Mtume mwito mtukufu alioitiwa nao ni kuitwa mja wa Allah.

KHUTBA YA PILI

Ibada ni Uhai wa Roho

Kama unataka kujua ladha ya ibada waangalie wenye kufuata dunia na wakakufuru, Mwenyezi Mungu anawaambiaje katika maana ya Aya:

قال الله تعالى : ﴿وَٱلَّذِينَ كَفَرُواْ يَتَمَتَّعُونَ وَيَأۡكُلُونَ كَمَا تَأۡكُلُ ٱلۡأَنۡعَٰمُ وَٱلنَّارُ مَثۡوٗى لَّهُمۡ ١٢﴾ [محمد: ١٢].

{{Wale walio kufuru wanastarehe na kula kama wanavyokula wanyama na moto ndio marejeo yao}}. Kwa hivyo, kama hujaonja utamu wa imani na ibada basi utakuwa ni kama mnyama katika pori.

Kwa hivyo, wale Waislamu waliohadaika kwa kuwaigiza maadui wa uislamu na wakatutaka na sisi pia tuachane na dini. Hao ni maadui wa dini yetu na aqida yetu na wao kwa hakika wanataka tuangamie kama wao na wanatuhusudu kwa imani zetu. Na tujue ya kuwa hakuna kufaulu ila kwa kushikana na dini hii, ni hakika iliyothibitishwa katika kitabu cha Allah na sunnah za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). na hatuna shaka yoyote isipokuwa tunaogopea baadhi ya vijana wa kiislamu kwa kuhadaika nao.

Ndugu Muislamu, angalia jamii ya kiislamu utaona ndio wenye wagonjwa kidogo na wenye uhalifu kidogo na ndio wenye maisha mazuri zaidi, na ukitaka mfano ni uangalie miji mikubwa ya kenya, Nairobi na Mombasa kuna tofauti, Nairobi uhalifu ni mwingi kuliko Mombasa na Serikali kuu iko Nairobi, makao makuu ni Nairobi na ni kwa nini kuwa hivyo, hii ni sababu Waislamu kule ni kidogo.

Kuna watu wanaofahamu Ibada Kimakosa.

Kuna watu wamefahamu ibada kimakosa wakapotea na wakapoteza watu wengine, na watu hao wako **sampuli tatu:-**

Sampuli ya kwanza: ni waliofahamu ibada nusu nusu na wakaona ibada ni mtu kuswali, kufunga, kutoa zaka na kwenda kuhiji. Mtu huyo huingia Msikitini na akitoka huamiliana kwa riba na mke wake na watoto wake huzunguka uchi, huamini mengine na hukanusha mengine Mola anatuambia katika mafhuum ya Aya:

قال الله تعالى : ﴿أَفَتُؤۡمِنُونَ بِبَعۡضِ ٱلۡكِتَٰبِ وَتَكۡفُرُونَ بِبَعۡضٖۚ فَمَا جَزَآءُ مَن يَفۡعَلُ ذَٰلِكَ مِنكُمۡ إِلَّا خِزۡيٞ فِي ٱلۡحَيَوٰةِ ٱلدُّنۡيَاۖ وَيَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ يُرَدُّونَ إِلَىٰٓ أَشَدِّ ٱلۡعَذَابِۗ وَمَا ٱللَّهُ بِغَٰفِلٍ عَمَّا تَعۡمَلُونَ ٨٥﴾ [البقرة: ٨٥].

{{Munaamini baadhi ya kitabu na mnakufuru baadhi yake, hayakuwa malipo ya mwenye kufanya hivyo ila ni khizaya kaika uhai wa duniani na siku ya qiyama watarejeshwa katika adhabu kali na Mungu si Mwenye kughafilika kwa mambo wanayoyafanya}}.

Sampuli ya pili: ni ya watu ambao wanaabudu asiyekuwa Mungu na kumtegemea asiyekuwa Mungu na anaitakidi ya kuwa kuna watu Maaqtaada na Maautaada na Maabdaali wanaopelekesha ulmwengu na mambo yake, Anasema Mungu katika mafhuum ya Aya:

قال الله تعالى : ﴿قُلۡ إِنَّ ٱلۡأَمۡرَ كُلَّهُۥ لِلَّهِۗ﴾ [آل عمران: ١٥٤].

{{Sema mambo yote ni ya Mungu}}.

Na wengine wanasema: sisi usiku tunamsherehekea Walii fulani ambaye ukiwa hata baharini atakuitikia. Allah (Subhaanahu wa Taala) Anawaambia katika mafhuum ya Aya:

قال الله تعالى : ﴿أَمَّن يُجِيبُ ٱلۡمُضۡطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكۡشِفُ ٱلسُّوٓءَ وَيَجۡعَلُكُمۡ خُلَفَآءَ ٱلۡأَرۡضِۗ أَءِلَٰهٞ مَّعَ ٱللَّهِۚ﴾ [النمل:٦٢]

{{Ukipatikana na madhara hukuna mwenye kuondosha isipokuwa Yeye}}.

Sampuli ya tatu: ni watu ambao ibada zao wanafanya kwa ajili ya Mungu, lakini ibad zao wanazifanya kwa njia ambayo hajafundisha Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). Basi ibada za watu hao wanarejeshewa wenyewe, kwani Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) ametuambia ya kuwa katika maana ya hadithi yake: [Mwenye kuzusha katika jambo letu (dini yetu hii) jambo ambalo si katika dini, basi jambo hilo litarudishwa]. Hadithi hii imepokewa na Bukhari kutoka kwa 'Aisha. Watu kama hawa wanapoteza muda wao bure na wataenda kupata hasara siku ya kiyama.

Kufa ndio mwisho wa mtu kufanya Ibada.

Kwani Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Anatuambia katika maana ya Aya:

قال تعالى ﴿وَٱعۡبُدۡ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأۡتِيَكَ ٱلۡيَقِينُ ٩٩﴾ [الحِجر:٩٩]

{{Na umuabudu Mola wako mpaka ikujilie wewe yakini (kifo)}}.

Na hii inamaanisha kuwa hukuna muda maalumu ila ni kuondoka katika hii dunia. Na kufa ndio ule uhakika ambao ni mchungu, na watu kimaumbile yao huwa hawataki kufa. Allah (Subhaanahu wa Taala) Anatuambia katika maana ya Aya:

قال تعالى: ﴿كُلُّ نَفۡسٖ ذَآئِقَةُ ٱلۡمَوۡتِۗ﴾ [الأنبياء: ٣٥]

{{Kila Nafsi itaonja mauti}}.

Na neno la yakini katika maana ya Aya iliyotangulia linakusudiwa Mauti, kama alivyopokea Bukhari neno lake Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alipokufa 'Uthman ibn Madh-uuni: [Hakika imemjilia yeye yakini, lakini tunaamtarajia kheri kwa Mungu]. Hapo ndio tunajua kuwa maana ya yakini ni mauti

Na vile vile, kikundi cha Maswahaba na Tabiina wametafsiri ya kuwa "yakini" ni mauti kama vile Ikrima na Qataada. Na pia Aya nyingine Allah akituelezea kuhusu watu wa motoni, Allah atuepushe na moto. Akisema katika maana ya Aya:

قال تعالى: ﴿مَا سَلَكَكُمۡ فِي سَقَرَ ٤٢ قَالُواْ لَمۡ نَكُ مِنَ ٱلۡمُصَلِّينَ ٤٣ وَلَمۡ نَكُ نُطۡعِمُ ٱلۡمِسۡكِينَ ٤٤ وَكُنَّا نَخُوضُ مَعَ ٱلۡخَآئِضِينَ ٤٥ وَكُنَّا نُكَذِّبُ بِيَوۡمِ ٱلدِّينِ ٤٦ حَتَّىٰٓ أَتَىٰنَا ٱلۡيَقِينُ ٤٧﴾ [المدثر:٤٢-٤٧].

{{Ni jambo gani lililowatia katika moto wa saqar?, watasema tulikuwa hatuswali na tulikuwa hatulishi maskini na tulikuwa tukizungumza pamoja na wenye kuzungumza na tulikuwa tukikanusha siku ya malipo mpaka ikatujilia sisi yakini}}.

Mwisho

Tumeona katika yaliyotangulia ya kwamba ibada sio ile iliyowekewa wakati na sehemu kama swala na hija, bali hata chakula unachokula au kulisha mkeo na watoto wako huwa ni ibada na wapata thawabu.

[10] KUJILAZIMISHA NA SUNNA YA MTUME (Swalla Llahu 'alayhi wasallam)

Lengo la Khutba:

1. Kubainisha mapenzi ya kweli kwa Mtume rehma na amani zimfikie.
2. Kubainisha ya kwamba ibada haikubaliwi mpaka iende sawa na mafunzo sahihi ya bwana Mtume rehma na amani zimfikie.
3. Kubainisha kwamba maana ya kushuhudia kwamba Muhammad ni Mtume wa Mungu ni kumfuata Mtume.
4. Kubainisha faida za kushikamana na Sunna.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Shukrani za dhati ni za Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Bwana wa viumbe vyote. Na rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad. Ama baada ya hayo, Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, Maswali yafuatayo yafaa tujiulize:

- Ni nani kati yetu ambaye hapendi apendwe na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam)?
- Ni nani kati yetu ambaye hampendi Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam)?
- Ni nani kati yetu ambaye hatarajii kuwa pamoja na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam)?
- Ni nani kati yetu ambaye hatarajii maombezi ya Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam)?

Jawabu ni kuwa hakuna mtu asiyetaka yote tuliyoyataja. Na njia ya pekee ya kutufikisha kumpenda yeye ni kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Na miongoni mwa alama za mapenzi ya kweli ya kumpenda Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) ni kumtii na kufuata Sunna zake**.** Mola (Subhaanahu wa Taala) amesema:

قال تعالى: ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ وَأُوْلِي ٱلۡأَمۡرِ مِنكُمۡۖ فَإِن تَنَٰزَعۡتُمۡ فِي شَيۡءٖ فَرُدُّوهُ إِلَى ٱللَّهِ وَٱلرَّسُولِ﴾ [النساء: ٥٩].

{{Enyi mlioamini, Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume wake na viongozi wenu na mukizozana katika jambo lolote liregesheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake}}.

Pia amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿قُلۡ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَٱلرَّسُولَۖ فَإِن تَوَلَّوۡاْ فَإِنَّ ٱللَّهَ لَا يُحِبُّ ٱلۡكَٰفِرِينَ ٣٢﴾ [آل عمران: ٣٢].

{{Sema mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume na mukienda kinyume na hivyo basi Mwenyezi Mungu hawapendi wakanushaji}}.

Katika aya nyingine Amesema tena Mola: (Subhaanahu wa Taala):

وقال : ﴿مَّن يُطِعِ ٱلرَّسُولَ فَقَدۡ أَطَاعَ ٱللَّهَۖ وَمَن تَوَلَّىٰ فَمَآ أَرۡسَلۡنَٰكَ عَلَيۡهِمۡ حَفِيظٗا ٨٠﴾ [النساء: ٨٠].

{{Atakaye mtii Mtume basi amemtii Mwenyezi Mungu na atakaye kwenda kinyume basi hatukukufanya wewe kuwa ni mtunzi wao}}. Na ziko Aya nyingi zenye maana kama haya lakini tulizozitaja zinatosha.

Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam), alituhimiza sana kumtii yeye katika hadithi nyingi sana. Miongoni mwa hadithi hizo; Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema : [Nawausia uchaji Mwenyezi Mungu na kusikiliza na kutii na hata akiwa kiongozi wenu ni mtumwa. Na atakayeishi katika nyinyi ataona tofauti nyingi, basi shikamaneni na Sunna yangu na Sunna ya makhalifa wema waongofu, ishikeni kwa magego].

Pia Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema tena: [Umma wote utaingia peponi isipokuwa atakayekataa kuingia peponi. Maswahaba wakamuuliza: Ni nani atakayekataa ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) : Atakaye nitii mimi ataingia peponi na atakayeniasi basi atakuwa amekataa].

Katika maneno ya maswahaba juu ya kushikamana na Sunna. Amesema Ibn Khatwab alipokuwa akilibusu Hajar Aswad (jiwe jeusi): "Hakika mimi najua wewe ni jiwe hunufaishi wala hudhuru, na lau nisingelimuona Mtume akikubusu basi nisingelikubusu."

Ndugu katika imani! Ningependa kuchukua fursa hii adhimu kuwatajia faida anazopata Muislamu endapo atashikamana na Sunna za Bwana Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). Na miongoni mwa faida hizo;

1. Kushikamana na Sunna ni kinga na hifadhi ya Waislamu wasifarikiane kwani ndiyo ambayo huleta mshikamano baina ya waumini na kuwa watu hawafarakani madamu watashikamana kwao na Sunna ya Bwana Mtume rehma na amani zimfikie.
2. Faida ya pili ya kushikamana na sunna ni kuokoka na kipote kipotofu kitakacho kwenda motoni. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Jua ya kwamba waliokuwa kabla yenu waliopewa kitabu waligawanyika mapote sabini na mbili, na umma huu utagawanyika vipote sabini na tatu, vipote sabini na mbili vitaenda motoni na kimoja pekee ndicho kitakachoenda peponi nacho ni kinachoshikamana na Sunna].
3. Faida nyengine ya kushikamana na Sunna ni kupata uongofu na kusalimika na upotofu. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Enyi watu, hakika mimi nimewaachia kitu mutakaposhikamana nacho hamtapotea milele: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna yangu]. Kwani kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Bwana Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) vinamuongoza aliyeshikamana navyo.
4. Miongoni mwa faida za kushikamana na sunna ni kwamba mtu atakaposhikamana na Sunna ataingia katika kundi la Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). Anahadithia Anas Ibn Malik Mwenyezi Mungu awe radhi naye, ya kwamba walikuja watu watatu katika nyumba za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam).

Wakaulizia ibada ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Wakaelezewa ibada yake basi waliiona kidogo sana. Wa kwanza akasema: Mimi nitaswali usiku kucha milele wala sitolala. Wa pili akasema : Mimi nitafunga siku zote na wala sitokula hata siku moja. Wa tatu akasema: Mimi nitajiepusha na wanawake milele sitaoa. Alipokuja Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akaelezewa kuhusu maswahaba wale akawaambia: [Nyinyi ndio mliosema hivi na hivi na hivi? Ama mimi naapa kwa Mwenyezi Mungu ya kwamba mimi ni mchaji Mwenyezi Mungu zaidi pamoja na hivyo, mimi naswali usiku nalala nafunga na siku nyingine nala na vile vile naoa wanawake. Basi anayejiepusha na mwenendo wangu si katika mimi]. Na kujiepusha na Sunna ya Mtume inaweza kuwa maasi au ni ukafiri, tunamuomba Mwenyezi Mungu atulinde na ukafiri. Na mtu atakapoacha Sunna kwa kuipuuza na kuipinga na kuikosoa atakuwa ameikosoa Dini na kuikosoa Dini ni katika sampuli za ukafiri.Tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) na ukafiri.

Na endapo mtu ataacha Sunna kwa uvivu, sio kwa njia ya kuikosoa basi ni kulingamana na Sunna yenyewe, ikiwa ni jambo la wajibu, atapata dhambi kwa kuacha wajibu na akiacha lililopendekezwa atakuwa amepitwa na fadhila kubwa kabisa.

KHUTBA YA PILI

Faida za Kushikamana na Sunna.

Shukrani zote zamstahiki Allah (Subhaanahu wa Taala) Mola wa viumbe wote. Na rehma na amani tunumuombea kipenzi chetu Mtume Muhammad mbora wa viumbe vyote.

Nikiendelea kuzitaja faida za kushikamana na Sunna;

1. Ni kuepukana na njia za shetani. Katika hadithi, swahaba Ibn Mas’uud, Mwenyezi Mungu amuwie radhi, amesema: “Alituchorea Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) msitari mmoja kisha akasema hii ndio njia ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) kisha akachora vijisitari kuliani mwa msitari, ule na kushotoni kisha akasema huu msitari mmoja ni njia yangu na vijisitari hivi katika kila kijisitari kuna sheitani awalingania watu kwenye njia ya motoni na upotofu. Kisha akasoma Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) Aya hii:

قال تعالى : ﴿وَأَنَّ هَٰذَا صِرَٰطِي مُسۡتَقِيمٗا فَٱتَّبِعُوهُۖ وَلَا تَتَّبِعُواْ ٱلسُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمۡ عَن سَبِيلِهِۦۚ ذَٰلِكُمۡ وَصَّىٰكُم بِهِۦ لَعَلَّكُمۡ تَتَّقُونَ ﴿١٥٣﴾﴾ [الأنعام: ١٥٣].

{{Na hii ndio njia yangu iliyonyooka ifuateni, wala msifuate vijinjia mtapotea na njia yake Mwenyezi Mung}}.

2. Miongoni mwa faida za kushikamana na Sunna ni kuitekeleza sheria na dini ya Mwenyezi Mungu, kwani Sunna humfanya Muislamu kutekeleza sheria bila ya kupunguza wala kuzidisha. Hii ni kuonesha kuwa sunna imekusanya dini yote.
3. Ni katika faida za kushikamana na Sunna kuondosha udhalili na unyonge kwa mtu, kwani udhalili na madhila wanayoyapata Waislamu popote walipo ni

kwa sababu ya kuacha kwao Sunna ya Bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

4. Miongoni mwa faida za vile vile ni kwamba katika Sunna kumetajwa ugonjwa na dawa pale Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alipotaja ugonjwa wa kutofautiana Waislamu kisha akataja dawa yake ambayo ni kushikamana na Sunna yake na Sunna ya makhalifu wema waongofu.

5. Miongoni mwa faida ya kushikamana na sunna ni kupambika mtu na tabia njema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Hakika nimetumilizwa kukamilisha tabia njema]. Amesema Ibn Abdulbar: Hadith hii ameizungumza Madina na ni sahihi na ina maana ya kutengenea na kheri zote dini na dunia - ubora, utu, wema nadhifu- ni katika tabia njema za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Na kwa haya yote ametumilizwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) ayatimize.

Mwisho

Nikimalizia kutaja faida za kushikamana na Sunna ni kuokoka na misukosuko na adhabu kali. Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

قال تعالى : ﴿فَلْيَحْذَرِ ٱلَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِۦٓ أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦٣﴾﴾ [النور: ٦٣].

{{Na watahadhari wanaokwenda kinyume na amri ya Mtume, isije ikawapata wao misukosuko, au wapate adhabu inayoumiza}}. Mwisho kabisa nawausia ndugu zangu kushikamana na Sunna ya Bwana Mtume na huko ndio kutengea nafsi na kutengenea nafsi yako ni kutengenea familia, na kutengenea familia ni kutengenea jamii na kutengenea kwa jamii ni kutengenea kwa ujumla.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Atuongoze katika njia ya sawa na atujaaliye ni wenye kushikamana na Sunna mpaka mwisho wa uhai wetu.

[11] KUTAHADHARI NA UZUSHI KATIKA DINI

Lengo la Khutba:

1. Kubainisha hatari ya uzushi katika dini.
2. Kutahadhari watu kuzua katika dini.
3. Kubainisha baadhi ya sababu za uzushi katika dini.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Shukrani za dhati ni za Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Aliyesema:

قال تعالى: ﴿ٱلۡيَوۡمَ أَكۡمَلۡتُ لَكُمۡ دِينَكُمۡ وَأَتۡمَمۡتُ عَلَيۡكُمۡ نِعۡمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ ٱلۡإِسۡلَٰمَ دِينٗاۚ﴾ [المائدة: ٣].

{{Leo nimewakamilishieni Dini yenu na nimewatimizia neema yangu na nimewaridhia kuwa Uislamu ndio Dini yenu}}. Na rehma na amani zimfikie Mtume wetu aliyesema: [Atakayezusha katika jambo letu hili (Dini) ambalo si katika dini atarudishiwa mwenyewe].

Enyi waumini ! Mcheni Mwenyezi Mungu Ambaye amemtumiliza Mtume Muhammad pale walipokuwa watu wako katika upotofu wa ushirikina na kufuata dini ya baba zao potofu. Akawatoa katika ushirikina na kuwaleta katika Uislamu (Dini ya haki). Kwa Kweli, Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alisubiri mengi maovu aliyotendewa na waovu mpaka Dini ikakamilika.Pia aliweza kuwatahadharisha watu na kufuata hawaa zao na kuzusha katika Dini ya Mwenyezi Mungu baada ya kuondoka yeye.

Kwa kweli uzushi katika dini ulianza punde tu baada ya kuondoka Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam), kwani vipote vingi vilizuka kwa sababu ya watu kuacha Sunna ya Bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) na kufanya mambo bila ya elimu na kufuata matamanio ya nafsi. Na mfano wa vikundi hivyo ni Muutazila, Masufi, Khawaarij, Murjia na vikundi vyengine. Kuna ushahidi mwingi wa kushikamana na sunna na kujiepusha na bidaa. Mola (Subhaanahu wa Taala) amesema:

قال تعالى: ﴿قُلۡ إِن كُنتُمۡ تُحِبُّونَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُونِي يُحۡبِبۡكُمُ ٱللَّهُ وَيَغۡفِرۡ لَكُمۡ ذُنُوبَكُمۡ﴾ [آل عمران: ٣١].

{{Sema: ikiwa mnampenda Mwenyezi Mungu nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu Atawapenda na Atawasamehe dhambi zenu}}.

Pia Mola amesema:

قال تعالى: ﴿وَمَآ ءَاتَىٰكُمُ ٱلرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَىٰكُمۡ عَنۡهُ فَٱنتَهُواْۚ﴾ [الحشر: ٧].

{{Atakachowapeni Mtume kichukueni na atakachowakataza jiepusheni nacho}}. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) asema: [Atakayezusha katika Dini yetu hii jambo ambalo halimo katika Dini basi atarudishiwa mwenyewe]. Vile vile Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) asema katika hadithi yake: [Anayejiepusha na sunna yangu si katika mimi]. Na katika hadithi nyingine Mtume anasema: [Hakika Mwenyezi Mungu Anaizuia toba ya kila mzushi mpaka

ache uzushi], “[Jiepusheni na kuzusha mambo (katika dini) kwani kila uzushi ni upotofu]. Inatakiwa waumini washikamane na Sunna na wajiepusha na uzushi katika Dini. Kwani ndiko kumkubali kikamilifu Bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam), na pia kumtii yeye. Wala haifai kwa Muislamu kwenda kinyume na Sunna ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Ametahadharisha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) hilo aliposema:

قال تعالى : ﴿ فَلْيَحْذَرِ ٱلَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِۦٓ أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦٣﴾ ﴾ [النور: ٦٣].

{{Na wajitadhari wanaokhalifu amri ya Mtume wasije wakapata fitna au adhabu kali}}. Vilevile, Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Anasema:

قال تعالى : ﴿ وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥٓ أَمْرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ ٱلْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَن يَعْصِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَٰلًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾ ﴾ [الأحزاب: ٣٦].

{{Haitakiwi Muislamu, mwanamume wala mwanamke atakapo amua jambo Mwenyezi Mungu na Mtume wake wawe na khiari kulifanya na atakaye muasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi amepotea upotevu wa wazi kabisa}}. Aya hizi zanaonesha kwamba yoyote atakayemuasi Mola na Mtume atakuwa katika upotevu na kupata adhabu kali ya Mwenyezi Mungu

Ndugu Muislamu kwenda kinyume na Sunna ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam), ni sababu ya kufarakana Waislamu katika Dini na kupotoka upotevu ulio wazi, Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ وَأَنَّ هَٰذَا صِرَٰطِى مُسْتَقِيمًا فَٱتَّبِعُوهُ ۖ وَلَا تَتَّبِعُوا۟ ٱلسُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِۦ ۚ ﴾ [الأنعام: ١٥٣].

{{Hakika njia yangu hii ifuateni wala msifuate vijinjia mtapotea katika njia ya Uislamu}}. Vilevile, kukhalifu Sunna ni sababu ya mtu kufuata matamanio ya nafsi. Mola (Subhaanahu wa Taala) ametutahadharisha kufuata matamanio kwa kusema:

قال تعالى : ﴿ أَفَرَءَيْتَ مَنِ ٱتَّخَذَ إِلَٰهَهُۥ هَوَىٰهُ ﴾ [الجاثية: ٢٣].

{{Je wamjua anaye yafanya matamanio yake kuwa ni mola wake}}. Na wanaofuata matamanio ni wale ambao Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Aliwataja kwa kusema:

قال تعالى : ﴿ أُو۟لَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ طَبَعَ ٱللَّهُ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ وَٱتَّبَعُوٓا۟ أَهْوَآءَهُمْ ﴿١٦﴾ ﴾ [محمد:١٦].

{{Hao ni wale ambao Mwenyezi Mungu amepiga muhuri katika nyoyo zao na wakafuata matamanio yao}}.

Uzushi katika Dini, Mtume ameuita kuwa ni upotofu kwa sababu mzushi amepotea kwa kufuata matamanio. Tusisahau Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alikuwa akijilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na tabia mbaya, na kufuata matamanio ya moyo. Enyi waja wa Mwenyezi Mungu ! Haifai kwa mtu yeyote kuleta maoni yaliyo kinyume na Sunna ya Bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Amesema ‘Abdillahi Ibn ‘Abbas: “ Atakayeleta maoni ambayo hayapo katika kitabu cha Mwenyezi Mungu wala hadithi za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) kwani hajui yatakayompata yeye atakapo kutana na Mwenyezi Mungu (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

Jueni kuwa mzushi ni dhalili na pia ana hasira za Mwenyezi Mungu aliyetukuka. Amesema Imam Shatwiby, Mwenyezi Mungu amrehemu: “Hakika mzushi atavishwa udhalili duniani na hasira za Mwenyezi Mungu”. Na hii ni kwa neno la Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Aliposema**:**

قال تعالى : ﴿ إِنَّ ٱلَّذِينَ ٱتَّخَذُواْ ٱلۡعِجۡلَ سَيَنَالُهُمۡ غَضَبٞ مِّن رَّبِّهِمۡ وَذِلَّةٞ فِي ٱلۡحَيَوٰةِ ٱلدُّنۡيَاۚ وَكَذَٰلِكَ نَجۡزِي ٱلۡمُفۡتَرِينَ ١٥٢ ﴾ [الأعراف: ١٥٢].

{{Hakika waliofanya kijing’ombe kwa muabudiwa watapata hasira za Mola wao na udhalili duniani na vile vile tunawalipa wazushi}}.

Adhabu hii itakuwa pia kwa wale wanaofanana nao kitabia kwani uzushi ni kumsingizia Mwenyezi Mungu. Asema Imam Malik Mwenyezi Mungu amrehemu: “ Atakayezusha katika Uislamu uzushi, akauona uzushi huo ni mzuri basi amedai ya kwamba Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amefanya khiana katika ujumbe, kwani Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema**: “** Leo nimewakamilishia Dini yenu”. Kwa hivyo, lile ambalo halikuwa siku hiyo Dini basi leo haliwi dini’.

Na ameweka bayana Mtume kama ilivyo katika sahihi Muslim kwamba wazushi watasogea katika birika la Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) na watafukuzwa kwa sababu ya uzushi wao unamaliza Dini sahihi ya Mwenyezi Mungu.

KHUTBA YA PILI

Sababu za Uzushi katika Dini.

Ndugu zangu katika imani ! Napenda kutaja miongoni mwa sababu za uzushi katika dini.

1. Kufuata matamanio ya nafsi zao na kuacha Sunna Sahihi za Bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Amesema mwanachuoni Muqaatil Ibn Hayan: ‘Watu wa matamanio ni maangamivu kwa umati Muhammad hali ya kuwa wanamtaja Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) na jamaa zake wakitaka kuwavutia kwa utajo huu mzuri, watu wasiojua chochote katika Dini na kuwatia katika maangamivu, na hao wamefanana zaidi na wanaotia sumu katika asali’.
2. Kufuata baba zetu bila ya uongofu. Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema pale Nabii Ibrahim alipowaambia watu wake:

   قال تعالى : ﴿ قَالُواْ نَعۡبُدُ أَصۡنَامٗا فَنَظَلُّ لَهَا عَٰكِفِينَ ٧١ قَالَ هَلۡ يَسۡمَعُونَكُمۡ إِذۡ تَدۡعُونَ ٧٢ أَوۡ يَنفَعُونَكُمۡ أَوۡ يَضُرُّونَ ٧٣ قَالُواْ بَلۡ وَجَدۡنَآ ءَابَآءَنَا كَذَٰلِكَ يَفۡعَلُونَ ٧٤ ﴾ [الشعراء: ٧١:٧٤]

   {{Je mnaabudu nini? Wakasema tunaabudu masanamu na hatuachi kulazimiana nayo, akasema: Je wanawasikia mnapowaomba au wanawanufaisha au wanawadhuru, wakasema: Tumewapata baba zetu wakifanya hivyo}}.
3. Kufuata maneno ya wanavyuoni yanayokwenda kinyume na mafunzo mazuri na sahihi ya Uislamu.

Madhara ya Uzushi

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu uzushi una madhara mengi ambayo yatakiwa tuyajue. Na katika madhara hayo ni:-

1. Uzushi huangamiza dini sahihi huku ukichukua nafasi ya Sunna. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Hawatazua watu uzushi isipokuwa ataondoa Mwenyezi Mungu kwao Sunna mfano wake].
2. Ufisadi wa uzushi ni kujiepusha mtu na Sunna na akawa mtu hataki kuzifanya sunna akawa na bidii kutekeleza uzushi, na kumbe anapoteza nguvu zake na pia wakati wa huku akiaona kuwa Dini ni pungufu akitaka kuikamilisha dini na uzushi wake.
3. Uzushi unarejesha watu katika jahiliya kwa kuwafanya watengane wawe mbali mbali, kila kikundi kinafurahia msimamo wake. Mola (Subhaanahu wa Taala) amesema:

   قال الله تعالى : ﴿كُلُّ حِزۡبِۭ بِمَا لَدَيۡهِمۡ فَرِحُونَ ٣٢﴾ [الروم: ٣٢]

   {{Kila kikundi kinafurahia msimamo wake}}. Kwani Sunna inafanya watu kuwa kitu kimoja. Mola Asema:

   قال تعالى : ﴿وَٱعۡتَصِمُواْ بِحَبۡلِ ٱللَّهِ جَمِيعٗا وَلَا تَفَرَّقُواْ﴾ [آل عمران: ١٠٣]

   {{Shikamaneni na Dini ya Mwenyezi Mungu wala msifarakane}}.
4. Uzushi unasababisha kuikataa haki anapolinganiwa mzushi katika Sunna hakubali na natija yake huendelea kushikamana na uzushi wake.
5. Uzushi unaharibu Dini sahihi ya Mwenyezi Mungu, kwani uzushi ndio silaha kubwa ya kuharibu Dini ya Mwenyezi Mungu. Kwani wengi katika wazushi hutaka maslahi ya kidunia katika ulinganizi wao.

Mwisho

Ndugu Waislamu ! Maswahaba walikuwa wakiwatahadharisha watu na uzushi katika Dini. Ilimfikia Ibn Mas’uud kuwa ‘Amru ibn ‘Utba ambaye ni katika wafuasi wake amejenga Msikiti mjini Kuufa akaamrisha Ibn Mas’uud uvunjwe Msikiti ule, kisha akasikia sasa wanajikusanya nje ya Msikiti huo wakileta nyiradi na adhkaar na takbira maalum kinyume na mafunzo mazuri ya bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Alifunga safari Ibn Mas’uud akawajia wao hali ya kuwa amejifunika uso wake ili wasimjue, kisha akakaa nao wakaanza kuleta adhkaar zao, kisha akafungua uso wake, kisha akawauliza mumekuwa wajuzi wa dini zaidi kuliko maswahaba wa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam), Kisha akawaonya watu hao na uzushi, na hapo hapo watu waliomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu kwa uzushi wao waliokuwa wakiufanya. Enyi mliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume ! Muogopeni Allah (Subhaanahu wa Taala), na mujue ya kwamba yaliyothibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) yanamtosha Muislamu katika maisha yake wala asijishughulishe na chochote cha uzushi. Na wausia mshikamane na Sunna kisawasawa.

Mwisho kabisa tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie ni miongoni mwa mwenye kushikamana na Sunna na kijiepusha na uzushi na atuongoze katika Dini Yake ya sawa.

[12] FADHILA ZA SIKU KUMI ZA MWEZI WA MFUNGO TATU

Lengo la Khutba:

1. Kueleza kwa uwazi kuwa Allah (Subhaanahu wa Taala) Anaumba Atakacho na Anachagua
2. Kuwakumbusha watu msimu wa kheri wa kufanya amali njema umefika ili waupatilize
3. Kueleza ubora na thawabu zinazopatikana katika siku kumi hizi
4. Kubainisha rehema ya Allah (Subhaanahu wa Taala) ni pana ili waja wa Allah waingie katika rehma.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Mwenyezi Mungu Alipomuumba mwanadamu ili aje afanye ibada na Akaumba Pepo na Moto, kwa mwenye kutwii na mwenye kuasi. Akawawekea misimu ya ibada nyakati mbalimbali ili wazidishe thawabu waingie peponi kwa usahali.

Allah Anaumba na Kuchagua

Ama baada ya kumshukuru Allah (Subhaanahu wa Taala). Enyi Waislamu muogopeni Allah Ambaye Anaumba na kuchagua, kwa mfano ameumba mbingu na Ardhi na akajichagulia mbingu ya saba na Makka pakawa ni patakatifu akaumba pepo na Malaika, akaifanya firdausi ndio pepo ya juu zaidi, na Jibril ndiye kiongozi wa Malaika na katika mwaka akaweka miezi, siku, nyakati za siku na saa. Akachagua mwezi mtukufu wa Ramadhani, siku bora ni Ijumaa, usiku mtakatifu ni Lailatul Qadri, na saa ya kukubaliwa dua ipo Ijumaa na masiku matukufu yapo kwenye siku kumi za mwanzo wa mfungo tatu. Allah akawaumba wanadamu, akawachagua aliowathamini ni muuminina, na akawachagua katika muuminina mitume, akawapandisha cheo mitume fulani, akaita rusul, na katika rusul akawapandisha wengine wanajulikana ulul–'azm, na katika hao akatubainishia vipenzi vyake, na bila shaka katika vipenzi vya Allah kiongozi wao ni Mtume wetu Muhammad (Swalla Llahu 'alayhi wasallam).

Mu'min anaishi akiwa amebarikiwa

Muislamu alibarikiwa na Mwenyezi Mungu, aliwekewa madaftari mawili, moja kuandikiwa mazuri yake na jengine kuandikiwa mabaya yake. Ama kafiri aliwekewa daftari moja tu analoandikiwa mabaya tu. Ni juu ya Muislamu awe na lengo la kwenda peponi ajizatiti kiibada kila zama na awe na malengo kwa kila msimu, kwani Mola na Mtume walitueleza siri hiyo. Mungu (Subhaanahu wa Taala) amesema:

قال تعالى: ﴿مَن جَآءَ بِٱلۡحَسَنَةِ فَلَهُۥ عَشۡرُ أَمۡثَالِهَاۖ﴾ [الأنعام: ١٦٠]

{{Mja akifanya jema nitamlipa kwa hisabu ya mema kumi}}. Na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akaongezea: [Hata kama hakulifanya hilo jema

lakini alitia nia pia atalipwa thawabu. Na aliyetia nia ya ubaya na akalifanya hilo ataandikiwa alifanya ubaya moja na Mwenyezi Mungu hamwangamizi ila atakayekuangamia]. Hivi ina maana ya kuwa twa-a ya Muislamu kwa Mola Muumba ina baraka kote kote, katika matamshi na vitendo vyake, ulimi wake umtaje Allah na kutaja mazuri mpaka kufa kwake, na yeye afanye mema mpaka awe na mwisho mwema. Maneno haya yametafsiriwa na swahaba, Maliki Ibn Swa'aswaa alikuwa akisema: "Vitendo vitano vya Muislamu, atalipwa malipo ya vitendo hamsini na saumu ya Ramadhani moja atalipwa miezi kumi, na siku sita za mwezi wa Shawwal, kila siku moja atalipwa siku kumi, kwa hivyo mwenye kufunga Ramadhani na siku sita za Shawwal ni kama aliyefunga mwaka."

Ama sadaka, Mola atampa daraja mtoaji mpaka daraja mia saba. Na hijja isiyokuwa na makosa, malipo yake ni ya juu sana isipokuwa kustahiki Pepo. Twaa ni kisafisho cha kujisafishia dhambi, kama Mtume alivyofananisha swala na kuoga mara tano, jee atabakiwa na uchafu? Na kila ibada ina baraka zake.

Zama zenye Baraka zaidi kiibada ni Siku Kumi za Mfungo Tatu

Allah (Subhaanahu wa Taala) anavyotupendelea tupate thawabu zaidi, alitudokezea kuwa kuna siku kumi ambazo ni muhimu sana na akaziapia nazo, na Allah huapia kwa viumbe vitukufu au nyakati tukufu, au Ardhi tukufu. Kama mbingu na Ardhi, Alfajiri na Alasiri, au Makkah au akaapa kwa chochote Alichoumba.

Fadhila za Siku Kumi za Mfungo Tatu

1. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Alikutanisha ibada tukufu zaidi kwa wakati mtukufu zaidi, kwa mfano swalatul fajri na swalatul asri kwa nyakati zake ambapo wanakutana Malaika wa vipindi viwili na kuchanganikana na waumini, ndio Anaapa kwa Alfajiri na Anaapa kwa Alasiri. Mwenyezi Mungu Amezitukuza siku kumi hizi, ndani imo siku ya 'Arafa, siku ya idd ya kuchinja na kadhalika. Na Amekutanisha swala ya usiku, na Yeye huteremka kila usiku, na Yeye amesema kwamba waja wema ni wale wanaoacha vitanda vyao wakaswali, kwa sababu ya kumuogopa Yeye, na kutaka pepo na mambo yao ya kilimwengu, Nami hapo usiku huwa nikiwauliza haja mbalimbali niwapatie, lakini kuna biri baina yao na shetani. Mmoja katika watu wema amesema: 'Haikubakia ladha ya dunia isipokuwa swala ya usiku, na swala ya jamaa na kutangamana na watu wema'.
2. Ulikamilika uislamu katika siku kumi hizi, ambapo ndani yake kuna ibada mbalimbali na watu wakajitenga na maovu, ilivyokamilika Dini, ndio Sunna ikapata nguvu na bid'a ikavunjika. Allah (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

   قال تعالى: ﴿ٱلۡيَوۡمَ أَكۡمَلۡتُ لَكُمۡ دِينَكُمۡ وَأَتۡمَمۡتُ عَلَيۡكُمۡ نِعۡمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ ٱلۡإِسۡلَٰمَ دِينٗاۚ﴾ [المائدة: ٣]

   {{Leo nimewakamilishia Dini, na nimewatimizia neema yangu}}. Anasema Sahaba 'Umar bin Khatwab: 'Mimi naijua vizuri Aya hii ilipoteremka, iliteremshwa siku ya Arafa, siku ya Ijumaa, maswahaba wengi miongoni

mwetu tukafahamu dini imekamilika na Mtume yuko safarini kuondoka'. Mmoja katika wanavyuoni wa kiyahudi anaelezea umuhimu wa siku hii na kuteremka kwa Aya hii nzito, "Lau kama ni dini ya kiyahudi, siku hii ingekuwa iddi ya kila mwaka."

3. Kabla ya kuhuishwa tena uislamu, kulikuwepo na dini nyingi ambazo ziliwapeleka motoni kama vile ukiristo, uyahudi, umajusi na kadhalika. Lakini ulipohuishwa uislamu, dini zote ziliyayuka na uislamu ndio utakaobaki mpaka Qiyama, na siku hii ya 'Arafa ndio neema ilipotimia na makafiri wakawa wamekatazwa wasiingie Makkah, Waislamu wakazidi kuwa kitu kimoja.
4. Kuna ibada zinazokusanyikana hapa, siku za hija, kuna swala, sadaka, kufunga sunna au kufunga kwa ambaye hakupata kuchinja, kuna dhikri na kadhalika mpaka imalizike hija.
5. Msimu wa ibada wa siku hizi kumi, haupatikani ila kwa mwaka mara moja. Dakika zake, saa, siku na wiki, ndizo zinazompendeza Mwenyezi Mungu, lau mwanadamu atajitahidi kiibada siku hizi, atakuwa amefaulu sana. Kwa hadithi iliyopokewa na Ibn 'Abaas kuwa amesema bwana Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Hakuna siku bora kwa Mwenyezi Mungu anazolipa thawabu nyingi kama siku hizi kumi. Wanafunzi wa Mtume wakamuuliza: hata kwenda jihadi?, Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akawajibu: Hata kwenda jihadi, isipokuwa aliyetoka jihadi na mali yake, akafa huko na mali yake isipatikane ndio atakuwa ana thawabu nyingi kushinda huyu mwenye kufanya amali katika siku kumi]
6. Katika siku hizi kumi, siku ya tisa inajulikana ni siku ya 'Arafa, inajulikana kwa thawabu na msamaha mwingi kutoka kwa Allah, ndio siku waumini wanapeleka dua zao kwa wingi. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Dua bora nzito ni ya siku ya 'Arafa]. Na kwa sababu waumini wengi wameacha machafu yao kwa ajili ya 'Arafa, mahujaji na wasiokuwa mahujaji na ndio siku ya hijja kubwa. Na mwenye kufunga siku hii husamehewa madhambi ya mwaka uliopita na mwaka ujao.
7. Ipo siku ya mwisho, siku ya kumi ya mfungo tatu, inayojulikana kuwa ni siku ya kuchinja, zipo ibada tofauti tofauti, kutupa vijiwe, kunyoa, kutufu, kukimbia baina ya Swafaa na Marwaa, kuchinja na kuswali Iddi.

Fadhila za siku hii ni nyingi. Muislamu anatakikana asizipoteze, bali azipatilize na ashindane katika mambo ya kheri na ajishughulishe kwa amali njema.

KHUTBA YA PILI

Amali zinazokubaliwa kisheria

Baada ya himidi na kumswalia Mtume, katika amali zilizokubaliwa na sheria ni kumtaja Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Allah Anasema:

قال تعالى: ﴿ لِّيَشْهَدُوا۟ مَنَٰفِعَ لَهُمْ وَيَذْكُرُوا۟ ٱسْمَ ٱللَّهِ فِىٓ أَيَّامٍ مَّعْلُومَٰتٍ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّنۢ بَهِيمَةِ ٱلْأَنْعَٰمِ ۖ فَكُلُوا۟ مِنْهَا وَأَطْعِمُوا۟ ٱلْبَآئِسَ ٱلْفَقِيرَ ﴿٢٨﴾ ﴾ [الحج:٢٨]

{{Ili washuhudie katika hija manufaa yao na wamtaje Allah kwa wingi katika siku hizi maalum}}.

Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Katika Siku hizi tukufu mtajeni sana Allah kwa Tahliil na Takbiri na Tahmiid]. Hadith hii imepasishwa na Imam Ahmad.

Maswahaba wengi hasa wale wapokezi wa hadithi, baadhi yao ni Abu Huraira na Ibn ‘Umar, ilikuwa wakiona siku kumi zimeingia wakitoka mpaka sokoni, na wakipiga Takbiri, kila mtu kivyake na wale waliopo sokoni wakiitikia kila mtu kivyake na hapo ikishika kasi kila mtu huendelea na dhikri mbali mbali na wengine wanaendelea kusoma zaidi Qur’an, kwani kumtaja Allah mara kwa mara ndivyo anavyotaka Allah, ni njia ya kufaulu duniani na akhera, na ndio sababu ya kuhifadhika na ukafiri na shetani na moto mpaka Malaika humtaja mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa fulani ni mja mwema. Ndio silaha na amali bora ya kujisafisha na kupandisha daraja na kuongeza thawabu kwa wingi na kusamehewa kwa wingi, na Mizani inakuwa nzito. Kazi yenyewe ni hafifu na huzungukwa na Malaika na fadhila nyingi. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) amezishikanisha Swala na Dhikri, Mola (Subhaanahu wa Taala) Anasema:

قال: ﴿فَإِذَا قَضَيْتُمُ ٱلصَّلَوٰةَ فَٱذْكُرُوا۟ ٱللَّهَ﴾ [النساء:١٠٣]

{{Mukimaliza kuswali mtajeni Mwenyezi Mungu}}.

Na Amezishikaniza swala ya Ijum’aa na Dhikri, Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala):

وقال: ﴿ فَإِذَا قُضِيَتِ ٱلصَّلَوٰةُ فَٱنتَشِرُوا۟ فِى ٱلْأَرْضِ وَٱبْتَغُوا۟ مِن فَضْلِ ٱللَّهِ وَٱذْكُرُوا۟ ٱللَّهَ ﴾ [الجمعة: ١٠]

{{Naitakapokwisha Swala, tawanyikeni katika ardhi mtafute fadhila za Allah na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi}}.

Na ibada ya Hijja na dhikri Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala):

وقال: ﴿فَإِذَا قَضَيْتُم مَّنَٰسِكَكُمْ فَٱذْكُرُوا۟ ٱللَّهَ كَذِكْرِكُمْ ءَابَآءَكُمْ أَوْ أَشَدَّ ذِكْرًا ۗ﴾ [البقرة:٢٠٠]

{{Na mwishapo kutimiza ibada zenu za hijja, basi mtajeni Allah kama mlivyokuwa mkiwataja wazee wenu”, na Saumu Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala):

وقال: ﴿وَلِتُكْمِلُوا۟ ٱلْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُوا۟ ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَىٰكُمْ﴾ [البقرة: ١٨٥]

{{Na kamilisheni hisabu hiyo, na mtukuzeni Mwenyezi Mungu}}.

Kuukaribisha Mwezi wa Mfungo Tatu

Katika amali tukufu ni kuukaribisha mwezi wa hajji kiibada na kujikurubisha kwa Allah na kufunga siku ya Arafa, kama Mtume (Subhaanahu wa Taala) alivyojibu: [Inafuta dhmbi za mwaka uliopita na mwaka ujao].

Kuzidisha Amali za Sunna baada ya kumaliza za Faradhi

Kuswali sana Swala za Sunna baada ya kila faradhi kama Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alivyotufundisha nazo ni rakaa kumi na mbili. Na Swala za usiku nazo ni rakaa kumi na moja na Swala ya Dhuha na Swala nyenginezo. Kuhifadhi Sunna ni sababu ya kupata mapenzi ya Allah na mwenye kufaulu mapenzi yake anamuhifadhi, amjibu dua zake na humpa cheo.

Kutoa Sadaka kwa wingi

Katika siku kumi hizi Muislamu huzidisha kama vile ilivyo kwenye Saumu ya Ramadhani na Iddil adh-ha na mengineyo, kwani sadaka humuongezea thawabu nyingi na humpa kivuli siku ya Qiyama na humfungulia milango ya kheri na milango ya pepo na humpenda yeye Mwenyezi Mungu na humsafisha na madhambi yeye na mali yake na familia yake duniani na akhera.

Kufunga Siku Tisa

Muislamu azidishe kufunga katika siku hizi, sababu ni moja katika amali njema na lau atafunga siku tisa hizi imeruhusiwa na sheria. Imethibiti kuwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alifunga siku ya 'Ashura na akasema atafunga na tisa. Na hapo ndani zipo siku nyeupe na hadithi zilizopokewa kuhusu kufunga huku ni nyingi sana lakini wanazuoni wa hadithi wanasema zikigongana hadithi mbili moja inathibitisha na nyengine inapinga basi tunaitanguliza inayo thibitisha.

Ibada ya Kuchinja

Siku kumi zikianza na mtu anataka kuchinja aendelee na ibada zake kama kawaida na ingawaje hakufika hajj lakini ajihisi yuko katika siku tukufu kwa hivyo asikate kucha, nywele, na kukata chochote kutoka mwilini mwake mpaka baada ya kuchinja mnyama wake, hivi ndivyo ilivyopokewa kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) na maswahaba zake, Mtume alikuwa akichinja wanyama wawili, mmoja ni wake na ukoo wake na mwingine ni wa ummati wake. Mwenyezi Mungu Atujaze sote na Atujaalie sisi ni katika wafuasi wake na atufufue na kundi lake na Atukutanishe naye peponi, yeye Mwenyenzi Mungu ni mpaji. Vilevile, ni muhimu kuzidisha kumswalia Mtume, kufanya hivyo humzidishia Muumini malipo makubwa kama alivyobainisha Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) katika hadithi zake.

Enyi ndugu katika imani, tushindane katika amali njema na dua na kutaka msamaha na tujikurubishe kwa Allah huenda ikawa ndio kufaulu kwetu na tuonyaneni na uvivu na dharau na tupatilize haya masiku. Ewe Mwenyezi Mungu Tuafikie utuongoze kimaneno na kivitendo na hakuna mwenye kutuafikia

isipokuwa wewe. Ewe Mwenyezi Mungu Tuepushie maneno maovu na vitendo viovu na hawaa, na hakuna yeyote mwenye kutuepushia hayo isipokuwa wewe. Ewe Mwenyezi Mungu Tuongoze na utuelekeze kwenye usawa na Anibarikie mimi na nyinyi na aninufaishe mimi na nyinyi kwa Aya na utajo mtukufu na Atunufaishe kwa uongozi wa Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) na maneno yaliyo sawa. Naomba msamaha kwa mola na nawaombea nanyi Waislamu mliobakia, nanyi jiombeeni kwani Mola wetu ni msamehevu sana na mwenye sikitiko.

Mwisho

Ndugu Muislamu, Usighafilike, Mwenyezi Mungu ndiye aliyekuumba hivyo ulivyo na akakuchagulia alichokuchagulia na akakupa nawe nafasi ya kujichagulia vile utakavyo, kuwa na moyo, uchume juani kwa muda mfupi na ukale kivulini kwa muda mrefu kwenye maisha ya milele, Allah ametudokezea misimu tofauti tofauti yenye malipo mbali mbali, kwa mfano, lailatul-Qadri na masiku kumi ya mfungo tatu. Tuzidishe ibada katika siku hizi kumi kwa kuswali, kufunga, kutoa sadaka, kuleta tasbihi, tahlili na mwisho kuswali idd na kuchinja.

Ewe Mweyezi Mungu, tujaalie tuwe waja wema, tupatilize kiibada hizi siku kumi, tufaulu. Na wajaalie waliokwenda hajj waende salama na warejee salama na hizi siku kumi zikiisha tuwe tumekuwa safi, hatuna madhambi. Amiin Wal-hamdulillahi.

[13] KUSOMA QUR’AN NA ADABU ZAKE

Lengo la Khutba:

1. Kueleza fadhila na ubora wa kujifundisha kusoma Qur’an
2. Kutahadharisha watu wasishughulike sana na Dunia mpaka wakasahau Qur’an
3. Kubainisha adabu za kusoma Qur’an.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Ewe Muislamu ulipoumbwa na ukaletwa hapa Duniani uliwekewa katiba na mfumo wa kuishi na njia ya kupita mwanzo mpaka mwisho, nzuri na mbaya, yote hayo utayapata kwenye Qur’an ukifundishwa na Bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

Kusoma Qur’an na Adabu zake

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumtakia rehema Bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) na kutakia radhi Maswahaba na waliokuja baada hao mpaka qiyama.

Ama baadu: mazungumzo yetu ni kuhusu kitabu ambacho ndio msingi wa kufaulu kwenu, chenye kuwatoa kwenye kitua, ndani yake kuna khabari ya waliokuja kabla yenu na watakaokuja baada yenu na hakimu kati yenu, chenye kupambanua baina ya haki na batili. Mwenye kukiacha ameumia, mwenye kutaka uongofu kwa hicho ataongoka, na mwenye kutaka kuongoza na kitabu kingine amepotea; ni kamba ya Allah ya kuaminika isiyokatika; ni utajo wa Mwenyezi Mungu ni njia iloyonyoka, mwenye kuifuata hapotei na mwenye kuifuata hachanganyikiwi. Hawashibi nayo wanavyuoni na maajabu yake hayapungui. Atakaye ukweli ataupata humo na mwenye kuhukumu nacho atahukumu kwa usawa. Matakwa ya Allah ni tuisome Qur’an ili atuongoza na atuingize peponi.

Enyi waumini, Someni Qur’an na muwasomeshe watoto wenu au wenzenu, muwe mumebebwa na mazingira yake, frikra zenu na mawazo yawe katika mazingira ya Qur’an, muwahifadhisha watoto wenu kwa udogoni, kwani mkifanya hivyo, inaifanya igande vizuri zaidi ndani ya nyoyo zao, kwani kuhifadhi udogoni ni kama kutia naqshi kwenye jiwe.

Ewe waja wa Mwenyezi Mungu, Muongopeni Mola na muwe na hamu na Kitabu hiki. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله عز وجل: ﴿ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَتۡلُونَ كِتَٰبَ ٱللَّهِ وَأَقَامُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَأَنفَقُواْ مِمَّا رَزَقۡنَٰهُمۡ سِرًّا وَعَلَانِيَةً يَرۡجُونَ تِجَٰرَةً لَّن تَبُورَ ﴿٢٩﴾ لِيُوَفِّيَهُمۡ أُجُورَهُمۡ وَيَزِيدَهُم مِّن فَضۡلِهِۦٓۚ إِنَّهُۥ غَفُورٌ شَكُورٌ ﴿٣٠﴾ ﴾ [فاطر: ٢٩:٣٠]

{{Hakika wanaosoma hiki Kitabu cha Allah na wakasimamisha swala na wakatoa kwa mali yao tulizowapa kwa siri na dhahiri, wanatarajia biashara isiofilisika, na hakika Allah atawalipa awaongeze, kwani yeye mweyekusamehe saana na ni mwenye kushukuriwa}}. Na mke wa Mtume ‘Aisha akazidi kutufafanulia akisema:

‘Kusoma kwa Qur’an kunatafautiana, kuna anayesoma hodari. Hivyo, thawabu zake ni nyingi kiasi cha kutangamana na Malaika na anayesoma akigongagonga atapata malipo mara mbili. Vilevile Abi Umama akamwambia amemsikia Mtume akisema: [Someni Qur’an, itakufaa siku ya Qiyama kuwaombea shufaa. Haya yote ni fadhila za Qur’an na fadhila za kusoma Qur’an]. Na Mtume wetu (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alimuusia Abu Said akimwambia : [Nakuusia umche Mwenyezi Mungu, kwani hilo ndio kichwa cha kila kitu, na utoke kwenda Jihad kwani hilo ndio daraja kuu la Uislamu na umtaje Mwenyezi Mungu kwa wingi, na usome Qur’an ukifanya hivyo roho yako itakuwa mahali pazuri mbinguni na utakuwa na utajo upo ardhini].

Adabu za kusoma Qur’an

1. Kusoma kwa ajili ya Allah (Subhaanahu wa Taala)

   Waja watalipwa kulingana na nia zao. Mtume anatutolea khabari kuwa watu watalipwa vibaya japokuwa tunawaona wakifanya mema, nao ni sampuli tatu:-

   a. Mtu anajishughulisha na Qur’an kuisoma vizuri, kuikusanya n.k

   b. Mtu aliyeuliwa jihad fi sabilillahi.

   c. Mtu tajiri anaye toa sana.

   Kumbe wote hawa watatu, wanafanya riya, Allah atamwambia msomaji Qur’an: Si nilikufundisha Qur’an? Atajibu: Ndio ewe Mola; baadaye ulifanya nini? atajibu nilikua nikiisoma usiku na mchana, Mwenyezi Mungu atasema: ‘Umesema urongo, na Malaika watazidi kumkaripia ‘muongo we, na watasema Ewe Mola: huyu bwana, alikuwa akisoma kwa ajili ya watu, na tukaachia watu wamlipe kule kule duniani. Mungu atawaamrisha Malaika wamtie motoni (Mwenyezi Mungu atulinde na hayo)

2. Kusoma hali akiwa na utwahara

   Hapana shaka kuyasoma maneno ya Allah ukiwa msafi, ndio bora kama vile kupiga mswaki, kutawadha n.k. Kwa sababu Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Hakika midomo yenu, ndiyo njia za kusoma Qur’an, isafisheni kwa miswaki]. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akasema tena: [Ikiwa mja anaswali, Malaika humjia, na wakamsimamia nyuma yake wakimsikiliza Qur’an na wanaendelea hivyo mpaka anyamaze]. Na je ikiwa mja kinywa chake chanuka? Malaika watakaa kando.

3. Kusoma kisawasawa

   Mola wetu anatuamrisha kuisoma Qur’an na Mtume wetu anatushinikiza hivyo, na maswahaba wakisoma Aya Aya, mmoja wao ni Anas bin Malik Anatuambia Mtume akiwafundisha hata kuvuta Bismillahi na kadhalika. ‘Abdallah bin Masuud amesema, “Kusoma haraka haraka ni mbaya bali ni usome pole pole, ipate kugonga ndani ya moyo, na usimame katika Aya za maajabu, igonge moyo”. Albara amesema: ‘Nimemsikia Mtume akisoma

Wattini Wazzaytuni kwenye Swala ya Ishaa. Sijawahi kusikia sauti nzuri kama hiyo'. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Tengenezeni sauti zenu mnaposoma Qur'an]. Na hizo hadithi ni swahihi. Ni vizuri asome kwa sauti ya kuimbia ya kughani, imepokewa kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Si katika sisi yule mtu atasoma Qur'aan na haghani]. Na kughani kwenyewe ni mume kwa sauti ya kiume na mke ajikaze, sio sauti kuwavutia wengine, na asome asimame kwenye mwisho wa kila Aya kama anavyotueleza mke wa Mtume Ummu Salama.

4. K usoma kwa kwa sauti ya chini

Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alitufundisha, tusisome kwa sauti ya juu, mpaka tukawaudhi wengine. Kwa mfano, wengine wanaswali na majirani wamelala, soma kwa kiasi. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) anatuambia katika maana ya hadithi: "Nyote mtaitwa na mola wenu, msiudhiane wala msipandishiane sauti nyingi na kama mtu anasinzia aache kusoma alale, asije akasoma makosa makosa asijijue, na asiache sura zile fadhila zaidi kama suratul-Ikhlas, ambayo ni theluthi ya Qur'an. Na katika riwaya kadhaa Mtume amekuwa akisema: [Suratul-Ikhlas, ni theluthul ya Qur'an. na alikuwa akisoma Suratul Sajdah na Suratul Insaan katika Sala ya Alfajiri, na Tabaraka na Surat Al-Falaq na An-Nisa kabla ya kulala. Na vile vile akisoma Surat Al-Falaq na An-Nisa na Ayatul-Kursiyu baada ya kila swala].

5. Kukatazwa kusoma Qur'an katika rukuu na Sijida

Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) mwenyewe ametukataza hilo kwenye hadithi swahihi akisema: [Enyi watu, hakukubakia kwenye bishara za mitume isipokua ndoto za watu wema, nami nimekatazwa kusoma Qur'an kwenye rukuu na sijida. Mtukuzeni Allah na mjitah idi kwa dua]. Na sababu yake ametaja Sheikhul-Islam, kukaa rukuu na sijida ni pahali pa kujidhalilisha Muislam kwa Mola wake.

KHUTBA YA PILI

1. Kulia wakati wa kusoma Qur'an

Mola Anasema kulingana na maana ya Aya Akiwasifu waumini ya kuwa; wanaposomewa Qur'an wanapomoka kusujudu huku wanalia na hio linawanazidisha kumcha Mwenyezi Mungu. Maswahaba wengi walikua wakilia kwa sababu ya ucha Mungu na kumfuata Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). Mmoja wao ni Ibnu Mas'uud aliyesema: ' Siku moja Mtume aliniambia nimsomee, nikamjibu kwani Qur'an, inakuteremkia wewe iweje mimi nikusomee?. Mtume akasema: [Napenda nimsikie mtu akisoma. Nikasoma suratul Nisaa mpaka nikafika Aya fulani, nikaona macho ya Mtume yakitoka machozi].

Mmoja katika maswahaba amesema: 'Nilimjia Mtume naye akiwa anaswali na ana kitambaa akijifutia nacho machozi. Na habari mashuhuri kwa Abu Bakr anaposoma Qur'an katika kuwasalisha alikua akilia. 'Umar ibnu Khattwab alipokuwa akisoma Aya, alisikia sauti za kilio na yeye akalia akadondokwa na

machozi. Mke wa Mtume ‘Aisha amewahi kupita sehemu mbalimbali watu wasoma na ukali. ‘Abdullah Ibnu ‘Abbas alikuwa akisoma Qur’an na akirudia rudia na wasikilizaji wakilia.

Kilio wakati wa kusoma Qur’an ni dalili ya kumcha Mwenyezi Mungu ikiwa ni kilio cha kweli, kwani kilio kiko namna nyingi:- kilio cha rahma na sikitiko, kilio cha kumuogopa Allah, kilio cha mapenzi na shangu, kilio cha furaha na kilio cha huzuni. Kilio kinachotakikana ni cha kumuogopa Mwenyezi Mungu na sio cha kinafiki na riya cha kujifanya unamuogopa Allah. Na kilio cha kumuogopa Mungu, yule msikilizaji naye huhisi kumuogopa Mwenyezi Mungu. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Hakika sauti nzuri ya Qur’an ni ukisikia wamuona mwenzio anamuogopa Mwenyezi Mungu].

Ama kujiliza na kujikamua kulia ni sampuli mbili:-

1. Namna imesifiwa nzuri
2. Namna imesifiwa vibaya.
    1. Kusifiwa vizuri, kama alivyojiliza ‘Umar alipomuona Mtume na Abubakar wanalia, alipowauliza sababu, wakachelewa kumjibu, na ‘Umar akakianza chake. Watu wema waliotangulia wanasema: lieni kwa kumuogopa Mwenyezi Mungu au lizaneni.
    2. Ama kilio kinacholaumiwa ni mtu kujifanya mwema mbele ya watu kwa kulia hiki ni kilio cha unafiki. Kwa yote hayo ni Muumini alie anaposoma Qur’an, khabari zikitokana na mama ‘Aisha, amemsikia mmoja kati ya masahaba watukufu akisema yeye kama ni kulia basi ni moja katika aina tatu:-
        1. Akisoma Qur’an na akisikia inasomwa.
        2. Akisikia khutba ya Mtume.
        3. Akiona jeneza.

2. Kuizingatia Qur’aan

Ukisoma Qur’an na ukizingatia, ndio jambo muhimu zaidi ambalo linazaa matunda Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Anasema:

قال الله تعالى: ﴿كِتَٰبٌ أَنزَلۡنَٰهُ إِلَيۡكَ مُبَٰرَكٞ لِّيَدَّبَّرُوٓاْ ءَايَٰتِهِۦ وَلِيَتَذَكَّرَ أُوْلُواْ ٱلۡأَلۡبَٰبِ ٢٩﴾ [ص: ٢٩]

{{Tumeteremsha kitabu kilicho barikiwa, basi kisomeni na mkizingatie enyi mulio na akili}}. Basi tukisome na tukifikirie na tukifahamu vilivyo. Na ikiwa hatuzingatii Mwenyezi Mungu Atatuuliza ilikuaje wasikizingatie ama nyoyo zao zimefungwa, nyuma ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) baada ya Fatiha akaanza Baqarah akarukuu baada ya kumaliza Aya mbili akaanza rakaa nyengine baada ya fatiha akasoma suratul Al-‘Imran na yote hayo, akipita tasbihi, anasabihi, na kadhalika mpaka tukamaliza swala na maswahaba wengi hivi ndivyo wakifahamu na kuizingatia, mmoja ni AbdulRaman anasema, wenzetu wakisoma Qur’aan kwa Mtume baadae wakaendea wenzao, basi wale wenzao wakichukuwa Aya kumi kumi wakienda nazo, baada ya kufahamu na kuzingatia

wakija wakijiongezea nyingine

3. Kusujudu kwa sababu ya kusoma Qur'an

Msomaji akipitia sehemu ya sijda, ni muhimu asujudu. Na wamekhitalifiana wanavyuoni kuhusu jambo hili, Abu Hanifa amesema ni wajibu kusujudu, ama kauli yenye nguvu ni kauli ya 'Umar Ibnu Khatwab, kwamba kusujudu ni sunna na hivyo ndio kauli ya wanavyuoni wengi. Msomaji awe katika hali ya adabu, inafaa asome akiwa amekaa, amesimama, au akitembea na kadhalika. Kama Allah (Subhaanahu wa Taala) anavyosema:

قال تعالى: ﴿ٱلَّذِينَ يَذۡكُرُونَ ٱللَّهَ قِيَٰمٗا وَقُعُودٗا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمۡ وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلۡقِ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِ﴾ [آل عمران: ١٩١].

{{Waja wema wanamtaja Mwenyezi Mungu ikiwa wamesimama au wamekaa au wamelala}}. Lakini vizuri zaidi ni mtu akae kisawasasa kikao cha heshima, kama Mtume alivyokua akikaa na akielekea kibla, akisoma baada ya swalatul Fajri mpaka jua kuchomoza, na asikae sana, isipite siku tatu pasina kusoma Qur'an,

Kutahadharisha Kusahau Qur'an

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, watu wameshughulika na dunia wakasahau kusoma Qur'an, na watoto wameshughulika na masomo ya kilimwengu mpaka hawana wakati wa kutosha na walimu hawashughulikiwi ikapelekea wasifanye kazi yao vizuri. Yote hayo, yamefanya Qur'an kuwa kitu kigeni, dhaifu na hata wasomao Dini wanapata shahada nzuri nzuri, hawasomi Qur'aan kisawasawa imepelekea kuipa mgongo Qur'an. Tumekua wajinga na hata katika mambo ya kidini tunaongozwa na wajinga hii ndio hasara, hatuipi kipaombele Qur'an. Hali hii itafanya Qur'an itushitaki kesho akhera ikisema: " Ewe Mola hawa waja wako duniani walinitupa na wakanidharau, walikuwa hawanisomi, hawanifikirii na hawanizingatii, Wala hawanitumii katika maamrisho wala makatazo, bali wao wakishughulikia machezo, nyimbo na maneno ya upuzi.

Hatuna budi tupate Walimu Wazuri

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu hatuna budi mpaka tupate walimu wazuri, wa kutusomeshea watoto, sio kila mtu au mtoto apate msahafu ajisomee mwenyewe mpaka Mwalimu amsikilize kwani maandishi peke yake hayatoshi, tupate utatuzi wa kuwaweka walimu wa kisawa na utatuzi wa matatizo ya wanafunzi, na mipangilio ya masomo yao, bali ziko madrasa nyingi kubwa kwa ndogo, vichochoroni na upenuni, kumbi na vyumba, vyote havina matokeo mazuri, tunachekwa na dini nyinginezo, walimu na wanafunzi na majengo, yapo katika hali ya kudharauliwa, sababu hatuna mwelekeo, lakini lau tungekuwa na wasimamizi wa mijini, mashambani tungepata matokeo mema.

Tuhifadhi Kitabu Kitukufu

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, Tujifundishe na tukihifadhi kitabu chake, tukisomeni kwa kumuogopa Allah. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Mwenye kusoma herufi moja ana thawabu kumi, na utahesabiwa

harufu moja moja]. Amesema ibnu-ll-Qayyim: ‘ Hebu zingatia, Allah ni mfalme wa wafalme, Atubembeleza tujipatie thawabu nyingi, Atutie moyo tupate thawabu hizo kwa urahisi, na ametunasihi saana, hii neema ya uhai isitupotee, vile vile ametuahidi raha kubwa kwa kumtii, na Ametuonya adhabu kali kwa kumuasi, na waja wema, inawapeleka kwenye wema ni kumtaja Allah kwa wingi kuwa ni Nuru, ni dawa, ni uongofu ni upambanuzi na ni hoja.

Mwisho

Mwenyezi Mungu alituumba kwa lengo la kiibada, kisha akatutumia Mtume akatufundisha vile atakavyo Yeye Mola, lakini Mungu huyo hatumuoni wala hatumsikii sauti, na tunaona dalili zake, alama zake na miujiza yake, kama mbingu na ardhi usiku na mchana na maneno yake matukufu. Mwenye kuyasoma atapata thawabu nyingi kwa kila herufi moja thawabu kumi na faida tofauti tofauti utazipata utakapoisoma Qur’an.

Nyoyo zetu na akili zetu zimejaa mashughuli ya kilimwengu hata hatuna nafasi ya kusoma Qur’an. Kwa hivyo ni kuangalia akhera yetu tupate taqwa, na tufuate utaratibu wa kuisoma. Tuisome tuijuwe maana huenda Qur-an ikarudi kwenye vifua vyetu na mienendo yetu.

Ewe Mwenyezi Mungu, Tujaalie waja wema, tuisome Qur’an kama maswahaba, tuisome na kuifahamu, tuisome kwa nidhamu, adabu na kuiheshimu.

[14] MAANA YA HIJJA

Lengo la Khutba:

1. Kuwakumbusha watu siri za Haji na maana yake
2. Kuwakumbusha watu neema ya Uislamu.
3. Kuwabainisha watu dharura ya Dini na umuhimu wa Ibada kwa mtu mmoja na wengi
4. Kuwaeleza kuwa suluhisho la kupatikana amani ni kupatikana Dini

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Ibada ya hija haikuanza leo, ilianza toka zama za Nabii Ibrahim. Ni moja katika nguzo za Uislamu. Ni lazima kwa Muislamu kuhiji, akiwa anaweza na ikiwa atahiji ataona na atapata faida mbalimbali

Maana ya Hija na Siri Zake

Enyi watu, Je mumeona ibada ya Hijja na ukubwa wake? Je mumeona imani na nuru zake? Je mmeona mrundiko wa msamaha wake? Ni vipi msimtukuze Mwenyezi Mungu na kumsifu?. Maangalizi yake mazuri yakuvutia, wanafurahika waumini, wanatukuka wanaompwekesha, wanasemehewa wenye madhambi, wanasafika walioghafilika.

Maana ya Hija

Je inamaanisha nini hija. Enyi Waislamu? Sidhanii kwamba ibada hii kwako haina mawaidha, idadi kubwa ya watu inaenda hija na wengi wao wanasamehewa madhambi na wanabadilika kiimani, baadaye yeye eti asiathirike.

Enyi mabwana watukufu, hakika katika hija pana viwanja, pana kukusanyikana, pana minara yenye vyeo baada ya kudharauliwa, na lengo lake ni uende ukafute dhambi kabla hujafa. Inavyotakikana ni kwamba umma usisahau siri za hija. Miongoni mwa faida zake; ni kupata ufungamano wa kisawasawa na kujuana na kujadidisha imani na kuingia hamu na ghera ya kiibada na kuzidi kumcha Mungu.

Visimamo katika Aya za Hija

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, hakika Aya za sura ya hajj zinabeba siri na hikma za hajj lau tutazisoma kwa makini tutapata hivyo visimamo kama mafumbo na misemo, kama Mungu anavyosema katika maana ya Aya:

قال تعالى: ﴿وَإِذْ بَوَّأْنَا لِإِبْرَٰهِيمَ مَكَانَ ٱلْبَيْتِ أَن لَّا تُشْرِكْ بِى شَيْـًٔا وَطَهِّرْ بَيْتِىَ لِلطَّآئِفِينَ وَٱلْقَآئِمِينَ وَٱلرُّكَّعِ ٱلسُّجُودِ ﴿٢٦﴾﴾ [الحج:٢٦].

{{Tulipomtilisha nanga Ibrahim katika Makkah ili afanye makazi, tulimuusia asimshirikishe Mwenyezi Mungu, na aisafishe nyumba ya Mwenyezi Mungu kwa wenye kutufu na wenye kusimama, kurukuu, kusujudu katika kuswali}}.

Hakika kumpwekesha ndio tegemeo la mwanadamu, kila balozi katika nchi hii na ndivyo inavyotakikana na Mwenyezi Mungu. Na kama tutaishi kama anavyotaka Allah, tungetawala ulimwengu na wapinzani wa Allah watakuwa wanyonge.

Hakika kumpwekesha Allah kihakika ungetupelekea sisi tupate ulimwengu na watu wapate amani na ulinzi kutoka kwetu, hapo waja wangalimuabudu Allah, vilivyo na ushirikina ungeondoka, lakini sisi wenyewe wenye Tawhidi, tunayo matatizo, tuna kasoro nyingi, vipi tunaweza kuwa makhalifa wa Allah? Ama washirikina wataenda Jahannam.

Allah (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

قال تعالى: ﴿وَمَن يُشْرِكْ بِٱللَّهِ فَكَأَنَّمَا خَرَّ مِنَ ٱلسَّمَآءِ فَتَخْطَفُهُ ٱلطَّيْرُ أَوْ تَهْوِى بِهِ ٱلرِّيحُ فِى مَكَانٍ سَحِيقٍ ﴿٣١﴾﴾ [الحج:٣١].

{{Ambaye atamshirikisha Mwenyezi Mungu, ni kama kwamba anaporomoka kutoka mbinguni, na ndege wakanyakuwa au achukuliwe na upepo akaanguke pahali pa mbali}}.

Sisi Waislamu tunayo nafasi nzuri ya kuingia peponi na kuipata dunia. Al-Kaaba ilijengwa ili watu wahiji na ndani yake kuna jiwe jeusi. Maswahaba walikuwa na Tawhidi ya juu, mmoja ni ‘Umar ambaye amesema: ‘Mimi najua wewe ni jiwe hudhuru wala hunufaishi, na lau sikumuona Mtume anakubusu, nisingekubusu. Hii ina maana Muislamu ni ajue kuwa kutufu na kubusu na kuanzia na kumalizia, asifahamu kuwa kuna madhara au manufaa akivitekeleza na kumdhuru akiziacha, bali afahamu kuwa uchamungu wake ndio unaokusudiwa, ndio Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akamtuma Abubakar mwaka wa tisa aende hija, atangaze siku ya idi ya kuchinja kwamba washirikina wasije kuhiji wala wasije kutufu tuputupu sababu ya kumtukuza na kuheshimu ibada ya Mwenyezi Mungu na sehemu zake.

Mahali pa Ibada sio pa Kuchezea

Katika Aya za sura ya hajj zinatueleza kwa undani kuwa hapo hija ni pahali pa ibada takatifu, kwa sababu ibada hii ni ya msimu, na tuiheshimuni ibada hii ili mkiondoka hapa ili tuwe tumesafika na ambaye hatosafika ni ajilaumu mwenyewe, kwani adhabu iliyo huko akhera ni kali sana na sio mchezo.

Hija ni Mwalimu anayetufundisha kusaidiana

Aya za sura ya haji zinatuhimiza kusaidiana na kujitolea sana. Mola (Subhaanahu wa Taala) Anasema kumuambia Ibrahim awatagazie watu waje Hija, waone manufaa yao na wataje jina la Mwenyezi Mungu kwenye siku maalumu, kwa kumshukuru kwa kuwaruzuku wanyama na kuchinja ili wale wao wanyama na kulisha wenzao wenye umaskini na utajiri.

Hija inatukuza Thamani ya Taqwa

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, Hija inatia moyo upate uchaji Mungu zaidi, na athari zake utazipata kwenye Aya na hadithi. Kwa mfano Mola (Subhaanahu wa Taala) Anasema katika maana ya Aya:

[قال تعالى: ﴿وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَۖ إِنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلۡعِقَابِ ٧﴾ [الحشر: ٧

{{Muogopeni Allah na mjue Allah ana adhabu kali}}.

Vile vile Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala) :

وقال أيضًا: ﴿ذَٰلِكَ وَمَن يُعَظِّمۡ شَعَٰٓئِرَ ٱللَّهِ فَإِنَّهَا مِن تَقۡوَى ٱلۡقُلُوبِ ٣٢﴾ [الحج:٣٢]

{{Mwenye kumtukuza Allah hakika huyo ameshapata taqwa ya moyo}}. Huko mwendako ni akhera, bebeni zawadi, na zawadi za huko zitawafaa wenyewe, zawadi za huko ni taqwa, zawadi nyingine hazifai.

Amesema tena Allah (Subhaanahu wa Taala):

[وقال سبحانه: ﴿لَن يَنَالَ ٱللَّهَ لُحُومُهَا وَلَا دِمَآؤُهَا وَلَٰكِن يَنَالُهُ ٱلتَّقۡوَىٰ مِنكُمۡ﴾ [الحج: ٣٧

{{Hazimfikii Mwenyezi Mungu nyama zenu wala damu zenu, kinacho mfika yeye ni uchaji Mungu kutoka kwenu}}.

Tukizisoma hizi Aya za hajj zinatuliza moyo kumcha Mmwenyezi Mungu, kufanya na kuepukana na mabaya. Ukifika hijja wajisikia wewe na wenzako muko sawa iwapo mumetoka miji mbalimbali, rangi mbalimbali, lugha mbalimbali, majumba mbalimbali, lakini yote hayo si kitu mpo pamoja kwenye hema, mnaswali Msikiti mmoja lugha za ibada zote ni moja, mavazi ni mamoja na ibada zote, mko pamoja katika twawafu, kusai na kadhalika.

Baada ya hija wajiona mko sawa umejuana na watu wengi, wajihisi mwenye kufanya ibada ndiye mbora kwa Mola kama alivyosema Mwenyezi Mungu na ndio tunamuona Suhayb Ar-Rumiyy na Salmaan Al-Faarisiyy walikuwa na cheo kikubwa mbele ya Mola wao kwa sababu ya taqwa mbele hata ya waarabu, hata Ammi ya Mtume Abu Lahab, kuondosha huo ubwana, Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). alipomuoa Zeinab binti Jahshi kwa Zeid ibn Harith, Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akaamrisha maswahaba wamuoze Abu Hind na waoe watoto wake.

Hija ni Muungano wa Kiislamu

Hija inatulingania tuwe Dini moja, malengo mamoja. Hii inaonekana wazi kwa wenye akili na wenye macho. Mahujaji wanakusanyana kwenye swala moja, uwanja mmoja na wanafunga mwezi mmoja. Kwa hivyo baada ya hajj tutakuwa na shabaha moja, hatutafaulu ikiwa hatutashikana sisi kwa sisi. Mola anatuonya ikiwa tutakuwa mbali mbali. Maadui wa Uislamu wanafurahika wakituona tuko madhehebu mbalimbali, ulinganizi wetu watafautiana, utawala wetu umegawanyika.

Allah (Subhaanahu wa Taala) Anasema:

قال تعالى: ﴿وَلَا تَنَٰزَعُواْ فَتَفۡشَلُواْ وَتَذۡهَبَ رِيحُكُمۡۖ﴾ [الأنفال:٤٦].

{{Wala Msizozane msije mkaharibikiwa na kupoteza nguvu zenu}}.

Hija ni sehemu ya kujadidisha Imani

Katika maana ya hija ni kujadidisha imani na kutengeneza nafsi, kwa sababu imani za watu zinapanda na kushuka na watu hukumbana na fitna na vivutio. Kwa hivyo hutibiwa kwa Tawhidi na ibada na makosa aliyoyafanya yakafutika. Kama Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alivyosema katika maana ya hadithi: [Mwenye kuhiji wala asifanye madhambi yoyote wakati wa kuhiji kwake, basi atarejea huko kwao akiwa hana dhambi hata moja kama siku aliyozaliwa na mamake]. Amepokea hadithi hii Bukhari na Muslim.

KHUTBA YA PILI

Hija ni ukumbusho wa Akhera

Maana ya hija ni kukumbusha akhera na siku ya kufufuliwa, kama Mungu anavyosema katika maana ya Aya:

قال تعالى: ﴿رَبَّنَآ إِنَّكَ جَامِعُ ٱلنَّاسِ لِيَوۡمٍ لَّا رَيۡبَ فِيهِۚ﴾ [آل عمران: ٩].

{{Ewe Mola wewe ndiye wewe mwenye kuwakusanya watu siku hiyo isiokuwa na shaka}}. Siku ya ‘Arafa ni mfano mdogo ya siku ya kufufuliwa, watu hukusanyika kumtwii Mola na kufutiwa dhambi zao. Mkusanyiko wetu huo wa kiibada, hakujapatikana kuendesha ibada ya mkusanyiko vizuri namna hii. Ingawa tuna matatizo yetu ya ndani, lakini maadui wanatamani hivi.

Aliyepata bahati mbaya huenda haji kwa kujifakhiri na kujidai na iwapo huona fujo la watu, ibada tofauti tofauti, haathiriki kwa sababu ya riyaa. Huzidisha alikotoka na madhambi yake na hurejea yale yale madhambi yake, moyo wake umepotea, hakujaaliwa kuongoka na mwenye kudharauliwa na Mola hakuna mwenye kumtukuza.

Ulinganizi wa Habari Njema

Enyi ndugu zangu, wabashirieni umma wenu kheri, huu ni umma wa uadilifu na uongozi, inaongoza usalama na raha na kheri yote. Huu umma utakuja kuhukumu ulimwengu kwa kutumia Qur’an tukufu, Waislamu hawapo katika uongozi, bali wamepotea uongozi, ni giza na ujinga ulioenea na watu wamekosa mwangaza na ushindi. Kwa nini ikawa hivyo? Kwa sababu uongozi haupelekwi na wanaostahiki, wao ni waovu wanaongoza kwa hawaa na mapenzi ya nafsi zao; na hiyo ndio dini yao, akili zikaharibika, mawazo yakapotea, wakawaua wanadamu pasi na hatia. Huyo ndiye mwanadamu wa kimagharibi, au ndye aliyeendelea ambapo amefilisika roho na mawazo. Utafaulu vipi bila Dini? Utauongoza vipi ulimwengu pasina kuutengeza? Wao wako mbio kuua wanadamu, kutengeneza mabomu na vifaru, ati wao ndio wanatengeneza ulimwengu, wao ndio wanaotisha usalama wa ulimwengu na bidii yao kubwa ni ulimwengu uwaogope na wamesahau Allah amesema.

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema katika maana ya Aya:

قال تعالى: ﴿ يَعۡلَمُونَ ظَٰهِرٗا مِّنَ ٱلۡحَيَوٰةِ ٱلدُّنۡيَا وَهُمۡ عَنِ ٱلۡأٓخِرَةِ هُمۡ غَٰفِلُونَ ﴾ [الروم:٧].

{{Wanayajua maisha wanayoyaona, lakini kuhusu akhera wamesahau}}.

Utulivu unapatikana katika Dini

Hakika utulivu unaopatikana ulimwenguni ni hali palipo na Dini, na pakikosekana dini hakuna utulivu na msimu wa hija unatuelekeza kwenye Dini na nafsi zetu ziwe safi na zijiandae kubadilika, ili Mola naye atubadilishie hali zetu. Dini yetu katika ibada ya hija inahimiza kwa njia tofauti tofauti, Uchaji Mungu, umoja na kuhurumiana.

Jamii ambayo haina Dini huhesabiwa haina imani na iko mbali na Mola na ndipo Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akasema: [Watatu watapata ladha ya imani:- wa kwanza ni yule anayempenda Mungu na Mtume wake kushinda kitu chochote, wa pili ni yule anayempenda mwenzake kwa ajili ya Mungu tu, wa tatu, ni yule anayechukia kurejea kwenye ukafiri baada ya Mungu kumuokoa nao kama alivyo chukia kutiwa motoni].

Na Muislamu, imani imempatia yeye muongozo kwenye usawa na utulivu, inatakikana tushike mafunzo hayo kwa magego ili sisi wenye Dini tupambane na wasiokuwa na dini mpaka tuwarejeshe kwenye Dini na tuwache huru ili tupate kuingia kwenye kundi zuri la Mwenyezi Mungu ambalo ndilo kundi zuri. Na wale mahasidi wanaochukia ukweli aliowapa Allah na wakawa hawataki kusikia. Na lau wangesikia na wakawapelekea wenzao wangepinga vile vile. Na wale waja wema wameamini hawakalifishwi isipokuwa wawezalo, kwani ni waja wema na huwa wanashukuru kwa neema ya Uislamu walioupata na neema ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam)

Mwisho

Enyi Waislamu wenzangu, tukumbukeni neema ya Uislamu, na kama si uislamu tungekuwa kwenye hasara. Mungu alituumba tufanye ibada, lakini makafiri wakafanya vile watakavyo mpaka akaja Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akatufundiisha yale ambayo Mola anayataka na kuyapenda, kama mfano hija. Makafiri walikuwa wakiabudu watakavyo na ikawa hawalipwi na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akatufundisha vile atakavyo Mola na kwahivyo, tunalipwa vizuri. Muislamu atasafiri kwa ndege au meli akiwa amejaa madhambi, lakini baada ya hija anarejea kwao akiwa amesafishika hana hata doa la dhambi, kwa hivyo biri utazipata kutoka kwa sheitwani.

Ewe Mwenyezi Mungu, tupe uwezo wa kwenda kuhiji, utuongezee imani na utukubalie hija zetu, ziwe ni hija zisizo na doa. Ewe Mola, tusamehe madhambi yetu.

[15] UTWAHARA WA MGONJWA

Lengo la Khutba:

1. Kuwakumbusha watu umuhimu wa kutunza swala
2. Kuwabainishia watu kuwa wao wameumbwa na mitihani ya magonjwa, ni juu yao wamuombe kwa Allah apate afya
3. Kuwatahadharisha Waislamu wasidharau swala hata kama ni wagonjwa.
4. Kuwakabili matabibu na wasimamizi wa wagonjwa na jamaa za wagonjwa kuwasaidia wagonjwa na kuwasaidia kwa swala zao.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Ewe Muislamu, Mola amekuumba na atakupa mitihani, basi utakapopata mitihani hiyo usisahau ibada Yake kama kawaida, tena haswa ibada ya swala.

Utwahara wa Mgonjwa na Swala zake

Baada ya himidi na swala na salamu, Enyi watu, muogopeni Mwenyezi Mungu kisawa sawa. Ewe muislamu, ujuwe Mola alituafikia, mimi na wewe tupate kheri ya Uislamu na bila shaka, maadamu ni Waislamu tutapata mitihani kila aina, ya siri na ya dhahiri ili tumtambue, tumshukuru na kusubiri. Na ndio Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) akasema katika maana ya Aya:

يقول الله جلّ وعلا: ﴿وَلَنَبۡلُوَنَّكُمۡ حَتَّىٰ نَعۡلَمَ ٱلۡمُجَٰهِدِينَ مِنكُمۡ وَٱلصَّٰبِرِينَ وَنَبۡلُوَاْ أَخۡبَارَكُمۡ ٣١﴾ [محمد:٣١].

{{Hakika tutawaonja mpaka tujue waumini wa kweli na wavumilivu miongoni mwenu}}.

Mwanafunzi wa Mtume, Suhaib Ar-Rumii amesema kwamba Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Ajabu ni ya huyu Muislamu, kwa kuwa kila jambo lake ni nzuri. Akipata la kumfurahisha atashukuru na ni kheri kwake, na akipata la kumuudhi atavumilia na ni kheri kwake]. Amepokea hadithi hii Muslim. Kwa hivyo, Muislamu atavumilia na ataridhike alivyomuahidi Mola.

Allah (Subhaanahu wa Taala) Amesema katika maana ya Aya:

قال تعالى: ﴿إِنَّمَا يُوَفَّى ٱلصَّٰبِرُونَ أَجۡرَهُم بِغَيۡرِ حِسَابٖ ١٠﴾ [الزُّمَر: ١٠]

{{Hakika watalipwa wavumilivu malipo mengi pasi kuwa na hesabu}}. Bishara njema kutoka kwa Allah (Subhaanahu wa Taala) kwa wenye kuvumilia na kusubiri. Amaesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿وَبَشِّرِ ٱلصَّٰبِرِينَ ١٥٥ ٱلَّذِينَ إِذَآ أَصَٰبَتۡهُم مُّصِيبَةٞ قَالُوٓاْ إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيۡهِ رَٰجِعُونَ ١٥٦ أُوْلَٰٓئِكَ عَلَيۡهِمۡ صَلَوَٰتٞ مِّن رَّبِّهِمۡ وَرَحۡمَةٞۖ وَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُهۡتَدُونَ ١٥٧﴾ [البقرة:١٥٥-١٥٧]

{{Tena wape habari njema wavumilivu, ambao wakipatwa na msiba husema, hakika sisi ni wa Allah kwa hakika sisi kwake yeye tutarejea, hao watapata msamaha na rehma kutoka kwa Mola wao na wao ndio waongofu}}.

Na katika Hadithi, Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) anasema: [Muumini akikumbwa na shida yoyote, huzuni na kadhalika, hata kudungwa na mwiba, yote humfutia madhambi].

Mja hapendelei Mitihani

Mja hatakikani apende mitihani wala apatikane na shida yoyote kwa sababu hajui ataweza kuvumilia au la. Kwa hivyo Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alimjibu Ammi yake ‘Abbas alipomuomba amuombee dua, Mtume akamwambia: [Ewe Ami, omba Mungu akupe afya, na akamkariria hilo]. Habari nyingine kutoka kwa babake Mu’adh Ibn Rafai anasema kuwa alisimama Abu Bakar Swiddiq akihutubu kisha akalia akasema: Mtume alisimama katika mimbari hii akahutubu kisha akalia akawa anatuambia: [Muombeni Mungu msamaha na afya kwani hakuna kitu muhimu baada ya imani na yakini isipokuwa ni afya na kila wakati mja atake msamaha na Mola ampe afya].

Ewe Muislamu, ukiwa na afya yako jikurubishe kwa Mwenyezi Mungu vile utakavyoweza na siku ukiwa mgonjwa akashindwa kufanya kama ulivyokuwa ukifanya basi fanya utakavyoweza na Mola atakulipa kama ulivyokuwa ukifanya ulipokuwa mzima, kama vile swala ya mgonjwa na swala ya msafiri.

Umuhimu wa Swala na Uwajibu wa Kuitunza

Enyi waja wa Allah, Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) amesema katika maana ya Aya: “Hakika swala ni lazima kwa muumini kwa wakati niliopanga” na Mtume akawaeleza kwa uwazi zaidi. Ewe Muislamu hakika tabia ya muumini ni kuifanya umuhimu wa swala kwa wakati vile alivyotufundisha Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Allah (Subhaanahu wa Taala) Anasema:

قال تعالى: ﴿ٱلَّذِينَ هُمۡ عَلَىٰ صَلَاتِهِمۡ دَآئِمُونَ ﴿٢٣﴾﴾ [المعارج:٢٣].

{{Waja wema ni wale wanaofululiza swala zao pasina kuacha}}. Kwa hivyo, swala iwe ndani ya moyo wa muumini, afuzu nayo na ajisikie nayo, na maadamu akili yake ni nzima basi anaamrishwa kuswali kwa vyovyote vile kama Mola alivyomuamrisha Mtume Issa Ibn Mariam, alimuamrisha kuswali na kutoa Zaka maadamu yuko hai.

Jitahadhari na Wenye kudharau Swala.

Ewe Muislamu, baadhi yetu wanaacha swala sio kwa sababu ya uvivu, bali dunia imeingia ndani ya nyoyo zao mpaka wakati ukapita, tena sana. Ikiwa mtu ni mgonjwa ni ajitahidi kuswali kwa hali yoyote mpaka apoe maradhi, na akipoa ataswali kama mwenye afya yake.

Utwahara kwenye Swala ni lazima.

Hili ni jambo lililo maarufu na ya kuwa utwahara kwenye swala ni lazima, katika nguo utakazoswalia na mwili wako wakati ule unaswali na mahali unaposimama kuswali. Mola (Subhaanahu wa Taala) Anasema katika maana ya Aya:

قال تعالى: ﴿وَثِيَابَكَ فَطَهِّرۡ ﴿٤﴾﴾ [المدّثر:٤]

{{Na nguo zako, ewe Muhammad, uzitwahirishe}}.

Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alikuwa akitembelea makaburini akateremshiwa wahyi ya kuwa makaburi mawili kati ya hayo waliomo ndani wanaadhibiwa, kosa la mmoja wao alikuwa hamalizi kujisafisha mkojo na hamalizi mkojo]. Hadith nyingine Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: {{Adhabu wanayoadhibiwa watu wengi ni kuwa hawamalizi mikojo}}, na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema [Haikubaliwi swala ya mmoja wenu ikiwa hana udhu mpaka atawadhe]. Hivi inamaanisha utwahara wa kila pahali ndio sharia inavyotakikana.

Kujisafisha Magonjwa.

Kujisafisha kwa malengo mawili :-

- Kuwa safi mbele ya viumbe wenzako
- Kuwa safi mbele ya viumbe wenzako na mbele ya Muumba wako.

Kuwa safi mbele ya viumbe ni kujisafisha choo, mkojo, damu na kadhalika. Na kujisafisha mbele ya Allah ni kujisafisha hivyo na kutawadha au kuoga au kutayammam.

Kutayamam ni pale unapokosa maji au ukiwa mgonjwa. Vilevile yawezekana maji yakawapo lakini ikawa viungo vya udhu vikipata maji utadhurika, ndipo utatayamam, haya yamesemwa na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) katika maana ya hadithi ya kuwa: [Ikiwa mnataka kuswali na hamna maji tayamam kwa mchanga kwani huo pia ni wenye kutwaharisha].

Ewe Muislamu mja huenda akakumbwa na maradhi kwenye viungo vya udhu, hapo atafuata moja katika njia mbili:- (1) Atatawadha na pale penye maradhi atapangusa na aende na udhu wake. (2) Ikiwa hivyo vitamdhuru, basi atatayamamu kama kawaida. Swahaba Ibn ‘Abbas alisema: ‘Mwenzetu aliyekuwa na kidonda kwa bahati mbaya alikumbwa na janaba kwa njia ya kuota, wenzetu hawakufahamu wakamueleza aoge, na swahaba akaoga kidonda kikaingia maji maradhi yakamzidi na akafa, tuliporejea mjini, Mtume akapelekewa habari ile, akasema: “Nyinyi mumemuuwa, kama angetayamamu angeendelea kuishi”

Swala ya Mgonjwa.

Ikiwa wewe ni Muislamu na akili yako inafanya kazi, inafahamu na kuelewa, basi swala ni juu yako kwa utakavyoweza, ulazima wake sio kama faradhi nyenginezo, nguzo hiyo iko juu ya mabega yako kwa kila kipindi kikiingia. Ndio utaona Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) mwenyewe na maswahaba na tabiina na waja wema wa kwanza wakitekeleza swala zao kwa afya na maradhi, Anas Ibn Maalik asema: ‘Siku moja nilipanda farasi, nikaanguka chini nikaumia, nikaswali kwa kukaa’.

Swahaba mwengine 'Imran ibn Huswain amesema kuwa yeye alikuwa mgonjwa wa bawasiri akawa ahisi dhiki kusimama na kukaa. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akamuambia: [Swali kwa kusimama, ikiwa huwezi, swali kwa kukaa, ikiwa huwezi swali kwa ubavu. Baadaye Mtume akaondoka, aliporejea akamkuta anaswali kwa kukaa lakini amekalia mto. Mtume akakasirika akauondosha ule mto akautupa kando na akasema: 'Swali juu ya ardhi ukiweza na kama huwezi swali kwa vyovyote lakini usikose khushui hata kama utaswali ni kwa kuashiria kwa kichwa katika kurukuu na kusujudu, ukirukuu utainamisha kichwa kidogo na ukisujudu ndio sana na iwapo huwezi hivyo, hata ishara ya macho inatosha'. Ama ishara ya kuswali kwa kidole sio sahihi. Haiko kwenye Qur-an, hadithi wala kwenye ilimu. Na wala si vizuri ukiwa unaumwa kidogo ukaswali kwa kukalia kiti, ndipo Misikiti yetu inakaribia kuwa holi kwa viti.

KHUTBA YA PILI

Mgonjwa kuelekea Qibla

Ewe Muislamu, Hapana budi kuelekea Qibla ili swala ikubaliwe, na hii iko wazi kwa wanazuoni wote, lakini mgonjwa akiwa hajiwezi na hakupata mwenye kumsaidia kumuelekeza Qibla na ikiwa kitanda hakikulenga Qibla, ataswali vile alivyojaaliwa, na wakati mwingine mgonjwa huwa ana najisi au hana udhu na hakupata mwenye kumsaidia kwa udhu au kumsafisha uchafu, majeraha yakawa yana damu na usaha, basi ataswali kama alivyojaaliwa. Habari kutoka kwa swahaba mtukufu, Mansuur ibn Makhramah anasimulia ya kuwa aliingia nyumbani mwa 'Umar ibn Khattwab kwa swala ya asubuhi na 'Umar alikuwa amedungwa na Abuu lu'lu'ah aliyekuwa katika dini ya kimajusi, lakini 'Umar alikuwa hajafa bado, majeraha yanamwaga damu na Khalifa akaendelea na swala kama kawaida. Hivi ndivyo waumini wanavyokuwa kipindi cha swala hakiwapiti.

Ni wajibu kwa Msimamizi wa Mgonjwa kumsaidia kumtwahirisha na kumkumbusha swala.

Ewe Muislamu, unaemsimamia mgonjwa nyumbani au hospitalini, Muogope Allah, na ujue ya kuwa swala ni muhimu, umsaidie mgonjwa wako kwa kumsafisha, umkumbushe swala na dhikri na zaidi ikiwa ni wazazi wako, kwani wao unapaswa uwasaidie zaidi kwa kazi hiyo tukufu kama Mola (Subhaanahu wa Taala) Alivyotuamrisha katika maana ya Aya:

قال تعالى: ﴿وَأۡمُرۡ أَهۡلَكَ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱصۡطَبِرۡ عَلَيۡهَاۖ﴾ [طه:١٣٢].

{{Na uamrishe watu wako swala na uvumilie}}

Ulinganizi kwa Matabibu wamche Mwenyezi Mungu.

Ni sisi Waislamu tuwaelimishe matabibu kuwa Muislamu ni wajibu aswali na kuwa kuswali ndio chakula cha roho. Hao matabibu huwapatia dawa wagonjwa kwa vipindi, nyakati na saa maalumu, tuwakumbushe ilivyo muhimu dawa ya mwili, dawa ya roho ni muhimu zaidi, haifai kujitukuza wala kudharau. Kila kitendo kina wakati wake na Mungu aliyetuumba amesema katika maana ya Aya:

والله يقول: ﴿وَتَعَاوَنُوا۟ عَلَى ٱلْبِرِّ وَٱلتَّقْوَىٰ ۖ وَلَا تَعَاوَنُوا۟ عَلَى ٱلْإِثْمِ وَٱلْعُدْوَٰنِ﴾ [المائدة:٢].

{{Saidianeni katika wema na kumcha Mwenyezi Mungu na wala msisaidiane katika madhambi na uadui}}.

Hukumu ya kukusanya Swala Mbili kwa Wakati Mmoja.

Sheria ya kiislamu imemuhurumia mgonjwa ikamruhusu aswali swala mbili kwa kipindi kimoja, kwa vile ana shida ya ugonjwa, maumivu ya madawa, kutawadha na kumsumbua mwenye kumshughulikia, kwa hivyo atakusanya swala ya Adhuhuri na Alasiri aziswali kipindi cha Adhuhuri au kipindi cha Swala ya Alasiri. Na swala ya Magharibi na Isha aziswali kipindi cha Magharibi, au kipindi cha Ishi. Haya yote ni kwa sababu ya kumhurumia mgonjwa.

Nasaha kwa Waislamu Wote.

Ewe Muislamu, swala iwe ndani ya moyo wako, akili yako roho yako na damu yako, uiswali kwa wakati wake, na sharti zake. Hakuna litakalo kuachisha Swala isipokuwa kufa, ili uingie kwenye pepo ya Firdausi iliyo bora kuliko pepo zote kama vile Mola (Subhaanahu wa Taala) alivyosema katika maana ya Aya:

قال تعالى: ﴿وَٱلَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَوَٰتِهِمْ يُحَافِظُونَ ﴿٩﴾ أُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْوَٰرِثُونَ ﴿١٠﴾ ٱلَّذِينَ يَرِثُونَ ٱلْفِرْدَوْسَ هُمْ فِيهَا خَٰلِدُونَ ﴿١١﴾﴾ [المؤمنون:٩:١١].

{{Waja wema ni wale wanaohifadhi Swala zao. Hao wataingia pepo ya Firdausi watakaa humo milele}}. Na hata mkiwa kwenye vita mtaswali kwa kutembea au ikiwa mmepanda vipando au mtaswali kwa zamu, bora kipindi kiingie, mswali kwa hali yoyote ile. Namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie sisi tuwe waja wema wenye kutunza swala zetu na hakika yeye kwa kila kitu ni Muweza.

Jueni, Mungu awarehemu, hakika maneno mazuri ni kitabu cha Mungu na uongofu bora ni uongofu wa Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) na mambo mabaya zaidi ni yale yaliozuliwa katika Dini, kwani kila lenye kuzuliwa huitwa ni uzushi. Kwa hivyo ni juu yenu mshikamane na Sunnah za Mtume na Maswahaba zake na mumswalie Mtume wenu Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) kwa kufuata amri ya Mola (Subhaanahu wa Taala) wetu Aliposema katika maana ya Aya:

قال تعالى: ﴿إِنَّ ٱللَّهَ وَمَلَٰٓئِكَتَهُۥ يُصَلُّونَ عَلَى ٱلنَّبِىِّ ۚ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ صَلُّوا۟ عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا۟ تَسْلِيمًا ﴿٥٦﴾﴾ [الأحزاب:٥٦]

{{Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamswalia Mtume, Enyi waumini pia nyinyi mswalieni}}.

Ewe Mwenyezi Mungu, Mswalie na umbariki Mtume Muhammad na watu wake wa kwanza na wa mwisho na uwe radhi na Maswahaba zake na Makhalifa wake na waliokuja baada yao mpaka Qiyama.

Mwisho

Ewe mwanadamu mwenzangu, wewe umeumbwa, hukujiumba, umeletwa hukuletwa, na siku ya kuondoshwa hutajua. Kwa hivyo ni juu yako kumtwii Allah katika saa zote, siku zote, wiki zote, miezi yote, miaka yote mpaka mwisho wa umri wako.

Katika maisha yako, utapata mitihani ya kila aina, magonjwa na kadhalika. Ukipatikana na mtihani wa ugonjwa utaswali kama kawaida na ukishindwa utaswali utakavyoweza, muhimu ni kuwa kipindi cha Swala kisikupite, maadamu akili yako inafanya kazi, swala imekulazimu. Ewe Mwenyezi Mungu, Tupe mitihani mipesi ili tusiepukane na Swala.

(3) SEHEMU YA MAADILI NA TABIA

Malengo Muhimu :

1. Kudhihirisha tabia nzuri za kiislamu
2. Kutahadharisha tabia mbaya na madhambi
3. Kumlinda Mtu kutokana na Ibada na Mila zinazokhalifu Uislamu

Anuani ya Khutba katika Sehemu ya Maadili na Tabia:-

1. Tahadhari na Kuteleza Ulimi
2. Athari ya kusuhubiana na Rafiki Mwema
3. Tahadhari na Fitna za Wanawake
4. Uhimizaji juu ya Subira
5. Uhimizaji wa kusema Ukweli na Utahadharishaji wa Kusema Urongo
6. Toba baada ya Kufanya Maasi
7. Rehema
8. Dhana Mbaya
9. Hatari ya Mwanamke Kujipamba na Kudhihirisha Mwili Wake
10. Madawa ya Kulevya na Athari yake katika Kumuangamiza barobaro

[1] TAHDHARI NA KUTELEZA KWA ULIMI

Lengo la Khutba:

1. Kulea nafsi katika kusema maneno mazuri.
2. Kufaulu kwa kupata radhi za Mwenyezi Mungu.
3. Kujiepusha na maneno mabaya.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Ulimi ni kiungo muhimu katika mwili wa mwanadamu. Ulimi ni neema kubwa miongoni mwa neema alizo neemeshwa mwanadamu na Allah (Subhaanahu wa Taala). Kiungo hiki ni silaha yenye makali mawili, silaha ya kusababisha mwanadamu kufaulu hapa duniani na kesho Akhera, au ni silaha ya kumuangamiza mwanadamu hapa duniani na kesho akhera.

Kumcha Mwenyezi Mungu ni njia ya kuokoka duniani na kesho akhera Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالي : ﴿وَمَن يَتَّقِ ٱللَّهَ يَجۡعَل لَّهُۥ مَخۡرَجٗا ٢ وَيَرۡزُقۡهُ مِنۡ حَيۡثُ لَا يَحۡتَسِبُۚ وَمَن يَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱللَّهِ فَهُوَ حَسۡبُهُۥٓۚ إِنَّ ٱللَّهَ بَٰلِغُ أَمۡرِهِۦۚ قَدۡ جَعَلَ ٱللَّهُ لِكُلِّ شَيۡءٖ قَدۡرٗا ٣﴾ [الطلاق:٢:٣].

{{Na anayemuogopa Mwenyezi Mungu humtengenezea njia ya kuokoka (na kila balaa). Na humpa riziki kwa namna asiyotizamia, na anayemtegemea Mwenyezi Mungu Yeye humtoshea. Kwa yakini Mwenyezi Mungu amekwisha kiweka kila kitu kipimo chake}}. Na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ni mjuzi wa kila kitu na hapitiwi na kitu chochote kilichoko mbinguni na ardhini. Tahadhari juu yetu kufanya jambo lisilomridhisha.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) ushahidi juu ya yaliyopita:

وقوله : ﴿وَسِعَ رَبِّي كُلَّ شَيۡءٍ عِلۡمًاۗ أَفَلَا تَتَذَكَّرُونَ ٨٠﴾ [الأنعام: ٨٠].

{{Mola wangu anakijua vyema kila kitu. Basi je, hamsikii mawaidha (hamzinduki)}}.

Ulimi ni neema aliompa Mwenyezi Mungu mja wake.

Amesema Mwenyezi

قال تعالي : ﴿أَلَمۡ نَجۡعَل لَّهُۥ عَيۡنَيۡنِ ٨ وَلِسَانٗا وَشَفَتَيۡنِ ٩ وَهَدَيۡنَٰهُ ٱلنَّجۡدَيۡنِ ١٠﴾ [البلد: ٨]

{{Je hatukumpa macho mawili ? na Ulimi na Midomo miwili. Na tukambainishia zote njia mbili (iliyo njema na iliyo mbya)}}. Maiti wangapi wamesababisha vifo vyao kwa ajili ya ndimi zao. Je hawatatupwa watu motoni isipokuwa kwa mavuno ya ndimi zao. Inapasa kwa muumini kuhifadhi ulimi wake kwa hali yoyote ile na kujiepusha na kila ambalo linapingana na sheria, mfano wa kusengenya. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالي: ﴿وَلَا يَغۡتَب بَّعۡضُكُم بَعۡضًاۚ أَيُحِبُّ أَحَدُكُمۡ أَن يَأۡكُلَ لَحۡمَ أَخِيهِ مَيۡتٗا فَكَرِهۡتُمُوهُۚ﴾ [الحُجرات:١٢].

{{Wala baadhi yenu wasiwasengenye wengine. Je Mmoja wenu anapenda kula nyama ya nduguye aliyekufa? La, Hampendi}}. Imepokewa na Barzah al-Aslamy

Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Enyi mlioamini, kwa ndimi zenu, wala imani haijaingia katika vifua vyenu msiwasengenye Waislamu, wala msichunguze aibu zao na mwenye kuchunguza aibu ya muislamu Mwenyezi Mungu atafunua aibu yake na kumfedhehesha mbele ya watu].

Kuhadharishwa juu ya Fitna:

Hadithi imepokewa na Ibn 'Abass kuwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alipita katika makaburi mawili akasema: [Maiti hawa wawili wanaadhibiwa wala hawaadhibiwi kwa jambo kubwa, mmoja wao alikuwa hajisafishi anapokojoa na mwengine alikuwa akieneza fitna].

Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) Kutilia umuhimu kuhifadhi Ulimi

Kuhifadhi ulimi ndiko kumiliki kheri zote. Amepokea hadithi Mu'adh Ibn Jabal kuwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) Amesema: Je nisikujuze kwa mambo yote hayo zuia ulimi wako (chunga ulimi wako). Akasema. Mu'adh: Je tutahisabiwa kwa tunachokizungumza. Mtume akashangaa na kumuambia: Je hawatupwi watu motoni ila kwa mavuno ya ndimi zao". Na alikuwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akiwahimiza wake zake kujihifadhi na maneno yasiomridhisha Mwenyezi Mungu. Imepokewa na 'Aisha nimemuambia Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) tosheka na bibi Safia kwa jambo kadha na kadha akimaanisha ya kuwa ni mfupi Mtume akamuambia: [Umetamka neno ambalo kwamba likichanganywa na maji ya baharini litachanganyika].

Hali ya Waislamu Leo kupuuza kuhifadhi Ndimi Zao

Inapatikana katika hali zifuatazo:

1. Maneno yasiokuwa na faida
2. Kuingilia jambo lisilo kuhusu.
3. Kuingilia heshima za Waislamu.
4. Ulimi mchafu
5. Kuomboleza katika msiba.

Ushahidi wa mambo yaliyopita amehutubu na akarefusha maneno yake mbele ya 'Umar akasema 'Umar kurefusha maneno ni ya shetani. Na imepokewa hadith' kutoka kwa Abu Hureira, Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) Amesema: [Muislamu bora ni yule asiyeingilia mambo ya watu, na kuingilia heshima za Waislamu ni katika sifa za wanafiki]. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Ni haramu kwa ndugu yako Muislamu damu yake, heshima yake na mali yake, Muislamu ndugu yake ni Muislamu hamdhulumu wala hamkhini na akashiria katika kifua chake taqwa ni kwenye moyo]. Maneno machafu yaliyoenea katika jamii ya kiislamu leo huenda kuwa sababu kubwa ni vyombo vya habari. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Hapana kitu kizito katika mizani siku ya kiyama kama tabia nzuri na Mwenyezi Mungu anachukia maneno

mabaya].

Ama kuomboleza katika msiba ni jambo la kijahilia ambalo limekatazwa, na tumeamrishwa tusubiri pindi tu tunapopatikana na msiba. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alipita kwenye kaburi na akamuona mwanamke analia akamuambia muogope Mwenyezi Mungu na usubiri, mwanamke akajibu hujali kilichonisibu wala hakujua kwamba anayejibizana nae kuwa ni Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akamwambia hakika ya subira ni katika tukio la Mwanzo.

Tahadhari Kueneza Uongo kwa Watu

Imepokewa hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema: [Tahadharini na muongo, kwani uongo unapeleka kwa uovu, na uovu unapeleka mtu kuingia motoni, na mtu anasema uongo mpaka anaandikwa mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa ni muongo]. Na Akasema tena Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) : [Uongo haufai hata kwa dhihaka]. Wala kuahidi mtu mtoto wake wala asimtimizie. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) kuamrisha waumini kuwa imara katika kupokea habari:

قال الله تعالي: ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِن جَآءَكُمۡ فَاسِقُۢ بِنَبَإٖ فَتَبَيَّنُوٓاْ أَن تُصِيبُواْ قَوۡمَۢا بِجَهَٰلَةٖ فَتُصۡبِحُواْ عَلَىٰ مَا فَعَلۡتُمۡ نَٰدِمِينَ ٦﴾ [الحُجُرات: ٦].

{{Enyi mlioamini, kama fasiki akikujieni na habari yoyote msimkubalie tu, bali pelelezeni kwanza, msije mkawadhuru watu kwa ujahili na mkawa wenye kujuta juu ya yale mliyoyatenda}}.

KHUTBAH YA PILI

Mwenyezi Mungu pamoja na Malaika wake wanaandika wanachozungumza mwanadamu. Na wao wanahifadhi amali zote za kheri na shari. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالي: ﴿وَإِنَّ عَلَيۡكُمۡ لَحَٰفِظِينَ ١٠ كِرَامٗا كَٰتِبِينَ ١١ يَعۡلَمُونَ مَا تَفۡعَلُونَ ١٢﴾ [الانفطار:١٠:١٢]

{{Na hakika juu yenu kuna wenye kuwatunza. Watukufu wenye kuandika. Wanayajua yote mnayoyatenda}}.

Na Neno lake Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقوله: ﴿إِذۡ يَتَلَقَّى ٱلۡمُتَلَقِّيَانِ عَنِ ٱلۡيَمِينِ وَعَنِ ٱلشِّمَالِ قَعِيدٞ ١٧ مَّا يَلۡفِظُ مِن قَوۡلٍ إِلَّا لَدَيۡهِ رَقِيبٌ عَتِيدٞ ١٨﴾ [ق:١٧:١٨].

{{Wanapopokea wapokeaji wawili, anayekaa kuliani na anayekaa kushotoni. Hutoi kauli yoyote isipokuwa karibu naye yuko mngojeaji tayari (kuandika)}}.

Amepokea Abu Huraira kuwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Kuwa Malaika wanapokezana usiku na mchana wakikutana katika swala ya alfajiri na al-asri, kisha wanakwenda wale walio kuwa ni wa usiku. Na mola akiwauliza naye akijua; mumewaacha vipi waja wangu? Wakijibu; tumewaacha wakiswali na tukawajia hali ya kuwa wanaswali].

Wito wa Kuwajibika kwa Maneno Mazuri

Kuwajibika kwa maneno mazuri ni sababu ya kufaulu na kusamehewa madhambi na kupata radhi zake Mola kwa ajili hiyo anasema Mola:

قال الله: ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَقُولُواْ قَوۡلٗا سَدِيدٗا ٧٠ يُصۡلِحۡ لَكُمۡ أَعۡمَٰلَكُمۡ وَيَغۡفِرۡ لَكُمۡ ذُنُوبَكُمۡۗ وَمَن يُطِعِ ٱللَّهَ
وَرَسُولَهُۥ فَقَدۡ فَازَ فَوۡزًا عَظِيمًا ٧١﴾ [الأحزاب: ٧٠: ٧١].

{{Enyi mlioamini, Muogopeni Mwenyezi Mungu na semeni maneno ya haki. atakutengenezeni vizuri vitendo vyenu na atakusemeheni madhambi yenu; Na anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, bila shaka amefanikiwa mafanikio makubwa}}.

Mwisho

Ndugu Waislamu, Ulimi ni kiungo muhimu katika mwili wa mawnadamu. Na kikiwa kizuri basi mwili wote huwa mzuri. Ni jukumu la kila Mislamu kuulinda ulimi wake kwa kutumia katika kuzungumza mambo ya kheri, kuamrisha mema na kukataza mabaya. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumefaidika na neema ya ulimi, na kupata radhi za Allah (Subhaanahu wa Taala). Namuomba Mwenyezi Mungu asituhisabu kwa yale tuliyoyazungumza ikiwa ni ya makosa, na kutupa ujira kwa maneno mazuri tuliyoyazungumza.

[2] ATHARI YA KUSUHUBIANA NA RAFIKI MWEMA

Lengo la Khutba:

1. Kumlea mja ni katika Tabia ya kiislamu.
2. Kuwatahadharisha na marafiki wabaya.
3. Kuwahimiza katika kuwalea mabanati wetu na kusuhubiana na marafiki Wema.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Mwanadamu hawezi kuishi peke yake ana haja ya usaidizi na kutangamana na watu wengine. Kwa ajili hiyo uislamu umekuja kuitikia mwito wa maumbile, uislamu ukaweka ibada ambazo zinafanywa na watu wengi kwa pamoja mfano wake Swala. Uislamu ni dini ya maumbile, ushahidi wa hayo ni Hadithi iliyopokewa na Abu Hureira: “ Yoyote anayezaliwa huzaliwa katika uislamu isipokuwa wazazi wake humfanya mtoto wao kuwa myahudi au mnaswara au majusi”. Kama Mwenyezi Mungu alipomuumba Adam na Hawaa ili waishi pamoja wala hakumuacha peke yake amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالى : ﴿ هُوَ ٱلَّذِي خَلَقَكُم مِّن نَّفۡسٖ وَٰحِدَةٖ وَجَعَلَ مِنۡهَا زَوۡجَهَا لِيَسۡكُنَ إِلَيۡهَاۖ ﴾ [الأعراف:١٨٩].

{{Yeye ndiye aliyekuumbeni katika nafsi moja; na katika nafsi hiyo ameumba wake wao ili mpate utulivu kwake}}. Uislamu umetiliwa nguvu kutokana na sababu nyingi kama kuwekwa ibada za pamoja mfano wake swala ya ijumaa, swala ya jamaa na nyenginezo. Dhihirisho la haya alipoazimia Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) kuchoma nyumba za wasio kuja kuswali swala za jamaa. Na dharura kwa uhai ni kuchagua mtu anayesuhubiana nae ili amkumbushe anaposahau na kumjuza anapokuwa mjinga, amesema mshairi wa kiarabu: “ Mja usimuulize bali muangalie rafiki yake kila rafiki kutokana na marafiki huongozana. Akiwa rafiki huyo ni muovu jiepusheni nae kwa haraka, na ikiwa ni mwema husuhubiana nae utaongoka”.

Uchaguzi wa rafiki mwema umejengwa kutokana na msingi wa kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake na dini yake. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالى : ﴿إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱلَّذِينَ يُقِيمُونَ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤۡتُونَ ٱلزَّكَوٰةَ وَهُمۡ رَٰكِعُونَ ٥٥﴾ [المائدة: ٥٥].

{{Hakika rafiki yenu khasa ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walioamini ambao husimamisha sala na hutoa zaka, na hali wakiwa wananyenyekea. Na atekayefanya urafiki na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walioamini. Kwani kundi la Mwenyezi Mungu ndio litakalo shinda}}. Na katika matunda ya imani ni kuchagua rafiki mwema. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

ويقول: ﴿لَّا تَجِدُ قَوۡمٗا يُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ وَٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِ يُوَآدُّونَ مَنۡ حَآدَّ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ وَلَوۡ كَانُوٓاْ ءَابَآءَهُمۡ أَوۡ أَبۡنَآءَهُمۡ أَوۡ إِخۡوَٰنَهُمۡ أَوۡ عَشِيرَتَهُمۡۚ﴾ [المجادلة:٢٢].

{{Huwapati watu wanaomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, kuwa wanawapenda wale wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake}}. Na

kemeo kubwa ni kuwapenda maadui wa Mwenyezi Mungu.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقوله تعالى: ﴿مُّحَمَّدٌ رَّسُولُ ٱللَّهِۚ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥٓ أَشِدَّآءُ عَلَى ٱلۡكُفَّارِ رُحَمَآءُ بَيۡنَهُمۡۖ﴾ [الفتح: ٢٩].

{{Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye ni wenye nyoyo thabiti mbele ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao}}.

Na akasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقوله تعالى: ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مَن يَرۡتَدَّ مِنكُمۡ عَن دِينِهِۦ فَسَوۡفَ يَأۡتِي ٱللَّهُ بِقَوۡمٖ يُحِبُّهُمۡ وَيُحِبُّونَهُۥٓ أَذِلَّةٍ عَلَى ٱلۡمُؤۡمِنِينَ أَعِزَّةٍ عَلَى ٱلۡكَٰفِرِينَ﴾ [المائدة: ٥٤].

{{Enyi mlioamini, Atakayeiacha miongoni mwenu dini yake, basi hivi karibuni Mwenyezi Mungu ataleta watu ambao atawapenda, nao watampenda, wanyenyekevu kwa Waislamu wenzao, wenye nguvu juu ya makafiri}}.

Mwenye akili siku zote huwakimbia marafiki waovu kama anavyo mkimbia mtu Simba, tazama Neno lake Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قوله تعالى: ﴿وَيَوۡمَ يَعَضُّ ٱلظَّالِمُ عَلَىٰ يَدَيۡهِ يَقُولُ يَٰلَيۡتَنِي ٱتَّخَذۡتُ مَعَ ٱلرَّسُولِ سَبِيلٗا ٢٧ يَٰوَيۡلَتَىٰ لَيۡتَنِي لَمۡ أَتَّخِذۡ فُلَانًا خَلِيلٗا ٢٨ لَّقَدۡ أَضَلَّنِي عَنِ ٱلذِّكۡرِ بَعۡدَ إِذۡ جَآءَنِيۗ وَكَانَ ٱلشَّيۡطَٰنُ لِلۡإِنسَٰنِ خَذُولٗا ٢٩﴾ [الفرقان:٢٧:٢٩].

{{Na siku dhalimu atajiuma mikono yake vidole vyake na huku akisema: Laiti ningalishika njia ya haki nikawa pamoja na Mtume}}. Dhalimu aliyekusudiwa katika Aya iliyotangulia ni 'Uqbatu ibn Abi Mu'ayit na aliyempoteza katika uongofu Ummayah ibn Khalaf.

Amefananisha Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) rafiki mwema na rafiki muovu kama mfano wa anayebeba miski na mwenye kufua vyuma kwa anae beba miski ima atakuuzia ima utapata kutoka kwake harufu mzuri na mfua vyuma ima atachoma nguo zako au utapata harufu mbaya]. Je hauoni neno la Luqman juu ya mtoto wake: Ewe mwanangu tangamana na wanavyuoni hakika Mwenyezi Mungu hukuhuisha nyoyo kwa nuru ya hikima, kama anavyohuisha ardhi iliyokufa."

KHUTBA YA PILI

Matunda ya kusuhubiana na rafiki mwema kuongoka kwa mtu mmoja ni kuongoka kwa jamii na kuongoka kwa jamii ndio sababu ya kupata baraka inayotoka mbinguni na ardhini. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿وَلَوۡ أَنَّ أَهۡلَ ٱلۡقُرَىٰٓ ءَامَنُواْ وَٱتَّقَوۡاْ لَفَتَحۡنَا عَلَيۡهِم بَرَكَٰتٖ مِّنَ ٱلسَّمَآءِ وَٱلۡأَرۡضِ وَلَٰكِن كَذَّبُواْ فَأَخَذۡنَٰهُم بِمَا كَانُواْ يَكۡسِبُونَ ٩٦﴾ [الأعراف: ٩٦].

{{Na lau kama watu wa miji wangaliamini na kuogopa, kwa yakini tungaliwafungulia baraka za mbingu na ardhi. Lakini walikadhibisha; tukawapatiliza kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma}}. Watu wa peponi wote ni marafiki wema.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ كَانَتۡ لَهُمۡ جَنَّٰتُ ٱلۡفِرۡدَوۡسِ نُزُلًا ١٠٧﴾ [الكهف:١٠٧].

{{Kwa yakini walioamini na kufanya vitendo vizuri, makazi yao yatakuwa hizo za Firdaws}}.

Na Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) :

وقوله تعالى: ﴿وَنَزَعۡنَا مَا فِي صُدُورِهِم مِّنۡ غِلّٖ تَجۡرِي مِن تَحۡتِهِمُ ٱلۡأَنۡهَٰرُ﴾ [الأعراف:٤٣].

{{Na tutaiondoa bughudha vifuani mwao (wawe wanapendana wote kweli kweli) mbele yao iwe inapita mito}}. Wema waliotangulia ni mfano bora wa kusuhubiana. Pindi Salman alipomtembelea Abu Dardai akamuona Mama Dardai nae akamuuliza kuhusu Abu Dardai nae akamjibu kuwa ametoka na muda si mrefu atarudi. Ummu Dardai akamjulisha Salman tabia ya Abu Dardai ya kuachana na dunia na kutoangalia watu wake. Pindi aliporudi Abu Dardai mazungumzo yao yalikuwa kama hivi ifuatavyo:

Abu Dardai alimwambia Salama: Kula chakula hichi mimi nimefunga. Salman akajibu sili chakula hichi mpaka ule wewe. Abu Dardai akala chakula hicho. Ilipofika usiku Abu Dardai alitaka kusimama (Qiyamulail). Salman akamwambia: lala. Abu Dardai akalala, jambo hilo likaendelea mara mbili tatu ilipofika usiku wa mwisho Salman akasema: amka sasa Mola wako na nafsi yako pia ina haki kwako. Vile vile pia mke wako ana haki kwako, ipe kila haki haki yake. Aliposikia Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akasema: " Amesema kweli Salman." Tazama vipi waja wema wanavyosaidiana kwa amali njema na kumcha Mwenyezi Mungu.

Mfano wa rafiki muovu na mwisho wake, Abu Talib alipokuwa anafikiwa na mauti Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alimtembelea na hapo alikuwepo Abu Jahal na 'Abdallah Ibn Abi Umaya Ibn Mughaira. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akasema kumuambia Abu Talib aseme "Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu " neno ambalo litakutolea hoja mbele ya Mwenyezi Mungu, akasema Abu Jahal na 'Abdillah Ibn Abi Ummayah unaipa nyongo mila ya AbdulMutwalib. Hakuacha Mtume wa Mwenyezi Mungu kumkariria, na wao pia wakikariri "Unaipa nyongo mila ya AbdulMutwalib" mwishowe akasema yeye yuko katika mila ya AbdulMutwalib.

Enyi baba zangu nyote ni wachunga na kila mmoja ataulizwa kwa kile anacho kichunga. Itakuwa ni khiana baba kuwaacha watoto wake bila ya kuwauliza wanakwenda wapi, hali ya siku hizi hawaulizi wanapokwenda au walikuwa pamoja na nani? Na wapi wamelala? Wala hajui baba kwamba mtoto wake alikuwa na rafiki wa kishetani wakimuharibu dini, akili yake na uislamu wake. Tahadhari na marafiki waovu, na ni juu ya barobaro kuchagua rafiki mwema ambao watakaomsaidia katika haki na kumjuza.

Mwisho

Ndugu katika Imani, ni muhimu sana kuchagua rafiki mwema ambaye atakusaidia katika kufanya mambo ya kheri. Pindi unapo sahau anakukumbusha na ukikosea anakunasihi kwa njia mzuri.

Ewe Mwenyezi Mungu turuzuku rafiki wema na utuepushie na rafiki waovu, uturuzuku rafiki wema ambao watatusaidia katika kukushukuru na kukutaja na kukuabudu na uturuzuku kusuhubiana na Mtume wako.

[3] TAHADHARI NA FITNA ZA WANAWAKE

Lengo la Khutba:

1. Kujihifadhi na fitna za wanawake.
2. Kuwalea wanawake katika malezi ya kujiheshimu.
3. Kuwakumbusha Waislamu majukumu yao.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Leo Mwanamke amekuwa ni bidhaa isiyo na thamani. Kila mtu anaweza kununua bidhaa hiyo kwa thamani ndogo kabisa kwa lengo la kujistarehesha, Mwanamke ni fitna kubwa katika jamii, pindi akijiweka mbali na mafundisho ya Allah. Jamii nyingi zina haribikiwa kwasababu ya maadili na tabia mbaya za wanawake. Athari ya Mwanamke ni kubwa sana katika jamii na kwa Umma wote. Katika Khutba ya leo tutaangazia suala hili muhimu la Fitna za wanawake, na jukumu la Waislamu katika kupambana na fitna hizo.

Mwenyezi Mungu ametuusia sisi na watu waliotangulia kumcha yeye. Na ushahidi wa hayo. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) katika Quraan tukufu:

قال تعالى : ﴿ وَلِلَّهِ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِي ٱلْأَرْضِ ۗ وَلَقَدْ وَصَّيْنَا ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْكِتَٰبَ مِن قَبْلِكُمْ وَإِيَّاكُمْ أَنِ ٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ۚ وَإِن تَكْفُرُوا۟ فَإِنَّ لِلَّهِ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِي ٱلْأَرْضِ ۚ وَكَانَ ٱللَّهُ غَنِيًّا حَمِيدًا ﴿١٣١﴾ ﴾ [النساء:١٣١].

{{Na ni vya Mwenyezi Mungu vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini, na kwa hakika tuliwausia waliopewa kitabu kabla yenu, na nyinyi pia kwamba mumche Mwenyezi Mungu na mkikufuru hakika ya Mwenyezi Mungu ni vyake vilivyomo mbinguni na ardhini na Mwenyezi Mungu ni mkwasi na mwenye kusifiwa}}.

Amrisho hilo la kumcha Mwenyezi Mungu ni kwa wote wanaume na wanawake. Lakini kwa vile wanaume ndio wasimamizi wa wanawake inapaswa juu yao kuwalazimisha wake zao juu la suala la kumcha Mwenyezi Mungu kwa njia yoyote ile iliopaswa kisheria. Ushahidi wa haya; Anasema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿ٱلرِّجَالُ قَوَّٰمُونَ عَلَى ٱلنِّسَآءِ بِمَا فَضَّلَ ٱللَّهُ بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ وَبِمَآ أَنفَقُوا۟ مِنْ أَمْوَٰلِهِمْ ۚ﴾ [النساء:٣٤].

{{Wanaume ni wasimamizi wa wanawake kwa vile walivyofadhilishwa na Mwenyezi Mungu baadhi juu ya baadhi na kwa mali wanayotoa}}. Na yote hayo isipokuwa kwa sababu za kimsingi kama utoaji na utazamaji wao wa mambo kibusara. Amesema Shanqiti: Mwenyezi Mungu ameashiria kuwa mwanamume ni bora kuliko mwanamke kutokana na utukufu na ukamilifu alionao, na mwanamke ana upungufu wa kimaumbile kutokana na kujipamba.

Inafahamika kuwa wanawake waliokuwa katika zama hizi wanatofautiana na wanawake wa zama za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). Mbali na wanawake wetu hawatafautiani na wanawake wasiokuwa na dini na kukhalifu

miongozo ya dini kwa mfano:

a. Kutangamana wanaume na wanawake katika serikali kazini.

b. Kutangamana na wanaume katika vyuo vikuu

c. Kutangamana na wanaume katika masoko.

d. Kutangamana na wanaume katika gari za abiria.

Vyote hivyo vimeharamishwa na ushahidi wa hayo ni pindi alipotoka Musa na kuelekea Madyana kufika kisimani alikuta pote la watu wanaywesha wanyama wao na akawakuta wanawake wawili wanazuia wanyama wao wasitangamane na wanyama wengine. Akauliza sababu ya kufanya jambo hilo. Wakasema hatunyweshi sisi mpaka wamalize hao kunywesha (yote hayo ni kutokana na unyonge wetu na kutopenda kutangamana na watu).

Amesema Mwenyezi Mungu kusimulia tukio hilo ndani ya Quraan tukufu: "Na alipoyafikia maji ya Madyana alikuta umati wa watu wananywesha (wanyama wao) na akakuta karibu yao wanawake wawili na wanyama wao akawauliza mna nini? Wakasema hatunyweshi sisi mpaka wamalize hao kuchunga, na baba yetu sisi ni mzee sana". Zingatieni msimamo huo ulinganishwe na yanayo fanyika leo.

Na katika hadithi ya Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Waamrisheni watoto wenu kusali hali wakiwa na umri wa miaka saba, na wapigeni wakifika miaka kumi na watenganisheni katika malazi]. Hadithi hii inamaanisha kutengamana kati ya mwanamume na mwanamke.

Na miongoni mwa ukiukaji wa maaadili ya kiislamu ni wanawake kudhihirisha mapambo yao jambo ambalo linapelekea katika uasharati kwani Mwenyezi Mungu kaamrisha kuvaa hijabu, kuhifadhi macho na kukataza kujishaua na kudhihirisha mapambo yake.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿قُل لِّلْمُؤْمِنِينَ يَغُضُّوا مِنْ أَبْصَارِهِمْ وَيَحْفَظُوا فُرُوجَهُمْ ذَٰلِكَ أَزْكَىٰ لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا يَصْنَعُونَ ﴿٣٠﴾ وَقُل لِّلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَارِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَلْيَضْرِبْنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوْ آبَائِهِنَّ أَوْ آبَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ أَبْنَائِهِنَّ أَوْ أَبْنَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي أَخَوَاتِهِنَّ أَوْ نِسَائِهِنَّ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُنَّ أَوِ التَّابِعِينَ غَيْرِ أُولِي الْإِرْبَةِ مِنَ الرِّجَالِ أَوِ الطِّفْلِ الَّذِينَ لَمْ يَظْهَرُوا عَلَىٰ عَوْرَاتِ النِّسَاءِ وَلَا يَضْرِبْنَ بِأَرْجُلِهِنَّ لِيُعْلَمَ مَا يُخْفِينَ مِن زِينَتِهِنَّ وَتُوبُوا إِلَى اللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهَ الْمُؤْمِنُونَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٣١﴾﴾ [النور: ٣٠-٣١].

{{Na waambie waumini wanaume wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao, wala wasionyeshe uzuri wao kwa unao dhihirika, na waangushe shungi zao kwa mpaka vifuani mwao, na wasionyeshe mapambo yao ila kwa wanaume zao, au baba zao, au baba za waume zao, au watoto wao, au watoto wa waume zao, au kaka zao, au wana wa kaka zao, au wana wa dada zao, au wanawake wenziwao, au wale iliyowamiliki mikono yao ya kiume au wafuasi wanaume wasio na matamanio, au watoto ambao hawajajua mambo yaliyokhusu ukwe wala wasipige miguu yao ili yajulikane wanayoyaficha katika mapambo yao. Na tubuni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi waumini ili mupate kufanikiwa}}.

Wamesema wanazuoni: macho ndio mlango mkubwa wa moyo, na ndiyo kuimarika kwa hisia kwa ajili hiyo tunapaswa kutahadhari nayo (macho) na kuhifadhi tupu, ima ni kujilinda na uzinifu au kuhifadhi uchi, na wasionyeshe uzuri wao isipokua kwa wale walio ruhusiwa kama Aya iliyotangulia. Imethibitu katika Musnad ya Imam Ahmad kwamba Abu Huraira amepokea hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akisema: (Aina mbili za watu wa motoni na mmoja wao ni mwanamke avaae nguo nyepesi isiositiri na inaonyesha uchi).

KHUTBA YA PILI.

Wanawake wema waliotangulia walikua wakijiheshimu na wakivaa hijabu na kumcha Mwenyezi Mungu, tazama kisa cha Uzushi, pindi Mama yetu 'Aisha hakumsemesha swahaba Swafwan hata neno na hivyo ndivyo walivyo fika Madina. Na pindi walipoamrishwa kuvaa hijabu waliitikia kwa haraka wito huo bila ya kuchelewa. Ummu Salama amesimulia akisema pindi ilipoteremka Neno lake Mwenyezi Mungu: »Wateremsha nguo zao». Wamefika wanawake wa kianswaari kama juu ya vichwa vyao kuna kurabu, na wakivaa vazi jeusi Mwenyezi Mungu mkubwa kwa kuitika wito wake na wito wa Mtume wake.

Imepokewa na Ummu Salama kuwa akisema mwanamke akimwambia Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) kuwa mimi ni mwanamke kurefusha vazi langu na natembea katika maeneo yenye uchafu? Akasema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [itatwahirika baada yake]. Amesema kuwa mwanamke huyo anakusudia kuficha nguo zake pindi anapotembea kama ilivyo ada ya waarabu. Wanawake wetu na mabanati wetu wakiachwa bila ya muongozo wa dini watafanya maovu na Mwenyezi Mungu kajaalia kuwa wanaume ndio wasimamizi wao kutokana na upungufu wa akili na dini na hilo Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) anausia wanaume akisema: [Nakuusieni kuwafanyia wema wake zenu kuweni ni wasaidizi wenu].

Mwisho

Ndugu Waislamu, tumeona khatari kubwa ya Fitna za Wanawake na athari mbaya katika jamii. Ni jukumu la kila Muislamu kujitolea kubadilisha hali mbaya tunaoishi kwa sasa katika jamii yetu. Ikiwa ni mkeo, mamako, binti yako, binti wa Muislamu mwenzako, wote ni jukumu la kila Muislamu kuwafundisha wanawake maadili na tabia njema. Tukifanya hivyo, kwa hakika jamii yetu itabadilika na tutapata rehma za Allah (Subhaanahu wa Taala) pamoja na hifadhi yake kutokana na kila fitna. Namuomba Mwenyezi Mungu atulinde na fitna za wanawake, na awalinde wao na moto uumizao, Ewe Mwenyezi Mungu tupe mema hapa duniani na kesho akhera.

[4] UHIMIZAJI JUU YA SUBIRA

Lengo la Khutba:

1. Kuwafundisha watu Subira na ni sera ya waumini.
2. Kujua vigawanyo vya subira.
3. Dharura ya kuwa na subira katika maisha yetu.

KHUTBA YA KWANZA.

Utangulizi

Ikiwa subira ni chungu mwisho wake ni tamu. Subira ndio silaha ya Muislamu ya kupambana na mitihani ya ulimwengu. Bila ya subira Muislamu hawezi kufaulu katika kufanya ibada na mambo ya akhera. Ombeni msaada kwa kusubiri na kuswali. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) yuko pamoja na wanaosubiri. Subira huvuta kheri. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) katika Qur'an tukufu:

قال تعالى: ﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱصۡبِرُواْ وَصَابِرُواْ وَرَابِطُواْ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ ٢٠٠ ﴾ [آل عمران:٢٠٠].

{{Enyi mulioamini subirini na shindaneni na kueni macho na mcheni Mwenyezi Mungu ili mupate kufanikiwa}].

Jueni waja wa Mungu kuwa subira ni ukarimu usiokwisha, na ulinzi usioshindwa, na ngome isiyovunjika, subira na nusra ni ndugu wawili na asie vaa vazi la subira basi hushindwa na nafasi na sheitwani.

Subira ni ndugu yake muumini wala hana Imani kwa asie kuwa na subira, na akiwa nayo basi Imani yake ni ndogo na mtu asiekuwa na subira ni kama anavyosema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿ وَمِنَ ٱلنَّاسِ مَن يَعۡبُدُ ٱللَّهَ عَلَىٰ حَرۡفٖۖ فَإِنۡ أَصَابَهُۥ خَيۡرٌ ٱطۡمَأَنَّ بِهِۦۖ وَإِنۡ أَصَابَتۡهُ فِتۡنَةٌ ٱنقَلَبَ عَلَىٰ وَجۡهِهِۦ خَسِرَ ٱلدُّنۡيَا وَٱلۡأٓخِرَةَۚ ذَٰلِكَ هُوَ ٱلۡخُسۡرَانُ ٱلۡمُبِينُ ١١ ﴾ [الحج: ١١].

{{Na katika watu wapo wanao muabudu Mwenyezi Mungu kwa ukingoni. Ikimfikia kheri hutukia kwayo, na ikimfikia misukosuko hugeuza uso wake, amekhasiri duniani na akhera hii ndiyo khasara iliyo wazi}}. Subira ni tabia za waumini waliokamilika, hawezi kuwa nayo mtu ila baada ya kujaaliwa na Mwenyezi Mungu. Amesema Imam Ahmad; Mwenyezi Mungu ametaja subira katika Qur'an mara tisini (90) katika sehemu tofauti.

Faida ya kusubiri

a. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) atawapa malipo yao bila ya hesabu. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿ إِنَّمَا يُوَفَّى ٱلصَّٰبِرُونَ أَجۡرَهُم بِغَيۡرِ حِسَابٖ ١٠ ﴾ [الزُمَر:١٠].

{{Hakika wenye subira watapewa ujira wao bila ya hesabu}}.

b. Mwenyezi Mungu yuko pamoja nao katika kuwaongoza na kuwanusuru. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَاصْبِرُوا إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿٤٦﴾﴾ [الأنفال: ٤٦].

{{Subirini hakika Mwenyezi Mungu yupo pamoja na wenye kusubiri}}.

c. Mwenyezi Mungu kuifanya subira ni sehemu katika uongozi. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَجَعَلْنَا مِنْهُمْ أَئِمَّةً يَهْدُونَ بِأَمْرِنَا لَمَّا صَبَرُوا وَكَانُوا بِآيَاتِنَا يُوقِنُونَ ﴿٢٤﴾﴾ [السجدة:٢٤].

{{Na tukafanya miongoni mwao waongozi wanao ongoza watu kwa amri yetu, walipo subiri na wakawa na yakini}}.

d. Subira ni bora kwa aliyekuwa nayo. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَلَئِن صَبَرْتُمْ لَهُوَ خَيْرٌ لِّلصَّابِرِينَ ﴿١٢٦﴾﴾ [النحل:١٢٦].

{{Na ikiwa mutasubiri, basi hakika hiyo ni bora zaidi kwa wanaosubiri}}.

e. Subira na Taqwa ni kinga ya vitimbi vya maadui. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَإِن تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا لَا يَضُرُّكُمْ كَيْدُهُمْ شَيْئًا إِنَّ اللَّهَ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ﴿١٢٠﴾﴾ [آل عمران:١٢٠].

{{Nyinyi mkisubiri na mkamcha Mwenyezi Mungu, hila zao hazitakudhuruni kitu}}.

f. Subira inaleta manufaa. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اصْبِرُوا وَصَابِرُوا وَرَابِطُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٢٠٠﴾﴾ [آل عمران:٢٠٠].

{{Enyi mulioamini subirini, na shindaneni kusubiri na kuweni macho na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kufanikiwa}}.

g. Kuwabashiria Mwenyezi Mungu wenye subira kwa kheri tatu. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَبَشِّرِ الصَّابِرِينَ ﴿١٥٥﴾ الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُم مُّصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿١٥٦﴾ أُولَئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُهْتَدُونَ ﴿١٥٧﴾﴾ [البقرة:١٥٥-١٥٧].

{{Wabashirieni subira wale ambao ukiwasibu msiba husema hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake yeye hakika tutarejea, hao juu zao zitakua baraka zitokazo kwa mola wao mlezi na rehema nao ndio wenye kuongoka}}.

h. Subira hutia mtu peponi na humuokoa kutokana na moto. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال عز وجلّ : ﴿إِنِّي جَزَيْتُهُمُ الْيَوْمَ بِمَا صَبَرُوا أَنَّهُمْ هُمُ الْفَائِزُونَ ﴿١١١﴾﴾ [المؤمنون:١١١].

{{Hakika Mimi leo nimewalipa (Pepo) kwa sababu ya kusubiri kwao, bila shaka hao ndio wenye kufaulu}}.

Uhakika wa subira

Subira katika lugha ya kiarabu ina maana kuzuia, na maana inayokusudiwa ni kufunga nafsi kutokana na huzuni, kuzuia ulimi kwa kushtaki, viungo kwa kupiga makofi na kupasua mifuko. Na akasema Nun Misri: “Ni kujiepusha na makosa na kutulia pindi unapopatwa na balaa na kudhihirisha utajiri pindi unapofikwa na umaskini”.

Aina za mashtaka:

a. Mashtaka yasiyopingana na subira, kama alivyosema Mtume Yaakub. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال عز وجلّ : ﴿قَالَ إِنَّمَآ أَشۡكُواْ بَثِّي وَحُزۡنِيٓ إِلَى ٱللَّهِ﴾ [يوسف: ٨٦]

{{Hakika mimi namshtakia Mwenyezi Mungu sikitiko langu na huzuni yangu}}.

Na akasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال عز وجلّ ﴿فَصَبۡرٞ جَمِيلٞۖ﴾ [يوسف:١٨].

{{Subira ni njema}}.

b. Mashtaka ya saa zote na ya kusimulia

Vigawanyo vya subira:

a. Subira katika maamrisho ya Mwenyezi Mungu
b. Subira katika makatazo ya Mwenyezi Mungu
c. Subira kutokana na kudra zake Mwenyezi Mungu.

Na kama alivyosema Sheikh AbdulKadir Jeilani: hapana budi kwa mja kufanya jambo, na kukatazika kwa jambo na kusubiri kwa Qadar.

Mambo haya matatu Luqman amemuusia mwanawe akisema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿يَٰبُنَيَّ أَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ وَأۡمُرۡ بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَٱنۡهَ عَنِ ٱلۡمُنكَرِ وَٱصۡبِرۡ عَلَىٰ مَآ أَصَابَكَ﴾ [لقمان:١٧].

{{Ewe mwanangu shika sala, na amrisha mema, na kataza maovu, na subiri kwa yanayokupata}}. Muumini hatamani matatizo na anasubiri pindi anapopatwa na balaa. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) siku miongoni mwa siku alipokutana na adui akimnyemelea mpaka kupinduka jua akamsimamisha akasema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Enyi watu musitamani kukutana na adui na muombe Mwenyezi Mungu afya na mukikutana nao subirini na jueni kuwa pepo iko chini ya upanga].

Na Abubakar Sidiq amesema “Napenda kuwa na afya nishukuru ni bora kuliko kupatwa na mitihani nisubiri, na muumin anajua lolote linalompata ni kheri. Kama alivyopokea hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Ajabu ya muumin ni kuwa mambo yake yote ni kheri, akipata furaha hushukuru na akipata msiba husubiri na yote ni kheri].

Maisha yote ni mitihani. Anasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالى: ﴿وَنَبۡلُوكُم بِٱلشَّرِّ وَٱلۡخَيۡرِ فِتۡنَةٗۖ وَإِلَيۡنَا تُرۡجَعُونَ ٣٥﴾ [الأنبياء:٣٥].

{{Na tunakujaribu kwa mitihani wa shari na kheri na kwetu sisi mtarudi}}. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) anawaonya waja wake wakati wowote ili apate kujua alie na subira na wakweli.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله: ﴿أَمۡ حَسِبۡتُمۡ أَن تَدۡخُلُواْ ٱلۡجَنَّةَ وَلَمَّا يَعۡلَمِ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ جَٰهَدُواْ مِنكُمۡ وَيَعۡلَمَ ٱلصَّٰبِرِينَ ١٤٢﴾ [آل عمران:١٤٢].

{{Je mnadai mtaingia peponi na hali Mwenyezi Mungu hajawapambanua wale miongoni mwenu waliopigana jihadi na hawajapambanua walio na subira}}.

Na akasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقوله تعالى: ﴿وَلَنَبۡلُوَنَّكُمۡ حَتَّىٰ نَعۡلَمَ ٱلۡمُجَٰهِدِينَ مِنكُمۡ وَٱلصَّٰبِرِينَ وَنَبۡلُوَاْ أَخۡبَارَكُمۡ ٣١﴾ [محمد:٣١].

{{Na bila shaka tutawajaribu mpaka tuwadhihirishe wapiganao jihad katika nyinyi na wanao subiri, nasi tutazifanya mitihani khabari zenu}].

Na akasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقوله تعالى: ﴿إِن يَمۡسَسۡكُمۡ قَرۡحٞ فَقَدۡ مَسَّ ٱلۡقَوۡمَ قَرۡحٞ مِّثۡلُهُۥۚ وَتِلۡكَ ٱلۡأَيَّامُ نُدَاوِلُهَا بَيۡنَ ٱلنَّاسِ وَلِيَعۡلَمَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَيَتَّخِذَ مِنكُمۡ شُهَدَآءَۗ وَٱللَّهُ لَا يُحِبُّ ٱلظَّٰلِمِينَ ١٤٠ وَلِيُمَحِّصَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَيَمۡحَقَ ٱلۡكَٰفِرِينَ ١٤١﴾ [آل عمران:١٤٠:١٤١].

{{Kama yamekupateni majeraha basi na hao watu wengine yamewapata majeraha mfano wa haya na si kwa namna hii tunawaletea watu kwa zama ili Mwenyezi Mungu awapambanue walioamini na awachague miongoni mwenu mashahidi na Mwenyezi Mungu hawapendi madhalimu}}.

Na akasema mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

و قال تعالى: ﴿إِنَّمَآ أَمۡوَٰلُكُمۡ وَأَوۡلَٰدُكُمۡ فِتۡنَةٞۚ وَٱللَّهُ عِندَهُۥٓ أَجۡرٌ عَظِيمٞ ١٥﴾ [التغابن:١٥].

{{Hakika mali yenu na watoto wenu ni jaribio na kwa Mwenyezi Mungu upo ujira mkubwa}}.

KHUTBA YA PILI

Inadhihiri pindi Mtume alipokuwa Makkah kama alivyopokea hadith na Khabbab bin Arat akisema: [Tumemshitakia Mtume ((SWALLA LLAHU ‘ALAYHI WASALLAM)) tukisema: je utuombee nusra kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Akasema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) huchukuliwa mtu kabla yenu akizikwa na hupasuliwa mara mbili kwa msumeno kuanzia kichwani na hukatwa nyama, mifupa yake kwa msumeno wa chuma,na huridhika na adhabu hiyo ili ahifadhike na dini yake, Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akapiga mfano akisema aende mtu kutoka Sana’a mpaka Hadhramut hamuogopi isipokuwa Mwenyezi Mungu, na mbwa mwitu yuko pamoja na mbuzi lakini munafanya haraka yaani mutapata adhabu ya washirikina basi subirini kama walivyosubiri kabla yenu].

Fadhila za Subira katika Hadith za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam)

a. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Muislamu yoyote akifikiwa na msiba basi na aseme kwako wewe Mwenyezi Mungu ndio marudio, Mwenyezi Mungu nilipe kutokana na msiba huo na unipe kheri baada yake].

b. Alipokufa Baba Salama akasema Mama Salama nani mbora kama Baba Salama? Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akamuoa Mama Salama ambaye ni bora kuliko yoyote.

c. Imepokewa na Aisha akisema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) : [Muumin yoyote akipatikana na msiba isipokuwa Mwenyezi Mungu humtosheleza hata kama amedungwa na mwiba].

d. Imepokewa na Abi Musa amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Akiwa mgonjwa mwanadamu au akisafiri, Mwenyezi Mungu humuandikia kama alivyokuwa mzima au akiwa mwenye kukaa].

Maneno ya baadhi ya Salaf juu ya Subira:

a. Amesema Sufyan kuhusu Neno lake Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قوله تعالى : ﴿ وَجَعَلْنَا مِنْهُمْ أَئِمَّةً يَهْدُونَ بِأَمْرِنَا لَمَّا صَبَرُوا ۖ وَكَانُوا بِآيَاتِنَا يُوقِنُونَ ﴿٢٤﴾ ﴾ [السجدة:٢٤]

{{Na tukafanya miongoni mwao waongozi wanao ongoza watu kwa amri yetu, walipo subiri na wakawa na yakini}}. Walipochukua Kichwa cha kila jambo (Subira) tukawafanya viongozi.

b. Walipotaka kumkata mguu Urwa bin Zubeir wakamwaambia: tukunyweshe kinywaji usisikie maumivu akasema Urwa: Mwenyezi Mungu amenipa mitihani ili aone subira yangu. Je nipinge amri yake? (kunywa kinywaji)

c. Amesema ‘Umar Ibn ‘Abdulaziz: Mwenyezi Mungu ampe neema mja na akampokonya neema hiyo na akasubiri basi subira hiyo inakuwa ni bora kuliko alichopokonywa.

d. Abubakar alipokuwa mgonjwa aliambiwa je hatukuitii tabibu? Akasema ashaniona tabibu, akaambiwa amekwambia nini? Akasema Abubakar ameniambia kuwa yeye ni mtendaji kwa anachotaka.

Ndugu yangu Muislamu: subiri udhia wa jirani yako na umfanyie wema, ima atatengana na wewe kwa kugura au kwa mauti. Ndugu yangu Muislamu subiri kwa jamii yako ukipata udhia kwao na utoshelezeke. Subiri kwa mke wako kutokana na makosa na upungufu. Huwezi kupata mwanamke aliye kamilika sifa zake, lazima usubiri na uridhike kwa tabia yake. Hapana budi kwa mwanamke kumsubiria mume wake kwani ndio sababu ya kudumu mapenzi.

Lazima uwasubirie wafanyikazi kwani hakuna mtu anayefanya wajibu wake kwa ukamilifu, na tabia za watu zinatafautiana basi hapana budi kuwa na subira na kutazama mambo kwa mwisho wake. Asiyekuwa na subira hupoteza kheri zote.

Namuomba Mwenyezi Mungu pamoja nanyi uwafikie na usaidizi katika kheri zote. Yeye ni muweza wa kila kitu. Namuomba Mwenyezi Mungu atusamehe na Waislamu, basi muombeni Mwenyezi Mungu msamaha na mtubie kwani yeye ni msamehevu na mwingi wa rehema.

Mwisho

Ndugu Muislamu mafanikio ya mwanadamu hapa Duniani na kesho siku ya Mwisho yanafungamana na Subira. Allah (Subhaanahu wa Taala) atamlipa Mwanadamu Kwa kiasi ya subira yake katika maisha yake hapa duniani.

Namuomba Mwenyezi Mungu mwafaka na usaidizi katika kila kheri, yeye ni muweza juu ya kila kitu, namuomba Mwenyezi Mungu msamaha kwa kila dhambi tuliofanya basi mtakeni Mwenyezi Mungu na muregee kwake, yeye ndiye mwingi wa kusamehe.

[5] UHIMIZAJI WA KUSEMA UKWELI NA UTAHADHARISHAJI WA KUSEMA UONGO

Lengo la Khutba:

1. Kuwazoesha Umma kusema ukweli katika muamala wao.
2. Kuwatahadharisha na sifa ya uongo.
3. Kuwajengea kujiamini kati yao.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Asili ya mwanadamu kuwa muovu katika zama zetu inatokana na kuacha dini kubwa nao ni ukweli waja wa Mwenyezi Mungu na kuusieni pamoja na kuusia nafsi yangu juu ya kumcha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala): "Enyi mlioamini, Mcheni Mwenyezi Mungu na kuweni pamoja na wakweli". Kuwa na ukweli na Mwenyezi Mungu ndio inaleta imani ya sawa, mkweli huwa anamtegemea Mwenyezi Mungu anasubiri anapopatwa na msiba, anashukuru anapopata neema, anakuwa mzuri kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na anakuwa mbaya pia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kwa ajili hiyo amewaamrisha waumini kuwa wakweli, akasema Mwenyezi Mungu:

Uhakika wa ukweli ni pale inapodhihiri katika jamii, na mpaka kuwa na imani kati yao, ienee kati yao heshima na mapenzi, amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Wenye kuuziana wana khiari madamu hawajatengana, wakiwa wakweli hubarikiwa na wakiwa waongo huondolewa Baraka].

Ukweli katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu

Ametaja Mwenyezi Mungu ukweli katika Qur'an tukufu katika Aya nyingi miongoni mwa Aya hizo ni:- Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قوله تعالى: ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَكُونُواْ مَعَ ٱلصَّٰدِقِينَ ١١٩﴾ [التوبة:١١٩]

{{Enyi mlioamini, Mcheni Mwenyezi Mungu nakuweni pamoja na wakweli}}. Maamrisho haya ya Allah kwa Waislamu ni wawe wakweli kwa hali yao yote, kwa maneno na vitendo. Na Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقوله تعالى: ﴿لِّيَجۡزِيَ ٱللَّهُ ٱلصَّٰدِقِينَ بِصِدۡقِهِمۡ﴾ [الأحزاب:٢٤]

{{Ili awalipe wa kweli kwa sababu ya ukweli wao}}. Na neno lake Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال الله تعالى: ﴿هَٰذَا يَوۡمُ يَنفَعُ ٱلصَّٰدِقِينَ صِدۡقُهُمۡۚ لَهُمۡ جَنَّٰتٞ تَجۡرِي مِن تَحۡتِهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدٗاۚ﴾ [المائدة:١١٩]

{{Mwenyezi Mungu Atasema: Hii ndiyo siku ambayo ukweli utawafaa ukweli wao}}. Siku ya kiama kitu kitakacho msaidia mwanadamu ni ukweli. Kama alikuwa mkweli duniani basi siku ya kiama ataokoka na Moto wa jahannam.

Aina ya Ukweli

Wanakosea wengi miongoni mwa watu wanapodhani kuwa ukweli ni ule wa maneno pekee, lakini ukweli pia ni wa vitendo na hali. Tunaweza kuweka wazi kama ifuatavyo.

- Ukweli wa maneno, inampasa kila mwanadamu kuhifadhi ulimi wake na kutozungumza isipokuwa ukweli, na Mwenyezi Mungu atauliza jambo hilo.
- Ukweli wa vitendo ni awe sawa siri yake na dhahiri bila ya kutofautiana kati ya dhahiri yake na usiri wake alikuwa Hassan Basri akiamrisha jambo huwa wa kwanza kulifanya, na akikataza jambo huwa wa kwanza kuliacha. Amesema Mutrif ukiwa sawa usiri wa mja na udhahiri wake, Mwenyezi Mungu husema huu ni mja wangu ni mkweli.
- Ukweli katika hali, nao ndio daraja ya juu kuwa mkweli katika ikhlas na kuogopa, toba, kutarajia na nyinginezo.

KHUTBA YA PILI

Uislamu umeheshimu haki ya ukweli, na unachukia uongo na urongo ni alama ya unafiki. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Alama za mtu mnafiki ni tatu: akisema husema uongo, akiahidi huenda kinyume na ahadi yake, akiaminiwa hufanya khiyana". Ukiangalia hali ya Waislamu leo utaona wana upungufu katika upande wa ukweli, na ndio sababu ya kudhoofika kwa imani, na kuenea kwa maasi, na kupenda dunia. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Ukweli una utulivu na uongo una wasiwasi].

Sura za Uongo:-

1. Kusema uongo wazazi kuwaambia watoto wao, na uislamu umebainisha kuwa malezi ya watoto yanatakiwa yasipatikane ndani yake uongo, ili wapate kuzoea ukweli. Amepokea 'Abdallah Bin 'Amir akisema: "Aliniita mamangu nikiwa mdogo na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amekaa nyumbani kwetu, akamuuliza mamangu unataka kumpa kitu gani? Akasema: tende, kama hutampa kitu basi utakuwa muongo"
2. Kuenea uongo katika mazungumzo ya watu, na vitendo vyao.
3. Amepokea Anas hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akisema: [Mwenye kuwa na mambo matatu huwa mnafiki, akizungumza husema uongo, akiahidi huenda kinyume, akiaminiwa hufanya khiana].
4. Kuvunja ahadi, na sura za kuvunja ahadi, kutohudhuria sehemu bila ya sababu, kuchelewa kufika kwa wakati wake.
5. Kuhini amana, watu wengi hawafanyi wajibu wao kwa namna inavyotakiwa kama kuchelewa kazini na akija mapema utamuona anajishughulisha na simu, kusoma gazeti, kuchukua likizo ya ugonjwa na si mgonjwa.
6. Kufanya khiana katika mauzo, kama kuficha aibu ya bidhaa na kununuliwa bidhaa yake kwa bei mzuri.

7. Kutaka kitu na kudai umasikini. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Mwenye kuomba watu ili apate kuzidisha mali yake basi anaomba kaa la moto].
8. Kuficha mwenye kuposa au kuposwa kwa aibu aliokuwa nao na kudhihirisha uzuri.

Wanaosema uongo mwingi leo ni wafanya biashara, ili kula mali ya watu kwa dhulma. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Madhambi makubwa ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu, kuwaasi wazazi wawili, kuua nafsi na kuapa kiapo cha uongo].

Mcheni Mwenyezi Mungu na kumbukeni neno lake Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): "Wakisema ukweli hubarikiwa katika biashara yao, na wakificha na kusema uongo huondolewa baraka" na lau kama wafanya biashara watasema ukweli watabarikiwa katika biashara yao.

Faida ya Ukweli:-

1. Kuingia peponi, ameulizwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amali ya peponi akasema ni Ukweli na hakuna kitakachomuokoa mwanadamu siku ya kiyama isipokuwa ni ukweli.
2. Kuafikiwa kwa kila jambo la kheri. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) kumuambia Ka'ab siku ya vita vya tabuuk: [Huyu amesema ukweli].
3. Kusalimika kutokana na maangamivu, kisa cha watu watatu walio funikwa na pango, mmoja wao akasema: "Haitokuokoeni isipokuwa ukweli, aombe kila mmoja wenu kwa jambo ambalo alilokuwa nalo ukweli"
4. Kuwa mzuri ndani yake.
5. Ukweli unaleta maslahi ya duniani na kesho akhera,
6. Ukweli unaleta utulivu.
7. Mkweli hadhuriwi na fitna.
8. Ukweli ndio asili ya wema, na uongo ndio asili ya uovu, kama alivyosema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Jilazimisheni na ukweli kwani ukweli unaleta wema, na hatowacha mtu kusema ukweli mpaka ataandikiwa kuwa yeye ni mkweli, na tahadhari na uongo kwani uongo unaleta uovu, na uovu unapeleka mtu kuingia motoni, na hatoacha mtu kusema uongo mpaka ataandikwa kuwa muongo].
9. Mkweli hawi mnafiki amesema Mtume Mwenyezi Mungu: [Mnafiki akizungumza husema uongo, akiaminiwa hufanya khiyana, akiahidi hatimizi].
10. Mkweli huruzukiwa firasa (kuona mbali).
11. Mkweli husifiwa na sifa nzuri, kama alivyowasifu Mwenyezi Mungu manabii wake
12. Ukweli huleta Baraka katika mauzo.

Tumuombe Mwenyezi Mungu atujalie ni miongoni mwa waja wake wa kweli na wenye kufaulu siku ya kiama kwa kuingia peponi.

Mwisho

Ndugu Waumini, tumeona wazi umuhimu wa ukweli na kusema ukweli katika mafundisho ya dini yetu. Ukiwa mkweli utapendwa na Mwenyezi Mungu na utapendwa na watu wote. Ukweli ndio ufunguo wa mambo yote ya kheri. Na uongo ni ufunguo wa mambo yote ya shari. Mwenyezi Mungu atuepushe na uongo, na atuafikie kushikamana na ukweli mpaka tuondoke duniani tukiwa wakweli na tukutane na yeye tukiwa wa kweli.

[6] TOBA BAADA YA KUFANYA MAASI

Lengo la Khutba:

1. Kurudi kwa Mwenyezi Mungu.
2. Kuwalea watu kufanya suluhu kwa Mwenyezi Mungu.
3. Kukata tama kwa rehema ya mwenyezi Mungu.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Kutubia kwa Mwenyezi Mungu ni jambo ambalo hatochoka nalo Muislamu, vipi na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alikua akitubia kwa Mwenyezi Mungu kwa siku mara mia.

Ndugu zangu Waislamu wadhifa wa mwanadamu ni kufanya ibada ya Mwenyezi Mungu, ameumbwa kwa ajili ya hiyo ibada akifanya jema amejifanyia nafsi yake na ametekeleza wajibu wake, akifanya maasia basi ni upungufu katika kazi yake, na madhara inamrejea mwenyewe.

Je mnajua ndugu zangu Waislamu? Kwamba maasi ni uchafu. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Mwenye kufanya uchafu huo basi ajistiri na stara ya Mwenyezi Mungu hata kama hatuoni uchafu huo wala hatusikii harufu ya uchafu huo katika moyo].

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالى: ﴿كَلَّا ۖ بَلْ ۜ رَانَ عَلَىٰ قُلُوبِهِم مَّا كَانُوا۟ يَكْسِبُونَ ١٤﴾ [المطفِّفين:١٤].

{{Sivyo hivyo, Bali yanatia kutu juu ya nyoyo zao maovu waliyokuwa wakiyachuma}}.

Na Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Mwanadamu akifanya dhambi huwa inaingia nukta nyeusi katika moyo wake, akitubia husafishwa dhambi hilo, na akizidisha huzidi weusi]. Madhambi ambayo yanakusanyika katika moyo bila ya toba hupandana na kuziba moyo. Ndugu zangu Waislamu, nguo ikizidi kuwa chafu bila ya kusafisha matokeo yake inakuaje? Moyo mfano wake ni huo.

Ndugu zanguni Waislamu tunafanya madhambi usiku na mchana bila ya kumuomba Mwenyezi Mungu msamaha tunasubiri nini kutokana na moyo hoyo?

Ndugu zangu Waislamu, sote tunafanya madhambi, lakini kinacho tupambanua kati yetu kuna wanao tubia baada ya kufanya madhambi, na kuna wanao ghafilika kwa kutubia.

Umuhimu wa Toba katika Qur'an

Ndugu zangu Waislamu, mlango wa toba uko wazi, na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) anatuitia tutubie Akisema neno lake tukufu:

قال الله تعالى: ﴿قُلْ يَٰعِبَادِيَ ٱلَّذِينَ أَسْرَفُوا۟ عَلَىٰٓ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا۟ مِن رَّحْمَةِ ٱللَّهِ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ يَغْفِرُ ٱلذُّنُوبَ جَمِيعًا ۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلْغَفُورُ ٱلرَّحِيمُ ﴿٥٣﴾﴾ [الزُّمَر:٥٣].

{{Sema, Enyi waja wangu mliodhulumu nafsi zenu, Msikate tamaa na rehma ya Mwenyezi Mungu; bila shaka Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote; hakika yeye ni mwingi wa kurehemu}}.

Moja wapo ya majina ya Mwenyezi Mungu ni msamehevu, mwenye kukubali toba, Mwenyezi Mungu anakielezea kisa cha Musa alipomuua mtu bila ya kukusudia akisema:

قال الله تعالى: ﴿قَالَ رَبِّ إِنِّى ظَلَمْتُ نَفْسِى فَٱغْفِرْ لِى فَغَفَرَ لَهُۥٓ ۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلْغَفُورُ ٱلرَّحِيمُ ﴿١٦﴾﴾ [القصص:١٦]

{{Akasema: Mola wangu, Bila shaka nimedhulumu nafsi yangu, basi nisamehe. Naye Mwenyezi Mungu akamsamehe. Kwa yakini yeye ni mwingi wa kusamehe na Mwingi wa rehema}}.

Mwenyezi Mungu Ametuhimiza na kusisitiza waja wake kurudi kwake kwa kuomba msamaha na maghfira.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقوله تعالى: ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ تُوبُوٓا۟ إِلَى ٱللَّهِ تَوْبَةً نَّصُوحًا عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَن يُكَفِّرَ عَنكُمْ سَيِّـَٔاتِكُمْ﴾ [التحريم:٨].

{{Enyi mlioamini, tubuni kwa Mwenyezi Mungu toba iliyo ya kweli. Huenda Mola wenu akakufutieni maovu yenu}}.

Umuhimu wa Toba katika Sunna za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam)

Amepokea Abi Musa ‘Abdallah bin Kais Asha’ari hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Mwenyezi Mungu hunyosha mikono yake ili atubiye aliyekosea wakati wa usiku, na hunyosha mkono wakati wa mchana ili atubiye aliyekosea wakati wa usiku].

Inapaswa kutubia kwa makosa yote, na ndio kufaulu, na kuchelewa kutubia ni uovu. Amepokea Abu Huraira hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema: [Mimi natubia kwa Mola wangu zaidi ya mara sabini]. Na amesema tena Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Enyi watu tubieni kwa Mwenyezi Mungu na muombe msamaha, mimi natubia kwa siku moja mara mia]. Mwenyezi Mungu ameamrisha waja wake watubie taubatu nasuha, Amesema Mwenyezi Mungu: “ Enyi mlioamini, tubuni kwa Mwenyezi Mungu toba iliyo ya kweli. Huenda Mola wenu akakufutieni maovu yenu”.

Masharti ya Tawbatu Nasuha:

1. Kujivua na dhambi.
2. Kujuta kwa kosa alilolifanya.
3. Kuazimia kutorudia tena kwa kosa lile.

Wamesema wanazuoni akirudia kosa la kwanza baada ya kutubia hamlazimu kutubia toba ya nasuha kwa mara ya pili. Na miongoni mwa masharti ya toba ni kurudisha haki ya mtu.

Hali ya Wenye Kutubia

Wenye kutubia leo wanaendelea kufanya makosa, na wakidai kutubia na wakitarajia mazuri mbele ya Mwenyezi Mungu na kutoogopa adhabu yake. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله ﴿أَفَأَمِنُوا۟ مَكْرَ ٱللَّهِ ۚ فَلَا يَأْمَنُ مَكْرَ ٱللَّهِ إِلَّا ٱلْقَوْمُ ٱلْخَٰسِرُونَ ﴿٩٩﴾﴾ [الأعراف:٩٩]

{{Je, wameaminisha kuadhibiwa na Mwenyezi Mungu? Hawaaminishi adhabu ya Mwenyezi Mungu ila watu wenye khasara}}.

Amesema Hassan Basri: “Muumini anafanya matendo mazuri na yeye anaogopa adhabu ya Mwenyezi Mungu lakini mtu muovu anafanya maasi na anayo matarajio”

Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) anawahimiza watu kuswali rakaa mbili anapotubia. Amesikiwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema: [Mtu yoyote akifanya maasi na akatawadha kuswali rakaa mbili, isipokuwa Mwenyezi Mungu humsamehe mja huyo].

Na amesema tena Mtume wa Mwenyezi Mungu: [Mtu yoyote anayetawadha na akakamilisha udhu wake na akasema nashuhudia kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu na Muhammad ni Mtume wake, isipokuwa hufunguliwa milango ya pepo minane aingia atakao].

KHUTBA YA PILI

Toba haifai wakati mtu anapotolewa roho au jua linapotokea upande wa magharibi, anasema Mwenyezi Mungu:

Amepokea Abu Huraira hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema: [Haisimami kiyama mpaka jua litoke upande wa magharibi]. Na amesema tena Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Anayetubia kabla ya jua kutoka upande wa magharibi, basi Mwenyezi Mungu hukubali toba yake].

Na amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) : [Mwenyezi Mungu aliyetukuka hukubali toba ya mja kabla ya kukata roho.

Na amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَلَيْسَتِ ٱلتَّوْبَةُ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ ٱلسَّيِّـَٔاتِ حَتَّىٰٓ إِذَا حَضَرَ أَحَدَهُمُ ٱلْمَوْتُ قَالَ إِنِّى تُبْتُ ٱلْـَٰٔنَ وَلَا ٱلَّذِينَ يَمُوتُونَ وَهُمْ كُفَّارٌ﴾ [النساء:١٨]

{{Hawana toba yake ambao Hufanya maovu mpaka mauti yamewahudhuria mmoja wao akasema: Hakika mimi sasa na tubu}}. Hakubaliwi toba yake wakati wa kukata roho ikiwa hakuomba msamaha kabla ya hapo.

Faida ya Toba:-

1. Kupata msaada wa milele katika uhai wa dunia na kesho akhera, amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِّن ذَكَرٍ أَوْ أُنثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهُ حَيَاةً طَيِّبَةً ۖ وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُم بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩٧﴾﴾ [النحل:٩٧]

{{Wafanyaji mema, wanaume na wanawake, hali yakuwa ni Waislamu, tutawahuisha maisha mema, na tutawapa ujira wao mkubwa Akhera. Kwasababu, ya yale mema walikuwa wakiyatenda}}.

Qur'an imetaja kuwa amali njema ni iliyokamilika mambo matatu nayo ni:-

a. Kuafikiana kwa yale alichokuja nacho Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا ۚ﴾ [الحشر: ٧]

{{Na anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho}}.

b. Iwe kwa ajili yake Mwenyezi Mungu. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ﴾ [البيّنة: ٥]

{{Wala hawakuamrishwa ila kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia dini, wawache dini za upotofu}}.

c. Iwe imejengwa na misingi ya akida, Amesema Mwenyezi Mungu:

قال تعالى : ﴿مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِّن ذَكَرٍ أَوْ أُنثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ﴾ [النحل:٩٧]

{{Wafanyaji mema, wanaume na wanawake, hali ya kuwa ni wenye imani}}. Kinyume chake, lau kama si muumini haitokubaliwa amali yake.

2. Kupata uongofu na amani kutoka kwa Allah (Subhaanahu wa Taala). Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالى : ﴿الَّذِينَ آمَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُم بِظُلْمٍ أُولَٰئِكَ لَهُمُ الْأَمْنُ وَهُم مُّهْتَدُونَ ﴿٨٢﴾﴾ [الأنعام:٨٢]

{{Hapana shaka kuwa wale walioamini na hawakuchanganya imani yao na ushirikina kuwa hao ndio watakao pata amani, nao ndio waliongoka}}.

3. Ubadilishaji wa maovu kwa amali njema, kama alivyosema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قوله تعالى: ﴿إِلَّا مَن تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ عَمَلًا صَالِحًا فَأُولَٰئِكَ يُبَدِّلُ اللَّهُ سَيِّئَاتِهِمْ حَسَنَاتٍ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٧٠﴾﴾ [الفرقان:٧٠]

{{Ila Yule atayetubia na kuamini na kufanya vitendo vizuri; basi ndio Mwenyezi Mungu atawabadilisha maovu yao kuwa mema}}.

4. Kufaulu kupata radhi zake Mwenyezi Mungu na kuokoka na moto. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قوله تعالى: ﴿وَٱلَّذِينَ إِذَا فَعَلُواْ فَٰحِشَةً أَوۡ ظَلَمُوٓاْ أَنفُسَهُمۡ ذَكَرُواْ ٱللَّهَ فَٱسۡتَغۡفَرُواْ لِذُنُوبِهِمۡ وَمَن يَغۡفِرُ ٱلذُّنُوبَ
إِلَّا ٱللَّهُ وَلَمۡ يُصِرُّواْ عَلَىٰ مَا فَعَلُواْ وَهُمۡ يَعۡلَمُونَ ١٣٥ أُوْلَٰٓئِكَ جَزَآؤُهُم مَّغۡفِرَةٞ مِّن رَّبِّهِمۡ وَجَنَّٰتٞ تَجۡرِي مِن تَحۡتِهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ
خَٰلِدِينَ فِيهَاۚ وَنِعۡمَ أَجۡرُ ٱلۡعَٰمِلِينَ ١٣٦﴾ [آل عمران:١٣٥:١٣٦]

{{Na ambao wanapofanya uchafu au kudhulumu nafsi zao, hukumbuka Mwenyezi Mungu na kuomba msamaha kwa dhambi zao. Na nani anaye samehe dhambi isipokuwa Mwenyezi Mungu? Na hawaendelei na maovu waliyoyafanya, hali wanajua. Hao ndio ambao malipo yao yatakuwa msamaha kwa Mola wao na Bustani zinazopita mito mbele yake, ambamo watakaa milele. Na ni wema ulioje ujira wa watendao mema}}. Maana yake, baada yakufanya madhambi wanaudi nyuma na kumkubuka Allah na kuaomba msamaha kwa madhambi waliyoyafanya.

Amepokea Abu Huraira hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema: [Kuna mtu amefanya madhambi, akasema Mola wangu nimefanya madhambi, basi nisamehe, akasema Mwenyezi Mungu mja wangu amefanya madhambi na akajua ana Mola ambae atakae msamehe makosa yake, basi nimemsamehe. Kisha akafanya dhambi tena na akaomba msamaha na Mwenyezi Mungu akamsamehe, kisha akafanya dhambi kwa mara ya tatu na kuomba msamaha akasema Mwenyezi Mungu mja wangu amejua ana Mola atakae msamehe, shuhudieni kuwa nimemsamehe na afanye atakavyo].

Mwisho

Ewe Mwenyezi Mungu, sisi ni waja wa kufanya madhambi, sisi ni waja wenye makosa mengi, sisi tumefanya madhambi yetu kwa siri, sisi ni waja wagonjwa kwa makosa tuliyofanya. Tumekuja tunataka toba yako. Sisi ni waja wako maskini tumenyoosha mikono yetu basi tusamehe madhambi yetu. Tunataraji kutoka kwako Mola wetu msamaha na maghfira.

[7] REHEMA

Lengo la Khutba:

1. Kuwa na rehema, sifa ambayo aliyosifika nao Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam)
2. Kuwalea watu katika kutaraji rehma ya Mwenyezi Mungu.
3. Kuepukana na kukata tama kwa rehema za Mwenyezi Mungu.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Mwenyezi Mungu anasifika kwa sifa ya rehema kwa watu wake mwenye kurehemu na mwingi wa huruma. Ni sifa mbili za Mwenyezi Mungu, mwingi wa huruma kwa viumbe vyote hapa duniani, na kwa waumini siku ya kiyama, mwenye rehema pekee siku ya kiyama. Rehema zake Mwenyezi Mungu hazihesabiki, amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالى : ﴿ مَّا يَفْتَحِ ٱللَّهُ لِلنَّاسِ مِن رَّحْمَةٍ فَلَا مُمْسِكَ لَهَا ۖ وَمَا يُمْسِكْ فَلَا مُرْسِلَ لَهُۥ مِنۢ بَعْدِهِۦ ۚ ﴾ [فاطر:٢].

{{Rehema anayoifungua Mwenyezi Mungu kwa watu, hakuna wa kuizuia; Na Anayozuia hakuna wa kuipeleka mbele}}.

Amesema Shinqiti: rehema zake Mwenyezi Mungu ni kwa watu wote duniani na kesho akhera kama kuteremsha mvua. Kama Alivyosema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿ فَٱنظُرْ إِلَىٰٓ ءَاثَٰرِ رَحْمَتِ ٱللَّهِ كَيْفَ يُحْىِ ٱلْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَآ ۚ ﴾ [الروم:٥٠].

{{Basi ziangalie alama za rehma ya Mwenyezi Mungu, jinsi anavyoihuisha ardhi baada ya kufa kwake}}. Enyi Waja wa Mwenyezi Mungu, sisi tunatakiwa tuwe na rehema kati yetu, na baina ya viumbe vyote, kwasababu tofauti kama:-

a. Mwenyezi Mungu ametuamrisha kama alivyosema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): “Kuweni na rehema mtarehemewa, sameheni mtasahemewa”
b. Tukisifika na tabia hii tutapata watakaoturehemu katika dunia. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Warehemuni walio duniani mtarehemewa na walio mbinguni]. Na amesema tena Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Asiyerehemu watu, Mwenyezi Mungu pia nae hamrehemu].

Sampuli za Rehema za Mwenyezi Mungu

1. Kuwaumba wanadamu kwa sura nzuri, Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ لَقَدْ خَلَقْنَا ٱلْإِنسَٰنَ فِىٓ أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿٤﴾ ﴾ [التين:٤].

{{Bila shaka tumemuumba mwanadamu kwa umbo lililo bora kabisa}}.

2. Kumtukuza mwanadamu na kumfadhilisha kuliko viumbe vyote. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال : ﴿ وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِيٓ ءَادَمَ وَحَمَلْنَٰهُمْ فِي ٱلْبَرِّ وَٱلْبَحْرِ وَرَزَقْنَٰهُم مِّنَ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَفَضَّلْنَٰهُمْ عَلَىٰ كَثِيرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا ٧٠ ﴾ [الإسراء:٧٠].

{{Kwahakika tumewatukuza wanadamu na tumewapa ya kupanda barani na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri, na tumewatukuza kuliko wengi katika wale tuliowaumba, kwa utukufu ulio mkubwa}}.

3. Kumpatia mwanadamu riziki, Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال تعالى : ﴿ وَمَا مِن دَآبَّةٍ فِي ٱلْأَرْضِ إِلَّا عَلَى ٱللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا ۚ كُلٌّ فِي كِتَٰبٍ مُّبِينٍ ٦ ﴾ [هود:٦].

{{Na hakuna nyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko juu ya Mwenyezi Mungu. Na Anajua makao yake ya milele, na mahali pa kupita tu. Yote yamo katika kitabu kinachodhihirisha}}.

4. Kudhalilisha vilivyomo mbinguni na ardhini kwa ajili yetu, amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) :

قال تعالى: ﴿ وَسَخَّرَ لَكُمُ ٱلَّيْلَ وَٱلنَّهَارَ وَٱلشَّمْسَ وَٱلْقَمَرَ ۖ وَٱلنُّجُومُ مُسَخَّرَٰتٌۢ بِأَمْرِهِۦٓ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَءَايَٰتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ١٢ ﴾ [النحل:١٢]

{{Na amekutiisheni usiku na mchana, na jua na mwezi. Vyote vimeumbwa kwa ajili ya maslahi yenu. Na pia nyota zimetiishwa kwa amri yake}}.

5. Kutumilizwa Mtume na kubainishia watu pepo na kuwakhofisha na moto, amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِٱلْبَيِّنَٰتِ وَأَنزَلْنَا مَعَهُمُ ٱلْكِتَٰبَ وَٱلْمِيزَانَ لِيَقُومَ ٱلنَّاسُ بِٱلْقِسْطِ ۖ وَأَنزَلْنَا ٱلْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنَٰفِعُ لِلنَّاسِ وَلِيَعْلَمَ ٱللَّهُ مَن يَنصُرُهُۥ وَرُسُلَهُۥ بِٱلْغَيْبِ ﴾ [الحديد:٢٥]

{{Kwahakika tuliwapeleka Mitume wetu kwa dalili waziwazi na Tukateremsha vitabu na uadilifu pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu}}.

6. Kutumilizwa kwetu Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

و قال : ﴿ رُّسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى ٱللَّهِ حُجَّةٌۢ بَعْدَ ٱلرُّسُلِ ﴾ [النساء:١٦٥]

{{Nasi hatukukutuma, ila uwe rehema kwa walimwengu wote}}.

7. Kupewa sheria ya kiislamu, na sheria yenyewe ni nyepesi. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Fanyeni upesi wala msifanye uzito, na wabashirieni watu wala msiwakhofishe]. Ndugu Waislamu, tufanye bidii kufanya mambo ya kheri ili tupate rehema za Allah. Rehema za Allah hazipatikani kwa kutamani bali ni lazima Muislamu kufuata sababu zote zitakazo mfiksha yeye kupata rehema za Mwenyezi Mungu.

KHUTBA YA PILI

Rehema ya kutumilizwa Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam)

Mtume Muhammad Ametumilizwa kwa wanadamu wote akiwa ni rehema kwao. Ameshuhudia Mwenyezi Mungu rehema ya kutumiliza Mtume wetu Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Kwa kusema (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى ﴿لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُم بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢٨﴾﴾ [التوبة:١٢٨].

{{Kwahakika amekufikieni Mtume aliye jinsi moja na nyinyi, yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni. Na kwa walioamini ni mpole na mwenye huruma}}.

Sura za Rehema za Mtume wetu Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam)

1. Pamoja na maadui zake, aliенда Twaif kuwalingania, walimpiga mawe mpaka akatokwa na damu na wakamtukana hapo Mwenyezi Mungu alimpeleka Malaika wa jabali akasema ukitaka niwafunike na jabali nitafanya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akasema: [Usifanye huenda wakatokea katika watoto wao mwenye kumuabudu Mwenyezi Mungu].
2. Tukio moja la bedui kukojoa Msikitini na maswahaba wakataka kumpiga, Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akawakataza na kusema mwacheni amalize mkojo wake na baada ya hapo akamuambia [Msikiti umejengwa kumuabudu Mwenyezi Mungu].
3. Ni mpole mno
    a. Anakuja mtu na kumshika Mtume wa Mwenyezi Mungu mabegani kwa nguvu na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) anamgeukia na kumwangalia kwa tabasamu.
    b. Mtu anamkopesha Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) na anakuja kudai deni lake kabla ya wakati wake na kusema: [Enyi watu wa Abdul Mutwalib mnachelewesha kulipa madeni, mpaka maswahaba wanataka kumpiga mtu huyo, na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema “Mwenye haki ana haki ya kusema”].
4. Pamoja na waumini, amepokea Malik bin Huweinth akisema: “Tumekaa kwa Mtume siku ishirini akadhani kuwa tunawatamani watu wetu, akatuuliza kuhusu hali zao, tukamfahamisha akasema nendeni mkawafundishe kuswali kama mnavyoniona nikiswali pamoja na kuadhini na kukimu”.

Kiongozi wa Kiislamu Kuwa na Rehema

Mtume wa Mwenyezi Mungu amemuomba Mwenyezi Mungu yoyote atakaye shika madaraka katika nchi akisema: [Atakaye shika madaraka katika umma wangu na kuwa na huruma basi Mwenyezi Mungu pia huwa na huruma, na atakae wafanyia uzito umma wangu basi Mwenyezi Mungu pia atamfanyia uzito]. Uongozi si utukufu bali ni ukalifishaji. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) kumwambia Aba Dharr: [Uongozi ni amana, na siku ya Qiyama ni majuto, isipokuwa kwa atakayechukua uongozi huo kwa haki, na kupeana haki hiyo].

Viongozi wema waliotangulia walikuwa walikuwa wakifuatilia hali za watu wao, 'Umar Bin Khattab alikuwa akienda kwa mwanamke mzee kipofu akisafisha mkojo wake na choo, na kumpelekea chakula 'Umar akaona kuwa kuna mtu anayemtangulia katika kumhudumia mama huyo mzee, akamkuta ni Abubakar ambaye alikuwa ni kiongozi wa Kiislamu.

Kuwarehemu Wanyama

Kuna baadhi za hali imeharamishwa kuwafanyia wanyama:-

1. Kumfunga mnyama: Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Ameingia mwanamke motoni kwa ajili ya paka aliyemfungia bila ya kumlisha, na kutomuacha kula wadudu katika ardhi].
2. Kuwapiganisha wanyama: Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amekataza kuwapiganisha wanyama.
3. Kuuwa wanyama bila ya sababu (mchezo). Neno lake Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) : [Ndege anadai haki yake mbele ya Mwenyezi Mungu siku ya Qiyama kuuliwa bila ya sababu].
4. Kufanya hisani katika kuchinja wanyama. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Mkichinja fanyeni wema na mtie kisu makali].

Mwisho

Ndugu Muislamu, ili tuweze kupata rehema za Mwenyezi Mungu, ni wajibu juu yetu kutekeleza sababu zifuataao:-

- Kubadilika kutoka hali moja na kwenda katika hali nyingine ni njia moja ya kupata rehma za Mwenyezi Mungu. Mfano kutembelea mayatima na kuwasaidia, kujua hali za maskini wasio jiweza.
- Kujuwa malipo makubwa watakaopata wenye kupata rehema za Mwenyezi Mungu
- Kuwaheshimu wazazi na kila mtu ambaye ni mkubwa wako kwa umri.
- Tunamuomba Allah Atufinike kwa rehma zake hapa duniani na kesho siku ya mwisho.

[8] DHANA MBAYA

Lengo la Khutba:

1. Tiba ya maradhi haya.
2. Kuwalea watu kwa moyo uliosalimika.
3. Kutia nguvu utengamano kati ya Waislamu.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Miongoni mwa maafa yaliyowasibu watu na jamii ni dhana mbaya, jambo ambalo linakata mapenzi kati ya watu, na mwenye dhana mbaya huwaangalia watu kwa jicho ovu, na bila shaka dhana mbaya ni kinyume na sheria ya kiislamu.

Ili mafungamano baina yetu na watu yabaki kuwani imara ni kuwakabili watu hali ya kuwa nyoyo zetu zimesalimika pia kuwa safi na nyuso kuwa na bashasha na kuwadhania watu kwa dhana nzuri pindi tunaposalimiana nao. Tunapozingatia mafungamano ya Waislamu yamesambaratika kutokana na dhana mbaya. Unaposikia maongozi ya Waislamu tunasikia wakisema fulani amekusudia hivi, na fulani ametaka jamabo hili. Yote yanapelekea kupatikana kwa chuki na mwisho ni kuvunjika au kusambaratika kwa mafungamano. Dhana mbaya inapeleka kufuatilia aibu za watu na kuchunguzana kwa ajili hiyo utasikia kwa mwenye dhana mbaya akisema 'Nitajaribu kuhakikisha' basi atachunguza na kusengenya na kumtaja mwenzake kwa uovu. Kuenea kwa dhana mbaya kunakosekana uaminifu kati ya watu na kukatana jambo ambalo kwamba linapelekea kutofaulu katika mambo yetu.

Anasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله نعالى : ﴿وَأَطِيعُوا۟ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ وَلَا تَنَٰزَعُوا۟ فَتَفْشَلُوا۟ وَتَذْهَبَ رِيحُكُمْ ۖ وَٱصْبِرُوٓا۟ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ مَعَ ٱلصَّٰبِرِينَ ﴿٤٦﴾﴾
[الأنفال:٤٦]

{{Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake wala msizozane, msije mkaharibikiwa na kupotea nguvu}}.

Dhana mbaya haileti kheri na ni njia ya kuenea kwa uadui na kupatikana kwa madhambi hayo duniani ama kesho akhera ni majuto. Tazama watu waovu walivyo wakejeli Waislamu na kuwadhania maovu pindi Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Aliposema:

قال تعالى: ﴿وَقَالُوا۟ مَا لَنَا لَا نَرَىٰ رِجَالًا كُنَّا نَعُدُّهُم مِّنَ ٱلْأَشْرَارِ ﴿٦٢﴾ أَتَّخَذْنَٰهُمْ سِخْرِيًّا أَمْ زَاغَتْ عَنْهُمُ ٱلْأَبْصَٰرُ ﴿٦٣﴾﴾ [ص:٦٢:٦٣]

{{Kisha wale wabaya watasema: Imekuwaje, Mbona hatuwaoni wale watu tulikuwa tukiwahesabu katika waovu kwa kumfuata Muhammad. Je, tuliwafanyia mzaha (huko duniani, na hali yakuwa ni watu wakubwa Akhera au wamo Motoni humu pamoja na sisi) ila macho yetu haya waoni tu ?}}.

Anasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿فَٱلْيَوْمَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنَ ٱلْكُفَّارِ يَضْحَكُونَ ﴿٣٤﴾ عَلَى ٱلْأَرَآئِكِ يَنظُرُونَ ﴿٣٥﴾ هَلْ ثُوِّبَ ٱلْكُفَّارُ مَا كَانُوا۟ يَفْعَلُونَ ﴿٣٦﴾﴾ [المطفّفين:٣٤:٣٥].

{{Basi leo walioamini watawacheka waliokufuru. Watakuwa Juu ya viti vya fahari, wakitazama (neema zao). Je, makafiri wamepewa malipo ya yale waliyokuwa wakiyatenda?}}.

Anasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱجْتَنِبُوا۟ كَثِيرًا مِّنَ ٱلظَّنِّ إِنَّ بَعْضَ ٱلظَّنِّ إِثْمٌ﴾ [الحُجرات:١٢].

{{Enyi mlioamini, Jiepusheni sana na dhana mbaya. Kwani dhana mbaya ni dhambi}}.

Inajulisha Aya katika kuhifadhi heshima ya Muislamu kwa kutangulia na katazo la dhana. Ni uzuri ulioje kwa mujtama ulio salimika na dhana mbaya. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Jiepusheni na dhana hakika ya dhana ni maongezi ya uongo wala msichunguzane wala msichukiane kuweni ndugu katika waja wa Mwenyezi Mungu].

Wamesema baadhi ya wanavyuoni dhana ambayo inafaa kuepukwa ni ile ambayo kwamba haijulikani njia yake kuwa ni ya sawa na sababu iliyokuwa ya wazi, mfano anayedhaniwa akiwa ni mtu mwema na akapewa amana kuwadhania kuwa amekhini ni haramu. Kinyume na ambae anajulikana anayefanya maovu wazi wazi kwa ajili hiyo wamesema wanavyuoni dhana mbaya kwa mtu mwema haifai na hapana tatizo kudhania uovu mtu muovu.

Imepokewa hadithi Said ibn Musaib akisema: "Amewaandikia baadhi ya maswahaba kutowacha kufanya wema kwa jambo la ndugu yake maadamu hujashindwa wala asidhani neno baya limetoka kwa ndugu yako ikiwa inawezekana kuchukulia kwa uzuri na huo ndio mfano wa watu wema pindi wanaposhindwa kuelewa baadhi ya maneno, kwa kuwahukumu makosa watu wengine bila ya kuzingatia nia na hali ya yule mtu". Ibn Qayyim amesema: "Neno moja husemwa na watu wawili mmoja wao anakusudia haki na mwingine wao anakusudia batili kwa ajili hiyo hahukumiwi mtu kuwa kafiri kwa aliyesema " Ewe mola wangu wewe ni mja wangu na mimi ni mola wako" hakukusudia kujifanya Mwenyezi Mungu. Amesema Sheikhul Islam Ibn Taymiyya pindi anaponukuu maneno ya wenye kumkhalifu akisema "Maneno haya yana upana, na haki huchukuliwa kwa uzuri na batili huwa na mambo mengi"

Mwanadamu hana haki kwa ndugu yake isipokuwa kwa mambo yaliyo wazi. Amepokea Abdulrazaq kutoka kwa 'Umar Ibn Khattab akisema: " Watu walikuwa wakipokea wahyi wakati wa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) na wahyi ukakatika, lakini tunachukua sasa kwa yale yaliyodhihiri kutokana na vitendo vyenu kwa atakae dhihiri kheri tutamuamini na tutamkaribisha haitujalishi sisi usiri wake na Mwenyezi Mungu ndiye atakaye muhesabu kutokana na usiri wake na atakae dhihiri shari lake kwetu hatutomuamini wala hatutomsadiki hata akisema kuwa usiri wake ni mwema". Kwa Muislamu ahesabu kuwa kila neno analozungumza au hukumu anayotamka na akumbuke Neno lake Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِۦ عِلْمٌ ۚ إِنَّ ٱلسَّمْعَ وَٱلْبَصَرَ وَٱلْفُؤَادَ كُلُّ أُو۟لَـٰٓئِكَ كَانَ عَنْهُ مَسْـُٔولًا ﴿٣٦﴾﴾ [الإسراء:٣٦].

{{Wala usifuate usiyo na ilimu nayo. Hakika masikio na macho na moyo, hivyo vyote vitaulizwa}}.

KHUTBA YA PILI

Waja wa Mwenyezi Mungu sababu za dhana mbaya ni kuinukia mtu katika mazingira maovu na atakayefuata matamanio yake ataingia katika dhana mbaya; kupenda kitu humfanya mtu kuwa kipofu na kiziwi, mwanadamu akifuata matamanio yake kwa kumpenda mtu mwingine makosa yake huwa ni mema na akimchukia mtu mwingine mema yake huwa ni maovu. Baadhi ya watu wanajiinua utu wao na kujiona saa zote kuwa wao au yeye siku zote yuko katika haki na watu wengine wako katika batili na kujitakasa nafsi yake kwa kudharau watu wengine jambo ambalo linaleta dhana mbaya kwa watu wengine.

Dhana mbaya ni sababu ya kupatikana tuhuma kwa watu na kuwagura bila ya sababu ya kisheria na kuwadhulumu kama alivyosema msemaji: "Naona uadui wala sioni sababu zake yote ni kutokana na mshikamano uliokatika, dhana ilivyokuwa na madhambi, na kusengenya kulikokuwa kuovu.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿وَٱلَّذِينَ يُؤْذُونَ ٱلْمُؤْمِنِينَ وَٱلْمُؤْمِنَٰتِ بِغَيْرِ مَا ٱكْتَسَبُوا۟ فَقَدِ ٱحْتَمَلُوا۟ بُهْتَٰنًا وَإِثْمًا مُّبِينًا ﴿٥٨﴾﴾

[الأحزاب:٥٨]

{{Na wale wanaowaudhi wanaume Waislamu na wanawake Waislamu pasipo wao kufanya kosa lolote, bila shaka wamebeba dhulma kubwa na dhambi zilizo dhahiri}}.

Suluhisho la dhana mbaya

a. Kuwadhania watu dhana nzuri, fikiri kwa kina kabla hujatoa hukumu na kutuhumu kwani kukosa kwa kumdhania mtu mwema ni bora kuliko kwa kumdhania mtu uovu. Amesema 'Umar : 'Dhania kheri kwa neno litakalo kwa ndugu yako baada ya kuwa na dhana, ikiwa panapatikana ndani yake kheri'.

b. Kutoa udhuru kwa watu na kutofuatilia aibu za watu na kuwajibika ni katika adabu za kiislamu katika kutoa hukumu kwa watu na kumuachia Mwenyezi Mungu mambo yaliyojificha.

Mwisho

Ndugu katika Imani, tumeona hatari mbaya ya Muislamu kumdhania Muislamu mwenzake vibaya, na athari yake katika jamii ya kislamu. Jamii ya kislamu ni jamii iliyo hifadhiwa na sheria za Allah (Subhaanahu wa Taala). Muislamu akipata khabari yoyote kuhusu Muislamu mwingine ni lazima kwanza apime khabari hiyo kwa mizani ya sheria, ili aweze kujuwa ukweli wa khabari hiyo.

Namuomba Mwenyezi Mungu atuondelee dhana mbaya na atuwezeshe kuwadhania watu dhana mzuri, na kuwapa udhuru watu.

[9] HATARI YA MWANAMKE KUJIPAMBA NA KUDHIHIRISHA MWILI WAKE

Lengo la Khutba:

1. Kutibu ugonjwa huu mbaya
2. Kuwahimiza wanawake wa Kislamu kuwa na heshma na kujisitiri
3. Kufunga mlango wa fitna.
4. Kuwatahadharisha wanawake kutokana na walinganizi waovu

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Miongoni mwa misingi ya kisheria ni kufunga mlango wa fitna. Na miongoni mwa Rehma za Mwenyezi Mungu kwa waja wake ni kufunga mlango wa shari, basi mwenye kufungua mlango huo atapata madhambi. Amesema mshairi:- Ikiwa mja hatovaa vazi la ucha Mungu, atakuwa uchi hata kama amevaa nguo. Na mja mwema ni yule amchaye Mola wake, wala hakuna ubora kwa anaye muasi Mola wake.

Ndugu Waislamu, Leo tunashuhudia wazi kabisa namna wanawake wanavyo dhihirisha mapambo yao, na kutovaa hijabu. Na bila shaka, kitendo hiki ni katika madhambi makubwa, na ni sababu ya kuteremshwa adhabu duniani, na kupata adhabu kali siku ya kiama. Ndugu zangu Waislamu, kuweni na adabu ya Mwenyezi Mungu na muwalazimishe wake zenu kuvaa hijabu na kusitiri miili yao kama alivyo amrisha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) katika Qur’an tukufu.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال عز وجل : ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِيُّ قُل لِّأَزْوَٰجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَآءِ ٱلْمُؤْمِنِينَ يُدْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِن جَلَٰبِيبِهِنَّ ۚ ذَٰلِكَ أَدْنَىٰٓ أَن يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذَيْنَ ۗ وَكَانَ ٱللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٥٩﴾﴾ [الأحزاب:٥٩]

{{Ewe Mtume, Waambie wake zako, na binti zako, na wanawake wa Kiislamu, wajiteremshie vizuri nguo zao. Kufanya hivyo kutapelekea upesi wajulikane kuwa ni watu wa heshima ili wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe na Mwingi wa kurehemu}}.

Jukumu la kila Muislamu kupiga vita Fitna ya Wanawake

Enyi Waislamu mcheni Mwenyezi Mungu na katazeni wanawake wenu na binti zenu kudhihirisha mapambo yao. Ni lazima kila Muislamu abebe jukumu la kuamrisha mema na kukataza mabaya. Kwani, tukiacha kufanya hivyo, tutalaaniwa na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) kama walivyo laaniwa watu waliotangulia. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Watu wakiona uovu na wasiukataze uovu huo huhofiwa kuwateremkia adhabu ya Mwenyezi Mungu].

Amesema Mwenyezi Mungu (SW):

قال عز وجل : ﴿لُعِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِن بَنِي إِسْرَائِيلَ عَلَىٰ لِسَانِ دَاوُودَ وَعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ ۚ ذَٰلِكَ بِمَا
عَصَوا وَّكَانُوا يَعْتَدُونَ ﴿٧٨﴾ كَانُوا لَا يَتَنَاهَوْنَ عَن مُّنكَرٍ فَعَلُوهُ ۚ لَبِئْسَ مَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿٧٩﴾﴾
[المائدة:٧٨:٧٩]

{{Walilaaniwa wale waliokufuru miongoni mwa wana wa Israil kwa ulimi wa Daudi na Isa bin Maryam. Hayo ni kwa sababu waliasi wakipindukia mipaka. Hawakuwa wenye kuzuiana (kukatazana) mambo mabaya waliyokuwa wakiyafanya. Uovu ulioje wa jambo hili waliokuwa wakifanya}}.

Na amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Atakaye uona uovu na auzuie kwa mkono wake, asipoweza kwa ulimi wake, asipoweza kwa moyo wake na ni udhaifu wa imani].

Ndugu katika imani, Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amewaamrisha wanawake kuvaa hijabu na kubakia majumbani mwao, na kutolegeza sauti zao. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿يَا نِسَاءَ النَّبِيِّ لَسْتُنَّ كَأَحَدٍ مِّنَ النِّسَاءِ ۚ إِنِ اتَّقَيْتُنَّ فَلَا تَخْضَعْنَ بِالْقَوْلِ فَيَطْمَعَ الَّذِي فِي قَلْبِهِ مَرَضٌ وَقُلْنَ قَوْلًا
مَّعْرُوفًا ﴿٣٢﴾ وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ وَلَا تَبَرَّجْنَ تَبَرُّجَ الْجَاهِلِيَّةِ الْأُولَىٰ ۖ وَأَقِمْنَ الصَّلَاةَ وَآتِينَ الزَّكَاةَ وَأَطِعْنَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ
ۚ﴾ [الأحزاب:٣٢:٣٣]

{{Enyi wake wa Mtume, nyinyi si kama yoyote tu katika wanawake wengine. Kama mnataka kumcha Mwenyezi Mungu, basi msiregeze sauti zenu ili asitamani mtu mwenye ugonjwa moyoni mwake, na semeni maneno mazuri. Na kaeni majumbani mwenu, wala msionyeshe mapambo yenu kama walivyo kuwa wakionyesha mapambo yao wanawake wa zama za ujahili}}.

Masharti ya Hijabu:

a. Kufunika mwili wote isipokuwa uso
b. Hijabu isiwe na mapambo juu yake
c. Hijabu iwe nzito wala isiwe yenye kuonyesha mwili
d. Hijabu iwe pana wala isiwe yenye kubana mwili
e. Hijabu isiwe na manukato
f. Hijabu isifanane na vazi la mwanamume
g. Hijabu isifanane na vazi la makafiri
h. Hijabu isiwe ni vazi lenye kujulikana

Ushahidi wa masharti yaliyopita, Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ قُل لِّأَزْوَاجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَاءِ الْمُؤْمِنِينَ يُدْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِن جَلَابِيبِهِنَّ ۚ ذَٰلِكَ أَدْنَىٰ أَن يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذَيْنَ ۗ
وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٥٩﴾﴾ [الأحزاب:٥٩]

{{Ewe Mtume, Waambie wake zako, na binti zako, na wanawake wa Kiislamu, wajiteremshie uzuri nguo zao. Kufanya hivyo kutapelekea upesi wajulikane kuwa ni watu wa heshima ili wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe na Mwingi wa kurehemu}}.

Na Akasema tena Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿وَقُل لِّلْمُؤْمِنَٰتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَٰرِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا ۖ وَلْيَضْرِبْنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ﴾ [النور:٣١]

{{Na waambie Waislamu wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasidhihirishe mapambo yao isipokuwa yanayodhihirika. Na waangushe shungi zao mpaka vifuani mwao}}.

Amesema Mtume (Subhaanahu wa Taala): [Watu wawili ni watu wa motoni, mmoja wao ni mwanamke aliyevaa nguo lakini yuko uchi].

Na akasema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) [Mwanamke yoyote atakaye jitia manukato na akapita mbele ya watu, ili watu wasikie harufu ya mafuta yake, basi mwanamke huyo ni mzinifu].

Amesema tena Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Amemlaani Mtume wa Mwenyezi Mungu mwanamke mwenye kuvaa vazi la mwanamume, na mwanamume mwenye kuvaa vazi la mwanamke].

Na amesema tena Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Atakaye jifananisha na watu basi ni katika wao].

Na amesema tena Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Atakae vaa vazi la kujionyesha, Mwenyezi Mungu Atamvisha vazi la udhalili siku ya kiyama].
Ndugu katika imani, ni wajibu juu kila mwanamume kuhakikisha masharti ya hijabu wakati anapo mnunulia mke wake au binti yake vazi la kuvaa. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Nyinyi wote ni wachunga, na kila mmoja ataulizwa juu ya kile alichokichunga]. Inatupasa kumuogopa Mola wetu na kutekeleza majukumu yetu kama alivyo tuamrisha Mwenyezi Mungu.

KHUTBA YA PILI

Sababu ya Uharibifu wa Wanawake

Ndugu Waislamu, inajulikana wazi ya kuwa wanawake wa leo wamezidi kuonyesha umbile lao na mapambo yao. Kuna sababu nyingi ambazo zimechangia kupatikana uharibifu katika jamii. miongoni mwasababau hizo ni:-

1. Mwanamke kukaa faragha na mwanamume ambaye si maharimu yake. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Hawatokaa faragha mwanamke na mwanamume isipokuwa shetani huwa watatu wao].
2. Kusafiri peke yake. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Asisafiri mwanamke isipokuwa awe na mahrimu yake (Wasioruhusiwa kumuoa) Wala asikae faragha mwanamke na mwanamume].
3. Wanawake wa kiislamu kujifananisha na wanawake wa kikafiri. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Atakaye jifananisha na watu basi ni katika wao].

Wajibu wa Viongozi na Mahakimu na Wanavyuoni

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, mcheni Mola wenu na tahadharini kwa mambo aliyoyaharamisha, na saidianeni kwa mambo mema na msiache kwa mambo ya haki na kusubiri. Na jueni ya kuwa Mwenyezi Mungu atawalipa kwa mambo mliyoyafanya. Na inalazimu kwa viongozi wa nyanja tofauti kutonyamaza

katika kuondosha uovu.

Imepokewa kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Hakutumilizwa Nabii isipokuwa alikuwa na wafuasi na wenye kuchukua uongozi wake, kisha wakawayapa mgongo yote yaliyokuja baada yake, wanazungumza mambo wasiyoyafanya, na wanafanya mambo wasiyoamrishwa, atakae pigana nao kwa mkono wake, basi huyo ni muumini. Atakaye pigana nao kwa moyo wake basi huyo pia ni muumini, wala hakuna baada ya ya hapo chembe yoyote ya imani (mkono, ulimi na moyo)].

Wito kwa Wanawake Wakiislamu

- Muogope Mwenyezi Mungu! Ewe mtoto wa kike
- Muogope Mwenyezi Mungu! Mwenye kujipamba na kwenda sokoni
- Muogope Mwenyezi Mungu! Mwenye kuvaa hijabu kama pambo wala si kwa kujistiri
- Muogope Mwenyezi Mungu! Kwa kile alichokukalifisha, ambapo mbingu na ardhi imekataa kubeba.
- Muogope Mwenyezi Mungu! Na hifadhi nafsi yako.
- Muogope Mwenyezi Mungu! Na kutangamana na wanaume na kutoka bila ya maharim
- Muogope Mwenyezi Mungu! Ewe Mwenye kuingia kwa matibabu bila maharim.
- Muogope Mwenyezi Mungu! Ewe mwenye kuwalea watoto wako malezi ya wanyama.
- Muogope Mwenyezi Mungu! Ewe mwenye kujitia manukato.
- Muogope Mwenyezi Mungu! Na mrejee katika uongofu, jua kama adhabu kali mbele ya Mwenyezi Mungu, na dunia si makazi.

Mwisho

Ndugu Waislamu, Na kariri tena kwa kuwakumbusha jukumu kubwa tulilo beba nalo ni kuwasimamia wanawake na kuwaamrisha mema na kuwakataza mabaya. Fitna kubwa leo ulimwenguni ni fitna ya wanawake, na maadui wanawatumia wanawake kama njia ya kufikia malengo yao. Jamii nyingi zimeharibikiwa kwasababu ya kuharibika mwanamke. Kwa hivyo, Ni lazima kila Muislamu ajitolee kwa hali na mali kuwahifadhi wanawake katika jamii yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awahifadhi mabanati wa kiislamu kutokana na vitimbi vya wenye kufanya vitimbi.

Ewe Mwenyezi Mungu wakusanye wao katika imani na kuwapa pepo siku ya akhera Mwenyezi Mungu sitiri aibu zetu na utuhifadhi mbele yetu, nyuma yetu na upande wa kulia na upande wa kushoto na juu yetu.

[10] MADAWA YA KULEVYA NA ATHARI YAKE KATIKA KUMUANGAMIZA BAROBARO

Malengo ya Khutba:

1. Akili ni neema inayopasa kushukuriwa
2. Kuwahadharisha barobaro juu ya madawa ya kulevya yanayoangamiza ubarobaro wao.

KHUTBA YA KWANZA.

Utangulizi

Allah amemkirimu mwanaadamu kwa kumpa akili na fahamu na akamuelekeza kwa kufikiri na kuzingatia, akili ikawa ndio neema kubwa ya Allah kwa huyu mwanadamu, akili ndio inayotufahamisha baina ya mwanadamu, wanyama na visivyokuwa na roho. Enyi waja wa Allâh! Allâh Mtukufu amewakirimu wanadamu juu ya viumbe vyake vingi, akasema (Subhaanahu wa Taala):

فقال سبحانه: ﴿ وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِيٓ ءَادَمَ وَحَمَلْنَٰهُمْ فِي ٱلْبَرِّ وَٱلْبَحْرِ وَرَزَقْنَٰهُم مِّنَ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَفَضَّلْنَٰهُمْ عَلَىٰ كَثِيرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا ٧٠ ﴾ [الإسراء:٧٠]

{{Hakika Tumewatukuza wanaadamu, na Tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini, na Tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na Tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa Tuliowaumba}}. Allâh amewakirimu wanaadamu kwa mambo mengi aliyowapambanua na viumbe vingine vikiwemo, visivyo na roho, wanyama, mimea na majini, alimkirimu kwa akili na fahamu na akamuelekeza kwa mazingatio na kutafakari, kwa hivyo akili ikawa ndio neema kubwa zaidi kutoka kwa Allâh, kwayo, mwanadamu huweza kupambanua baina ya kheri na shari madhara na manufaa, kwayo huweza akafurahia maisha yake, kuendesha mambo yake na kustarehe, kwayo ndio umati zote ziweze kupanda na maisha kuendelea.

Akili ni johari yenye thamani, wenye akili huwa wakiihifadhi na kuihami kwa kuukubali ubora wake na kuhofu wasije wakaipoteza.

Mwanadamu anapoikosa akili yake basi hakuna atakayemtofautisha baina yake na wanyama, anayeikosa akili yake huwa hana manufaa bali huwa ni mzigo kwa familia na jamii yake. Akili hii ya thamani hupatikana kwa wanadamu kwa watu wasiyoiangalia kuitunza na kuihami. Bali katika watu, yuko anayeikanyaga akili chini ya nyayo zake akifuata matamanio yake na macho yake yakawa hayaoni, hata jambo hilo likawa wazi kabisa.

Mtu anapokunywa pombe au kutumia madawa ya kulevya au akanusa ulevi, basi hapo huanza kukosa akili akajiinua kutoka katika ulimwengu wa ubinadamu na akavaa nguo ya maovu na mauaji. Hapo mlevi huanza kupooza na akamsahau Mola wake, akaidhulumu nafsi yake, akaondokana na haya aliyokuwa nayo, watoto wake akawafanya mayatima na mkewe akawa mjane kwa sababu ya kukosa akili.

Hapo akawa amelitupa jambo la dharura maishani mwake katika yale mambo matano ambayo sheria za mbinguni zimeafikiana kwamba ni wajibu mtu kuyahifadhi mambo hayo, nayo ni akili, ni wajibu mtu kuhifadhi akili na kuichunga, anayeikosa akili yake kwa kulewa, atakuwa ameikosa akili na jamii yake, na ataitumbukiza jamii yake na waumini wenziwe katika maporomoko ya udhalilifu na maangamizi, hapo amani ikakosekana na jamii ikatishia amani.

Watumiaji wa madawa ya kulevya hukosa kuyasimamia majukumu waliyonayo na kusimamia akili zao. Mamia ya Waislamu wamepotea kwa sababu ya madawa ya kulevya na ulevi. Roho zao zimeenda kwa Mola wao huku wakiwalalamikia wale mafasiki na waovu waliojiingiza wao wenyewe na kuwaingiza wengine katika maangamivu.

Haya madawa ya kulevya yamewapeleka watu waliokuwa na familia katika jela miaka mingi yakiwa ndio malipo ya yale makosa waliyoyateuwa familia zao zikabakia bila ya msimamizi, wake zao wakawa kama wajane, watoto wao kama mayatima, wakapoteza ubarobaro na maisha mazuri waliyokuwa nayo, mustakbali wao wakaupoteza kwa mitaimbo ya maadui zao jela zikawa zimejaa pomoni namna walivyokuwa wengi.

Wenye akili dhaifu huyapokea wanayoletewa na maadui na kuenezwa na madalali waovu.

Bila shaka ni misiba iliyowapata Waislamu, nao wameghafilika na mambo wanayopelekewa, maadui wamejua njia ya kuingia kwa Waislamu.

Allâh (Subhaanahu wa Taala) Amesema kweli wakati Alipotuambia:

قال سبحانه : ﴿وَلَا يَزَالُونَ يُقَٰتِلُونَكُمۡ حَتَّىٰ يَرُدُّوكُمۡ عَن دِينِكُمۡ إِنِ ٱسۡتَطَٰعُواْۚ﴾ [البقرة:٢١٧]

{{Wala hawatoacha kupigana nanyi mpaka wawatoe katika Dini yenu kama wakiweza}}. Ajabu kubwa ni kwa yule anayenunua ufisadi kwa mali yake!

Kwa nini mtumiaji wa madawa ya kulevya hawezi kupata mawaidha kwa wale waliopata mikasa katika familia zao, ikawaangamiza kabisa, na ni vipi ajitoe katika kundi la watu wenye akili na heshima zao ajipeleke katika kikundi cha wendawazimu wasio na akili?. Al-Hassan Al-Basry Amesema: “Lau kama akili ingalikuwa inauzwa bila shaka ingekuwa ni ghali mno.”

Basi iweje tena mtu aiharibu akili yake yeye mwenyewe? Kwa hakika huu ni msiba uliowashukia watoto wa Kiislamu. Tunamuomba Allâh atuongoze. Kwa ajili hiyo, kutumia kila kinachoondoa akili au kuilewesha kwa kinywaji au chakula au kinginecho, inakuwa ni haramu.

Katika Qur’an Allâh (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

قوله تعالى: ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِنَّمَا ٱلۡخَمۡرُ وَٱلۡمَيۡسِرُ وَٱلۡأَنصَابُ وَٱلۡأَزۡلَٰمُ رِجۡسٌ﴾ [المائدة:٩٠]

{{Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu}}.

Kwa mujibu wa Aya hii, pombe ni najisi, kwa sababu, Allâh Amesema: **“***rijs,* ni uchafu**”** Katika maneno ya Waarabu, *rijs* ni kila kilicho kichafu kinachochukiwa na watu. Bali Maswahaba watukufu wamefahamu katika Aya hii kwamba pombe si kama imeharamishwa pekee, bali imelinganishwa na shaka ambayo ndio dhambi kubwa zaidi inayotendwa na mwanadamu.

‘Abdullah Bin ‘Abbas amesema: “Ilipoteremka Aya ya kuharamisha pombe, Maswahaba wa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) waliendeana wao kwa wao na wakaambizana kuwa: [Pombe imeharamishwa na imelinganishwa na shirki]. Hadithi hii imepokewa na Tabarany, wapokezi wake ni wapokezi wa Hadithi Sahihi.

Kwa sababu Allâh Amesema kuhusu pombe: ni *rijs* katika matendo ya shetani. Na akasema kuhusu shirki: **“**Basi jiepusheni na (*rijs*) uchafu wa masanamu”

Hadithi za Mtume na Aya za Qur’an zimetilia nguvu uharamu wa pombe na kutahadharisha, na kukemea kuinywa au kuikaribia, pombe ni alama ya upotevu na anuani ya machafu na maovu kama ilivyopokewa, katika Hadithi ya AbdulRahman Bin Wa’lah amesema: Nilimwuliza ‘Abdullahi Bin ‘Abbas kuhusu biashara ya pombe, akaniambia: [Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alikuwa ana rafiki kutoka kabila la Thaqif au Daws, akakutana naye Siku ya Fat-hi Makka, akampa zawadi chombo kilichojaa pombe, Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akamwambia: “Ewe fulani kwani hujui kama Allâh Ameiharamisha?” Yule mtu akamwambia mtumishi wake: “Nenda ukaiuze”. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akamwuliza: “Ewe fulani, umemuamrishwa nini?” Akajibu: “Nimemuamrishwa nikaiuze.” Akamwambia: “Aliyeiharamisha kunywewa ndiye Aliyeharamisha kuuzwa”. Akaamrisha, ikamiminwa mchangani]. Muslim.

Katika Hadithi ya Abu Huraira, amesimulia: Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Usiku niliopelekwa Israa, huko Eliya (Baitul-Maqdis) nililetewa vikombe viwili vya pombe na maziwa, nikavitazama, nikachukua maziwa. Jibril akasema: Namshukuru Allâh Aliyekuongoza kuchukua fitra (Uislamu), lau ungalichukua pombe, umati wako wangaliangamia]. (Bukhari).

Katika jumla ya Hadithi zinazoonyesha uharamu wa pombe, ni iliyopokewa kuwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Yoyote anayekunywa hatakubaliwa Swala yake kwa muda wa siku arubaini, na anayekufa ilihali katika kibofu chake cha mkojo ana sehemu katika pombe ataharamishiwa Pepo. Na iwapo atakufa katika siku arubaini (tangu anywe pombe hiyo), atakuwa amekufa kifo cha kijahiliya]. (Tabarani, ameipokea kwa isnadi yake ni sahihi).

Anayekunywa pombe duniani atanyimwa Akhera kama ilivyopokewa katika Hadith ya ‘Abdullah Bin ‘Umar kuwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Atakayekunywa pombe duniani na asitubie dhambi hiyo, atanyimwa pombe ya Akhera]. (Bukhari na Muslim)

Hadithi nyingine kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) inasema: [Allâh amewalaani watu kumi katika pombe:- mgemaji, anayetaka kugemewa, mnyweshaji, mnywaji, muuzaji, mnunuaji, mbebaji, mwenye kubebewa, mwenye

kula thamani yake na mwenye kumnunulia mtu, wote hao wamelaaniwa kwa dua ya Muhammad].

Hikma ya Uislamu imepelekea kuharamisha uchache na wingi wa pombe na vilevi, kwa sababu uchache hupelekea katika wingi, halafu mazoea, kisha ikawa ndio uraibu. Jabir amesimulia kuwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Chochote kinacholewesha kwa wingi, na uchache wake pia ni haramu]. (Abu Dawud na an-Nasa-iy).

Katika mambo ambayo ni wajibu kuyahadharisha ni mti uliolaaniwa, nao ni mti wa bangi na aina nyingine ya miti ya motoni inayolevya inayoangamiza viwiliwili na akili za wanaotumia, ikawafanya wakose mizani na wawe dhaifu wa nguvu na azma, kutumia vichafu hivi huzima nuru ya macho na akili, humfanya mtu mbele ya watu kutokuwa na uadilifu na tabia mbaya. Hucheka na hulia bila sababu, macho humzunguka kama kwamba amefunikwa na mauti.

Maadui wa Uislamu wametengeneza aina nyingi ya madawa ya kulevya, wakatengeneza vidonge vinavyolevya vilivyochanganywa na heroin, haya ni matendo ya shetani, jiepusheni nayo ili mpate kufanikiwa.

KHUTBA YA PILI

Madhara ya kidini ya Madawa ya Kulevya na Ulevi

Enyi waja wa Allâh, madawa ya kulevya na ulevi, vitu hivyo vina madhara kwa upande wa dini. Allâh (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

قوله تعالى : ﴿إِنَّمَا يُرِيدُ ٱلشَّيْطَٰنُ أَن يُوقِعَ بَيْنَكُمُ ٱلْعَدَٰوَةَ وَٱلْبَغْضَآءَ فِى ٱلْخَمْرِ وَٱلْمَيْسِرِ وَيَصُدَّكُمْ عَن ذِكْرِ ٱللَّهِ وَعَنِ ٱلصَّلَوٰةِ ۖ فَهَلْ أَنتُم مُّنتَهُونَ ﴿٩١﴾﴾ [المائدة:٩١].

{{Hakika shetani anataka kutia kati yenu uadui na chuki kwa ulevi na kamari, na awazuie kumkumbuka Allâh na kuswali. Basi je, mmeacha?}}.

Ulevi huwazuia watu kuswali ambapo Swala ni nguzo ya dini, huzuia kumtaja Allâh na kusuhubiana na Malaika kwa dalii ya Hadithi ya al-Bazzaar kutoka kwa 'Abdullah Bin 'Abbas: "Malaika hawamkaribia mlevi''. Malaika wakiwa mbali naye, bila shaka mashetani watakuwa naye na yule shetani wake atazidi kufurahia. Kwa ajili hiyo mtumiaji yoyote wa madawa ya kulevya utamuona ni mzito kufanya ibada, moyo wake umeepushwa na mambo ya kheri na hupenda mambo ya haramu, kwa sababu moyo wake umejipa uchafu huu, ufuataji wa dini kwake huwa na mapungufu na hali yake daima ni ya kurudi nyuma.

Miongoni mwa Madhara ya kiafya yanayosababishwa na Madawa ya Kulevya

Enyi waja wa Allâh, miongoni mwa madhara ya kiafya yanayosababishwa na madawa ya kulevya, ni kwamba ubongo hukauka, husababisha kuchanganyikiwa, macho kuwa na giza, kisunzi, mapigo ya moyo kuwa dhaifu, mkakamo wa mishipa, kupooza viungo, mwanamke kutopata vizuri ada yake ya mwezi, kama ambavyo mtumiaji wa madawa hayo hupata wasiwasi na hamaniko, yeye huona

watu wako dhidi yake, hofu zimemzunguka kila upande, huogopa mwisho mbaya na maradhi mabaya. Ameepukana na kila fadhila, ameshikana na kila jambo duni. Ni makosa mangapi yaliyotendwa kutokana na taathira ya madawa ya kulevya ya kila aina, ni machafu na madhambi mangapi yaliyotendwa kwa kupotea kwa akili za watu? Ni heshima ngapi zimeharibiwa, mali kiasi gani zilizoibiwa, ni ajali ngapi zilizopatikana kwa sababu yake, ni watu wangapi walionyakuliwa ambao hawana kosa, yote hayo yanaingia katika athari ya madawa ya kulevya.

Enyi waja wa Allâh, maadui wa Uislamu hawahifadhi haki ya Muislamu, kila mara hujaribu kuwamaliza Waislamu na vijana wao. Kwa ajili hiyo ndio wanatengeneza madawa ya kulevya yanayoweza kutumiwa kiurahisi na wadogo kabla ya wakubwa, na kwa masikitiko madawa haya yameenea kwa vijana wengi wa Kiislamu, yanayosababisha baadhi yao kuwa katika hospitali teule na wengine kuwa jela maisha.

Mwisho

Wajibu wa akina Baba na Walezi kuhusu jambo hili Hatari

Nanyi enyi kina baba, nyinyi mna wajibu muhimu katika jambo hili, watoto wenu ndio wanaolengwa kwa haya madawa ya kulevya, wajibu wenu ni kuwahifadhi, kujihusisha nao na kumuomba Allâh kwa dua yenye ikhlasi na nia ya kweli Atuhifadhi sote dhidi ya maradhi haya yaangamizayo. Vile vile kusaidiana katika kupiga vita maradhi haya, hiyo ndio kinga madhubuti. Kuzungumzia juu ya maradhi haya hatari ni kwa njia ya kunasihiana, kuelekezana na kuchukua tahadhari. Maadui wa Uislamu walio kando yetu wanafuata kila njia ya kuudhuru Uislamu na wafuasi wake, na kuwamaliza vijana wao, yapasa akina baba kuwalea watoto wao malezi yaliyonyooka na utengevu, na kuacha kila lenye kudhuru na kuharibu, tukifanya hivyo tutakuwa tumeitika mwito wa Muumba wetu Mtukufu.

قال تعالى : ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ قُوٓاْ أَنفُسَكُمۡ وَأَهۡلِيكُمۡ نَارٗا وَقُودُهَا ٱلنَّاسُ وَٱلۡحِجَارَةُ عَلَيۡهَا مَلَٰٓئِكَةٌ غِلَاظٞ شِدَادٞ لَّا يَعۡصُونَ ٱللَّهَ مَآ أَمَرَهُمۡ وَيَفۡعَلُونَ مَا يُؤۡمَرُونَ ٦﴾ [التحريم:٦]

{{Enyi mlioamini! Jilindeni nafsi zenu na ahali zenu na moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanausimamia Malaika wakali, wenye nguvu, hawamuasi Allâh kwa anayowaamrisha, na wanatenda wanayoamrishwa}}.

Allâh Allâh tuwe kama anavyotutaka Allâh, tutekeleze wajibu wa Mola wetu unaotupasa, wala tusisahau kauli ya Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): "Nyote ni wachunga, na kila mmoja ataulizwa kuhusu alichokichunga". Tunaambizana wenyewe, ndugu zetu na kila mwenye ghera na nchi yake na haki za Waislamu wasaidiane na maafisa wa usalama – Allâh Awaafikie – katika kuwapa habari za wanaofanya biashara hii, kuwataja walanguzi, kuwatahadharsha wanaotumia na kuwataja wanachezea watu, kufanya hivi ni kufuata Kauli ya Allâh (Subhaanahu wa Taala):

قوله تعالى: ﴿وَتَعَاوَنُواْ عَلَى ٱلۡبِرِّ وَٱلتَّقۡوَىٰۖ وَلَا تَعَاوَنُواْ عَلَى ٱلۡإِثۡمِ وَٱلۡعُدۡوَٰنِۚ﴾ [المائدة:٢].

{{Saidianeni katika wema na uchamngu Wala msisaidiane katika dhambi na

uadui}}. Jambo hili latulazimu sote kushikamana bega kwa bega na tusaidiane, huenda Allâh Mtukufu Akaihami miji yetu, watoto wetu, vijana wetu na vizazi vyetu dhidi ya maradhi haya yaangamizayo. Yeye Allâh Ndiye mwenye kutusikia na kujibu dua. Mswalieni Mtume kwa kufuata amri ya Allâh alipotuamrisha:

قوله تعالى: ﴿ إِنَّ ٱللَّهَ وَمَلَـٰٓئِكَتَهُۥ يُصَلُّونَ عَلَى ٱلنَّبِىِّ ۚ يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ صَلُّوا۟ عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا۟ تَسْلِيمًا ﴿٥٦﴾ ﴾

[الأحزاب:٥٦]

{{Allâh na Malaika Wake wanamswalia Nabii. Enyi mlioamini! Mswalieni na mumsalimu kwa salamu}}.

Mwisho

Madhara ya madawa ya kulevya na athari yake mbaya inaonekana wazi kabisa katika jamii yetu. Yote haya ni kwasababu ya jamii kunyamaza kimya na kuacha kuamrisha mema na kukataza mabaya. Ili tuweze kuondosha maradhi ya madawa haya, ni lazima jamii yote kubeba jukumu la kuamrisha mema na kukataza mabaya.

Tunamuomba Allah Atuhifidhie watoto wetu, familia zetu na jamii yote. Tunamuomba Allah atuwezeshe kutekeleza wajibu wa kuamrisha mema na kukataza mabaya. Ewe Mola tuafikishe katika kila la kheri hapa duniani na kesho akhera.

(4) SEHEMU YA JAMII

Malengo Muhimu :

1. Kuijenga Jamii ya kiislamu kulingana na Sheria ya Allah, na kutukuzwa mwanadamu
2. Kueneza udugu wa Kiislamu kati ya Waislamu
3. Kuhifadhi haki na mambo ya wajibu ya kijamii.

Anuani ya Khutba katika Sehemu ya Jamii:-

1. Mizani na Namna ya kutengamana na Watu
2. Uhimizaji wa kuchuma Halali na kujiepusha na Haramu
3. Dini ya Kiislamu Imemtukuza Mwanamke wa Kiislamu
4. Kuwafanyia wema wazazi wawili na tahadhari ya kuwaasi
5. Haki za Jirani
6. Haki ya Muislamu juu ya Muislamu mwenzake
7. Kupeana nasaha na kutekeleza amana
8. Zaka na mchango wake katika kushikamanisha Jamii
9. Mahimizo katika kuunga Jamaa

[1] MIZANI NA NAMNA YA KUAMILIANA NA WATU

Lengo la Khutba:

1. Kubainisha mizani ya kisheria ya namna ya kuamiliana na watu.
2. Kupendana kati ya waumini.
3. Kuwa mbali na washirikina na kutowapenda kufanana nao.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Dini ya Kislamu imepanga sheria ya kila kitu. Na miongoni mwa sheria hizo, ni sheria ya kuishi na kufungamana na watu. Jamii moja inakusanya watu wa ina tofauti – makabila, utamaduni, tabia, Lugha na dini. Muislamu analazimika kuishi na watu wenye mila na dini tofauti kwa tabia mzuri kama tulivyo fundishwa na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Kila mwanadamu ana haki ya kuishi na ana haki ya kuabudu, kusoma na mengineyo. Lakini haki zote hizi ni lazima Muislamu azifahamu na kuzitekelza kulingana na misingi ya kisheria.

Mizani ya Mwenyezi Mungu katika kupima watu

Tunapozingatia Aya za Qur’an na Hadithi za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) tunaona Mwenyezi Mungu amejaalia utukufu kutokana na dini, taqwa na tabia njema na wala hakujaalia utukufu katika nasaba wala umaarufu. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قوله تعالى: ﴿إِنَّ أَكۡرَمَكُمۡ عِندَ ٱللَّهِ أَتۡقَىٰكُمۡۚ﴾ [الحُجُرات:١٣].

{{Hakika mtukufu miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni Yule amchae Mungu zaidi katika nyinyi}}.

Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Mbora wenu anayejifundisha Qur’an na akaifundisha].

Na akasema tena Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Mbora wenu anayetarajiwa kheri kutoka kwake na kuaminika na shari zake).

Ameulizwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Nani mbora kati ya watu? Akasema anayemcha Mwenyezi Mungu. Wakasema hatukuulizia swala hilo. Akasema Mtume Yusuf, wakasema hatukuulizia swala hilo, akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): Mbora wao katika ujahiliyya ni mbora wao katika uislamu, wakijuwa ubora mbele ya Mwenyezi Mungu ni kwa kumcha Mwenye na kufanya amali njema].

Mtume wa Mwenyezi Mungu anasawazisha mizani ya watu akasema: [Mwenyezi Mungu haangali sura zenu wala mali zenu lakini huangalia nyoyo zenu na vitendo vyenu].

Amepita mtu mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akamuuliza mtu aliyekaa nae, rai yako kwa huyu mtu aliyepita? Akasema ni mbora wa watu, akiposa huoa, akanyamaza Mtume wa Mwenyezi

Mungu, baada ya hapo akapita mtu mwingine akamuuliza rai yako kuhusu mtu huyu? Akasema huyu ni maskini, huyu ni mbora akiposa huoa, akisema hasikiwi, akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu huyu ni mbora.

Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alimuuliza Abu Dhari: [Huoni kuwa na mali nyingi ndio utajiri na kuwa na mali kidogo ni umaskini? Akasema ndio. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akasema utajiri ni utajiri wa moyo na umaskini ni umaskini wa moyo].

Walipozikwa mashahidi alikuwa Mtume akiuliza aliyehifadhi Qur’an zaidi akaashiriwa akawa humtanguliza mtu huyo katika kaburi. Mtume aliuliza pote la watu akamuuliza mzee wao kama amehifadhi Suratul Baqara akasema ndio, akamfanya kuwa kiongozi.

a. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amemfanya Ibn Ummi Maktoom ambae ni kipofu kuwa ni kiongozi wa Madina baada kusafiri Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).
b. Kama alivyomfanya Salmaa Faarisy kiongozi wa Madina baada kufungua Fursy.
c. Ameingia ‘Abdallah bin ‘Umar kwa babake akasema nimepewa elfu tatu na amepewa Usama elfu nne, akasema nimeshuhudia mambo asiyoshuhudia Usama. Akasema ‘Umar “Mzidishieni kwani yeye anapendwa na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) kuliko mimi, na Babake alikuwa akipendwa na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) kuliko mimi, kisha akawapa watu pesa kutokana na vyeo vyao, na kuhifadhi kwao Qur’an”

KHUTBA YA PILI

Ndugu Waislamu, hapana shaka ya kuwa neema ya udugu wa Kiislamu baina ya waumini na kupendana baina ya waja wa Mwenyezi Mungu ni katika neema kubwa juu ya umma huu. Na Mwenyezi Mungu Amewaamrisha waja wake kushikamana na udugu wa kiislamu, na kupendana.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَٱعۡتَصِمُواْ بِحَبۡلِ ٱللَّهِ جَمِيعٗا وَلَا تَفَرَّقُواْۚ﴾ [آل عمران:١٠]

{{Na shikamaneni kwa kamba ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane}}.

Kwa ajili hiyo Mwenyezi Mungu ametulazimisha kupendana, na sura za kupendana ni kama zifuatazo:-

1. Kuwanusuru Waislamu na kuwasaidia nafsi, mali na ulimi. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

   قال تعالى : ﴿وَإِنِ ٱسۡتَنصَرُوكُمۡ فِي ٱلدِّينِ فَعَلَيۡكُمُ ٱلنَّصۡرُ﴾ [الأنفال:٧٢]

   {{Na watakapo kuombeni nusra, basi wasaideni kwa kuwanusuru ndugu zenu}}.

2. Kuwa na uchungu kwa anachokipata muumini kwa jambo la huzuni na kufurahi wanapofurahika. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam):

[Waumini kupendana kwao na kuhurumiana kwao ni kama mwili mmoja].

3. Kuwanasihi waumini na kuwatakia kheri. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Hatoamini mmoja wenu mpaka ampendelee kheri ndugu yake anachokipendelea nafsi yake].
4. Kuwaheshimu waumini na kuwanyenyekea, kutowatia aibu na kutowasengenya, Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا يَسْخَرْ قَوْمٌ مِّن قَوْمٍ﴾ [الحُجرات:١١]

{{Enyi mlio amini, Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao}}.

5. Kuwa na waumini wakati wa furaha na shida.
6. Kuwatembelea na kuwa pamoja nao amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Mapenzi yangu yanastahiki kwa wenye kupendana kwa ajili yangu, na wenye kutembeleana kwa ajili yangu].
7. Kuheshimu haki ya waumini. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Asiuze Muislamu mauzo ya Muislamu mwenzake wala asipose posa ya mwenzake].
8. Kuwaombea waumini. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَٱسْتَغْفِرْ لِذَنۢبِكَ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَٱلْمُؤْمِنَـٰتِ﴾ [محمد:١٩]

{{Naomba msamaha kwa madhambi yako, na uwaombe msamaha waumini wa kiume na waumini wa kike}}.

Inapaswa kutowapenda makafiri na kutojifananisha nao, na akaamrisha waja wake kuwahalifu makafiri kwa kila jambo (Ibada, ada, itikadi). Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Atakayejifananisha na watu basi ni katika wao]. Kupendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu humuinua mja sehemu ya juu. Hadithi ya watu wa saba watakao funikwa na kivuli cha Mwenyezi Mungu siku ambayo hakuna kivuli, mmoja wao; [Watu wawili waliopendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wamekusanyika kwa ajili yake na kutengana kwa ajili yake].

Imepokewa na Abu Huraira kuwa mtu ametoka kumtembelea mwenzake katika kijiji kingine basi Mwenyezi Mungu akamtuma Malaika, akamuulize Yule mtu anaenda wapi? Akasema anamkusudia mtu fulani, akasema Malaika je ana neema? Akasema namtembelea kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, akasema Malaika basi mimi ni Malaika shuhudia kuwa Mwenyezi Mungu anakupenda kwa kumpenda ndugu yako"

Imepokewa hadithi ya Mtume kuwa: [Imani thabiti ni kupendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kuchukia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu].

Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Enyi watu sikieni na mtie akili, kwamba Mwenyezi Mungu ana waja si manabii wala sio mashuhadaa, wanatamaniwa na manabii na mashuhadaa kwa daraja waliyonao na ukaribu wao kwa Mwenyezi Mungu]. Hao ni watu kutoka maeneo tofauti na kabila tofauti tofauti, hawana kati yao ukaraba, wamependana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu,

watakalia makalio ya nuru siku ya Qiyama yaliyoandaliwa na Mwenyezi Mungu, na nyuso zao kuwa na nuru, na nguo zao kuwa na nuru, wanaogopa watu wala hawaogopi, hao ndio mawalii wa Mwenyezi Mungu hawana hofu wala huzuni"

Mwisho

Ndugu Waislamu, tabia njema na maadili mema ndio mizani ya sheria ya kupima kila jambo wakati ukitaka kuamiliana na jambo hilo. Vilevile, ni mizani ya kuamiliana na watu aina tofauti – Muislamu na asiyekuwa Muislamu. Muislamu ana haki zake juu yako. Na asiyekuwa Muislamu ana haki zake kulingana na misingi ya kisheria.

Tunamuomba Allah atuwafikishe tuweza kutekeleza haki za waja kama alivyo tuamrisha kupitia mafundisho ya Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). Ewe Mola wetu turuzuku mwisho mwema, na utupe hapa duniani mema na kesho akhera, Ewe Mola wetu usitupe chuki katika vifua vyetu, na utusamehe wewe ndio mwenye kusamehe.

[2] UHIMIZAJI WA KUCHUMA HALALI NA KUJIEPUSHA NA HARAMU

Lengo la Khutba:

1. Kuwalingania watu kuchuma chakula cha halali
2. Kubainisha umuhimu wa kupanga maisha ya dunia na kutoathirika na maisha hayo
3. Kutahadharisha kuzuia haki za wanaostahiki
4. Kubainisha fadhila na ubora wa kuchuma chakula cha halali na kujieupusha na chumo la haramu

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, hakika Allah ametuneemesha neema nyingi zisizo na idadi kama; neema ya afya, macho, masikio na n.k. Na neema kubwa kushinda neema zote ni neema ya Uislamu. Neema hii Allah (Subhaanahu wa Taala) anachagua katika waja wake wale ambao watapata hidaya yake na kuwa Waislamu. Ndugu katika imani, ni nani katika sisi ambaye hataki kuishi maisha mazuri hapa duniani na kesho akhera. Nani katika sisi ambaye hataki kuwa na afya njema yeye na familia yake?. Yote hayo yanapatikana katika kuchuma halali.

Ndugu Muislamu, ukitaka afya njema na maisha mazuri hapa duniani na kesho akhera, jitahidi kutafuta riziki ya halali, ndio ufunguo wa kila kheri. Hakika Mwenyezi Mungu Ametuhalalishia vitu vingi vizuri, na Akatuharimishia vitu vichache viovu. Kila kitu ambacho kina manufaa kwa mwanadamu Allah kahalalisha na kila kitu ambacho kina madhara kwa mwanadamu, Allah kaharimisha. Ndugu Waislamu, hiyo ndio rehema ya Allah kwa waja wake baada ya kutuongoza katika Uislamu kisha aliwafundisha kila kitu ambacho mwanadamu anahitaji katika maisha yake, na akawatahadharisha na kila kitu ambacho kinadhuru maisha ya mwanadamu.

Fadhila za Kuchuma Mali ya Halali

Ndugu Waislamu, Dini ya Kiislamu imeamrisha kuchuma halali na kuishi maisha mazuri. Imeamrisha watu kufanya kazi ya halali kwa bidii, kwa lengo la kujisaidia katika maisha. Na imekataza watu kuwa wavivu na kuomba omba njiani. Qur'an na Hadithi zimeweka wazi umuhimu wa kutafuta riziki na fadhila za kuchuma halali. Miongoni mwa fadhila za kuchuma halali:-

1. Kuchuma halali na kula chakula cha halali ni njia ya Mitume. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلرُّسُلُ كُلُواْ مِنَ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَٱعۡمَلُواْ صَٰلِحًاۖ﴾ [المؤمنون:٥١]

{{Enyi Mitume Kuleni vyakula vizuri na fanyeni mema. Hakika mimi ni Mjuzi wa yote mnayoyatenda}}. Na amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Hajakula mtu chakula kizuri kuliko chakula alicho kichuma kwa mikono yake, na Mtume Dawud alikuwa akila chakula kilicho chumwa na mikono yake].

2. Kutafuta chakula cha halali imeshikamanishwa na kwenda jihadi. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَءَاخَرُونَ يَضۡرِبُونَ فِي ٱلۡأَرۡضِ يَبۡتَغُونَ مِن فَضۡلِ ٱللَّهِ وَءَاخَرُونَ يُقَٰتِلُونَ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِۖ﴾ [المزمل:٢٠]

{{Na wengine watasafiri katka ardhi wakitafuta fadhila za Mwenyezi Mungu, na wengine watapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu}}.

3. Kuamrishwa kutafuta riziki ya halali baada ya kutekeleza ibada tukufu ya Swala. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

5. قال تعالى : ﴿فَإِذَا قُضِيَتِ ٱلصَّلَوٰةُ فَٱنتَشِرُواْ فِي ٱلۡأَرۡضِ وَٱبۡتَغُواْ مِن فَضۡلِ ٱللَّهِ﴾ [الجمعة:١٠]

{{Na itakapokwisha Sala, tawanyikeni katika ardhi mtafute fadhila za Mwenyezi Mungu}}.

4. Kuchuma halali na kula chakula cha halali ni sababu ya Allah (Subhaanahu wa Taala) kukubali dua zetu. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) : [Enyi watu, hakika Mwenyezi Mungu ni mzuri, na hakubali ila kitu kizuri. Kisha akataja mfano wa mtu anaye safiri safari ndefu hali akiwa amechoka, nywele zake zimejaa vumbi, anainuwa mikono yake kuelekeza mbinguni huku akisema: Ewe Mola wangu, Ewe Mola wangu, na hali kwamba chakula chake ni cha haramu, Kinywaji chake cha haramu na mavazi yake ni ya haramu. Vipi Allah ataikubali Dua yake].

Athari ya kuchuma Chakula cha haramu

Ndugu katika imani, Hakika kuchuma haramu na chakula cha haramu kina athari mbaya kwa mwenye kuchuma na kadhalika kwa jamii nzima. Miongoni mwa athari hizo ni:-

1. Kukosekana baraka na kuzidi ukame katika ardhi
2. Kuzidi magonjwa
3. Kuenea machafu katika ardhi
4. Dhulma na udhalimu kuzidi katika ardhi. Mfano wa watu kula mali kwa njia ya dhulma kama; kula Riba, kunyang'anya, kudanganya, kula Rushwa, na n.k.
5. Kupungua nafasi za kazi na kuzidi uhaba wa kazi
6. Dua kutokubaliwa

Ndugu Waislamu, mtu hawezi kuendelea katika maisha yake akiwa anachuma haramu. Vilivile, jamii haiwezi kuendelea ikiwa watu wake wanakula haramu. Leo watu hawachagui baina ya halali na haramu. Mtu hajali kula haramu na kulisha watu wake haramu. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Itawafikia watu wakati, mtu hatojali kula haramu]. Enyi Waislamu, tujihadharini sana na kula haramu. Na tujuwe wazi ya kuwa Allah (Subhaanahu wa Taala) Atatuliza siku ya akhera kila tulicho kichuma hapa duniani. Je ulichuma kwa njia gani? Njia ya halali au ya haramu?. Tuandae jibu la kumjibu mola wetu siku hiyo nzito.

Mifano ya Watu Wema katika kujiepusha na Haramu:

1. Swahaba Abubakar Siddiq alileletewa kitu na mfanyakazi wake. Abubakar akala, baada ya kula, yule mfanya kazi akamuliza Abubakar: Je wajua nimekipata wapi? Akasema Abubakar sijui. Akamuambia hicho kitu nilimdaganya mtu siku za jahalia (zama za ujinga) nilimfanyia uganga. Kisha akanipa hicho kitu ulicho kula kama zawadi. Abubakar akaingiza mkono wake mdomoni na akajitapisha na akatapika vyote vilivyokuwa tumboni.
2. Swahaba 'Umar Bin Khattab alikunywa maziwa, kisha akamuuliza yule aliyemletea maziwa: Je umepata wapi maziwa haya? Akamuambia nimechukuwa maziwa hayo kutoka kwa ngamia wa Sadaka katika Baitul maal. 'Umar akaingiza mkono wake mdomoni na akajichapisha maziwa aliyokunywa.
3. Mmoja katika wanawake wema alimuusia mumewe kwa kumuambia: Ewe mume wangu mche Mwenyezi Mungu, hakika sisi tunaweza kuvumilia njaa, lakini hatuwezi kuvumilia ukali wa moto wa jahannam.

Ndugu Muislamu, hivi ndivyo walivyo kuwa watu wema wakishi, na ndio siri kubwa ya kufaulu kwao nayo ni kwa ajili ya kujiepusha na haramu. Kwa hivyo, ni jukumu letu sisi Waislamu kujiepusha na haramu na kujifananisha na watu wema. Kufanya hivyo ndio kufaulu kukubwa hapa ulimwenguni na kesho akhera.

KHUTBA YA PILI

Ndugu katika imani, nawausieni na kujiusia nafsi kumcha Mwenyezi Mungu, na kufanya bidii kufuata maamrisho yake na kujiepusha na makatazo yake. Hakika jambo muhimu la Muislamu kujiepusha nalo ni kufuata matamanio ya kilimwengu, na kuwa hamu yake yote ni kupata ulimwengu, na akasahau akhera. Mtume Muhammad (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) anatufundisha ya kuwa dunia ni shamba la akhera. Muislamu akifanya bidii hapa duniani na kulima mazao mazuri, basi kesho atavuna mavuno mazuri.

Mambo yanayo sababisha kuchuma haramu

a. Kupenda ulimwengu na kuathirika na maisha ya ulimwengu na kusahau akhera. Amesema 'Abdillahi Ibnu 'Umar: ' Ishi katika dunia kama mgeni au mpita njia'
b. Kufuata matamino na hawaa ya nafsi. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Hatakuwa muumini mmoja wenu mpaka matamanio yake yafuatane sawa na niliyokuja nayo].
c. Kupenda kukusanya mali nyingi, mpaka mtu kumsahau muumba wake na kufanya mali ndio muumba wake. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Ameangamia mwenye kuabudu Dinari na Dirham].

Mwisho

Ndugu Muislamu, Ukitaka kheri na baraka katika maisha yako basi chuma mali ya halali, Mwenyezi Mungu Atakubariki katika mali yako na watoto wako na mambo yako yote. Hakika wale wanao chuma haramu na kula haramu wamo katika khatari kubwa hapa ulimwenguni kwa kuishi maisha ya dhiki na mwisho mbaya wakiondoka duniani. Vilevile, siku ya kiama watapata khasara kubwa nayo ni kukasirikiwa na Mola wao (Subhaanahu wa Taala). Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Hakika Mwenyezi Mungu ni mzuri na hakubali isipokuwa mazuri]. Ikiwa mtu anakula haramu na kuchuma maali ya haramu, kwa hakika huyo atakuwa mbali na rehma ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Ndugu Waislamu, Tujiepusheni na chakula cha haramu, mali ya haramu kama kula maali ya Riba, kudhulumu watu katika biashara, kula mali ya mayatima na n.k. Tunamuomba Allah Atuepushe na mali ya haramu, Atuwezeshe kutafuta riziki ya halali, tutosheke na kichache cha halali, na Atuhifadhi sisi na watu wetu na kila njia ya haramu.

[3] DINI YA KISLAMU IMEMTUKUZA MWANAMKE WA KIISLAMU

Lengo la Khutba:

1. Kubainisha hali ya mwanamke kabla ya kuja Dini ya Kiislamu
2. Kubainisha namna ya Uislamu ulivyo mpa cheo mwanamke wa Kiislamu
3. Kubainisha usawa wa mwanamke na mwanamume katika baadhi ya masuala
4. Kubainisha uwazi wa kutukuzwa mwanamke wa Kiislamu

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Ndugu katika imani, suala la mwanamke ni suala ambalo liliwashughulisha watu wengi walio pita, na linaendelea kuwashughulisha wengi katika zama zetu hizi. Dini na mila mbalimbali zimezungumzia hali ya mwanamke katika jamii. Wasomi wa elimu na falsafa tafauti wamejaribu kuzungumzia cheo cha mwanamke katika jamii. Lakini kila kundi linajaribu kumzungumzia mwanamke kwa misingi ya kufikia malengo yao. Katika khutba hii tutajaribu kuangazia cheo cha mwanamke katika jamii mbalimbali. Tutaangalia hali ya mwanamke kabla ya kuja Uislamu, na hali yake katika Uislamu, na hali yake katika mataifa ya magharibi.

Hali ya Mwanamke kabla ya kuja Dini ya kiislamu

Alikuwa mwanamke katika zama za ujinga akionekana kama bidhaa ambayo haina thamani. Kila mtu anaweza kumiliki bidhaa hiyo wakati wowote. Wanaume wakioa wanawake bila ya idadi maulumu na kuacha bila ya idadi ya talaka. Mwanamke haruhusiwi kumiliki chochote, hana haki ya kurithi, anaweza kuolewa na zaidi ya mume mmoja. Mwanamke hakuwa na cheo katika jamii ya ujahiliyah, bali alikuwa akionekana ni mtu anayeleta aibu katika jamii. Ikafikia hali hiyo, baadhi ya wanaume kuwazika mabanati wao wakiwa wadogo kuogopea kuleta aibu katika jamii. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Anatueleza hali ya mwanamke Akisema:

قال تعالى: ﴿ وَإِذَا بُشِّرَ أَحَدُهُم بِٱلْأُنثَىٰ ظَلَّ وَجْهُهُۥ مُسْوَدًّا وَهُوَ كَظِيمٌ ۝٥٨ يَتَوَٰرَىٰ مِنَ ٱلْقَوْمِ مِن سُوٓءِ مَا بُشِّرَ بِهِۦٓ ۚ أَيُمْسِكُهُۥ عَلَىٰ هُونٍ أَمْ يَدُسُّهُۥ فِى ٱلتُّرَابِ ۗ أَلَا سَآءَ مَا يَحْكُمُونَ ۝٥٩ ﴾ [النحل:٥٨-٥٩]

{{Na mmoja katika wao anapopewa khabari ya kuzaliwa mtoto wa kike, unabadilika uso wake huwa mweusi na akajaa sikitiko. Anajificha na watu kwa sababu ya khabari mbaya ile alioambiwa. (anafanya shauri) Je, akae naye juu ya fedheha hiyo, au amfukie udongoni. Ni mbaya mno hukumu yao hiyo}}. Hii ndio hali halisi ya mwanamke kabla ya kuja Dini ya kislamu. Na hali hii ilikuwa sawa katika mataifa yote, sawa taifa la kiarabu na wasiokuwa waarabu.

Hali ya Mwanamke katika Uisalmu

Baada ya mwanamke kuishi katika dhulma kwa muda mrefu, bila ya kupata haki zake. Allah (Subhaanahu wa Taala) Alimtumiliza Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) kuja kumkomboa mwanamke na dhulma na udhalilifu alikuwa akipata kutoka katika jamii anayo ishi. Dini ya Kiislamu inamtukuza mwanamke na inampa haki zake zote katika jamii. Miongoni mwa haki hizo:-

1. Mwanamke sawa na mwanamume katika kutekeleza majukumu ya Dini. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿مَنْ عَمِلَ صَٰلِحًا مِّن ذَكَرٍ أَوْ أُنثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهُۥ حَيَوٰةً طَيِّبَةً ۖ وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُم بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴿٩٧﴾﴾ [النحل:٩٧]

{{Wafanyaji mema, wanaume au wanawake, hali ya kuwa ni Waislamu, tutawahuisha maisha mema, na tutawapa ujira wao mkubwa kabisa}}. Na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) alimfadhilisha mwanamume kuliko mwanamke katika baadhi ya mambo, kwasababu ya majukumu mazito ya mwanamume katika kusimamia familia.

2. Mwanamke anastahiki kurithi. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

وقال سبحانه : ﴿لِّلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ ٱلْوَٰلِدَانِ وَٱلْأَقْرَبُونَ وَلِلنِّسَآءِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ ٱلْوَٰلِدَانِ وَٱلْأَقْرَبُونَ مِمَّا قَلَّ مِنْهُ أَوْ كَثُرَ ۚ نَصِيبًا مَّفْرُوضًا ﴿٧﴾﴾ [النساء:٧]

{{Wanaume wana sehemu katika mali wanayoacha wazazi wao na jamaa walio karibu. Na wanawake pia wanayo sehemu katika yale waliyaacha wazazi wao na jamaa walio karibu. Sawa yakiwa kidogo au mengi. Ni sehemu zilizofaridhishiwa (na Mwenyezi Mungu)}}.

3. Mwanamke ana haki ya kuchagua mume wa kumwoa. Hawezi kuolewa bila ya ridhaa yake. Kinyume na zama za jahiliyah, mwanamke alikuwa ni bidhaa na chombo cha starehe kila mtu anakichukuwa kwa thamani ndogo, na kwa lengo la kutekeleza matamanio yake.
4. Mwanamke ana haki ya kujikomboa kutokana na mume dhalimu. Sheria ya kiislamu imempatia mwanamke haki ya kutoa talaka kwa mwanamume mwenye tabia mbaya, mwenye kumnyima mkewe haki zake.

Haya ni baadhi ya mambo muhimu mabao mwanamke amepewa katika Dini ya kiislamu. Na hii ndio hali halisi ya mwanamke katika Uislamu. Uislamu ulimrejeshea mwanamke hadhi na utukufu wake katika jamii, na ikatambua mchango wake mkubwa katika kuandaa kizazi cha kesho na kulea viongozi wa kusimamia Dini ya kislamu. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) katika Hija: [Mcheni Mwenyezi Mungu katika kuwasimamia wanawake, kwa sababu wao ni wasaidizi wenu]. Mtume anaweka wazi cheo cha mwanamke nacho ni wasaidizi wa wanaume, sio mtumwa au mtumishi kama wanavyomdai watu wengine kwamba uislamu umemfanya mwanamke kuwa ni mtumwa hana haki yoyote katika jamii.

Enyi waja wa Allah, tumcheni Allah na tufanyeni bidii kuwasimamia wake zetu kulingana na alivyo tufundisha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

KHUTBA YA PILI

Ndugu Waislamu, nawausieni na kujiusia nafsi yangu kumuogopa Allah (Subhaanahu wa Taala), kwani wachaji Mungu ndio wenye kufaulu. Ndugu katika imani, tuangalieni hali ya mwanamke katika nchi zilizoendelea kama wanavyo dai nchi za kikafiri.

Hali ya Mwnamke katika nchi za kikafiri.

Hakika hali ya mwanamke katika nchi hizi ni mbaya sana kushinda hali ya mwanamke katika zama za jahiliyah. Mwanamke amefanywa kuwa ni kivutio cha kila badhaa au biashara kwa kudhihirisha uchi wake bila ya kujali wala kuona haya. Kila tukiangalia runinga, kusoma magazeti, internet tunashuhudia mwanamke ndiye wa kwanza kuonyeshwa hali akiwa uchi kabisa kwa lengo la kuvutia watu katika biashara hiyo. Kwa kweli mwanamke amepokonywa haki zake zote za kimsingi, haki ya kusimamia majukumu ya nyumba, kulea watoto, kuandaa familia juu ya misingi ya tabia njema na maadili mazuri.

Leo mwanamke hana nafasi nyumbani, kazi yake kubwa ni kutoka nje na kwenda kushindana na wanaume, na kudai haki za wanaume katika kazi. Imekuwa hakuna tafauti baina ya mume na mke. Na hili ndilo lengo kubwa la makafiri kumtoa mwanamke nje na kumvunjia heshima yake aliyopewa na Allah (Subhaanahu wa Taala). Na baadhi ya wanawake wa kiislamu wameathirika na tabia mbaya za makafiri. Wakaona haya ndio maendeleo na kuonekana kuwa mtu ameendelea.

Ndugu waumini, ni wajibu wetu kama wazazi kuwatahadharisha wake zetu mabanati wetu na kasumba mbaya za makafiri. Na tujue makafiri hawatokuwa radhi mpaka tufuate mila zao. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿وَلَن تَرْضَىٰ عَنكَ ٱلْيَهُودُ وَلَا ٱلنَّصَٰرَىٰ حَتَّىٰ تَتَّبِعَ مِلَّتَهُمْ ۗ قُلْ إِنَّ هُدَى ٱللَّهِ هُوَ ٱلْهُدَىٰ ۗ وَلَئِنِ ٱتَّبَعْتَ أَهْوَآءَهُم بَعْدَ ٱلَّذِى جَآءَكَ مِنَ ٱلْعِلْمِ ۙ مَا لَكَ مِنَ ٱللَّهِ مِن وَلِىٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿١٢٠﴾﴾ [البقرة:١٢٠]

{{Hawatukuwa radhi juu yako Mayahudi wala Wakristo mpaka ufuate mila yao. Sema hakika uongozi wa Mwenyezi Mungu ndio uongozi wa sawa. Na kama ukifuata matamanio yao baada ya yale yaliyokufikia ya ujuzi, hutapata msaidizi yoyote wala mlinzi kwa Mwenyezi Mungu}}.

Mwisho

Mwisho ndugu Waislamu, tukumbuke malipo na fadhila atakazopata mwenye kumlea msichana malezi ya kiislamu kisha amuozeshe mume mwenye tabia njema basi huyo amedhaminiwa kuingia peponi. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Mwenye kuruzukiwa mabinti watatu, na akasubiri juu ya kuwalea, kwa hakika mtu huyo amewajibika kuingia peponi. Akasema mtu kumuuliza Mtume: vipi ukiwa na wasichana wawili?. Akasema Mtume na wawili pia ni sababu ya

kuingia peponi].

Ndugu waumini, angalieni rehma ya Allah juu yetu katika kusimamia majukumu ya Allah kwa kuwalea wasichana kwa maadili mema na tabia njema, Allah atakulipa pepo yake ambayo si rahisi kuingia kila mtu, isipokuwa watakao simamia majukumu hayo.

Tunamuomba Allah atuwafikishe tuweze kutekeleza majukumu yote kwa njia ya kumridhisha yeye peke yake. Na tunamuomba Mwenyezi Mungu awahifadhi watoto wetu na kila shari ilio dhahiri na siri.

[4] KUWAFANYIA WEMA WAZAZI WAWILI NA TAHADHARI YA KUWAASI

Lengo la Khutba:

1. Amrisho la kumcha Mwenyezi Mungu la kuwafanyia wema wazazi wawili.
2. Amrisho la kusuhubiana na wazazi wawili kwa wema hata kama ni makafiri.
3. Namna ya kuwafanyia wema wazazi wawili.
4. Kubainisha cheo cha kuwafanyia wema wazazi wawili na thawabu zake na fadhila zake.
5. Kutahadharishwa na kuwaasi wazazi wawili.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Wazazi wawili wanayo haki kubwa kutoka kwa watoto wao, kama walivyo na haki watoto kutoka kwa wazazi wao. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Ameweka wazi kabisa haki za Pande zote mbili. Mwenyezi Mungu hakuwaachia wanadamu wajipangie wenyewe haki zao, bali Yeye Mwenyewe Amechukua jukumu la kuwapangia kila moja haki yake ili asipatikane na upungufu au dhulma katika kugawa hizo haki. Wazazi wana nafasi kubwa katika Dini ya Kiislamu. Wao ndio sababu ya kupatikana mtoto, baada ya kuvumila na kusubiri juu ya shida nyingi kisha kuzaliwa mtoto. Kwa kuvumilia kwao na kusubiri juu ya shida zote, wamepata cheo kikubwa mbele ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, mazungumzo yetu ya leo yataambatana kuhusu haki ambayo amelinganisha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) haki hiyo na haki yake katika maneno mengi katika kitabu chake kitukufu, nayo ni haki ya wazazi wawili. Jueni kwamba mafungamano makubwa baina ya mja na Mola wake ni kuumcha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) na kusimamia haki za wazazi na kusimamia haki za waja wake.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ ۞ وَٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا۟ بِهِۦ شَيْـًٔا ۖ وَبِٱلْوَٰلِدَيْنِ إِحْسَٰنًا وَبِذِى ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْيَتَٰمَىٰ ۞ ﴾ [النساء:٣٦]

{{Mwabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni wema wazazi wawili na jamaa na mayatima}}.

Jueni waja wa Mwenyezi Mungu kwamba kuwafanyia wema wazazi wawili ni wajibu hata kama ni makafiri, imepokewa na Asma " Amenijia mamangu na yeye ni mshirikina nikamshauri Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) kwa kumkata, Akasema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Mfanyie wema mamako]. Wema kwa wazazi haukatiki hata kama watakuamrisha kumkufuru Mwenyezi Mungu na kumshirikisha.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ وَوَصَّيْنَا ٱلْإِنسَـٰنَ بِوَٰلِدَيْهِ حَمَلَتْهُ أُمُّهُۥ وَهْنًا عَلَىٰ وَهْنٍ وَفِصَـٰلُهُۥ فِى عَامَيْنِ أَنِ ٱشْكُرْ لِى وَلِوَٰلِدَيْكَ إِلَىَّ
ٱلْمَصِيرُ ﴿١٤﴾ وَإِن جَـٰهَدَاكَ عَلَىٰٓ أَن تُشْرِكَ بِى مَا لَيْسَ لَكَ بِهِۦ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا ۖ وَصَاحِبْهُمَا فِى ٱلدُّنْيَا مَعْرُوفًا ۖ وَٱتَّبِعْ سَبِيلَ
مَنْ أَنَابَ إِلَىَّ ۚ ثُمَّ إِلَىَّ مَرْجِعُكُمْ فَأُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾ ﴾ [لقمان:١٤-١٥].

{{Na tumemuusia mwanadamu kuwafanyia ihsani wazazi wake – mama yake ameichukua mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na kumnyonyesha na kuja kumuachisha kunyonya katika miaka miwili- basi unishukuru Mimi na wazazi wako; marejeo yenu ni kwangu. Na wazazi wako wakikushurutisha kunishirikisha na yale ambayo huna ilimu nayo, usiwatii; lakini kaa nao kwa wema hapa duniani}}.

Na Mtume wa Mwenyezi Mungu alitanguliza haki za wazazi wawili kuliko jihadi. Imepokewa Hadithi na ‘Abdillah Ibn Mas’oud Amesema: [Nimemuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu amali gani ni bora Mbele ya Mwenyezi Mungu? Akasema: Swala katika wakati wake. Akasema kisha ni amali gani? Akasema: kuwafanyia wema wazazi wawili. Nikasema kisha amali gani? Akasema: jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu. Imepokewa na Muawiya bin Jahim Amesema: Amekuja mtu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema nataka kwenda jihadi, na nimekuja kukushauri. Akasema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) je una mama? Akasema ndio. Akasema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) jilazimishe na mama yako, kwani pepo iko chini ya miguu yake. Na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) anaomba kwa aliyepata wazazi wawili au mmoja wao na hakuingia peponi kwasababu yao basi mtu huyu amekhasirika].

Na visa vya wale watu watatu waliofunikwa na pango na hawakuweza kutoka akasema mmoja wao angalieni amali njema mliyomfanyia Mwenyezi Mungu, mumuombe Mwenyezi Mungu kupitia amali hiyo huenda Mwenyezi Mungu akatufariji, akasema mmoja wao: nilikuwa na wazazi wawili watu wazima na nilikuwa na watoto wadogo na nilikuwa nikiwachungia na ninapokamua nawanywesha wazazi wangu kabla ya watoto wangu, nilipokuja jioni na maziwa nimewakuta wamelala, nikaona vibaya kuwaamsha, pia nikachukia kumtanguliza mtoto wangu kabla yao na mtoto wangu alikuwa akilia na ilikuwa hivyo mpaka alfajiri, ewe Mwenyezi Mungu ukijua tendo langu hilo nikutaka radhi zako basi tufariji, Mwenyezi Mungu akawafariji mpaka wakawa wanaona mbingu.

Na katika kuwatendea wema ni kuwatii maadamu hujakhalifu amri ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ وَصَاحِبْهُمَا فِى ٱلدُّنْيَا مَعْرُوفًا ۖ ﴾ [لقمان:١٥]

{{Kaa na wao kwa wema hapa duniani}}. Na haki yao ni kuwapatia matumizi na kuwavisha ikiwa ni maskini, na kuwaombea Mwenyezi Mungu wakiwa hai na baada ya kufa Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ ۞ وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوٓا۟ إِلَّآ إِيَّاهُ وَبِٱلْوَٰلِدَيْنِ إِحْسَـٰنًا ۚ إِمَّا يَبْلُغَنَّ عِندَكَ ٱلْكِبَرَ أَحَدُهُمَآ أَوْ كِلَاهُمَا فَلَا
تَقُل لَّهُمَآ أُفٍّ وَلَا تَنْهَرْهُمَا وَقُل لَّهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا ﴿٢٣﴾ وَٱخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ ٱلذُّلِّ مِنَ ٱلرَّحْمَةِ وَقُل رَّبِّ ٱرْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيَانِى
صَغِيرًا ﴿٢٤﴾ ﴾ [الإسراء:٢٣-٢٤]

{{Na Mola wako amehukumu kuwa msimuabudu yoyote ila Yeye tu. Na kuwafanyia wema wazazi. Kama mmoja wao akifikia uzee, naye yuko pamoja nawe, au wote wawili, basi usiwaambie hata Ah. Wala usiwakemee. Na useme nao kwa msemo wa heshima}}.

Imepokewa na Ibn 'Umar kwamba yeye akitoka kuelekea Makkah alikuwa na punda na kilemba amejifunga nacho kichwani, siku moja alikutana na Bedui, akasema Bedui yule kumwambia Ibn 'Umar Je, wewe si mtoto wa fulani? Ibn 'Umar akasema ndio. Pale pale Ibn 'Umar akampa punda yule Bedui ampande na kilemba ajifunge. Baadhi ya Maswahaba wakasema Mwenyezi Mungu akusamehe umempatia bedui huyu punda ambaye kwamba ulikuwa ukitembea naye na kilemba uliyokuwa umejifunga nacho. Akasema amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Bora ya wema ni kuunga mtu vipenzi vya babake baada ya kuondoka duniani].

Kubainisha Cheo cha Kuwatendea Wema Wazazi Wawili, Thawabu zake na Fadhila zake.

a. Enyi Waislamu kuwatendea wema wazazi wawili ni sababu ya kuingia peponi, je umepata kujua kisa cha Uweis Bin Annur Al-Qarni? Huyu ni mtu aliyesimuliwa na Mtume kisa chake na akaamrisha maswahaba zake kutaka dua kutoka kwake, na kukurubishwa kwa Mwenyezi Mungu na haikuwa alama yake isipokuwa kuponya, hadithi ambayo ameipokea Imam Muslim inaeleza kuwa 'Umar alijiwa na pote kutoka Yemen akauliza jee kuna Uweis kati yenu? Mpaka alipokuja Uweis akasema wewe ndio Uwes? Akasema 'Umar jee ulikuwa na ugonjwa wa ukoma ukapona isipokuwa sehemu kama ya shilingi, akasema ndio, akasema 'Umar jee una mama? Akasema ndiyo. Akasema nimemsikia Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akisema: [Atakujieni Uweis na pote kutoka Yemen na alikuwa na ukoma na akapona ila sehemu ya shilingi na alikuwa mwema kwa mamake akimuapia Mwenyezi Mungu huwa jambo hilo ukiweza akuombee msamaha]. Akasema 'Umar niombee msamaha na akamuombea 'Umar msamaha.

b. Na Muhammad Ibn Sirin alikuwa akinyenyekea anapozungumza na mamake.

c. Hassan bin 'Ali Ibn Hussein Zeinul 'Abidin alikuwa akimfanyia wema mamake mpaka akaulizwa siku moja, kwa nini hatukuoni ukila sahani moja na mamako? Akasema naogopa kutangulia mkono wangu sehemu ambao kwamba jicho la mama limekwisha kutangulia, na hapo nitakuwa nimemuasi.

d. Na huyu Shureyh alikuwa ni miongoni mwa wanazuoni wakubwa alikuwa akiwafundisha wanafunzi wanaokuja kutoka sehemu mbali mbali na mamake alikuwa akimtuma kwa kumwambia awapatie chakula kuku, basi husimama na kuacha kufundisha. Huu ni mfano wa watu wema waliotangulia, vipi hali ya barobaro wetu leo huenda mmoja wao kukosea heshima mzazi wake na kumridhisha rafiki yake. Nakuusieni kuwafanyia wema wazazi wenu na kwenda mbio kuwaridhisha wao.

KHUTBA YA PILI

Ndugu zangu Waislamu kuwaasi wazazi wawili ni katika madhambi makubwa baada ya kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Je sikufahamishieni madhambi makubwa? Tukasema ndio ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, akasema ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu na kuwaasi wazazi wawili].

Imepokewa na Ibn 'Umar (Radhiya Llahu 'anhu) akisema, amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) : [Watu watatu hawatoangaliwa na Mwenyezi Mungu, mmoja wao ni Mwenye kuwaasi wazazi wake wawili].

Kuwaasi wazazi wawili kuna namna nyingi:-

a. Kukunja uso unapokabiliana nao.

b. Kuinua sauti unapozungumza nao.

c. Kuwakata maneno yao kwa kuwakemea au kuwalazimisha rai yako kwao.

d. Kuwatizama kwa jicho la dharau.

e. Kuchelewesha kukidhi haja zao.

Tahadhari kuwatangulizia Wasiokuwa Wazazi Wawili kwa Kuwafanyia Wema.

Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) : [Hapana dhambi ambayo adhabu yake huletwa kwa haraka kama kukata kizazi na dhulma]. Imepokewa kisa cha mtu mkubwa alimchukua babake katikati ya jangwa. Baba akasema: wanipeleka wapi mtoto wangu?. Mtoto akasema : umenichosha. Baba akasema: unataka nini? Mtoto: nataka kukuchinja umenichosha babangu. Baba: ikiwa hauna budi basi nichinje katika bonde lile. Mtoto: akasema kwa nini? Baba: nimemchinja babangu katika bonde lile lile, niuwe na utaona watoto wako watakuuwa katika bonde lile lile.

Mwisho

Ndugu katika imani, tujihadhari sana kutowafanyia wazazi wema. Adhabu yake ni kali sana na ni ya haraka kuadhibiwa hapa duniani na kesho akhera. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) Aliweka wazi suala hili kwa lengo la kumtahadharisha mwanadamu na maangamivu atakayo pata pindi akiwaasi wazazi wake. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) : [Hakuna dhambi ambalo Mwenyezi Mungu Anatanguliza kumuadhibu mja wake hapa duniani kuliko kukata jamaa, na kumuwekea adhabu nyingine siku ya kiama]. Waja wa Allah, rudini kwa Allah kwa kumuomba msamaha kwa makosa yote tuliyo mfanyia. Na tuweke azma ya kuwafanyia wema wazazi wawili kama tulivyo fundishwa na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam).

Tunamuomba Allah Atukubalie ibada zetu na atuwafikishe kufuata Kitabu chake na Sunna za Mtume Muhammad (Swalla Llahu 'alayhi wasallam).

[5] HAKI ZA JIRANI

Lengo La Khutba

1. Wasia wa kuwafanyia wema majirani na kuchunga haki zao
2. Kuweka wazi haki za jirani
3. Kubainisha fadhila za kuwafanyia wema majirani
4. Hadharisho la kuwaudhi majirani.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Ndugu zangu Waislamu, kila mmoja anahitaji mazungumzo hayo, maongezi ambayo Jibril hakuacha kumuusia Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) kuhusu jirani mpaka akadhani ana haki ya kurithi. Jirani ana haki zinapaswa kulindwa na hizo haki za jirani huyo ni sawa awe Muislamu au kafiri, mwema au muovu, rafiki au adui aliyekuwa karibu au mbali. Na kila mmoja ana daraja kuliko mwingine inazidi au inapungua kutokana na ukaribu wake, dini yake, tabia yake na ukaribu wake. Uislamu umeusia kuhusu jirani na kuhifadhi haki zake ambazo hazijatambuliwa na kanuni. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ وَٱعۡبُدُواْ ٱللَّهَ وَلَا تُشۡرِكُواْ بِهِۦ شَيۡـٔٗاۖ وَبِٱلۡوَٰلِدَيۡنِ إِحۡسَٰنٗا وَبِذِي ٱلۡقُرۡبَىٰ وَٱلۡيَتَٰمَىٰ وَٱلۡمَسَٰكِينِ وَٱلۡجَارِ ذِي ٱلۡقُرۡبَىٰ وَٱلۡجَارِ ٱلۡجُنُبِ ﴾ [النساء:٣٦]

{{Mwabuduni Mwenyezi Mungu wala msishirikishe na chochote. Na wafanyeni ihsani wazazi wawili, na jamaa, na mayatima, na maskini, na jirani walio karibu au jirani walio mbali}}.

Amepokea Ibn ‘Umar, amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Hakuacha Jibril kuniusia kuhusu jirani mpaka nikadhani kuwa jirani atarithi]. Amepokea Abu Huraira hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema: [Mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho azungumze mambo ya kheri au anyamaze, na anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho amkirimu jirani yake].

Amesema Sheikh Abu Muhammad: Kuhifadhi haki ya jirani ni katika kukamilika kwa Imani. Na watu katika zama za jahilia walikuwa wakihifadhi haki za jirani na wakiusia kwa kuwafanyia wema mfano kumpa zawadi, kumtolea salamu, kumuonyesha uso wa furaha na kujua hali yake na kumsaidia anacho kihitaji.

Amepokea Abu Huraira: ‘ Haki za Muislamu juu ya Muislamu mwenzake ni sita:-

1. Kumsalimia anapokutana naye
2. Kuitikia mwito anapokuita
3. Kupokea nasaha anapokuusia
4. Kumrehemu anapo chemua

5. Kumtembelea anapokuwa mgonjwa
6. Kufuata jeneza lake anapo kufa

Tahadhari Kuwaudhi Majirani

Ndugu zangu Waislamu ni haramu kuudhi majirani. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho basi asiudhi jirani zake]. I

mepokewa na Shureyh amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Naapa kwa Mwenyezi Mungu Haamini! Haamini! Haamini! Akaulizwa: Nani ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: Ni yule ambaye kwamba majirani zake hawasalimiki na shari zake].

Miongoni mwa sura za kuwaudhi majirani ni kuwaudhi watoto wake, kuchezea milki yake kuinua sauti kama ya nyimbo na kumpangisha mtu asiyeridhika nae.

Na kuwaudhi majirani kama kuwafanyia khiyana, kuwachunguza, kufuatilia aibu yake, kuangalia maharimu zake, kupitia dirisha lake au kumtembelea mke wake. Imetolewa onyo kali kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) kwa mwenye kufuatilia aibu za jirani zake, Ibnu Masoud alimueleza Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akisema: Ni dhambi gani kubwa? Ni kumkirisha Mwenyezi Mungu, kisha akasema ni dhambi gani? Akasema Mtume: ni kumuua mtoto wako kwa kuchelea kutomlisha, kisha akasema dhambi gani? Akasema ni kuzini pamoja na jirani yako". Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Kuzini mtu na wanawake kumi ni bora kuliko kuzini na mwanamke wa jirani yake].

Mcheni Mwenyezi Mungu, Enyi wenye kukhini jirani zenu ima kwa kuwapigia simu au kwa njia ya ujumbe au kwa njia ya kuangaliana. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

يقول الله سبحانه وتعالى : ﴿ وَٱلَّذِينَ يُؤۡذُونَ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ وَٱلۡمُؤۡمِنَٰتِ بِغَيۡرِ مَا ٱكۡتَسَبُواْ فَقَدِ ٱحۡتَمَلُواْ بُهۡتَٰنٗا وَإِثۡمٗا مُّبِينٗا ٥٨ ﴾ [الأحزاب:٥٨]

{{Na wale wanaowaudhi wanaume Waislamu na wanawake Waislamu pasipo wao kufanya kosa lolote, bila shaka wamebeba dhulma kubwa na dhambi zilizo dhahiri}}.

KHUTBA YA PILI

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu kuwaudhi majirani kuna namna nyingi kama zifuatazo; kutumia milki ya jirani mwenzake kwa kumuudhi mfano wake kuegemea matagaa ya mti wake kwa jirani mwenzake, kufanya kiwanda ambacho kinatoa moshi au sauti au upepo ambapo kinaudhi majirani wenzake yapaswa kuzuiwa mfano wa madhara haya.

Tahadhari na Mambo ya Futayo:-

a. Kuwakodisha majirani wasio swali wala wasio muogopa Mwenyezi Mungu
b. Kukodi duka au sehemu ya kuuza vitu vya haramu kama kaseti za nyimbo na nyenginezo

c. Kumzuia jirani kutoshughulika kwa milki ya jirani mwenzake kama kuweka mbao katika ukuta wa jirani mwenzake.

d. Kuwakataza jirani wenzake kunufaika kwa mambo ya shirika ya watu wote mfano wake kuteka maji katika kisima au mto. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): Watu ni washirika kwa mambo matatu:-

   1. Maji
   2. Moto
   3. Nyasi

e. Kuweka udhia katika njia.

Mcheni Mwenyezi Mungu na mbadilishane manufaa kati yenu na jirani zenu. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَتَعَاوَنُوا۟ عَلَى ٱلْبِرِّ وَٱلتَّقْوَىٰ ۖ وَلَا تَعَاوَنُوا۟ عَلَى ٱلْإِثْمِ وَٱلْعُدْوَٰنِ ۚ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ۖ إِنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلْعِقَابِ ﴿٢﴾﴾ [المائدة:٢]

{{Na saidianeni katika wema na twaa, wala msiaidiane katika dhambi na uadui}}

Mfano Mwema wa Waja Wema Waliopita na Jirani Zao

Tarekhe ya kiislamu imejaa mifano iliyokuwa ya juu kwa namna ya kuamiliana kati ya majirani. Imamu Dhahabi ametaja katika kitabu chake kwamba jirani wa Abi Hamza na huyu ni Walid Ibnu Kassim Bin Walid Hamdani ameulizwa Ahmad Ibni Hanbal akasema ni mwaminifu, na akaulizwa Abi Yaala akasema ni mtu bora na yeye ni jirani yetu tangu miaka hamsini iliopita na hatukumuona isipokuwa na kheri.

Ndugu katika imani, huo ni mifano ya watu wema waliopita namna walivyo ishi na majirani kwa wema na kusaidiana. Ni jukumu letu kuwaigiza watu wema na kufuata vitendo vyao, kwani huko ndiko kufaulu. Amesema Mshairi: Jifananisheni na watu wema hata kama hamtafanana nao, lakini kule kujifananisha nao ni kufaulu. Enyi Waumini fanyeni bidii kutekeleza haki za jirani kama alivyo tufundisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Mwisho

Ndugu Waislamu, tumeona wazi namna ya sheria ya Kiislamu ilivyo himiza juu ya haki za jirani. Na adhabu kali kwa wale watakao kiuka haki hizo. Kwasababu, mwanadamu ni lazima atekeleze haki mbili; haki ya kwanza ni ya Allah, na haki ya pili ni ya viumbe wenzake. Haki ya Allah anaweza mwanadamu kupata msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Yeye ni mwingi wa kusamehe. Lakini haki za mwanadamu ni lazima kutekeleza hapa duniani na ukishindwa, utadaiwa siku ya kiama. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Atuwezeshe kutekeleza haki zote zake na za viumbe vyake.

[6] HAKI YA MUISLAMU JUU YA MUISLAMU MWENZAKE

Lengo la Khutba:

1. Kubainisha haki ya Muislamu.
2. Uhakika wa udugu katika uislamu.
3. Fadhila za udugu katika dini.
4. Tahadhari na kukhitalifiana.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Enyi Waislamu,Uislamu ni dini kubwa imeweka muongozo ambao kwamba inakusanya haki na uwajibikaji, miongoni mwa haki hizo ni haki ya Muislamu juu ya Muislamu mwenzake. Lengo kubwa ya haki hizi ni kuleta mapenzi na udugu wa kiislamu. Kila Muislamu akijua haki yake na ya mwenzake, basi itakuwa ni wepesi Waislamu kushikamana na kuwa kitu kimoja.

Uhakika wa udugu katika dini

Umma wa kiislamu leo umekuwa kama povu la bahari, umevunjika nguvu zake na kuwa wanyonge. Na ulimwengu hauna heshima isipokuwa watu wenye nguvu. Na sababu ya kudhoofika umma wa kiislamu ni kufarikiana kati yao. Na nguvu ni matunda ya umoja na mapenzi na haukudhoofika umma huu ila baada ya kukosa umoja nao ni udugu.

Uhakika wa udugu ni pale Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alipounganisha maswahaba walipokuwa Makkah pamoja na kuhitalifiana rangi zao na maumbile yao na ndimi zao na malengo yao ya maisha. Amemuunga Hamza ambaye ni mkureishi na Salman ambaye ni mfursi na Bilal ambaye ni mhabasha na Suheib ambaye ni mrumi na wote wakawa wanaimba qaswida hii: Uislamu ndio baba yangu Wakijifakhiri kwa kabila la Qais au Tamim. Na wote walikuwa karibu na Neno lake Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالى: ﴿إِنَّمَا ٱلْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ فَأَصْلِحُوا۟ بَيْنَ أَخَوَيْكُمْ ۚ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿١٠﴾﴾ [الحُجُرات:١٠]

{{Kwa hakika Waislamu wote ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na Mcheni Mwenyezi Mungu ili mrehemewe}}. Hii ndio daraja ya kwanza katika udugu wa kiislamu, kisha Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akaunganisha watu wa Madina amabao ni kabila la Aus na Khazraj baada ya kupigana vita muda mrefu kati yao.

Kisha Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akaunganisha watu wa Makka (waliogura) na watu wa Madina. Kulipatikana tukio ambalo halina mfano kwa mwanadamu. Amepokea Anas hadithi akisema: [Alikuja AbdurRahman bin 'Auf kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akamuunga na Sa'ad bin Rabiya na alikuwa na mali nyingi, akasema Sa'ad: nitakugawiya nusu ya mali yangu na

nitakupatia mmoja kati ya wake zangu. Tazama anayekupendeza zaidi nimuache. Akasema AbdurRahman Mwenyezi Mungu akubariki, (nionyeshe soko)]. Kwa sasa hatuwezi kupata mfano wa Sa'ad!?. Mmoja wa watu wema alisema: Wako wapi wanaotoa mali yao usiku na mchana, siri na dhahiri akajibiwa: Wameenda pamoja na wasioomba watu wakafanya ung'ang'anizi. Enyi Waislamu haki ya Muislamu kwa Muislamu mwenzake ni kumpenda kwa ajili ya Mungu. Amepokea Anas Bin malik akisema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Mambo matatu mtu akiwa nayo anapata imani; moja wapo ni kumpenda mtu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu].

Miongoni mwa Haki ya Muislamu Juu ya Muislamu Mwenzake

1. Kupendana kwa ajili ya Allah (Subhaanahu wa Taala). Amepokea Abu Huraira hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akisema watu saba watafunikwa na kivuli siku ya kiama ambapo itakuwa hamna kivuli; mmoja wao ni watu wawili wapendanao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wameshikana kwa ajili yake Mwenyezi Mungu na wakatengana kwa ajili yake Mwenyezi Mungu.
2. Kutembeleana kwa lengo ya kujuana hali. Amepokea Abu Huraira hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akisema [Mtu alimtembelea ndugu yake katika kijiji kingine Mwenyezi Mungu akamtuma Malaika kwa sura ya binadamu, akamuuliza waenda wapi? Akasema: naenda kumtembelea ndugu yangu. Akasema: Je ana neema unayotarajia (kutoka kwake)? Akasema: Hamna neema yoyote, isipokuwa nimempenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Akasema Malaika: Mimi ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu nimetumwa kwako. Jua Mwenyezi Mungu anakupenda kama unavyompenda ndugu yako].
3. Kuitikia Salamu. Amepokea Abu Dawud akisema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) [Mguu hautoingia peponi mpaka muamini, na hamtomuamini mpaka mpendane. Je Nikujulisheni jambo mkilifanya mtapendana? Toleaneni salamu kati yenu].
4. Kufuata janeza na kwenda mazikoni. Amepokea Abu Huraira hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akisema: [Haki ya Muislamu juu ya Muislamu mwenzake ni sita kumsalimu pindi ukikutana nae, kuitikia wito anapo kuita, kuchukua nasaha yake anapo kunasihi, akichemua kumuambia Mwenyezi Mungu akurehemu, kumtembelea anapokuwa mgonjwa, kumzika anapokufa].
5. Kutokuwa na chuki. Anas amepokea hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Msichukiane, msifanyiene vitimbi, msishindane, kueni ndugu katika waja wa Mwenyezi Mungu]. Hasadi ni maradhi hatari jee huridhiki kwa aliyegawanya riziki ambaye ni Mwenyezi Mungu. Inapaswa kumuomba Mwenyezi Mungu yeye ndiye mtoaji. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى ﴿وَٱلَّذِينَ جَآءُو مِنۢ بَعۡدِهِمۡ يَقُولُونَ رَبَّنَا ٱغۡفِرۡ لَنَا وَلِإِخۡوَٰنِنَا ٱلَّذِينَ سَبَقُونَا بِٱلۡإِيمَٰنِ﴾

[الحشر:١٠]

{Na waliokuja baada yao wanasema: Mola wetu Tusamehe sisi na ndugu zetu waliotangulia katika Uisalmu}}.

Amepokea Anas akisema: Ilikuwa tumekaa pamoja na Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akasema Mtume: [Atakuja mtu wa peponi, akatokea mtu wa Answaar ndevu zake zilikuwa safi, na ameshika vitu vyake kwa mkono wa kushoto. Na siku ya pili Mtume akasema hivyo hivyo, na akatokea mtu yule yule hata siku ya tatu. Abdullah bin Amru akamfuata nyumbani kwake na akawa naye muda wa siku tatu, wala hakumuona akisimama usiku isipokuwa akishtuka usiku humtaja Mwenyezi Mungu katika kitanda chake mpaka ikifika swala ya alfajiri. Na alikuwa hamsikii isipokuwa akizungumza maneno ya kheri. Akamsimulia ‘Abdallah Bin ‘Amru sababu ya kumfuata kwa kuwa wewe ni mmoja kati ya watu wa peponi. Akasema: sina chuki na Muislamu yoyote].

6. Kumsaida Muislamu mwenzake akiwa na shida. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Mwenye kumsaidia Muislamu kwa kumuondoshea shida. Menyezi Mungu atamsaidia kumuondoshea shida ya siku kiyama. Na mwenye kumfanyia wepesi mtu mwenye uzito. Mwenyezi Mungu Atamfanyia upesi duniani na kesho akhera. Na mwenye kumsitiri ndugu yake Muislamu duniani na kesho akhera, Mwenyezi Mungu Atamsitiri dunuani na kesho akhera].
7. Kumnusuru Muislamu sawa akiwa amedhulumu au amedhulumiwa. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Mnusuru ndugu yako anayedhulumu au anayedhulumiwa. Akasema mtu: tunamnusuru anayedhulumiwa, lakini vipi tunamnusuru anayedhulumu? Akasema Mtume: ni kumzuia anapodhulumu].
8. Kusitiri aibu ya Muislamu na kumuombea Mungu msamaha kwa kosa lake. Kweli ndugu yako si Malaika wala si nabii kwani yeye ni mwanadamu.

   Wamesema wanavyuoni: Watu ni aina mbili:-

   1. Watu wanaojulikana kwa wema na kuepukana na maasi, basi wakikukosea unapaswa kusitiri na kutofunua aibu yake.
   2. Watu wanaofanya maasi kwa uwazi wala hawamuonei haya Mwenyezi Mungu, hao ni waovu.

KHUTBA YA PILI

Ndugu zangu Waislamu mafungamano ya uhakika ni mafungamano ya dini ambayo kwamba unafunga jamii kuwa kama mwili mmoja na pia kama jengo moja. Ndugu zangu Waislamu inapaswa juu yetu kusaidiana na kuwa ndugu moja.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَأَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ وَلَا تَنَٰزَعُواْ فَتَفۡشَلُواْ وَتَذۡهَبَ رِيحُكُمۡۖ وَٱصۡبِرُوٓاْۚ إِنَّ ٱللَّهَ مَعَ ٱلصَّٰبِرِينَ ٤٦﴾ [الأنفال:٤٦]

{{Wala msizozane (msigombane), msije mkaharibikiwa na kupotea nguvu, na vumilieni. Bila shaka Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wanaovumilia}}.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال تعالى : ﴿ وَٱعۡتَصِمُواْ بِحَبۡلِ ٱللَّهِ جَمِيعٗا وَلَا تَفَرَّقُواْۚ ﴾ [آل عمران:١٠٣]

{{Na shikamaneni kwa kamba (dini) ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane}}.

Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) kuweni ndugu katika waja wa Mwenyezi Mungu, mcheni Mwenyezi Mungu. Jueni kuwa Mwenyezi Mungu yuko pamoja na watu waliokuwa pamoja. Na umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Dini ya Kiislamu imewakataza waumini kuzozana na kubishana baina yao, kufanya hivyo, ni sababu ya umma kukosa nguvu na kuwa dhaifu mbele ya maadui. Umoja wetu na kupendana kwetu ni kushikamana na Kitabu cha Allah na mafundisho ya Sunna ya Mtume Muhammad (Swalla Llahu 'alayhi wasallam).

Mwisho

Ndugu katika imani, Msingi mkubwa wa kushikamanisha Umma na kuwa kitu kimoja ni udugu wa Kiislamu. Bila ya udugu wa kiislamu hatuwezi tukakushikamana. Na udugu unaanza chini kuanzia familia ndogo kupendana kwa ajili ya Allah, isiwe ni kwa ajili ya nasaba, kisha mapenzi katika jamii na baadae umma wote. Ni wajibu juu yetu kufuata mfumo wa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) katika kuleta udugu wa kiislamu. Ni lazima tufundishe familia zetu na jamii ya kiislamu mapenzi na udugu kwa ajili ya Allah (Subhaanahu wa Taala). Tukifanya hivyo, tutaweza kurejesha utukufu wa Dini ya kiislamu na kusimamisha serikali ya kiislamu.

Tumuombe Mwenyezi Mungu azidishe mapenzi baina yetu kwa ajili yake, na atuepushie na kila sababu ya kuchukiana na kutengana.

[7] KUPEANA NASAHA NA KUTEKELEZA AMANA

Lengo la Khutba:

1. Kubainisha kwamba nasaha ni katika Dini.
2. Kubainisha maana ya nasaha na ubora wake.
3. Kubainisha maana ya amana na ubora wa kuitekeleza.
4. Kutahadharisha kufanya khiana katika nasaha na kutekeleza amana.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu Aliyetuamrisha kukumbushana na kupeana nasaha katika mambo ya Dini yetu. Huku tukimtakia rehma na amani Mtume wetu Muhammad aliyekuwa mtoaji nasaha nambari moja vile vile mkweli mwaminifu.

Enyi Waislamu ! watukufu! Mazungumzo yetu ya leo ni kuhusu maudhui muhimu anayohitaji Muislamu katika maisha yake nayo ni nasaha, na nasaha ni kumtakia kheri apewaye nasaha. Tukijua ya kwamba nasaha ni msingi mkubwa wa dini, bali Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema kwenye hadithi yake: [Dini ni nasaha, Dini ni nasaha, Dini ni nasaha. wakamuuliza maswahaba: ‘Kwa nani ewe Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akasema : Kwa Mwenyezi Mungu na kitabu chake na Mtume wake na viongozi wa kiislamu na Waislamu kwa jumla].

Faida tunazozipata katika hadithi hii ni kule kuonesha ya kwamba nasaha ina daraja ya juu kabisa, na faida nyingine kutajwa sehemu ambazo nasaha hupatikana. Sehemu hizo ni nasaha kwa Mwenyezi Mungu Aliyetukuka nayo ni kufanya ibada kwa ajili Yake pekee na kutaka radhi Zake. Ama nasaha kwa kitabu chake ni kukisoma na kufuata maamrisho yaliyomo na kujiepusha na makatazo yaliyokatazwa ndani ya Kitabu hicho na kuziamini khabari zilizomo ndani yake. Ama nasaha kwa Mtume wake ni kumpenda na kufuata maamrisho yake na kujiepusha na makatazo yake na kuitetea heshima yake akiwa hai au akiwa amekufa. Ama nasaha kwa viongozi kuwaunga mkono kidhati kuwapa nasaha kwa maslahi ya umma katika ulimwengu wao na akhera yao. Pia kuwasikiliza na kuwatii katika mambo mema na kuitakidi kwamba ni lazima kufuata maamrisho yao ikiwa hawakuamrisha maasi. Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

فقال تعالى : ﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ وَأُوْلِي ٱلۡأَمۡرِ مِنكُمۡۖ ﴾ [النساء:٥٩].

{{Enyi mlio amini mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na viongozi katika nyinyi}}. Ama nasaha kwa Waislamu wa kawaida ni kuwapendea kheri na kuwaepushia uovu vile vile kuyazungumza mazuri yao na kuyaficha maovu yao na kuishi nao kwa upendo na udugu. Pia kuwasaidia endapo wanadhulumiwa. La kusikitisha ni kwamba Waislamu wamepuuza suala zima la kupeana nasaha. Tukijua ya kwamba kulipuuza suala hili ni kwenda kinyume na maamrisho ya Mwenyezi Mungu na hasara yake ni kubwa duniani na kesho akhera.

Sifa za Mtoaji Nasaha

Kuna mambo yatakiwa yazingaziwe na yafuatwe katika kadhia nzima ya nasaha Kati ya mambo hayo ni kama yafuatayo:

1. Ni lazima nasaha iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), na isiwe kwa ajili ya kutaka sifa au kuonekana na watu. Mola (Subhaanahu wa Taala), Amesema:

   قال تعالى : ﴿وَمَآ أُمِرُوٓا۟ إِلَّا لِيَعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ﴾ [البيّنة:٥].

   {{Na hawakuamrishwa isipokuwa wamuabudu Mwenyezi Mungu hali ya kumtakasia yeye ibada}}.

2. Ni lazima awe mtoaji nasaha ni mjuzi wa yale anayoyazungumza.

3. Ni lazima mtoaji nasaha awe mwaminifu. Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema akizungumza kuhusu Mtume Huud :

   قال تعالى حكاية عن هود عليه السلام : ﴿أُبَلِّغُكُمْ رِسَٰلَٰتِ رَبِّى وَأَنَا۠ لَكُمْ نَاصِحٌ أَمِينٌ ﴿٦٨﴾﴾ [الأعراف:٦٨]

   {{Nafikisha ujumbe wa Mola wangu na mimi kwenu ni mtoaji nasaha mwaminifu}].

4. Nasaha iwe kwa njia ya siri kwa kiongozi na raia, lakini ikishindikana basi hakuna ubaya ikiwa wazi na khaswa ikiwa ni mambo yaliyo kinyume na sheria waliyo kubaliana wanachuoni wote kwamba ni haramu.

   Haishurutishwi kwa mtoaji nasaha awe mwanachuoni mkubwa na wala si lazima awe mwadilifu zaidi kuliko anayepewa nasaha. Amesema Imam Ishaaq Ibn Ahmad katika Utangulizi wa nasaha kumwandikia Ibn Al-Jauzia Mwenyezi Mungu awarehemu: ‘Kama ingekuwa hakatazi ovu aliye na elimu chache kumkataza mwenye elimu nyingi ingekuwa watu hawakatazani maovu na tungekuwa kama Bani Israail pale Mwenyezi Mungu Aliposema: ”Walikuwa hawakatazani maovu waliyokuwa wakiyafanya’.

Enyi Waislamu ! Lau atafuatilia Muislamu hali za wema waliotangulia ataona vipi walipigiwa mfano katika kutoa nasaha na kuzikubali. Napenda nitaje mifano miwili nadhani itatosha:

1. Amesema Abubakar Swiddiq, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: “ Hana kheri katika sisi asiyekubali nasaha na hana kheri katika nyinyi asiyeitoa nasaha”.
2. Amesema ‘Umar ibn Khattwab radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: “ Mwenyezi Mungu amrehemu mtu aliyeniletea zawadi ya aibu zangu”.

Enyi waumini! Tujibidiisheni katika kutoa nasaha. Na tumtakasie Mwenyezi Mungu katika kadhia nzima ya kutoa nasaha.Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie miongoni mwa wanaosikiliza mema na wakawa ni wenye kuyafuata.

KHUTBA YA PILI

Umuhimu wa Kutekeleza Amana.

Shukrani za dhati ni za Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), na rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad. Enyi Waislamu! Mwanzo kabisa maana ya amana ni kulazimiana mwanadamu na haki ya Mwenyezi Mungu na ibada yake kama alivyoamrisha hali ya kumtakasia yeye ibada.

Ndugu katika imani! Ametuamrisha Mola kutekeleza amana na sehemu ambazo amana hupatikana. Miongoni mwa sehemu hizo ni kusimamisha Swala. Kwani Swala ni amana na atakayeipoteza Swala basi isiyokuwa swala ni wepesi zaidi kuipoteza. Zaka pia ni amana. Pale alipowapiga vita Abubakar Swiddiq radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, waliokataa kutoa zaka inaonesha kwamba yeye aliichukulia zaka kuwa ni jukumu muhimu la Dini, na kuwa wale waliokataa kutoa wameritadi. Saumu pia ni amana. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [kiwa mmoja wenu amefunga siku yoyote ile, basi asifanye uovo wala ujinga na akimtukana yeye mtu au akimpiga basi aseme mimi nimefunga]. Vile vile Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema : "Anayekusudia kufanya hija katika miezi ya hija basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika hija].

Na vile vile ulinganizi kwa Mwenyezi Mungu ni amana. Hizi na nyinginezo nyingi ni sehemu ambazo amana hupatikana. Nikiongezea baadhi ya mambo ambayo ni katika utekelezaji wa amana ni kuwa na nguvu katika kuhifadhi haki za watu, pia katika kuwafanyia wema wazazi wawili. Vilevile ni katika amana kwa Muislamu kuchunga masikizi yake, macho na vile vile moyo wake asifanye maasi. Pia ni katika utekelezaji wa amana Muislamu kuhifadhi vyema elimu aliyoisoma. Wanavyuoni wanasema: "Hakika hii elimu ni dini basi angalieni mnaichukua kutoka kwa nani".

Na walipokuja watu kutoka Yemen walipomtaka Mtume awape mtu wa kuwafundisha dini. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alimshika Abu 'Ubaidah mkono na akamwambia : [Huyu ni mwaminifu wa umma huu]. Pia kuwahudumia wanaohitajia ni utekelezaji wa amana. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Nyote ni wachunga na nyote mtaulizwa kwa munachokichunga].

Pia ni katika amana kuyatekeleza aliyoamuru Mungu na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). Kama ambavyo ni utekelezaji wa amana kuwaheshimu watu na kuwaweka daraja zao. Ni miongoni mwa utekelezaji wa amana ni kutoa ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu hata kama ni dhidi ya mtu wako wa karibu. Pia kuwabainishia haki. Aliulizwa mwanachuoni mkubwa kuhusu babake akasema: "Baba yangu ni dhaifu". Haya ni katika yanayohusiana na upokeaji wa hadithi. Tukijua kwamba mtu dhaifu, hadithi zake hazikubaliwi. Pia aliweza kutoa ushahidi Shu'ba ibn Hajjaj kuhusu mtoto wake: 'Nimemwita mwanangu mzuri lakini hakuwa mzuri kitabia na hakufaulu". Vile vile ni utekelezaji wa amana

mtu kuwacha madai ya uongo kudai kuwa ana kitu fulani au anajua kitu fulani na ukweli ni kwamba hana kitu kile. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Mwenye kudai asicho kuwa nacho ni kama aliyevaa nguo ya uzushi]..

Mwisho

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu! Nawausia tunasihiane kati yetu, kwani si lengine hii Dini ni watu kupeana nasaha na mawaidha, kuamrishana mema na kukatazana maovu. Hakuna ubora wala kheri yoyote katika umma ambao watu wake hawapeani nasaha katika Dini. Na tekelezeni amana alizowapa Mwenyezi Mungu kwa wenyewe. Najueni ya kwamba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Atawauliza mlivyo vichunga siku ambayo haitomfaa mtu mali yake wala watoto isipokuwa atakayekwenda kwa Mwenyezi Mungu na moyo ulio salimika na madhambi.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Atujaalie ni miongoni mwa wenye kutoa nasaha na wenye kuzikubali nasaha na wenye kutekeleza amana alizotupa!

[8] ZAKA NA MCHANGO WAKE KATIKA KUSHIKAMANISHA JAMII

Lengo la Khutba:

1. Kubainisha wajibu wa kutoa zaka na kubainisha mali zinazotolewa zaka.
2. Athari ya kutoa zaka kwa mtu na jamii kwa ujumla.
3. Onyo kwa wanaozuia zaka.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) na Anayestahiki shukran za dhati. Pia rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

Je, waijua ibada ya kutoa mali yako wewe Muislamu? Je, wajua kwamba ibada hii ukiifanya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Atakuzidishia baraka katika mali yako hapa duniani na malipo makubwa kesho Akhera? Je, hujui kwamba mali uliyonayo ni mali ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) na Amekupa mtihani katika mali hayo? Je, watarajia kufaulu mtihani huo?.

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu! tutazungumzia katika khutba yetu ya leo kuhusu ibada iliyo tukufu ambayo mtu inaambatana na mali. Mtu akitioa mali yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), mali yake huzidi na kupata malipo makubwa kwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) na ni nguzo ya tatu katika Uislamu si nyingine nayo ni zaka. Ni wajibu wa kila Muislamu mwenye mali yaliyofika kiwango kutoa fungu maalum. Mola (Subhaanahu wa Taala) amesema ndani ya Qur’an tukufu:

قال تعالى : ﴿وَأَقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتُوا۟ ٱلزَّكَوٰةَ﴾ [النور:٥٦]

{{Na simamisheni Swala na mtoe Zaka}}. Na katika hadithi za Bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: [Uislamu umejengwa na mambo matano; kupwekeshwa Mwenyezi Mungu, kusimamisha Swala, kutoa Zaka, kufunga mwezi wa Ramadhani na kufanya hija].

Yamekuja maonyo mbali mbali na tahadhari kwa Muislamu katika suala nzima la kuikwepa Zaka na kufanya ubakhili wa kutekeleza ibada hiyo. Mola (Subhaanahu wa Taala) ameahidi adhabu kali kwa kila ambaye haitekelezi ibada hii tukufu. Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala) :

قال الله عز وجل : ﴿وَمَا لَكُمْ أَلَّا تُنفِقُوا۟ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَلِلَّهِ مِيرَٰثُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۚ لَا يَسْتَوِى مِنكُم مَّنْ أَنفَقَ مِن قَبْلِ ٱلْفَتْحِ وَقَٰتَلَ ۚ أُو۟لَٰٓئِكَ أَعْظَمُ دَرَجَةً مِّنَ ٱلَّذِينَ أَنفَقُوا۟ مِنۢ بَعْدُ وَقَٰتَلُوا۟ ۚ وَكُلًّا وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلْحُسْنَىٰ ۚ وَٱللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿١٠﴾﴾ [الحديد:١٠].

{{Na wala wasidhani wale ambao wanafanya ubakhili katika yale aliyowapa Mwenyezi Mungu katika fadhila zake kuwa ni bora kwao. La ni vibaya kwao. Watafungwafungwa kwa yale waliyofanyia ubakhili Siku ya Kiama, na urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ana khabari

za yote mnayoyafanya}}. Vile vile Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) :

وقال تعالى : ﴿وَٱلَّذِينَ يَكۡنِزُونَ ٱلذَّهَبَ وَٱلۡفِضَّةَ وَلَا يُنفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ فَبَشِّرۡهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٖ ٣٤ يَوۡمَ يُحۡمَىٰ عَلَيۡهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فَتُكۡوَىٰ بِهَا جِبَاهُهُمۡ وَجُنُوبُهُمۡ وَظُهُورُهُمۡۖ هَٰذَا مَا كَنَزۡتُمۡ لِأَنفُسِكُمۡ فَذُوقُواْ مَا كُنتُمۡ تَكۡنِزُونَ ٣٥﴾ [التوبة:٣٤-٣٥]

{{Na wale wakusanyao dhahabu na fedha wala hawazitoi katika njia ya Mwenyezi Mungu, wape habari za adhabu inayoumiza. Siku mali yao yatakapotiwa katika moto wa jahannam, na kwa hayo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao (na huku wanaambiwa). Haya ndiyo (yale mali) mlio jilimbikizia nafsi zenu basi onjeni (adhabu) yale mliyokuwa mkiyakusanya}}.

Faida za Zaka kwa upande wa Dini

Ndugu zangu katika imani! Zaka ina faida nyingi sana, nyingine za kidini, za kitabia na pia faida za kijamii. Basi kaa makini nikutajie miongoni mwa faida zake za kidini:

1. Kutoa Zaka ni kusimamisha nguzo, katika nguzo za Uislamu ambayo ni sababu ya utukufu duniani na kesho akhera.
2. Zaka zinamkurubisha mja kwa Mola wake na zinamzidishia mtu imani.
3. Mtu atoapo zaka hupata ujira na malipo makubwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Asema Mola (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالى : ﴿يَمۡحَقُ ٱللَّهُ ٱلرِّبَوٰاْ وَيُرۡبِي ٱلصَّدَقَٰتِۗ﴾ [البقرة:٢٧٦]

{{Allah Anaiangamiza riba na Anaikuza sadaka}}.

4. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) humfutia madhambi Muislamu atoapo zaka. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) Amesema: [Na sadaka (zaka) inaondosha maovu kama maji yanavyozima moto].

Faida za Zaka kwa upande wa Tabia

Na miongoni mwa faida za kitabia:

1. Kutoa zaka inamuweka mtu katika kundi la watu wakarimu na wenye kujali maslahi ya watu,
2. Kutoa zaka kunamfanya mtu kusifika na sifa ya huruma na upole kwa ndugu zake.Kwani Waislamu wenye huruma Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) pia huwahurumia.
3. Kutoa zaka kunasafisha vifua vya watu wenye kupewa mali ile na watampenda mtoaji kwa kule kuwajali ndugu zake na kuwasaidia.
4. Kutoa zaka kunamsafisha mtoaji na sifa ya ubakhili na uchoyo. Na tabia mbaya hii ya ubakhili ni miongoni mwa tabia mbaya ambazo haitakiwi Muislamu kujipamba nayo. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema katika kitabu chake kitukufu:

قال تعالى : ﴿خُذۡ مِنۡ أَمۡوَٰلِهِمۡ صَدَقَةٗ تُطَهِّرُهُمۡ وَتُزَكِّيهِم بِهَا﴾ [التوبة:١٠٣]

{Chukua katika mali yao zaka ili uwasafishe na uwatakase}}. Kuwatakasa na

kuwasafisha kutokana na tabia ya ubakhili.

Faida za Zaka kwa upande wa Jamii

Na miongoni mwa faida za kijamii katika kutoa zaka:

1. Kutoa zaka huwaondolea watu matatizo ya kiuchumi waliyonayo na kama illvyo ni kwamba wanaohitajia ni wengi.
2. Kutoa zaka hutilia nguvu mambo ya Waislamu wanayotaka kuyafanya kwa mfano kupigana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).
3. Zaka huondoa chuki baina ya maskini na matajiri na kuleta mapenzi baina yao.
4. Zaka hukuza mali na kuyazidisha na kuwa na baraka. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Haipungui mali inayotolewa zaka].
5. Kutoa zaka hueneza mali baina ya watu na haibaki kwa matajiri bali huzunguka kati yao.

Na hizi faida tulizozitajaza ziwe ni za kijamii au za kidini au za kitabia zinaonesha kwamba kutoa zaka ni jambo muhimu sana na dharura Ili kutengeneza nafsi ya mtu na jamii kwa ujumla.

Enyi watukufu Waislamu! kutoa zaka kuna athari katika nafsi ya mtu na jamii kwa ujumla. Kwani kutoa zaka ndio nidhamu ya kwanza waliyoijua watu katika kuwasaidia wanaohitaji na uadilifu katika jamii nzima ya kiislamu. Kwani mali inatoka katika tabaka ya matajiri na kwenda katika tabaka ya maskini na wanaohitajia. Ukweli ni kwamba zaka inasafisha mali ya mtoaji na kuikuza kama ambavyo inamtakasa moyo wa mtoaji zaka kutokana na tabia ya ubakhili, tamaa na kutojali wanaohitajia. Vilevile inasafisha moyo wa anayepewa zaka kutokana na tabia mbovu ya uhasidi na chuki kwa mwenye mali.

Tukiangalia vyema pia kutoa zaka kunazidisha mshikamano kati ya jamii inayoishi pamoja na kuondoa umaskini na pia kuangamiza matatizo ya kijamii, kiuchumi na ya kitabia endapo itatolewa na kupewa wanaostahili.

KHUTBA YA PILI

Mali yanayotolewa Zaka

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Muumba wa mbingu na ardhi. Rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam).

Enyi waumini! mnaonisikiliza napenda kuchukua fursa hii adhimu kuwatajia mali ambayo inatakiwa kutolewa zaka kwa lengo la kukumbushana. Miongoni mwa mali ambayo hutolewa zaka ni dhahabu, fedha kwa sharti ifike kiwango na wajibu ni robo ya kumi ya dhahabu au fedha.Na katika mali ambayo ni lazima kutolewa zaka ni bidhaa za biashara nazo ni kila kilichofanyiwa biashara kwa mfano:majumba, magari, nafaka, mifugo, vitambaa na vyingenevyo. Na ni wajibu kutoa katika mali tuliyo yataja robo ya kumi.

Ama vitu vilivyoandaliwa kwa matumizi ya kawaida kama Magari ya matumizi, Majumba ya kuishi na vitu mfano wa vitu hivi havitolewi Zaka. Kwa neno la Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Haifai Muislamu kumtoa mtumwa wake wala farasi wake zaka].

Baada ya kuwaelezea mali ambayo yanayotakiwa tutoe Zaka na mali ambayo hayafai kuyatoa zaka. Sasa nachukua nafasi hii kuwatajia wanaostahiki kupewa zaka hizo. Miongoni mwa watu wanaostahiki Mwenyezi Mungu aliyetukuka ndani ya Qur’an Tukufu Aliposema :

قال تعالى : ﴿ ۞ إِنَّمَا ٱلصَّدَقَٰتُ لِلۡفُقَرَآءِ وَٱلۡمَسَٰكِينِ وَٱلۡعَٰمِلِينَ عَلَيۡهَا وَٱلۡمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمۡ وَفِي ٱلرِّقَابِ وَٱلۡغَٰرِمِينَ وَفِي سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱبۡنِ ٱلسَّبِيلِۖ فَرِيضَةٗ مِّنَ ٱللَّهِۗ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٞ ٦٠ ﴾ [التوبة:٦٠]

{{Hakika zaka hupewa mafukara na maskini na wanazikusanya na waliosilimu karibu na watumwa na wenye madeni na katika jihadi na kupewa msafiri zaka hii ni faradhi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye hikma}}.

Nachukue tena nafasi hii kuwafafanulia aliyowataja Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) katika wanaostahiki kupewa zaka.

Wanaostahiki Kupewa Zaka

1. Fukara; ni mtu ambaye hapati cha kumtosha isipokuwa kidogo chini ya nusu. Kwa hivyo ikiwa mtu hapati cha kujisimamia yeye na familia yake nusu mwaka basi huyo ni fukara. Kwa hiyo atapewa cha kumtosha yeye na familia yake mwaka mzima.
2. Maskini; ni mtu ambaye anapata cha kumtosha nusu na zaidi lakini hapati cha mwaka mzima kwa hiyo hupewa zaka ili kumkamilishia mahitaji.
3. Wenye kukusanya zaka; ni wale ambao wanamuwakilisha kiongozi kwa kukusanya mali ya zaka kutoka kwa wenye mali na kuwapelekea wanaostahiki na kuyahifadhi.
4. Waliosilimu karibu hawa hupewa ili kuzitia nguvu imani zao hatimaye wawe walinganizi wa dini ya kiislamu na kuwa mfano mzuri.
5. Mtumwa; anaingia katika tamko hili ni mtumwa ambaye husaidiwa kujikomboa kwa mali ya zaka.
6. Wenye madeni endapo hawana cha kulipa madeni yao na wenye madeni watapewa kile cha kulipa madeni yawe madeni yao ni mengi au machache.

   Hata kama wanao uwezo wa kujitafutia chakula lakini hawezi kulipa.
7. Kutoa zaka katika jihadi; hutolewa katika jihadi kinachowatosha wapiganaji katika vita kununulia silaha na matumizi mengine ya kivita.

8. Msafiri; ni msafiri aliyekatikiwa na safari. Msafiri hupewa mali ya zaka ili ziweze kumfikisha mjini kwake anakokwenda.

Na hawa ndio ambao Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amewataja kwenye Kitabu Chake, na Akaelezea kwamba ni lazima kutekelezwa ibada hii kwa ajili yake. Wala haifai kutolewa zaka katika sehemu nyingine kwa mfano; kujenga Misikiti, kutengeneza njia, kuchimba visima na mengineyo. Kwa sababu Mwenyezi Mungu Amewataja Mwenyewe wanaostahiki na wasiokuwa wao haifai kabisa kupewa zaka.

Mwisho

Mwisho napenda kuwausia waumini popote walipo kumcha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Aliye tukuka na kushikamana na ibada ya zaka, kutoa zaka si kupata hasara bali ni faida tupu mbele ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Na Zaka ni nguzo muhimu kuitekeleza katika Uislamu bali imetajwa sana pamoja na Swala. Kwa hiyo kuitekeleza nguzo hii ni kumsafisha mtoaji kutokana na sifa ya ubakhili na madhambi. Pia ni kutakasa mali yake na kuzidisha baraka kwa kutoa zaka, kuondoa chuki na uhasidi katika nafsi za wenye kupokea zaka, bali kuleta mapenzi kati ya tajiri na maskini.

Mwisho kabisa tunamuomba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Atujaalie tuwe miongoni mwa wanaotekeleza ibada ya zaka, pia tunamuomba Ayabariki mali zetu, Atupe ujira mkubwa kwa tunachokitoa kesho akhera.

[9] MAHIMIZO KATIKA KUUNGA JAMAA

Lengo la Khutba:

1. Maana ya kuunga jamaa.
2. Fadhila za kuunga jamaa.
3. Kutahadhari kuwakata.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Shukrani zote ni za Allah (Subhaanahu wa Taala) Aliyetuuisa kumcha yeye peke yake. Na rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad aliyesema: [Hatoingia peponi anayewakata jamaa zake].

Enyi waumini! leo tutazungumzia jambo ambalo kwalo Muislamu hukunjuliwa riziki yake na kurefushiwa umri wake nalo ni kuunga jamaa. Na jamaa ya mtu ni mamake, babake, watoto wake na kila ambaye karibu naye kinasaba.

Aya na hadithi zinazozungumzia jambo hili ni nyingi hebu niwatajie baadhi. Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

قال تعالى : ﴿ فَهَلۡ عَسَيۡتُمۡ إِن تَوَلَّيۡتُمۡ أَن تُفۡسِدُواْ فِي ٱلۡأَرۡضِ وَتُقَطِّعُوٓاْ أَرۡحَامَكُمۡ ﴿٢٢﴾ ﴾ [محمد:٢٢]

{{Ndiyo yanayotarajiwa kwenu kufisidi katika ardhi na kuwakata jama zenu wakati mkipata ukubwa}}.

Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) miongoni mwa mambo aliyoyalingania mwanzo ni kumuabudu Mwenyezi Mungu na kuacha ibada za mababu, kuswali, kutoa sadaka, kujihifadhi na uchafu na kuunga jamaa. Na kuunga jamaa ni kuwafanyia wema na kutowaudhi. Pia ni katika kuwafanyia wema kuwapa nasaha, kuwapa ushauri, kuwapenda na kuwapendelea kheri, kuwafanyia uadilifu, kuwaelekeza, kuwafundisha, kuwapa haki zao za lazima na kuvumilia na kusubiri katika maudhi yao.

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu! kuunga jamaa kuna fadhila nyingi na katika fadhila hizo ni kuzidishiwa mtu umri wake na vile vile kukunjuliwa mali yake. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Anayependa kukunjuliwa riziki yake na kurefushiwa umri wake basi aunge jamaa zake]. Na kuunga jamaa kuna daraja kubwa katika Uislamu.

Enyi ndugu Waislamu! Je nyinyi mmesimama katika mipaka ya Mwenyezi Mungu? Je mmezifuata amri zake? Je makemeo yake na makatazo mmeyaepuka? Je mmewafanyia wema jamaa zenu na mnawatembelea?

Enyi mnaotaka kheri duniani na kesho akhera ungeni jamaa zenu na kaeni nao vizuri. Enyi waumini! Je munajua faida za kuwafanyia wema jamaa zenu? Jueni ya kwamba kuna khabari njema za duniani na kesho akhera kwa wenye kuunga jamaa zao. Miongoni mwa faida hizo ni:

Faida za Kuunga Jamaa

1. Kuunga jamaa ni alama kubwa za ukamilifu wa imani.
2. Kuunga jamaa ni sababu ya kukunjuliwa mtu katika riziki.
3. Kuunga jamaa ni sababu ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu.

Nasaha za watu wema juu ya Kuunga Jamaa

Wema waliotangulia wametoa wasia unaoonesha umuhimu wa kuunga jamaa. Amesema 'Umar ibn Khattwab, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: 'Jifundisheni nasaba kisha muwafanyie wema jamaa zenu. Amesema 'Atwaa ibn Abi Rabaa: 'Kutoa dirham kumpa jamaa yangu inapendeza zaidi kuliko kutoa dirhamu elfu kumpa maskini, mtu akamuuliza: Hata kama jamaa yako ni tajiri? Akasema 'Atwaa : Ndio, hata kama jamaa yangu ni tajiri'.

Vile vile amesema Said ibn Musayyab Mwenyezi Mungu amrehemu hakika aliwacha Dinari kadhaa: 'Ewe Mwenyezi Mungu hakika wewe wajua sikuyakusanya mali zangu isipokuwa kwa ajili ya kuhifadhi Dini yangu,. Hana kheri asiyekusanya mali yake kulipa deni lake na kuwafanyia wema jamaa zake".

KHUTBA YA PILI

Kutahadharishwa Kuwafanyia Ubaya Jamaa Zako

Shukrani za dhati zinamstahiki Mola wa viumbe wote Aliyetuamrisha kuunga jamaa zetu na Akatukataza kuwafanyia ubaya. Na rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad ambaye ni kiigizo chema katika kuunga jamaa zake.

Ama baada ya hayo: Enyi waumini kama ambavyo kuunga jamaa kuna ujira mkubwa. Vilevile kuwavunja jamaa kuna hasara na madhambi makubwa Napenda nikutajie baadhi ya hasara hizo:

Hasara ya Kuwafanyia Ubaya Jamaa

1. Kuwakata jamaa ni miongoni mwa sababu za mtu kutoingia peponi. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema ya kwamba: [Hatoingia peponi mtu anayewakata jamaa zake].
2. Na katika hasara za kukata jamaa ni kupata laana ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema kwenye Kitabu chake kitukufu: Ndiyo yanayotarajiwa kwenu kuleta uharibifu katika ardhi na kuwakata jamaa zenu wakati mukipata ukubwa. Hao ndio waliolaaniwa na Mwenyezi Mungu Akawatia uziwi masikio yao na akayapofua macho yao.

Na kosa kubwa kabisa ni mtu kuwakata wazazi wake wawili kisha akawakata walio karibu zaidi naye. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Je siwajulishi dhambi ambalo ni miongoni mwa madhambi makubwa kabisa? Wakasema maswahaba: Tujulishe ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Akasema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): Kumshirikisha Mwenyezi Mungu na kuwakata wazazi wawili].

3. Pia miongoni mwa hasara za kukata jamaa ni kufanyiwa haraka mtu kuadhibiwa

hapa duniani kabla kuadhibiwa kesho akhera. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Hakuna kosa ambalo Mwenyezi Mungu analiharakisha zaidi adhabu yake kwa mwenye kulifanya duniani pamoja na kuwekewa adhabu nyingine akhera kuliko kuwakata jamaa na kufanya maasia].

Enyi ndugu katika imani! Hakika jamaa wana daraja tofauti tofauti katika kuishi nao:-

1. Jamaa wenye kushikamana na Dini na jamaa aina hii hufanyiwa wema kwa kule kushikamana kwao na Dini.
2. Jamaa ambao wazushi ni katika Dini na wenye kufanya maovu. Na hawa wamegawanyika vigawanyo viwili:-
   a. Wanaotangaza bidaa na uzushi wao na maovu yao tena wanalingania kwenye uovu huo. Jamaa hao hupigwa vita kabisa kwa ajili ya kushikamana kwao na uovu. Inafaa kuwaonesha uso wa bashasha, lakini haifai kuwa nyoyo zetu haziko radhi nao moyoni kwa ule uovu wao. Ushahidi wa hilo ni kwamba Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Alimwonesha bashasha 'Uyaina ibn Hiswhiy aliyekuwa mtu muovu kabisa. Alipokuwa akibisha kwake huku akisema : Ni ndugu muovu katika jamii. Alipoingia Mtume alizungumza naye vizuri akasema: Hakika tunawaonesha uso wa bashasha watu (waovu) na huku nyoyo zetu zawalaani].
   b. Jamaa wafichao bidaa na vitendo vyao viovu, jamaa aina hii hufanyiwa muamala wa Waislamu wasiojulikana maovu yao.
3. Jamaa walio makafiri na wanafiki na jamaa aina hii wamegawanyika mara mbili:-
   a. Jamaa wanaoupiga vita Uislamu jamaa aina hii hukatwa na hauwaungwi kwa ajili ya kuogopwa shari lao.
   b. Jamaa wasiopiga vita Dini yetu ya uislamu jamaa aina hii hufanyiwa wema kwa njia zifuatazo:-
      - Kuwalingania katika Uislamu kwa njia nzuri.
      - Kuwaombea dua Mwenyezi Mungu Awaongoze katika Uislamu.
      - Kuwasaidia wanapokuwa na shida na kuwafanyia wema kuwavutia katika Uislamu.

Mwisho

Tunawahimiza Waislamu popote waliopo kushikamana na maamrisho ya Mwenyezi Mungu hasa suala zima la kuwatendea wema jamaa. Tufahamu ya kuwa Jamaa ni msingi wa jamii ya kiislamu, na jamaa ikishikamana, jamii itashikamana. Tukifanya hivyo, tutaweza kujenga umma mmoja wa kiislamu, na kuanzishwa kwa serikali ya kiislamu. Bila ya kujenga msingi wa jamaa moja, hatuwezi kufikia lengo la kurejesha Ukhalifa katika ardhi. Ni jukumu la kila Muislamu kufanya bidii kuunga jamaa yake na kujenga jamii ya kiislamu iliyoshikamana. Tunamuomba Allah atuwezeshe kurejesha umoja wa kiislamu na Atujaalie ni wenye kuwatendea wema jamaa zetu na tufaulu kuipata pepo yake.

(5) SEHEMU YA ULINGANIZI

Malengo Muhimu :

1. Kubainisha umuhimu wa ulinganizi wa Mwenyezi Mungu
2. Kubainisha njia zinazonasibiana na ulinganizi wa Allah
3. Kufahamisha mfumo wa kati na kati katika kulingania katika njia ya Allah, na yanayokwenda kinyume na mfumo huo
4. Kuweka wazi umuhimu wa elimu katika kulingania kwa Allah.

Anuani ya Khutba katika Sehemu ya Ulinganizi:-

1. Umuhimu wa Kuamrishana Mema na Kukatazana Mabaya
2. Vyombo vya Utangazaji na Athari zake katika Jamii
3. Njia za Kuzivuta Nyoyo
4. Himizo juu ya kutafuta Ilimu na kuifanyia Kazi
5. Ukati na Kati (Al- Waswatwiya) katika Qur'an na Sunnah
6. Mfumo wa Mitume katka Ulinganizi

[1] UMUHIMU WA KUAMRISHANA MEMA NA KUKATAZANA MABAYA

Lengo la Khutba:

1. Maana ya kuamrishana mema na kukataza mabaya.
2. Tahadhari na tabia za kigeni.
3. Kubainisha daraja ya uzuiaji wa kukataza makosa.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Waja wameumbwa kwa ajili ya ibada, lakini iblisi amewaghuri waja wa Mwenyezi Mungu kwa kutofanya ibada (Swala, Swaum na zenginezo). Dini ya Mwenyezi Mungu ni kufanya maamrisho ya Mwenyezi Mungu, na mwenye kuacha haki za Mwenyezi Mungu basi atakuwa muovu kuliko mwenye kufanya maasi.

Tumewaachia mujtamaa watu waovu, na sisi tumekaa tukitoa aibu zama zetu lakini aibu ziko kwetu. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَلْتَكُن مِّنكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ ۚ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٤﴾﴾
[آل عمران:١٠٤]

{{Na wawepo katika nyinyi watu wanaolingania kheri, na wanaoamrisha mema na wakakataza maovu. Na hao ndio walio faulu}}.

Na Akasema tena Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ ۗ﴾ [آل عمران:١١٠]

{{Nyinyi ndio umma bora kuliko umma zote zilizodhihirishwa watu, mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza yaliyo maovu na mnamwamini Mwenyezi Mungu}} Amesema Ibn Qayyim: ‘Dini gani na kheri gani kwa mwenye kuona maasi yanafanywa, na mipaka ya Mwenyezi Mungu yanakiukwa na dini yake Mwenyezi Mungu na Sunna zake Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) zinaachwa, na moyo wake kuwa baridi na akinyamaza huyo ni shetani kiziwi, kama mwenye kuzungumza baatil huyu ni shetani anayezungumza na balaa ya dini hii ni kwa wale wanaopewa madaraka na kutojali jambo la dini’.

Ndugu yangu Muislamu una majukumu ya maovu yoyote yale na uweke mikakati ya kutengeneza jamii. Asili ya kuamrisha mema na kukataza maovu ni kwa uharaka, na umuhimu wa kuamrisha mema na kukataza maovu ni kuhifadhika umma kuangamia, na kumakinika katika ardhi hii, amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿الَّذِينَ إِن مَّكَّنَّاهُمْ فِي الْأَرْضِ أَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ وَأَمَرُوا بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا عَنِ الْمُنكَرِ ۗ﴾
[الحج:٤١]

{{Wale ambao tukiwamakinisha katika ardhi husimamisha sala na wakatoa zaka na wakaamrisha yaliyo mema na wakakataza yaliyo mabaya}}.

Na mwisho mbaya ni pale wanafunzi wa dini na mabarobaro wanapo jishughulisha na mambo mengine na kuwacha kutengeneza jamii, na kutoamrisha mema na kukataza maovu. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Mtaamrisha mema au mtakataza maovu, au nahofia itawateremkia adhabu, mumuombe Mwenyezi Mungu na asiwakubalie dua zenu]. Imepokewa na Zainab akisema “Je tutaangamia na kuwa watu wema? Akasema ndio ukizidi uchafu”.

Na Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿لُعِنَ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ مِنۢ بَنِيٓ إِسۡرَٰٓءِيلَ عَلَىٰ لِسَانِ دَاوُۥدَ وَعِيسَى ٱبۡنِ مَرۡيَمَۚ ذَٰلِكَ بِمَا عَصَواْ وَّكَانُواْ يَعۡتَدُونَ ٧٨ كَانُواْ لَا يَتَنَاهَوۡنَ عَن مُّنكَرٖ فَعَلُوهُۚ لَبِئۡسَ مَا كَانُواْ يَفۡعَلُونَ ٧٩﴾

[المائدة:٧٨:٧٩]

{{Walilaaniwa wale waliokufuru miongoni mwa wana wa Israil kwa ulimi wa Dawud na wa ‘Isa bin Maryam. Hayo ni kwa sababu waliasi na wakapindukia mipaka. Hawakuwa wenye kuzuiana mabaya waliyokuwa wakiyafanya. Uovo ulioje wa jambo hili waliokuwa wakilifanya}}.

Uovu ambao unapaswa kuzuiwa ni:

1. Uwe umekatazwa kisheria.
2. Uwe unafanyika sasa.
3. Uwe dhahiri uovu huo.
4. Usiwe uovu ni katika masuala ambayo wamehitilafiana wanazuoni.

Amesema Sheikh Ghazal, anayefanya maasi adhabu yake kuna aina tatu:-

- Kuwa nzito na ngumu, hii inakuwa kwa anayefanya makosa ya hudud na taaziri, hii ni kwa wenye majukumu.
- Kuwe maasi hayo inawezekana kufanyika kama kuvaa hariri kuzuia maasi hayo ni wajibu.
- Uwe uovu huo unawezekana kufanyika kama yule anayefurahika kufagia sehemu ya tembo, mtu kama huyu anafaa kupewa mawaidha, ama kupigwa haifai isipokuwa akijua sehemu siku zote ni ya kunywa tembo.

Kuweka wazi masharti manne yaliyotangulia:

1. Uwe ni uovu (munkar) mfano ukimuona mtoto mdogo au mwendawazimu anakunywa tembo inapaswa kuimwaga tembo (pombe) hilo na kumzuia, vile vile ukimuona mwendawazimu anazini na mwendawazimu mwenzake inapaswa kumzuia.
2. Uwe uovu huo unafanyika, kwa sasa pia kula atakayejua kwa makadirio kuwa uovu utafanyika, au mwenye kuazimia kunywa tembo (pombe) usiku, kwa huyu mtu wa mwisho inapaswa kupewa mawaidha.

3. Uwe uovu huo uko wazi bila ya kuchunguza, kwa hiyo kila atakayefanya maasi kwa kujificha na kufunga mlango wake haifai kumchunguza, kisa cha ‘Umar bin Khattab aliporuka ukuta wa mtu mmoja na kumuona katika hali ya kuchukiza akamkataza ‘Umar. Yule bwana alimuambia ‘Umar kuwa yeye amemuasi Mwenyezi Mungu kwa njia tatu:- kuchunguza, kuingia kwenye nyumba pasipo na mlango wake na kuruka ukuta, ‘Umar akamuacha na akamshurutisha kutubia kwa Mwenyezi Mungu. Kwa ajili hiyo haifai kuingia katika nyumba mpaka idhihirike kama kusikia sauti au herufu ya tembo (pombe), hapo ndipo unaruhusiwa kuingia na kuzuia munkar. Na kudhihirika kwa kitu ima ni kwa kusikia, kuniusa, kuona, kushika.
4. Uwe unajulikana munkar huo bila ya kujitahidi kuwa inafaa au haifai. Haifai kwa Hanafy kuwakataza Shafy Bismillah wala haifai Shafy kuwazuia Hanafy kwa kunywa (wabidh) aina ya tembo, kutokana na kuhitalifiana wanazuoni kwa masuala yaliyo magumu, wamesema baadhi ya wanazuoni haifai kuzuia uovu ila kwa mambo yaliyo haramu.

KHUTBA YA PILI

Amepokea Abi Said Khudhriy hadithi kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema: [Mwenye kuona uovu basi auzuie kwa mkono wake, na asipoweza basi atumie ulimi wake, na asipoweza atumie moyo wake, na huo ni udhaifu wa iman].

Daraja za kuzuia Uovu:-

1. Mwanzo kutumia mkono,
2. Kutumia ulimi
3. Kuchukia, na kama uko hapo inapaswa uondoke.

Adabu za kuzuia Uovu:-

1. Kujua uovu,
2. Kusubiri,
3. Kuwa na ikhlas,
4. Kuwa mpole,
5. Kuwa kiigizo chema.

Mwisho

Ndugu Waislamu, kwa hakika jamii haiwezi kusimama juu ya msimamo wa dini mpaka nguzo hii ya kuamrisha mema na kukataza maovu isimamishwe. Leo tunashuhudia katika jamii yetu ya kiislamu maadili na akhalaqi mbaya kwa sababu ya kukosekana nguzo ya kuamrisha mema na kukataza maovu. Ndugu katika imani, ni jukumu la kila Muislamu kubeba hamu ya nguzo hii muhimu kuanzia kwake nyumbani hadi kwa jamii yote.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu asituteremshie laana kama alivyo wateremshia wana wa Israel. Ewe Mwenyezi Mungu usituadhibu kwa makosa wanaofanya wengine. Ewe Mwenyezi Mungu tubariki na utusamehe madhambi yetu.

[2] VYOMBO VYA UTANGAZAJI NA ATHARI ZAKE KATIKA JAMII

Lengo la Khutba:

1. Watu kufanyia umuhimu vyombo vya utangazaji.
2. Kuhusisha vyombo vya utangazaji kutumikia Dini.
3. Matatizo yanayokabili vyombo vya utangazaji wa habari

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote na rehma na amani zmfikie Mtume Muhammad. Napenda kuitanguliza mada hii ya vyombo vya utangazaji, kuwatajia umuhimu wake. Na pia nitawabainishia vipi vyombo vya utangazaji vinaweza kuitumikia Dini na matatizo yanayo vikabili vyombo hivyo.

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Ametupa neema ya ulimi ili tumshukuru kwa neema hiyo kwa kuitumia vilivyo kwa mujibu wa mafunzo mema ya kiislamu. Ametuamrisha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) kuutumia ulimi vizuri tunapozungumza.

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَقُولُواْ قَوْلًا سَدِيدًا ﴿٧٠﴾﴾ [الأحزاب:٧٠]

{{Enyi mulioamini, Mcheni Mwenyezi Mungu na mseme maneno ya sawa}}. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) asema: [Aliyemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, basi aseme maneno mazuri au anyamaze].

Na Ametilia nguvu mshairi akisema: 'Zungumza vizuri uwezavyo kwani maneno yako ni yako na kunyamaza ni vizuri na ikiwa hutapata maneno mazuri ya kuzungumza basi kunyamaza bila ya kufanya vizuri ni vizuri'. Asema mshairi mwengine: 'Kuzungumza ni vizuri na kunyamaza ni usalama basi unapozungumza usiwe na maneno mengi kwani sijajuta kwa kunyamaza hata mara moja lakini nimejuta juu ya maneno yangu mara nyingi'.

Kwa mujibu wa Aya na hadithi na mashairi tuliyoyataja inaonesha wazi kuwa Muislamu hafai kabisa kuutumia ulimi wake kinyume na maagizo ya Allah (Subhaanahu wa Taala), huku tukijua ya kwamba kila siku watu wanawasilina kupitia njia tofauti tofauti kama kutumia simu, barua, na vyombo vingine vya mawasiliano, bali wengine kupitia vyombo vya utangazaji. Na kwa kweli watu wamevielekea mno vyombo hivyo ili kupata habari mbali mbali.

Kwa kweli vyombo vya utangazaji vina faida zake na hasara zake. Kwa hivyo hatusemi kwamba haifai kutumia vyombo hivyo, lakini isiyofaa ni kuvitumia katika njia mbaya isiyokubalika kiislamu. Kwani makafiri wakiwemo Waamerika na Wamagharibi wame vitumia vyombo hivi katika kuwapotosha wanaadamu

na njia ya sawa, vikiwemo vyombo vya kusikiliza kama redio na vyombo vya kuonesha kama runinga na vya kusoma kama magazeti, majarida na vyenginevvyo.

Kwa kweli vyombo vya utangazaji vimechukua nafasi kubwa kabisa katika kuwaathiri na kuwapotosha watu kimaadili. Sasa wajibu wetu ni mambo gani ya upotofu yanayoenezwa na makafiri katika vyombo vya utangazaji?. Bila shaka wajibu wetu ni kuwatahadharisha watu na uovu unaoenezwa na vyombo hivyo, kwa kuwalingania katika Uislamu na kuacha upotofu. Napenda kuchukua fursa hii kuwauliza maswali yafuatayo:-

1. Ulinganizi ni nini ndugu zangu katika imani?
2. Ni upi umuhimu na ubora wa ulinganizi?
3. Ni lipi lengo na hukumu ya ulinganizi?
4. Ni ipi misingi ya ulinganizi ?
5. Ni zipi nguzo za ulinganizi?
6. Ni zipi njia na aina za ulinganizi?

Umuhimu wa Ulinganizi

- Ulinganizi ni kuwaita watu na kuwafundisha uislamu na kuutekeleza kimatendo kwa ajili ya kuwatakia kheri katika maisha yao hapa duniani na kesho akhera.
- Umuhimu wa kulingania watu ni kwamba mlinganizi ana daraja kubwa sana mbele ya Mwenyezi Mungu kwa sababu anawaita watu kuwacha ibada zote mbaya na kushikamana na ibada ya Mwenyezi Mungu peke yake. Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): " Na hakuna mwenye maneno mazuri kuliko yule anayewalingania watu kwa Mwenyezi Mungu na akafanya vitendo vizuri na akasema Mimi ni katika Waislamu".
- Umuhimu wa ulinganizi ni kwamba anapata anayelingania ujira mkubwa. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema. [Anayelingania katika uongofu atapata ujira sawa na atakayeufuata uongofu huo na hatapunguziwa katika ujira wake kitu chcchote].
- Umuhimu wa kulingania vile vile ni kutii na kutekeleza amri ya Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) aliposema: [Nifikishieni hata kama ni Aya moja]. Kulingania hupatikana ndani yake ukamilifu wa kumfuata Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) katika ulinganizi wake wa busara. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Aasema:

قال تعالى : ﴿ قُلْ هَٰذِهِۦ سَبِيلِىٓ أَدْعُوٓا۟ إِلَى ٱللَّهِ ۚ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا۠ وَمَنِ ٱتَّبَعَنِى ۖ وَسُبْحَٰنَ ٱللَّهِ وَمَآ أَنَا۠ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ﴿١٠٨﴾ ﴾

[يوسف:١٠٨]

{{Sema hii ndio njia yangu nalingania kwa Mwenyezi Mungu kwa elimu na busara mimi na wanaonifuata na ametakasika Mwenyezi Mungu na sikuwa ni miongoni mwa washirikina}}.

- Wametofautiana wanavyuoni katika hukumu ya ulinganizi, je ni lazima kwa kila mtu au wakifanya baadhi huwatosheleza wengine?. Wanavyuoni wengine

wamesema kwamba ni lazima kwa kila Muislamu na wengine wamesema kwamba wakifanya baadhi ya Waislamu huwatosheleza waliobakia. Lakini ilivyo ni kwamba ulinganizi ni lazima kwa kila Muislamu kulingana na uwezo wake. Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ ﴾ [آل عمران:١١٠]

{Mumekuwa umma bora mliochaguliwa kwa watu munaolingania katika kheri munaamrisha mema na munakataza mabaya}}. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Atakayeona jambo baya katika nyinyi basi aliondoshe kwa mkono wake na ikwa hawezi basi aliondoshe kwa ulimi wake (kwa kusema) na ikiwa hawezi basi achukie kwa moyo wake].

Nachukua tena fursa hii kuitaja misingi inayotegemewa katika kulingania, nayo ni:

1. Qur'an Tukufu,
2. Hadithi
3. Sira ya Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) na
4. Historia ya makhalifa wema waongofu. Misingi tuliyoitaja ndiyo ambayo anayelingania huitumia kuwaita watu katika kheri.

Nguzo za Ulinganizi

Nisikilizeni kwa makini niwatajie nguzo ambazo ni lazima zipatikane ndio upatikane ulinganizi na nguzo hizo ni kama zifuatazo:

1. Mlinganizi
2. Anayelinganiwa
3. Kinacholinganiwa
4. Njia na aina za ulinganizi.

- Yatakiwa mlinganizi asifike na apambike na sifa njema alizokuwa nazo Mtume rehma amani zimfikie sifa hizo ni ukweli, uaminifu, kumtakasia Mwenyezi Mungu ulinganizi, ushujaa, upole, maneno mazuri, subira, uadilifu, na sifa nyingine nzuri.
- Wanaolinganiwa ni aina tofauti za watu. Kuna Waislamu, wanafiki, makafiri, viongozi, raia, wakubwa na wadogo. Na kila mmoja katika hawa kuna njia na namna yake ya kumlingania.
- Kinacholinganiwa ni Uislamu na hii kazi ya Mitume wote. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ ﴾ [النحل:٣٦]

{{Hakika tuliwatumiliza katika kila umma Mtume kuwalingania watu kwamba muabuduni Mwenyezi Mungu mujiepushe na sheitani}}.

- Njia za ulinganizi ni nyingi. Miongoni mwa njia hizo kuwasiliana na mtu moja kwa moja, kutoa khutba, kuandika vitabu, kufundisha madrasa au vyuo vikuu, kuandika makala gazetini, kutumia vyombo vya utangazaji kufikisha ujumbe kama redio, runinga na vyinginevyo. Kwa hivyo inatakiwa tuwe makini na ufisadi unaopatikana katika vyombo vya habari inatakiwa tuwatahadharishe Waislamu popote waliopo na uovu unaoenezwa na vyombo hivi.
- Miongoni mwa aina na sampuli za ulinganizi ni kuwa mfano mzuri wa katika jamii, kujadiliana kwa lengo la kuelimishana, kutumia hikma, pia kutumia mawaidha mazuri, kutumia mifano kwa kutoa visa, na kutumia vitisho na kutia moyo katika mawaidha. Na inatakiwa mlinganizi achague aina ya ulinganizi ambao anaona itakuwa wepesi kukubaliwa ulinganizi wake.

Kwa kweli kusisitiza na kufanya mambo kwa uhakika bila ya kubahatisha na kufuatilia mambo kwa makini ni jambo la kupongezwa sana. Bila ya kusahau kwamba inatakiwa tuwe wakweli na waaminifu katika kukusanya habari na kuwaelezea watu, ili kuhakikisha kuwa na habari ya ukweli**.** Amesema Mola Wetu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى: ﴿وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِۦ عِلْمٌ ۚ إِنَّ ٱلسَّمْعَ وَٱلْبَصَرَ وَٱلْفُؤَادَ كُلُّ أُو۟لَٰٓئِكَ كَانَ عَنْهُ مَسْـُٔولًا ﴿٣٦﴾﴾ [الإسراء:٣٦]

{{Na usiingilie jambo usilokuwa na ujuzi nalo. Hakika macho, masikio na moyo, vyote hivyo utaulizwa kuhusiana navyo}}.

Pia Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَإِذَا قُلْتُمْ فَٱعْدِلُوا۟﴾ [الأنعام:١٥٢]

{{Na mutakapozungumza fanyeni uadilifu}}.

Pia Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala):

وقوله تعالى : ﴿ وَقُل لِّعِبَادِى يَقُولُوا۟ ٱلَّتِى هِىَ أَحْسَنُ ۚ﴾ [الإسراء:٥٣]

{{Na sema kuwaambia waja wangu waseme maneno yaliyokuwa mazuri}}.

Misingi ya vyombo vya Utangazaji

Uislamu umeweka misingi kuvifanya vyombo vya utangazaji kuwa imara.

1. Msingi wa kwanza na muhimu kabisa katika maisha ya watu ni kumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake**.** Amesema Mwenyezi (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ فَٱعْلَمْ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ ﴾ [محمد:١٩]

{{Jua kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye}}. Mwingine ni kuhisi majukumu wa kuwalingania watu katika njia ya kheri, kuwa mkweli katika maneno na matendo, pia kuwa muadilifu na kuzingatia adabu za mjadala wakati anapojadiliana na kupeana mawaidha mazuri. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ ٱدْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِٱلْحِكْمَةِ وَٱلْمَوْعِظَةِ ٱلْحَسَنَةِ ۖ﴾ [النحل:١٢٥]

{{Walinganie watu katika njia ya Mola wako kwa hikima na mawaidha mazuri}}.

KHUTBA YA PILI

Matatizo yanayovikumba Vyombo vya Utangazaji

Shukrani zote za dhati ni za Allah (Subhaanahu wa Taala) Mola wa viumbe vyote, huku nikimtakia rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad.

Enyi Waumini! Ni vyema tujue ya kwamba matatizo ambayo yanavikabili vyombo vya utangazaji kiasi kwamba ilipelekea kukosekana habari za uadilifu na kupatikana habari potofu na za ufisadi ambazo hupotosha watu. Na miongoni mwa matatizo hayo ni:-

1. Kutoeneza vyombo hivyo habari za ukweli mpaka ikapelekea kutokubalika chombo hicho na kudharauliwa na watu na pengine kuzusha fujo baina ya watu na wasimamizi wa chombo hicho.
2. Kutosaidiwa kimali vyombo vya utangazaji ili kutangaza na kueneza habari kwa nzuri na nyepesi na pia kuzidi kuelimisha watu katika njia nzuri.
3. Katika matatizo yanayovikumba vyombo vya utangazaji na utangazaji ni ujinga na kufuauta matamanio ya nafsi, kwa kutoa habari bila ya ujuzi na bila kuhakikisha habari ile sawa sawa iwe inamhusu mtu au kikundi. Hii inaweza kuleta fujo pale atakapotoa habari bila ya elimu wala ushahidi.

   Katika mifano ya matukio tuliyoyataja ni pale makafiri walipo toa makala ya kumtusi na kumkejeli Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). Pia kueneza habari za uongo kuhusu Waislamu kuwa ni magaidi, kiasi kwamba inaleta tashwishi na chuki baina ya Waislamu na makafiri.
4. Katika matatizo ni kutodhaminiwa vyema magazeti na majarida ili kueneza faida katika jamii.

Michezo ya kuigiza katika vyombo vya utangazaji ina mafunzo kuhusu mambo yanayojiri maishani mwa watu. Mchungaji na mchezaji michezo hii lengo lao kubwa ni kuwafikishia ujumbe watu aidha kwa kuwahimiza kufanya jambo fulani au kujiepusha na jambo uvu fulani. Hii ni miongoni mwa faida zinazokusudiwa katika michezo hii. Kwa upande mwengine, kuna madhara ya michezo hii kama mtu kusema uongo, kujifananisha na mwanamke au mwanamume, yeye muigizaji kwenda kinyume na mafunzo anayoyatoa. Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala):

قوله تعالى : ﴿وَمَآ أُرِيدُ أَنْ أُخَالِفَكُمْ إِلَىٰ مَآ أَنْهَىٰكُمْ عَنْهُ ۚ إِنْ أُرِيدُ إِلَّا ٱلْإِصْلَٰحَ مَا ٱسْتَطَعْتُ ۚ﴾ [هود:٨٨]

{{Sitaki kuwakhalifu katika yale ninayowakataza sitaki isipokuwa kutengeneza niwezavyo}}.

Yanayoilazimu serikali na watu kwa jumla ni kusimama kidete kutoa nasaha kuwapatia wahusika wa vyombo hivi wamche Mwenyezi Mungu katika suala zima la uenezaji habari. Dini ni kupeana nasaha kwa kuamrishana mema na kukatazana mabaya ili vyombo hivi viwe vitafaidisha umma na vitatoa habari za kweli. Kwa hivyo inatakiwa Waislamu wakubwa kwa wadogo washikamane na ibada hii ya kupeana nasaha ili tufaulu duniani na kesho akhera.Tuna imani ya

kwamba endapo wahusika wa vyombo vya utangazaji watashikamana na maadili mema ya kiislamu, watu watafaidika sana.

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ ٱلَّذِينَ إِن مَّكَّنَّٰهُمْ فِى ٱلْأَرْضِ أَقَامُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَوُا۟ ٱلزَّكَوٰةَ وَأَمَرُوا۟ بِٱلْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا۟ عَنِ ٱلْمُنكَرِ ۗ ﴾

[الحج:٤١]

{{Wale ambao tukiwamakinisha katika hii ardhi wanasimamisha Swala na kutoa zaka na wakaamrishana mema na kukatazana mabaya}}.

Mwisho

Tumetaja japo kwa ufupi nukta zinazofungamana na vyombo vya utangazaji. Vile vile tumetaja umuhimu wa vyombo vya utangazaji katika jamii na vipi vinaweza kutumikia katika kutumikia Dini yetu ya Kiislamu pia tukagusia matatizo yanayokumba vyombo vya utangazaji.

Mwisho tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie ni miongoni mwa wenye kusikia yaliyo mazuri na tukawa ni wenye kuyafuata, tunamuomba Atuoneshe haki tuwe ni wenye kuifuata na atuoneshe batili tuwe ni wenye kuiepuka.

[3] NJIA ZA KUZIVUTA NYOYO

Lengo la Khutba:

1. Kuzifungamanisha nyoyo kwa Allah.-
2. Kuhakikisha maana ya udugu kwa ajili ya Allah.
3. Kufikisha ulinganizi kwa watu wote na kusubiri udhia wao.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote, na rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad. Moyo ni kiungo muhimu katika mwili wa mwanadamu. Moyo ukiwa mzuri, mwili utakuwa mzuri. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Katika mwili wa mwanadamu kuna kipande cha nyama, kikiwa kizuri, basi mwili wote unakuwa mzuri. Na kikiwa kibaya mwili wote unakuwa mbaya. Jueni ni moyo].

Kinyume na hayo, ni moyo kuwa nasifa ya ngumu, na kusababisha kupinga na kukata haki.

Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿فَأَمَّا ٱلۡإِنسَٰنُ إِذَا مَا ٱبۡتَلَىٰهُ رَبُّهُۥ فَأَكۡرَمَهُۥ وَنَعَّمَهُۥ فَيَقُولُ رَبِّيٓ أَكۡرَمَنِ ١٥﴾ [الفجر:١٥]

{{Hakika, ama mwanaadamu Mola wake atakapofanyia mtihani akamtukuza kwakumneemesha,basi atasema: Mola wangu amenitukuza}}.

Na neno lake Allah (Subhaanahu wa Taala):

قوله تعالى : ﴿وَلَئِنۡ أَذَقۡنَا ٱلۡإِنسَٰنَ مِنَّا رَحۡمَةٗ ثُمَّ نَزَعۡنَٰهَا مِنۡهُ إِنَّهُۥ لَيَـُٔوسٞ كَفُورٞ ٩ وَلَئِنۡ أَذَقۡنَٰهُ نَعۡمَآءَ بَعۡدَ ضَرَّآءَ مَسَّتۡهُ لَيَقُولَنَّ ذَهَبَ ٱلسَّيِّـَٔاتُ عَنِّيٓۚ إِنَّهُۥ لَفَرِحٞ فَخُورٌ ١٠ إِلَّا ٱلَّذِينَ صَبَرُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ أُوْلَٰٓئِكَ لَهُم مَّغۡفِرَةٞ وَأَجۡرٞ كَبِيرٞ ١١﴾ [هود:٩-١١]

{{Na Wallahi tutakapomneesha mwanaadamu kwa neema yoyote kisha tukamwondoshea hapana shaka Yeye ni mwingi wa kukata tamaa, mwenye kukanusha. Na Wallahi tutakapomneemesha baada ya kupata madhara Wallahi, atasema; imeniondokea mimi shida hapana shaka yeye ni mwingi wa furaha,mwenye kujivuna. Ila walio subiri na wakafanya amali nzuri, hao wanamsamaha wa madhambi yao na malipo makubwa}}.

Katika maudhui yetu ya leo tutazungumzia kuhusu namna gani nyoyo zinavutiwa kwa kufanyiwa mambo ya kheri na kupendelea zaidi kufika katika machumo ya kufaulu kwa haraka.

Hima ya Uislamu katika Njia za Kuzifikia Nyoyo zote na Kuziunganisha

Neno la bibi khadija katika kusifu kwake tabia za bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) : ‘Hakika wewe unaunga jamaa Na udugu alioufungumanisha bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) kwa baadhi ya maswahaba zake.

Na linashuhuduliwa vile vile kwa hadithi ya Jabir Ibn ‘Abdallah aliposema: “Tulikuwa katika jeshi wakagombana mtu katika muhajirina na mtu katika ansar, akasema huyu katika ansar «Enyi Maansar na akasema katika muhajirina «Enyi Muhajirina». Akalisikia jambo hilo Bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akasema : [Bado hamujaacha mambo ya ujinga? Wakasema maswahaba wamekosana mtu katika Muhajirina na mtu katika Ansar Mtume Akasema uacheni (ujamaa na ukabila) hakika ni uvundo akasikia maneno haya ‘Abdallah ibn Ubayya akasema wamefanya hivyo, basi Wallahi tukirejea Madina atamtoa mwenye nguvu yule mnyonge. Maneno hayo yakamfikia Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam)].

Umar akasema: “Ewe Mtume wa Allah niache nikate shingo yake huyu mnafiki, akasema Mtume muache wasije watu wakasema ya kuwa Muhammad anawauwa maswahaba wake na walikuwa maansar ni wengi kuliko Muhajirina. Walipo kwenda Madina kisha Muhajirina wakawa wengi baadaye.» Ameitoa hadithi hiyo Bukhari na Muslim. Na anasema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Enyi watu hakika miongoni mwenu mnakimbiza (fukuza watu) watu].

Kufungamanisha Nyenzo na Njia kwa Itikadi (Aqida) na Tabia.

Kupatikana kisa cha watu wa pango (as›habul kahfi) na kisa cha mtu aliyekuja kutoka mbali mpaka kwa Nabii Musa. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قوله تعالى : ﴿وَجَآءَ رَجُلٌ مِّنْ أَقْصَا ٱلْمَدِينَةِ يَسْعَىٰ قَالَ يَٰمُوسَىٰٓ إِنَّ ٱلْمَلَأَ يَأْتَمِرُونَ بِكَ لِيَقْتُلُوكَ فَٱخْرُجْ إِنِّى لَكَ مِنَ ٱلنَّٰصِحِينَ ﴿٢٠﴾ فَخَرَجَ مِنْهَا خَآئِفًا يَتَرَقَّبُ قَالَ رَبِّ نَجِّنِى مِنَ ٱلْقَوْمِ ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿٢١﴾﴾ [القصص:٢٠:٢١]

{{Na alikuja mwanamume kutoka (sehemu) ya mwisho wa mji akiwakimbia alisema: Ewe Musa, hapana shaka wakuu walifanya mpango ili wakuuwe. Basi utoke mji hapana shaka mimi kwako ni miongoni mwa wenye kukunasihi. Basi aliutoka mji ilhali ni mwenye khofu yuangalia (ni jambo gani litazuka). Alisema Ewe Mola wangu, niokoe na watu walio makafiri}}. Yote hayo ni kwa ajili ya kulinda mapenzi.

Sifa za Kimsingi

Ukweli wa kumuelekea Allah (Subhaanahu wa Taala) na kutafuta ilimu kwa njia ya Bwana Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) na wema waliotangulia katika kuzivuta nyoyo. Yenye kutoa ushahidi wa hayo ni neno lake Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالى: ﴿فَبِمَا ۖ وَلَوْ كُنتَ فَظًّا غَلِيظَ ٱلْقَلْبِ لَٱنفَضُّوا۟ مِنْ حَوْلِكَ ۖ﴾ [آل عمران:١٥٩]

{{Na lau ungelikuwa ni mkali, mgumu wa moyo basi wangelikukimbia walio pembeni (karibu) nawe}}.

Katika Aya nyingine Allah Alimuambia Mtume awasamehe na awaombee msamaha na awashauri katika mambo yote.

Baadhi za Njia za kuvutia Nyoyo:

1. Uso wa tabasamu.
2. Kupeana mikono.
3. Kusikiliza matatizo ya watu kwa uzuri
4. Kutoa nasaha nzuri.
5. Kutangamana na watu.
6. Kupenda kuwafikishia watu manufaa.
7. Kuwashajiisha na kuwasubiria watu mazito (wasiochukulika).
8. Kuwaondolea watu matatizo.
9. Kuinamisha macho.
10. Kujiepusha katika lisilowezekana.
11. Kufungamanisha hali ya matukio ya sasa na visa vya kweli katika Qur’an na Sunnah na habari za leo.
12. Kumshukuru na kutambua wenye kufanya mazuri (watendaji kheri).

Na ushahidi ya hayo, ni neno lake Allah (Subhaanahu wa Taala):

قوله تعالى: ﴿وَٱلۡكَٰظِمِينَ ٱلۡغَيۡظَ وَٱلۡعَافِينَ عَنِ ٱلنَّاسِۗ وَٱللَّهُ يُحِبُّ ٱلۡمُحۡسِنِينَ ١٣٤﴾ [آل عمران:١٣٤].

{{Na wenye kuzizuia hasira zao, wenye kusamehe watu na Mwenyezi Mungu huwapenda wenye kufanya mema}}.

Na inashuhudia hadithi ambayo imetaja haki za Muislamu, na msaada wa Allah kwa mja atakapokuwa ni mwenye kumsaidia ndugu yake. Ibn ‘Umar amepokea kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) ya kwamba Amesema: [Muumini mwenye kutangamana na watu na anayesubiri maudhi yao ni bora kuliko muumini ambaye hatangamani na watu wala hasubiri maudhi yao].

Na imepokewa na Nuuman Ibn Bashiir amesema: Nimemsikia Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema: [Mfano wa muumini katika mapenzi na huruma ni kama mfano wa kiwiliwili kimoja kitakapougua kiungo kimoja katika mwili vinashikwa na homa viungo vingine].

KHUTBA YA PILI

Miongoni mwa njia ya kufungamanisha nyoyo ni kutekeleza haki za watu alizozitaja Bwana Mtume rehma na amani zimfikie katika hadithi, kutoa salamu, na kuwa na maneno mazuri na kulisha chakula, na kuitikia ualishi, na kusindikiza jeneza na kuliswalia na kuinamisha macho.

Imepokewa riwaya nyingine ya sifa hizo amepokea Abu Huraira kwamba Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) Amesema: [Haki za Muislamu juu ya Muislamu mwenzake ni sita. Akaulizwa ni zipi (hizo haki) Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: ukikutana naye msalimie na akikualiaka itikia uwalishi wake na akichemua na kumshukuru Allah basi muombee rehma na akiwa

mgonjwa mtembelee na akifa sindikiza jeneza lake].

Kuzijumuisha nyoyo na amali ya kufanya jamii na kufanya peke yako hiyo ndio makusudio..Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَتَعَاوَنُوا۟ عَلَى ٱلْبِرِّ وَٱلتَّقْوَىٰ ۖ وَلَا تَعَاوَنُوا۟ عَلَى ٱلْإِثْمِ وَٱلْعُدْوَٰنِ ۚ﴾ [المائدة:٢]

{{Na saidianeni kwa kufanya mema na kumcha Allah na wala msisaidiane katika madhambi na uadui}}.

Na neno lake Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿لَوْ أَنفَقْتَ مَا فِى ٱلْأَرْضِ جَمِيعًا مَّآ أَلَّفْتَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ وَلَٰكِنَّ ٱللَّهَ أَلَّفَ بَيْنَهُمْ ۚ﴾ [الأنفال:٦٣]

{{Lau ungetumia yaliyomo ardhini yote hungeweza kuunganisha nyoyo zao lakini Allah aliunganisha baina yao}}.

Mwisho

Ndugu Muislamu, kama tulivyo sikia katika khutbah, ni wajibu kwa walinganizi wa kiislamu kujipamba na sifa za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) katika kuwaita watu kufuata Dini ya Allah (Subhaanahu wa Taala). Tukitaka Da’wah yetu ifaulu na kufikia lengo la Da’wah, basi ni lazima Waislamu wote kusoma Sira (Maisha) ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) na Mwasahaba. Kufanya hivyo, tutaweza kubadilisha ulimwengu mzima kama alivyo badilisha ulimwengu Mtume na Masahaba kwa kipindi kifupi.

Tunamuomba Allah Atupe uwezo wa kufahamu Sira ya Mtume na kuweza kuigiza katika maisha kwa jumla na katika Da’wah khaswa. Allah awanusuru Walinganizi wote katika njia yake.

[4] HIMIZO JUU YA KUTAFUTA ILIMU NA KUIFANYIA KAZI

Lengo La Khutbah:

1. Kuhimiza kutafuta ilimu yenye manufaa
2. Kukumbusha Adaabu ya kutafuta ilimu
3. Kutoa wito wa kutengeneza mtaala wa ilimu

KHUTBAH YA KWANZA

Utangulizi

Ilimu ni msingi muhimu katika dini ya Kiislamu. Dini ya Kiislamu imejengwa juu ya Ilimu. Kwasababu Ilimu ndio mwangaza wa kuonyesha njia ya sawa na kuonyesha njia ya mbaya. Aya za kwanza alizo teremshiwa Mtume Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) zilikuwa ni za kufundisha ilimu, na kuhimiza Waislamu wafanye bidii kutafuta ilimu. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ٱقۡرَأۡ بِٱسۡمِ رَبِّكَ ٱلَّذِي خَلَقَ ١ خَلَقَ ٱلۡإِنسَٰنَ مِنۡ عَلَقٍ ٢ ٱقۡرَأۡ وَرَبُّكَ ٱلۡأَكۡرَمُ ٣ ٱلَّذِي عَلَّمَ بِٱلۡقَلَمِ ٤ عَلَّمَ ٱلۡإِنسَٰنَ مَا لَمۡ يَعۡلَمۡ ٥﴾ [العلق:١:٥]

{{Soma, na Mola wako ni Karimu sana. Ambae Amemfundisha binadamu ilimu zote hizi kwa msaada wa kalamu. Amemfundisha mwanadamu mambo yaliyokuwa hayajui}}.

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Ametumia katika Aya hizo maneno kama; soma, ilimu, kalamu, kufundisha, yote haya ni kuonyesha umuhimu wa kutafuta ilimu kwa kupitia njia tofauti za kuweza kukufikisha wewe kupata ilimu hio. Katika Aya hizo kuna ishara ya kuonyesha kwanza kabla ya kufanya vitendo vingine ni lazima mwanadamu apate ilimu ili aweze kutekeleza vitendo vyake kwa ujuzi zaidi na maarifa ya kutosha kinyume na mafundisho hayo, basi mwanadamu atafanya mambo kwa ujinga na baada ya kupata faida na mambo hayo, atapata hasara tupu ima kwa kudhuru nafsi yake au jamii kwa jumla.

Wajibu wa kutafuta Ilimu kabla ya kila kitu katika Mafundisho ya Qur’an na Sunna

Katika Qur’an Tukufu,:

1. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

قال تعالى : ﴿فَٱعۡلَمۡ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ وَٱسۡتَغۡفِرۡ لِذَنۢبِكَ﴾ [محمد:١٩]

{{Jua ya kwamba hakuna aabudiwaye kwa haki ila Mwenyezi Mungu, na omba msamaha kwa dhambi zako}}.

Amesema Imam Bukhari katika kitabu chake Sahihi Al-Bukhari: ‘Mlango unaozungumzia kusoma ilimu kabla ya maneno na vitendo’. Makusudio ya Imamu Bukhari ni kutafsiri Aya iliyotangulia ya kumaanisha ilimu mwanzo kabla ya vitendo. Ilimu imetangulizwa kwanza kabla ya kusema au kutenda, kwa sababu, ikiwa maneno na vitendo havikujengwa juu ya msingi wa Ilimu, maneno hayo na vitendo hivyo havina faida kwa mwenye kufanya. Khasara yake ni kubwa kuliko faida yake. Ndio Dini ya Kislamu kwanza ikatilia mkazo watu kusoma na kujuwa kabla ya kufanya vitendo.

2. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال تعالى : ﴿إِنَّمَا يَخْشَى ٱللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ ٱلْعُلَمَٰٓؤُاْ﴾ [فاطر:٢٨]

{{Hakika wanao muogopa Mwenyezi Mungu ni wanazuoni}}. Katika Aya nyingine Anasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال: ((وما يعقلها إلا العالمون))

{{Na hawafahamu mifano hiyo, isipokuwa wajuao}}.

Katika Sunna za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam)

a. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Kutafuta ilimu ni Faradhi juu ya kila Muislamu].

b. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) : [Mwenye kufuata njia kwa ajili ya kutafuta Ilimu. Mwenyezi Mungu atafanyia wepesi njia ya kuingia peponi]. c) Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Mwenyezi Mungu akimtakia kheri mja wake humfundisha ilimu ya dini].

Muislamu hawezi Kufahamu Qur’an na Sunna za Mtume ila kwa Ilimu. Ni lazima kwanza ajilazimishe na kusoma ili apate ujuzi wa kufahamu. Bila ya kufanya hivyo, atakuwa ni miongoni mwa waliosifiwa na sifa ya ujinga. Ndugu katika Imani, haya ndio mafundisho ya Allah na Mtume wake, yameweka wazi umuhimu wa kusoma kabla ya vitendo. Kwa hivyo, Allah (Subhaanahu wa Taala) hatokubali kwa mja wake ibada au vitendo vilivyo fanywa bila ya ilimu. Kwa sababu hio, ndio Sheria ya Kiislamu ikaamrisha Waislamu kusoma na ikawa hukumu ya kusoma ni wajibu juu ya kila Muislamu.

Mambo Yanayo Lazimu Katika Kutafuta Ilimu:

a. Kuwa na Ikhlasi, nayo ni kusoma kwa ajili ya Allah (Subhaanahu wa Taala). Muislamu lazima awe na lengo kubwa katika kutafuta ilimu nalo ni kusoma kwa ajili ya kutaka raadhi za Allah (Subhaanahu wa Taala). Malengo mengine yanakuja baadae. Lakini, la msingi ni kusoma kwa ajili ya Allah (Subhaanahu wa Taala).

b. Kuchunga haki za Mwalimu, kwa kumuheshimu na kumsikiliza vizuri wakati wa kusoma na kuuliza masuali kwa njia ya heshima.

c. Kupanga mikakati ya kusoma, kwa kutanguliza ilimu ambayo ni muhimu sana. Mfano wa kusoma ilimu ya faradhi kabla ya ilimu ya sunna.
d. Kufanyia kazi ilimu, na kuwa na hisia ya jukumu kubwa ulilo libeba. Na kujuwa ya kwamba utaenda kuulizwa ilimu yako mbele ya Allah. Je ulifanyia nini?
e. Kufundisha watu. Ilimu ni amana kutoka kwa Allah (Subhaanahu wa Taala). Na ili tuweze kutekeleza amana hii kama anavyotaka Mwenyezi Mungu, ni lazima tufanye bidii ya kuwafundisha wengine wasio bahatika kusoma. Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) : [Mbora wenu, ni Yule aliye jifunza Qur'an na akafundisha].. Kwa hakika, ni jukumu kubwa juu ya wasomi kufanya bidii kuifundisha ilimu waliopewa na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

KHUTBA YA PILI

Ndugu katika imani, tumeona umuhimu wa ilimu katika dini yetu ya kislamu. Na umma wowote hauwezi kuendelea bila ya ilimu. Waislamu waliweza kumiliki ulimwengu mzima kwa sababu ya ilimu. Leo Waislamu walipo achana na ilimu, au kuchagua baadhi ya ilimu na kuacha nyingine, kwa kudai hio ni ilimu ya makafiri, basi umma umerudi nyuma tumekuwa sisi ni wafuasi wa makafiri, badala ya makafiri kutufuata sisi.

Ndugu Waislamu, kuna umuhimu mkubwa wa kurekebisha nidhamu ya ilimu katika mashule yetu na madrasa zetu. Mfumo wa ilimu ulioko sasa wa kubagua ilimu ya dini na ilimu ya dunia, na kujenga fikra ya kuwa ilimu ya dini ni ilimu ya akhera, haina usaidizi wowote hapa duniani. Kwa hakika, hii ni fikra ya makafiri wenye falsafa inayo sema: Ya Mungu ya baki kanisani na ya Qaysar yatawale nchi. Waislamu wengi waliosomea nchi za magharibi wamejazwa fikra hizo, na baada ya kurudi wakaendelea kufundisha watu fikra potofu za makafiri. Wanazuoni wa zamani walikuwa wamekusanya fani za ilimu mbali mbali na kuweza kuongoza Umma katika Nyanja zote za kimaisha. Mfano wa wanazuoni hao; Imam Al-Ghazali, Ibnu-Rushdi, Ibnu-Al-Haytham, Ibnu-Siiriin, Ibnu-Taymiyah, Ibnul-Qayyim, na wengine mfano wao.

Mwisho

Ndugu Waislamu, Ni wajibu kila Muislamu kufikiria suala hili muhimu, na kuangalia njia gani nzuri ya kurekebisha nidhamu ya ilimu. Ili tuweze kuandaa kizazi ambacho kitakuwa na uwezo wa kusimamia Uislamu na kurejesha utukufu wa Dini ya Kiislamu katika ardhi. Marekebisho muhimu katika ilimu ni kama ifutavyo:-

1. Kurekebisha Manhaj (Mtaala) wa masomo, kwa kuandaa mtaala wa masomo kwa mtazamo wa Kiislamu
2. Kujenga vyuo vikuu kwa lengo la kuandaa Waalimu Waislamu wenye uwezo wa kufundisha Manhaj ya masomo kwa mtizamo wa Kiislamu

3. Kujenga Taasisi na Vituo vya Ilimu ya chini kwa wingi, ili watoto wa kiislamu wapate nafasi ya kusoma
4. Taasisi zote za jamii Kufanya kazi kwa ushirikiano kwa lengo la kuboresha ilimu katika jamii.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe kujitolea kwa ajili yake kwa kufanya marekebisho katika ilimu. Na Atuafikishe tuweze kuandaa Waislamu wa baadae watakao tumikia Uislamu kwa ikhlas na kujitolea kwa hali na mali.

[5] UKATI NA KATI (AL- WASWATWIYA) KATIKA QUR'AN NA SUNNAH

Lengo la Khutba:

1. Kuweka wazi ya kuwa ukati na kati ni jambo muhimu katika uislamu
2. Uislamu ni Dini yenye kwenda na maumbile
3. Kuhadharisha fitna za kupita mipaka

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Makusudio ya Ukati na kati ni mfumo na njia ya kufuata Qur'an na Sunna za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) bila ya kuzidisha au kupunguza. Na huo ndio mfumo wa Mtume na Masahaba zake na watu wema walio tangulia. Dini ya Kiislamu imekamilika, hakuna mtu ambae atakuja baada ya Mtume na kudai ana mambo ya ziada katika dini. Na vile vile, hakuna mtu ambae atadai ya upungufu wa Dini. Njia zote mbili hazikubaliki, kwasababu, Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

وقال تعالى : ﴿ٱلۡيَوۡمَ أَكۡمَلۡتُ لَكُمۡ دِينَكُمۡ وَأَتۡمَمۡتُ عَلَيۡكُمۡ نِعۡمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ ٱلۡإِسۡلَٰمَ دِينٗاۚ﴾ [المائدة:٣]

{{Leo nimekukamilisheni dini yenu, na kuktimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe Dini yenu}}.

Na Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

وقال تعالى : ﴿إِنَّا نَحۡنُ نَزَّلۡنَا ٱلذِّكۡرَ وَإِنَّا لَهُۥ لَحَٰفِظُونَ ٩﴾ [الحجر:٩]

{{Hakika Sisi ndio tulioteremsha Qur'an, na hakika Sisi ndio tutakayoilinda}}. Kwa hivyo, Mfumo na Manhaj ya dini ya Kiislamu ni moja nayo ni kufuata Qur'an na Sunna bila ya ziada wala kupunguza.

Ukati na Kati katika Qur'an

Maelezo ya neno lake Allah (Subhaanahu wa Taala) Aliposema:

قال الله تعالى : ﴿وَكَذَٰلِكَ جَعَلۡنَٰكُمۡ أُمَّةٗ وَسَطٗا لِّتَكُونُواْ شُهَدَآءَ عَلَى ٱلنَّاسِ وَيَكُونَ ٱلرَّسُولُ عَلَيۡكُمۡ شَهِيدٗاۗ﴾ [البقرة:١٤٣]

{{Tumewafanya (nyinyi Waislamu) kuwa ni umma bora ili muwe ni mashahidi kwa watu (wafuasi wa mitume iliyotangulia kuwa mitume yao waliufikisha kwao ujumbe wa Allah}}.

Kwa sababu Allah amewaeleza vizuri katika Qu'rani Aliposema (Subhaanahu wa Taala).

قال تعالى : ﴿كُنتُمۡ خَيۡرَ أُمَّةٍ أُخۡرِجَتۡ لِلنَّاسِ تَأۡمُرُونَ بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَتَنۡهَوۡنَ عَنِ ٱلۡمُنكَرِ﴾ [آل عمران:١١٠]

{{Nyinyi ni umma bora uliotolewa miongoni mwa watu, mnaamrisha mambo mema na kukataza mabaya}}..

Ulinganizi wa Mitume wote ulikuwa Mfumo wake na Wakati Na kati

Ushahidi wake ni neno la Mtume lililopokewa kwa Abu Huraira amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) [Hakika dini ni nyepesi wala mtu hatoifanyia dini mkazo isipokuwa itamshinda fanyeni usawa na karibisheni na mubashirie mazuri].

Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالى : ﴿قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦٢﴾﴾ [الأنعام:١٦٢]

{{Sema, hapana shaka swala yangu na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu (zote) ni kwa Mwenyezi Mungu ambaye ni muumba wa walimwengu}}.

Enyi Waislamu, Hapana shaka Mwenyezi Mungu anawaamrisha kati ya watu kuhukumu kwa uadilifu. Hapana shaka Allah anawapa mawaidha mazuri, hapana shaka Allah ni mwenye kusikia, kuona.

Na amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالى: ﴿وَابْتَغِ فِيمَا آتَاكَ اللَّهُ الدَّارَ الْآخِرَةَ ۖ وَلَا تَنسَ نَصِيبَكَ مِنَ الدُّنْيَا ۖ وَأَحْسِن كَمَا أَحْسَنَ اللَّهُ إِلَيْكَ ۖ وَلَا تَبْغِ الْفَسَادَ فِي الْأَرْضِ ۖ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُفْسِدِينَ ﴿٧٧﴾﴾ [القصص:٧٧]

{{Na yote (mali) miongoni mwa aliyokupa Mwenyezi Mungu kwa kuitaka nyumba ya Akhera (Kwa kufanya mema na kutoa sadaka). Na wala usilisahau fungu lako la Dunia (kwa starehe). Na fanya wema (kwa waja wa Mwenyezi Mungu. Na wala (kwa sababu ya mali yako) usifanye uchafu katika ardhi. Hapana shaka Allah hawapendi wenye hufanya uchafu}}.

Ukati na kati wa Ahlu Sunnah wal Jamaah katika Itikadi na Kufuata Twaa

Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لَا تَغْلُوا فِي دِينِكُمْ وَلَا تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ إِلَّا الْحَقَّ ۚ إِنَّمَا الْمَسِيحُ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ رَسُولُ اللَّهِ وَكَلِمَتُهُ أَلْقَاهَا إِلَىٰ مَرْيَمَ وَرُوحٌ مِّنْهُ ۖ فَآمِنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ ۖ وَلَا تَقُولُوا ثَلَاثَةٌ ۚ انتَهُوا خَيْرًا لَّكُمْ ۚ إِنَّمَا اللَّهُ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ ۖ سُبْحَانَهُ أَن يَكُونَ لَهُ وَلَدٌ ۘ لَّهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ وَكِيلًا ﴿١٧١﴾﴾ [النساء:١٧١]

{{Enyi watu wa vitabu! msipite mipaka katika dini yenu (hawa ni wakristo wanaodai uungu wa nabi Issa na wala usiseme juu ya Mwenyezi Mungu (kwamba ana mke na watoto) ila mseme haki. Hapana shaka masihi Issa mtoto wa Maryam ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na neno lake alimpelekea Maryam na roho itokayo kwake. Basi muaminini Mwenyezi Mungu na muamini Mitume yake. Wanaamrishwa wakristo wanaoamini mitume ya Mwenyezi Mungu na miongoni mwao wamuamini Mtume Muhammad (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) na wala msiseme mungu ni nafsi tatu komeni bora kwenu. Hapana shaka Mwenyezi Mungu ni Mungu moja (hana ushirika) ametakasika kuwa ana watoto. Ni vyake vyote vilivyomo ndani ya ardhi na hakika hutosha kuutegemea Mwenyezi Mungu}}.

Kutoka kwa Anas Ibn Malik alisema: 'Walikuja watu watatu mpaka kwa nyumba za wakeze Mtume wakauliza namna ya ibada za Bwana Mtume (Swalla

Llahu 'alayhi wasallam). Walipoambiwa walisema sisi tuko wapi na Mtume na yeye amekwisha samehewa madhambi yake yaliyotangulia na yatakayo kuja. Akasema mmoja wao ama mimi nitaswali usiku siku zote. Na mwingine akasema mimi nitafunga siku zote na na sitoacha kufunga na akasema mwingine na mimi nitajiepusha na wanawake sitooa kabisa. Mtume akawajia akawambia: [Nyinyi ndio mliosema kadha wa kadha naapa kwa Allah mimi ni mnyenyekevu mno kwa Allah kuliko nyinyi na mimi numuogopa Allah kuliko nyinyi lakini nafunga na siku nyingine sifungi na naswali usiku na siku nyingine nalala na mimi huoa wanawake basi mwenye kuacha mwenendo wangu si miongoni mwa watu wangu].

Maneno ya Wanavyuoni Kuthibitisha Ukati na kati wa Ahlu Sunnah

Amesema ibn Jarir At-Twabary na amepokea ya kwamba Allah (Subhaanahu wa Taala) Amewasifu ya kwamba wao ni watu wakati na kati, kwa ajili ya ukati na kati wao katika dini hawakupita mpaka katika dini. Kama walivyofanya wakristo ambao wamepita mipaka katika (tarhib) na wakasema kuhusu nabi issa ambaye nabii issa hakuyasema wala wao si watu (watakasirika) na kama (taksira) ya mayahudi ambao wamebadilisha kitabu cha Allah na wameuwa Mitume yao na wakamsingizia uongo mola wao (Waislamu) ni watu wa kati na kati na wamelingana katika hilo, wakasifu Allah kwa hilo, likawa jambo linalo pendeza zaidi kwa Allah ni lililo kati na kati. Amesema Shatwiby. 'Ukiangalia katika kitendo cha sheria na ukazingatia utapata ndani yake kuna ukati na kati, na ukipata umelemea sehemu katika sehemu zake hilo ni kutoka na kukabiliana na ile hali ilivyo au ni kutokea katika sehemu nyingine. Sehemu (upande) uliomgumu sana ni kwa kulihofisha na kuhimiza na kukataza. Na upande au sehemu yenye ukhafifu sana inakuwa katika kutoa ruhusa na kuhimiza inakuwa mara nyingi ni uzito kulifanya jambo kuwa gumu, isipokuwa hivi au vile utaona Na upande wa usawa uko wazi nao ni msingi ambao wenye kurejelewa na mwenye akili ni yule ambaye atauelekea".

KHUTBA YA PILI

Umuhimu wa Ukati na Kati

Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala) katika Qur'an tukufu kueleza ukati na kati :

قال الله تعالى : ﴿ كَانَ ٱلنَّاسُ أُمَّةً وَٰحِدَةً فَبَعَثَ ٱللَّهُ ٱلنَّبِيِّـۧنَ مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ وَأَنزَلَ مَعَهُمُ ٱلْكِتَٰبَ بِٱلْحَقِّ لِيَحْكُمَ بَيْنَ ٱلنَّاسِ فِيمَا ٱخْتَلَفُوا۟ فِيهِ ۚ وَمَا ٱخْتَلَفَ فِيهِ إِلَّا ٱلَّذِينَ أُوتُوهُ مِنۢ بَعْدِ مَا جَآءَتْهُمُ ٱلْبَيِّنَٰتُ بَغْيًۢا بَيْنَهُمْ ۖ فَهَدَى ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لِمَا ٱخْتَلَفُوا۟ فِيهِ مِنَ ٱلْحَقِّ بِإِذْنِهِۦ ۗ وَٱللَّهُ يَهْدِى مَن يَشَآءُ إِلَىٰ صِرَٰطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٢١٣﴾ ﴾ [البقرة:٢١٣]

{{Walikuwa watu ni umma mmoja (juu ya imani mmoja) (wakakhitilafiana) na akapeleka Mwenyezi Mungu Manabii wenye kutoa habari njema (kuwa wenye kuamini kuwa wataingia peponi) na kutoa onyo (kuwa wakafiri kutamba wataingia motoni) na aliwateremshia vitabu vilivyoshikamana kwa haki ili ahukumu kati ya watu katika waliokhtalifiana na hawakukhitlifiana katika vitabu ila walio pewa

(hivyo vitabu) baada ya kuwajia wao hoja zilizo waziwazi kwa ajili ya wivu baina yao (uvivu wa makafiri juu ya wenye kuamini) na akawaongoza Mwenyezi Mungu walioamini kwa walivyokhitalifiana nayo katika haki kwa ruhusa yake) na Mwenyezi Mungu humwongoza amtakaye katika Uislamu}}.

Kutoka kwa ibn 'Abbas amesema: Aliulizwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) ni dini gani inayopendeza zaidi kwa Allah? akasema; [Al-Hanafiyat Samhaa] Amepokea Ahmad katika musnad. Maana yake ni dini ya kusimamisha Tawhidi ya Allah peke yake na kufuata mila ya baba yetu Ibrahim na kutoka kwa Anas Ibn Malik kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Fanyeni wepesi na mutoe biashara wala musifukuze watu hakika mimi nimetumilizwa kufanya wepesi].

Na kutoka kwa Abu Huraira amesema: Hakika Bedui alikojoa katika Msikiti watu wakampigia kelele. Mtume wa Allah akawaambia: [Mwacheni, kisha mwagieni maji].

Mwisho

Enyi Waislamu, Hakuna njia nzuri kuliko ile aliyofundisha Mtume na Masahaba zake baada yake na waja wema. Kwa hivyo, tufanyeni bidii kujilazimisha na manhaj ya Mtume sahihi bila ya kuangalia njia nyinginezo ambazo ni ziada ya manhaj ya Mtume au ni upungufu ukilinganisha na Manhaj ya Mtume na Masahaba zake. Ndugu katika imani, Mcheni Allah na jilazimisheni na Kitabu chake na Sunna za Mtume wake.

Tunamuomba Allah Atujalie miongoni mwa waliopata tawfiq yake ya kuweza kufuata Kitabu chake na Sunna za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam).

[6] MFUMO WA MITUME KATKA ULINGANIZI

Lengo la Khutba:

1. Kuwakumbusha watu juhudi za Mitume katika kufikisha ujumbe wa Allâh.
2. Kuwahimiza walinganizi kuwaigiza Mitume katika mfumo sahihi wa ulinganizi na wenye kufaulu.
3. Umuhimu wa kuzungumzia mfumo wa ulinganizi kulingana na hali zilivyo.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Kazi kubwa ya Mitume ni ulinganizi. Mitume wote walitumwa kuwalingania viumbe kushikamana na Tawhidi. Tawhidi ndio msingi wa ulinganizi.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ ﴾ [النحل:٣٦]

{{Na bila shaka tulimpeleka Mtume katika kila umma ya kwamba 'Muabuduni Mwenyezi Mungu na muepukeni Iblisi muovu}}.

Mitume ya Allâh ni watu waliochaguliwa walio bora kwa ulinganizi. Inawezekana kutolea ushahidi neno Lake Allâh (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ قَالُوا يَا صَالِحُ قَدْ كُنتَ فِينَا مَرْجُوًّا قَبْلَ هَٰذَا ۖ أَتَنْهَانَا أَن نَّعْبُدَ مَا يَعْبُدُ آبَاؤُنَا وَإِنَّنَا لَفِي شَكٍّ مِّمَّا تَدْعُونَا إِلَيْهِ مُرِيبٍ ﴿٦٢﴾ ﴾ [هود:٦٢]

{{Walisema: Ewe Swaleh! Hakika ulikuwa kati yetu ni mwenye kuheshimiwa kabla hujasema haya maneno yako. Je! watukataza kuyaabudu waliokuwa wakiyaabudu wazee wetu. Na hapana shaka sisi tuna shaka kwa unayotuitia na ni wenye kulituhumu jambo lako}}.

Neno Lake Allah (Subhaanahu wa Taala):

وقال تعالى : ﴿ وَاذْكُرْ عِبَادَنَا إِبْرَاهِيمَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ أُولِي الْأَيْدِي وَالْأَبْصَارِ ﴿٤٥﴾ إِنَّا أَخْلَصْنَاهُم بِخَالِصَةٍ ذِكْرَى الدَّارِ ﴿٤٦﴾ وَإِنَّهُمْ عِندَنَا لَمِنَ الْمُصْطَفَيْنَ الْأَخْيَارِ ﴿٤٧﴾ ﴾ [ص:٤٥:٤٧]

{{Na wakumbuke waja wetu, Ibrahim, Is-haqa na Ya'qubu waliokuwa na nguvu na busara. Sisi Tumewakhusisha wao kwa sifa ya ukumbusho wa Akhera. Na hakika wao kwetu sisi ni wateuliwa walio bora. Na mkumbuke Ismail, Ilyasaa na Dhulkifli, na wote hao ni katika walio bora}}.

Mitume wote walikuja na ulinganizi mmoja. Wote waliwaambia wafuasi wao kufuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu na kujiepusha na makatazo yake.

Mfumo wa Ulinganizi

1. Kutanguliza Tawhidi kuliko ibada nyingine. 'Abdullah bin 'Abbass amesema: Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alimwambia Mu'adh Ibn Jabal wakati alipomtuma kwenda Yemen: [Hakika unawaendea watu ambao ni Ahlul-Kitâb. Utakapowaendea, walinganie washuhudie kuwa hakuna mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allâh, na kuwa mimi ni Mtume wa Allâh. Watakapokutii kwa hilo, wajulishe kuwa Allâh Amewafaradhia

Swala tano kila mchana na usiku. Watakapokutii kwa hilo, wajulishe kuwa Allâh Amewafaradhia Zaka, inachukuliwa kutoka kwa matajiri wao na wanarudishiwa mafukara wao. Watakapokutii katika hilo, basi tahadhari mali yao yenye thamani. Na uogope dua ya mwenye kudhulumiwa, kwani hakuna pazia baina ya dua hiyo na Allâh]. Al-Bukhary.

2. Kutumia Lugha inayo fahamika na walinganiwa. Ushahidi ni Neno Lake Allâh (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَا مِن رَّسُولٍ إِلَّا بِلِسَانِ قَوۡمِهِۦ لِيُبَيِّنَ لَهُمۡۖ فَيُضِلُّ ٱللَّهُ مَن يَشَآءُ وَيَهۡدِي مَن يَشَآءُۚ وَهُوَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ ﴿٤﴾﴾ [إبراهيم:٤]

{{Hatukumtuma Mtume ila kwa lugha ya kaumu yake ili apate kuwabainishia. Basi Allâh Humuacha akapotea Amtakaye, na Akamwongoza Amtakaye. Naye ni Mtukufu Mwenye nguvu na Mwenye hikima}}.

Amesema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [Atakapowajia mkarimu wa watu basi mkirimuni]. Imepokewa na Ibu Majah.

Mwangalie Nabii Nuh aliwaambia watu wake: Wala mimi si wa kuwafukuza Waumini. Mimi si chochote ila ni Mwonyaji wa dhahiri shahiri. Wakasema: Ikiwa huachi, ewe Nuhu, bila ya shaka utapigwa mawe. Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika watu wangu wamenikanusha. Basi Hukumu baina yangu na wao kwa Hukumu Yako, na Uniokoe na walio pamoja nami, Waumini.

3. Kuchagua washirika wazuri katika kusaidiana kulingania watu. Ushahidi ni Neno Lake Allâh (Subhaanahu wa Taala) Alipomfanya Musa waziri wake kuwa ni Harun :

قال تعالى : ﴿وَٱجۡعَل لِّي وَزِيرٗا مِّنۡ أَهۡلِي ﴿٢٩﴾ هَٰرُونَ أَخِي ﴿٣٠﴾ ٱشۡدُدۡ بِهِۦٓ أَزۡرِي ﴿٣١﴾ وَأَشۡرِكۡهُ فِيٓ أَمۡرِي ﴿٣٢﴾ كَيۡ نُسَبِّحَكَ كَثِيرٗا ﴿٣٣﴾ وَنَذۡكُرَكَ كَثِيرًا ﴿٣٤﴾ إِنَّكَ كُنتَ بِنَا بَصِيرٗا ﴿٣٥﴾﴾ [طه:٢٩-٣٥]

{{Na Unipe waziri katika watu wangu, Harun, ndugu yangu. Kwake yeye Niongeze nguvu zangu. Na Umshirikishe katika kazi yangu. Ili tukutakase kwa wingi. Na tukukumbuke kwa wingi}}.

Muangalia Nabii Swaleh na watu wake katika Neno Lake Allâh (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿قَالُواْ يَٰصَٰلِحُ قَدۡ كُنتَ فِينَا مَرۡجُوّٗا قَبۡلَ هَٰذَآۖ أَتَنۡهَىٰنَآ أَن نَّعۡبُدَ مَا يَعۡبُدُ ءَابَآؤُنَا وَإِنَّنَا لَفِي شَكّٖ مِّمَّا تَدۡعُونَآ إِلَيۡهِ مُرِيبٖ ﴿٦٢﴾﴾ [هود:٦٢]

{{Wakasema: Ewe Saleh! Hakika kabla ya haya ulikuwa unatarajiwa kheri kwetu. Je, unatukataza tusiwaabudu waliokuwa wakiwaabudu baba zetu? Na hakika sisi tuna shaka na wasiwasi kwa hayo unayotuitia}}.

Mwangalie Mtume Muhammad (Swalla Llahu 'alayhi wasallam), Aliposema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَإِن كَادُواْ لَيَفۡتِنُونَكَ عَنِ ٱلَّذِيٓ أَوۡحَيۡنَآ إِلَيۡكَ لِتَفۡتَرِيَ عَلَيۡنَا غَيۡرَهُۥۖ وَإِذٗا لَّٱتَّخَذُوكَ خَلِيلٗا ﴿٧٣﴾ وَلَوۡلَآ أَن ثَبَّتۡنَٰكَ لَقَدۡ كِدتَّ تَرۡكَنُ إِلَيۡهِمۡ شَيۡـٔٗا قَلِيلًا ﴿٧٤﴾ إِذٗا لَّأَذَقۡنَٰكَ ضِعۡفَ ٱلۡحَيَوٰةِ وَضِعۡفَ ٱلۡمَمَاتِ ثُمَّ لَا تَجِدُ لَكَ عَلَيۡنَا نَصِيرٗا ﴿٧٥﴾﴾ [الإسراء:٧٣-٧٥]

{{Na hakika walikaribia kukushawishi uache Tuliyokufunulia ili utuzulie mengineyo. Na hapo ndio wangelikufanya rafiki. Na lau kuwa Hatukukuweka imara ungelikaribia kuwaelekea kidogo. Hapo basi bila shaka Tungelikuonjesha adhabu maradufu ya uhai, na adhabu maradufu ya kifo. Kisha usingepata mtu wa kukunusuru nasi }}.

Aya na Hadithi zinabainisha wazi mfumo wa Mitume ya Allah katika kulingania wanadamu. Na haya ni mafundisho kwa kila Muislamu atakaye fanya kazi hii ya mitume. Ni lazima afuate mfumo sahihi wa kulingania nayo ni mfumo wa Mitume.

KHUTBA YA PILI

Dalili za Kimaumbile na za Kisharia na za Kiakili

Zinachukuliwa hoja hizo kutoka kwa kisa cha Nabii Ibrahim na babake. Mtume Ibrahim alipomwambia baba yake, Azar: Unayafanya masanamu kuwa ni miungu? Hakika mimi nakuona wewe na watu wako mmo katika upotofu ulio wazi. Na kadhalika Tulimwonyesha Ibrahim Ufalme wa mbingu na ardhi, na ili awe miongoni mwa wenye yakini. Na ulipomuingilia usiku aliona nyota, na akasema: Huyu ni Mola wangu Mlezi. Ilipotua akasema: Siwapendi wanaotua. Alipouona mwezi unachomoza alisema: Huyu ndiye Mola wangu Mlezi. Ulipotua akasema: Kama Mola wangu Mlezi Hakuniongoza, nitakuwa katika kaumu waliopotea. Na alipoliona jua linachomoza akasema: Huyu ndiye Mola wangu Mlezi. Huyu mkubwa kuliko wote. Lilipotua, alisema: Enyi watu wangu! Mimi simo katika hayo mnayofanyia ushirikina. Hakika mimi nimeuelekeza uso wangu sawa sawa kwa Aliyeziumba mbingu na ardhi, wala mimi si miongoni mwa washirikina. Na watu wake wakamhoji. Akasema: Je, mnanihoji juu ya Allâh, na hali Yeye Ameniongoza? Wala siogopi hao mnaowashirikisha Naye, ila Mola wangu Mlezi Akipenda kitu. Mola wangu Mlezi Amekusanya ilimu ya kila kitu. Basi je, hamkumbuki? Na vipi niogope hivyo mnavyovishirikisha, hali nyinyi hamuogopi kuwa nyinyi mumemshirikisha Allâh na kitu ambacho Hakukiteremshia uthibitisho. Basi kundi gani katika mawili haya lina haki zaidi kupata amani, kama nyinyi mnajua? Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhulma - hao ndio watakaopata amani na wao ndio walioongoka. Na hizo ndizo hoja Zetu Tulizompa Ibrahim kuhojiana na watu wake. Tunamnyanyua kwa vyeo Tumtakaye. Hakika Mola Mlezi wako ni Mwenye hikima na Mwenye ujuzi.

Na pia hupatikana mfano vile vile katika kisa cha Musa na Firauni. Allâh Mtukufu Alimtuma Musa na Haruni Akawambia: Nendeeni kwa firauni, na mwambieni: Hakika sisi ni Mitume wa Mola wako Mlezi! Basi waache Wana wa Israili watoke nasi, wala usiwaadhibu. Sisi tumekuletea ishara itokayo kwa Mola wako Mlezi. Na amani itakuwa juu ya aliyefuata uwongofu. Hakika tumefunuliwa kwamba hapana shaka adhabu itamsibu anayekadhibisha na akapuuza. (Firauni) akasema: Basi Mola wenu Mlezi ni nani, ewe Musa? Akasema: Mola wetu Mlezi ni Yule Aliyekipa kila kitu umbo lake, kisha Akakiongoza. Akasema: Nini hali ya karne za kwanza? Akasema: Ilimu yake iko kwa Mola wangu Mlezi katika Kitabu.

Mola wangu Mlezi Hapotei wala Hasahau.

Hikima na Mawaidha Mazuri, Kusimulia visa, Kuhimiza, na Kuonya

Yanayoshuhudia hayo ni neno lake Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) kama alivyosimulia Mâlik bin al-Huwairith kwa kusema: [Tulimwendea Mtume nasi tulikuwa barobaro tuliokaribiana kwa umri. Tukaketi kwake masiku ishirini. Mtume alikuwa ni rahimu mwenye huruma. Akadhani kuwa tumewatamani jamaa zetu. Akatwambia: "Rudini kwa jamaa zenu, mukae nao, muwafundishe na muwaamuru, muswali Swala kadha wakati kadha na muswali kadha wakati kadha. Wakati wa Swala ukifika, mmoja wenu awaadhinie na mkubwa wenu awaswalishe]. Al-Bukhary.

Hudheifa amesema: "Walikuja kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) watu kutoka Najran, wakamwambia Mtume: [Tuletee mtu mwaninifu. Akawaambia: "Nitawatumia mtu mwaminifu wa kweli]. Akawatumia Abu 'Ubaidah bin al-Jarrah." Al-Bukhari.

Abu Burdah amesema: Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alimtuma Abu Musa na Mu'adh bin Jabal huko Yemen. Akasema: [Na akamtuma kila mmoja katika wao sehemu mbili kisha akawaambia: Fanyeni wepesi wala msifanye uzito, na wabashirieni na wabashirieni watu mazuri wala musiwakimbize watu]. Al-Bukhari.

Yameshuhudiwa hayo kwa haya maneno mashuhuri: "Hikma ni kitu kilichompotea Muumini, basi atakapoipata ni haki yake aichukue." Yatakikana ijulikane kuwa Hadithi hii imepokewa kuwa ni *mursal* na pia imepokewa kuwa Zaidi bin Aslam ameirufaisha kwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) imetolewa na Tirmidhi.

Mwisho

Ndugu katika imani, kwa hakika ni jukumu la kila Muislamu khaswa wale wanaofanya kazi ya ulinganizi kusoma manhaj na mtume wa Mitume katika kulingania. Ulinganizi ni ibada, na haiwezekani kukubaliwa ibada zetu mpaka tufuate mafundisho ya Mtume katika kutekeleza ibada zetu. Historia ya Mitume ina mafundisho mengi kwa kila mtu atakaye kufanya kazi ya Mitume. Kwa hivyo, tunawahimiza Waislamu kusoma Sera ya Mitume kwa lengo la kujuwa mfumo kamili wa maisha yao. Ili tuweze kuwafuata Mitume katika maisha yetu. Tunamuomba Allah Atuwezeshe kushikamana na mafundisho ya Mitume wake, na Atuwezeshe kufuata mfumo wa Mitume katika ulinganizi.

[6] SEHEMU YA MISIMU NA MINASABA

Malengo Muhimu :

1. Kuwafundisha watu hukumu za kisheria katika minasaba ya mwaka
2. Kutahadharisha watu kwenda kinyume na sheria katika minasaba hiyo
3. Kuwafungamanisha watu na Mola wao katika hali zote.

Anuani ya Khutba katika Sehemu ya Misimu:-

1. Iddi ya Kufungua Saumu
2. Iddi ya Kuchinja
3. Swala ya kuomba Mvua
4. Swala ya kupatwa Jua au Mwezi
5. Mnasaba wa Mwaka Mpya

[1] IDDI YA KUFUNGUA SAUMU

Lengo la Khutba:

1. Kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumuhimidi ni katika lengo la Iddi.
2. Kuwasaidia na kuwafanyia wema wanaohitaji.
3. Kudhihirisha mema ya kiislamu.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Iddi ya Fitri ni Iddi ya kwanza kwa Waislamu. Waislamu wanasherehekea katika mwezi wa Shawwal kinyume na Iddul adhha ambapo Waislamu wanasherehekea katika mwezi wa Dhulhijjah. Waislamu wanakula baada ya kufunga mwezi mzima, ni haramu kufunga siku hiyo. Na muda wa kusherehekea ni siku moja hadi siku sita.

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) kukamilisha kufunga mwezi wa Ramadhani. Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿شَهۡرُ رَمَضَانَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ فِيهِ ٱلۡقُرۡءَانُ هُدٗى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَٰتٖ مِّنَ ٱلۡهُدَىٰ وَٱلۡفُرۡقَانِۚ فَمَن شَهِدَ
مِنكُمُ ٱلشَّهۡرَ فَلۡيَصُمۡهُۖ وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوۡ عَلَىٰ سَفَرٖ فَعِدَّةٞ مِّنۡ أَيَّامٍ أُخَرَۗ يُرِيدُ ٱللَّهُ بِكُمُ ٱلۡيُسۡرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ
ٱلۡعُسۡرَ وَلِتُكۡمِلُواْ ٱلۡعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُواْ ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَىٰكُمۡ وَلَعَلَّكُمۡ تَشۡكُرُونَ ١٨٥﴾ [البقرة:١٨٥]

{{Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa katika mwezi huo Qur'an ili iwe uongozi kwa watu na hoja zilizo wazi wa uongozi na upambanuzi (wa baina ya haki na batili).

Atakayekuwa katika mji katika huu mwezi wa Ramadhani afunge. Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi atimize hisabu ya siku alizoacha kufunga katika siku nyingine. Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mapesi wala hakutakieni yalio mazito, na pia anakutakieni mtimize hesabu hiyo, na anakutakieni kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa kuwa amekuongozeni, ili mpate kushukuru}}. Amesema 'Umar siku mbili hizi Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amekataa kufunga yaani Iddul-fitr (baada ya mwezi wa Ramadhani) na Idul-Adhha (Baada ya Hajj).

Amepokea Anas kwamba Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alikwenda Madina na walikuwa wana siku mbili za kucheza, Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akasema {Mwenyezi Mungu amekubadilishieni siku mbili hizo kwa Iddul-fitr na Iddul Adhha].

Siku ya Iddi ni siku ya mapambo. Imepokewa kwa Ibnu 'Umar kuwa alinunua juba sokoni akamuuzia Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) kuwa ajipambe nalo siku ya Iddi, Amepokea Anas Ibnu Malik kuwa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amesema: [Haendi kuswali swala ya Iddul-fitr mpaka ale Tende].

Hukumu ya Utoaji wa Sadaka ya Fitri

Amepokea Ibnu ‘Abbas kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amefaradhisha Zakatul-fitri kumtakasa aliyefunga kutokana na michezo, pia kuwa ni chakula cha maskini. Mwenye kutoa kabla ya swala basi ametoa zaka na atakayetoa baada ya swala basi hio ni sadaka miongoni mwa sadaka.

Kupiga Takbir za Iddi

Asili ya jambo hilo Neno lake Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) :

قال الله تعالى: ﴿وَلِتُكْمِلُوا۟ ٱلْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُوا۟ ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَىٰكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٨٥﴾﴾ [البقرة:١٨٥]

{{Anakutakieni mtimize hisabu hiyo, na anakutakieni kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa kuwa amekuongozeni, ili mpate kushukuru}}.

Imepokewa na Ibnu ‘Umar akisema kuwa: [Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alikuwa akipiga Takbiri alipo kwenda kuswali swala ya Iddi].

KHUTBA YA PILI

Namna ya kuswali Swala ya Iddi

Imethibiti kwa Ibn ‘Abbas kuwa ameswali swala ya Idd pmoja na Mtume na Abubakar pamoja na ‘Umar na ‘Uthman kuwa wote wameswali kabla ya khutba. Amesema Ibnu Abbas kuwa Mtume ameswali Idd kwa rakaa mbili na hakuswali kabla ya hapo au baada ya hapo.

Ziara Baada ya Swala na kupeana Zawadi

Imethibiti Hadithi kutoka kwa Ibnu ‘Abbas kuwa ametoka pamoja na Mtume siku ya Iddul-fitr na Iddul-Adhha wakaswali kisha aka khutubu Mtume na akawatembelea wanawake na kuwapatia mawaidha na akawaamrisha kupeana sadaka. Abubakar aliingia nyumba Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) na ‘Aisha alikuwa na vijakazi viwili wakipiga matwari. Akawakataza Abubakar. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akasema: [Waache kwani kila jami ina Iddi yao].

Kufunga Siku sita za Shawwal.

Amesema Abu Ayub Answar kuwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema [Atakayefunga Ramadhani kisha akafuatilizia siku sita za Shawaal ni kama aliyefunga mwaka mzima].

Amesema Hasan Al-Basri kuwa Mwenyezi Mungu ameridhia kufunga siku sita za Shawwal na ufungaji wa mwaka mzima.

Kumshukuru Mwenyezi Mungu katika Siku za Iddi

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قوله تعالى : ﴿وَٱشْكُرُوا۟ لِى وَلَا تَكْفُرُونِ ﴿١٥٢﴾﴾ [البقرة:١٥٢]

{{Na mnishukuru Mimi na wala msikanushe}}.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ وَإِذْ تَأَذَّنَ رَبُّكُمْ لَئِن شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ وَلَئِن كَفَرْتُمْ إِنَّ عَذَابِي لَشَدِيدٌ ﴿٧﴾ ﴾ [إبراهيم:٧]

{{Na kumbukeni alipotangaza Mola wenu : kama mkishukuru, nitakuzidishieni; na kama mkikufuru, jueni kuwa adhabu Yangu ni kali sana}}.

Amesema ‘Imran Ibn Huswain kuwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema kuwa Mwenyezi Mungu amesema: [Mwenyezi Mungu akimneemesha mja hupenda kuona athari ya neema hiyo kwa mja wake]. Kwahivyo, ndugu Waislamu dhihirisheni neema za Allah (Subhaanahu wa Taala) kwa kuwasaidia maskini katika siku hii muhimu siku ya furaha.

Mwisho

Lengo la kufunga ni kumcha Mwenyezi Mungu kama alivyosema Mwenyezi Mungu. Na maana ya kumcha Mwenyezi Mungu ni kufuata maamrisho yake yote na kuachana na makatazo yote aliyo kataza. Kudumu na msimamo wa uchaji Mungu paka kufikiwa na mauti.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe Taqwa, na atupe maghfira, rehema na kuwachwa huru na moto wa Jahannam.

[2] IDDI YA KUCHINJA

Lengo la Khutba:

1. Kuwajulisha watu maana ya Idd
2. Kuwafikiwa kwa ‘Idul Fitr
3. lengo la Idd ni kumshukuru Mungu kwa mema yake pamoja na kuswali, kutembeleana na kupeana zawadi.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Idul Adhaha (Iddi ya kuchinja) ni mojawapo ya idd mbili katika Uislamu na inakuwa tarehe kumi Dhulhijaa baada ya kusimama Arafa sehemu ambayo wamesimama mahujaj katika kutekeleza Hijja, na kwisha Iddi hiyo tarehe 13 Dhulhija. Iddi hiyo ni kukumbuka kisa cha Nabii Ibrahim alipotaka kumchinja mwanawe Ismail kwa ajili hiyo wanasimama Waislamu kuchinja wanyama.

Hekima ya Swala ya Iddi

Imeshurutishwa swala ya Iddi ili kuzishukuru neema za Mwenyezi Mungu na kushibisha matamanio ya binadamu.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا ۚ فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا ۚ لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ ۚ ﴾ [الروم:٣٠]

{{Basi elekeze uso wako katika Dini iliyo sawa sawa, ndilo umbile Mwenyezi Mungu Alilowaumbia watu (yaani Dini hii ya kislamu inawafikiana barabara na umbo la binadamu) hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Mwenyezi Mungu}}.

Iddi ni Mkusanyiko wa Mambo Manne;

1. Kukusanyika kwa watu.
2. Kukusanyika kwa sehemu.
3. Kukusanyika kwa wakati.
4. Kukusanyika kwa ibada maalum.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال الله تعالى: ﴿ وَلِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنسَكًا لِّيَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّن بَهِيمَةِ الْأَنْعَامِ ۗ فَإِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ فَلَهُ أَسْلِمُوا ۗ وَبَشِّرِ الْمُخْبِتِينَ ﴿٣٤﴾ ﴾ [الحج:٣٤]

{{Na kila umma tumewafanyia mahali pa kuchinja, mihanga ya Ibada ili kulitaja jina la Mwenyezi Mungu juu ya vile alivyowaruzuku katika wanyama hao wenye miguu mine. Basi Mungu wenu ni Mungu mmoja tu; Jinyenyekesheni kwake. Na wape khabari njema wale wanyenyekevu}}.

Imepokewa na Anas kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) alipokwenda Madina aliwakuta watu wa Madina wana siku mbili wanacheza, Mtume (Swalla

Llahu ‘alayhi wasallam) akawaambia Mwenyezi Mungu amekubadilishieni siku mbili hizi kwa iddul Adha (kuchinja) na Iddul-fitr (baada ya Ramadhani). Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قوله تعالى: ﴿فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَٱنْحَرْ ﴿٢﴾﴾ [الكوثر:٢].

{{Basi Sali kwa ajili ya Mola wako na uchinje kwa ajili ya mola wako}}.

Hukumu ya Kuchinja katika Siku ya Iddi Pamoja na Sharti Zake na Namna ya Kuchinja.

Amesema Ibnu ‘Umar “Kuchinja ni sunnah”. Amesema Imam Sha’abi: “Haruhusiwi mtu kuacha kuchinja isipokuwa kwa mwenye kuhiji na kusafiri”. Imepokewa na Ibnu Majah kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) ameamrisha kugawanya nyama ya Udhiya mara tatu akisema kuleni, toeni sadaka na muhifadhi.

Kushurutishwa Kupiga Takbira pamoja na Hukumu Zake na Namna yake

Imepokewa na Ibnu Abbas amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) hakuna siku kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu, wala siku zinazopendekezwa kwake amali kama siku kumi za mwanzo wa mwezi wa Dhulhija, zidisheni Tasbihi na Takbiri na Tahlil (Lailaha ila Allah).

KHUTBA YA PILI

Kutembelea Jamii na kutumia Wakati kwa Michezo na Furaha

Amesema ‘Aisha kuwa wahabesha (watu wa Ethiopia) wanachezea siku ya Iddi, akaniita Mtume wa Mwenyezi Mungu na nikawa nawaangalia kupitia mabega ya Mtume, akaja Abubakar. Mtume akamwambia Abubakar amuwache kwani kila jamii wana Iddi yao. Ni makosa wanawake kudhihrisha mapambo yao na kujirembesha. Kunazidi kujirembesha kwa wanawake katika siku ya Iddi na hivyo ni kinyume ya sheria.

Katazo la kupigana na kuoneshana Silaha katika Siku ya Iddi

Imepokewa na Abu Huraira Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema atakayebeba silaha si katika sisi (kwa Waislamu). Amesema Hasan Al-Basri: kumekatazwa kubeba silaha katika siku ya Idd isipokuwa kwa atakayetishiwa na adui.

Kukutana Siku ya Iddi na Ijumaa

Imepokewa na Abu Huraira Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) amesema “Imekutana kwenu nyinyi Idd mbili atakayetaka hatoswali ijumaa, lakini mimi nitaswali Idd na Ijumaa (haimanishi kupomoka swala ya adhuhiri).

Kuombea Dua za Kheri Siku ya Iddi

Amesema Adham kijakazi wa Umar ibn Abdul Aziz "Tulikuwa tukimwambia 'Umar Ibn 'Abdul 'Aziz siku za Idd mbili: Mwenyezi Mungu Atukubalie sisi amali zetu na alikuwa akitujibu"

Mwisho

Ndugu Waislamu, siku ya Iddi ni siku muhimu katika maisha ya Muislamu kwa kufanya mambo ya kheri na kujikurubisha kwa Allah (Subhaanahu wa Taala). Siku hii si siku ya kufanya machafu na kumkasirisha Allah (Subhaanahu wa Taala). Kufanya hivyo ni kinyume na mafundisho ya Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) na Masahaba wake. Ni jukumu la kila Mzazi kuwafundisha familia yake hukumu ya siku hii muhimu katika Dini ya kislamu, ili jamii ya kiislamu iweze kujiepusha na mambo ya upuzi katika siku hii.

Tumuombe Mwenyezi Mungu Atupe baraka na kutusamehe madhambi yetu na kutupa mazuri hapa duniani na kesho akhera.

[3] SWALA YA KUOMBA MVUA

Lengo la Khutba:

1. Kumtii Mwenyezi Mungu ndio sababu ya kufaulu na kupata riziki.
2. Imeharamishwa kumuasi Mwenyezi Mungu
3. Kuwafundisha watu Sunnah ya Swalatul Istiskai (kuteremka mvua).

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Kila ugonjwa una tiba yake, ardhi ikiwa kavu na kupatikana ukame. Uislamu unamaanisha kuswali swalatul Istiskai nayo ni Swala ya kumuomba Mwenyezi Mungu kuteremsha mvua. Leo Swala hii imesahulika kabisa katika Umma wa kislamu. Waislamu wakipata matatizo ya uhaba wa Mvua, moja kwa moja wanaelekea kuomba majini na mashetani. Mafundisho ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) yako wazi kabisa kuwaelekeza Waislamu katika njia ya Allah (Subhaanahu wa Taala) wakati wowote na hali yoyote sawa wakati wa raha au shida. Kumtii Mwenyezi Mungu ndio mambo yote. Amesema Mwenyzi Mungu (Subhaanahu wa Taala) :

قال تعالى : ﴿وَلَوْ أَنَّهُمْ أَقَامُوا۟ ٱلتَّوْرَىٰةَ وَٱلْإِنجِيلَ وَمَآ أُنزِلَ إِلَيْهِم مِّن رَّبِّهِمْ لَأَكَلُوا۟ مِن فَوْقِهِمْ وَمِن تَحْتِ أَرْجُلِهِم ۚ مِّنْهُمْ أُمَّةٌ مُّقْتَصِدَةٌ ۖ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ سَآءَ مَا يَعْمَلُونَ ﴿٦٦﴾﴾ [المائدة:٦٦]

{{Na kama wangalisimamisha Taurati na Injili na yale yaliyoteremshwa kwao kutoka kwa Mola wao, kwa yakini wangalikula vya juu yao na vya chini ya miguu yao. Lakini wako watu miongoni mwao washikao njia nzuri. Lakini wengi wao wanayoyafanya ni mabaya kabisa}}.

Na Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَيَٰقَوْمِ ٱسْتَغْفِرُوا۟ رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوبُوٓا۟ إِلَيْهِ يُرْسِلِ ٱلسَّمَآءَ عَلَيْكُم مِّدْرَارًا وَيَزِدْكُمْ قُوَّةً إِلَىٰ قُوَّتِكُمْ وَلَا تَتَوَلَّوْا۟ مُجْرِمِينَ ﴿٥٢﴾﴾ [هود:٥٢]

{{Nikawaambia; Ombeni msamaha kwa Mola wenu. Hakika Yeye ni Mwingi wa msamaha. Atakuleteni mawingu yanyeshayo mvua nyingi}}.

Na akasema tena Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ ٱلْقُرَىٰٓ ءَامَنُوا۟ وَٱتَّقَوْا۟ لَفَتَحْنَا عَلَيْهِم بَرَكَٰتٍ مِّنَ ٱلسَّمَآءِ وَٱلْأَرْضِ وَلَٰكِن كَذَّبُوا۟ فَأَخَذْنَٰهُم بِمَا كَانُوا۟ يَكْسِبُونَ ﴿٩٦﴾﴾ [الأعراف:٩٦]

{{Na lau kama watu wa miji wangaliamini na kuogopa, kwa yakini tungaliwafungulia baraka za mbingu na ardhi. Lakini walikadhibisha; tukawapatiliza kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma}}.

Kumuasi Mwenyezi Mungu ndio sababu ya kuleta shari na kuondoka kwa baraka.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ وَٱلَّذِينَ إِذَا فَعَلُواْ فَٰحِشَةً أَوۡ ظَلَمُوٓاْ أَنفُسَهُمۡ ذَكَرُواْ ٱللَّهَ فَٱسۡتَغۡفَرُواْ لِذُنُوبِهِمۡ وَمَن يَغۡفِرُ ٱلذُّنُوبَ إِلَّا ٱللَّهُ وَلَمۡ يُصِرُّواْ عَلَىٰ مَا فَعَلُواْ وَهُمۡ يَعۡلَمُونَ ﴿١٣٥﴾ ﴾ [آل عمران:١٣٥]

{{Na ambao wanapofanya uchafu au kudhulumu nafsi zao, hukumbuka Mwenyezi Mungu na kuomba msamaha kwa dhambi zao. Na nani anayesamehe dhambi isipokuwa Mwenyezi Mungu}}.

Ametaja Ibn Qayyim baadhi ya maafa yanayoletwa na maasi; huleta udhalifu, huharibu akili, huwaondosha haya, hudhoofisha moyo, huondosha neema, hutia maradhi moyo, huleta nuksi, hupotosha ya moyo, hufanya moyo kuwa mdogo, huondosha karama, pia Baraka, na kulaumiwa, kutishika, huondosha hima ya kumcha Mwenyezi Mungu.

Ukame ni alama ya kuwa watu mbali na twaa ya Mwenyezi Mungu, na ishara ya kuzidi maasi. Hali ya anga inabadilika kutokana na maasi.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى ﴿ ظَهَرَ ٱلۡفَسَادُ فِي ٱلۡبَرِّ وَٱلۡبَحۡرِ بِمَا كَسَبَتۡ أَيۡدِي ٱلنَّاسِ لِيُذِيقَهُم بَعۡضَ ٱلَّذِي عَمِلُواْ لَعَلَّهُمۡ يَرۡجِعُونَ ﴿٤١﴾ ﴾ [الروم:٤١].

{{Uharibifu umedhihiri barani na baharini kwa sababu ya yale iliyoyafanya mikono ya watu, ili Awaonjeshe adhabu ya baadhi ya mambo waliyofanya, huenda wakarudi wakatubia kwa Mwenyezi Mungu}}.

Na anasema Anas bin Malik: Upepo ukiwa mkali hujulikana hilo kwa uso wa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Amepokea Abu Huraira hadithi: kutoka kwa Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema: [Hakisimami Qiyama mpaka iondoke ilimu, na kuzidi Zilzaal, na zahama kuwa karibu, na kudhihiri fitna, na kuzidi mauaji, mpaka itakua kwenu mali nyingi]. Ufupisho ni kujirudi nafsi, na kuomba msamaha kwa Allah pamoja na kufuata sheria za Allah (Subhaanahu wa Taala).

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ يُنَبَّؤُاْ ٱلۡإِنسَٰنُ يَوۡمَئِذِۢ بِمَا قَدَّمَ وَأَخَّرَ ﴿١٣﴾ بَلِ ٱلۡإِنسَٰنُ عَلَىٰ نَفۡسِهِۦ بَصِيرَةٞ ﴿١٤﴾ وَلَوۡ أَلۡقَىٰ مَعَاذِيرَهُۥ ﴿١٥﴾ ﴾ [القيامة:١٣-١٥]

{{Siku hiyo ataambiwa mwanadamu aliyotanguliza na aliyoyaakhirisha. Bali mtu ni shahidi juu ya nafasi yake}}.

Na neno lake Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akisema: [Tunajilinda na Mwenyezi Mungu kutokana na uovu wa nafsi zetu, na uovu wa matendo yetu]. Imepekewa kwa Masahaba wakisema: Alitusalisha Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) swala ya usubuhi Hudeibiyah kukiwa na mawingu usiku, baada ya hapo akatukabili na kusema: Je mnajua alivyosema Mwenyezi Mungu? Wakajibu maswahaba: Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanajua. Akasema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Baadhi ya waja wangu wamekua waumini ni wale waliosema tumeteremshiwa mvua kutokana na fadhila zake Mwenyezi Mungu, na makafiri tumeteremshiwa mvua kutokana na nyota fulani].

KHUTBAH YA PILI

Namna ya kuswali Swala ya Istiskai (Swala ya Mvua)

Ametoka 'Abdillah ibn Yazid pamoja na Burai Bin 'Azib na Zeid Bin Arkam kuswali ya Swala ya istiskai, akasimama na kumuomba Mwenyezi Mungu msamaha, kisha wakaswali rakaa mbili, kudhihirisha kisomo, bila adhani wala ikama. Na kama alivyopokea 'Abdillah bin Zaid kwamba Mtme (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) ameswali swala ya Istiskai kuelekea kibla, na kugeuza kishali chake na kuswali rakaa mbili. Amepokea Anas Bin Malik kuwa Mtume hainui mkono wake anapo omba isipokuwa katika swala ya istiskai, na alikuwa akiinua mkono wake mpaka ikionekana weupe wa makwapa yake.

Na ni sunna kuwalingania Waislamu wote kumcha Mwenyezi Mungu na kutaka radhi zake Mwenyezi Mungu kwa kutoa sadaka na kuunga kizazi. Amepokea Anas Bin Malik akisema: nimemsikia Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akisema: [Amesema Mwenyezi Mungu ewe mwanaadamu unaponiomba na ukataraji kutoka kwangu nitakusamehe kwa yale uliyo nayo bila kujali, ewe mwanaadamu madhambi yako yakafika mbinguni kisha ukaniomba msamaha nitakusamehe. Ukifanya madhambi kiasi cha 'arshi na hukunishirikisha Mwenyezi Mungu nitakusamehe madhambi hao]. Walipopatwa Makureish na ukame na kula mfu na mifupa. Abu Sufyan alikwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na kumuambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu umetuamrisha kuunga kizazi. Na waja wako wanaangamia, tuombee Mungu. Mtume wa Mwenyezi Mungu akaomba, ikateremka Mvua mpaka wakaogopa watu.

Amesema Hassan Basri: 'Zidisheni kutaka msamaha kwa Mwenyezi Mungu nyumbani kwenu, kwenye meza zenu, njiani, sokoni, makao yenu, na popote mlipo, kwani hamjui wakati gani utashuka msamaha wa Allah.

Mwisho

Ndugu katika Imani, Sababu kubwa ya kukosekana mvua ni kudhihiri machafu baharini na nchi kavu. Ili tuweze kupata rehma ya Mwenyezi Mungu na kuteremshiwa mvua kutoka mbiguni ni wajibu juu ya kila Muislamu kurudi kwa Allah kwa kuomba msamaha na kuendelea kufanya mambo ya kheri na kujiepusha na mambo mabaya.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Atuteremshie mvua na rehma na Baraka. Naelekeza wito wangu kwa watu wote kumuomba Mwenyezi Mungu Atubariki. Namuomba Mwenyezi Mungu kuteremsha mvua na kuwarehemu waja wake na miji yake.

[4] SWALA YA KUPATWA JUA AU MWEZI

Lengo la Khutba:

1. Kujua ukubwa wa Allah (Subhaanahu wa Taala), na ulazima wa kumtii na kumnyenyeka Allah (Subhaanahu wa Taala).
2. Kuweka wazi kuwa Allah (Subhaanahu wa Taala) Huona wivu kwa mtu kutenda maasi.
3. Kubainisha hukumu za Swala ya kupatwa jua na mwezi.
4. Kubainisha jinsi watu wanavyofanya katika hali ya jua kupatwa.

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Usiku na mchana kupishana ni miujiza ya Allâh ili mwanaadamu anufaike nayo, na Akajaalia iwe chini ya utumishi wake. Hakuna anayeweza kukhalifu kanuni ya mwendo wa jua na mwezi isipokuwa Allâh (Subhaanahu wa Taala) Peke Yake. Sababu za kimaumbile, Waumini na makafiri wote wanaikubali. Sababu za Sharia, Waumini wanazikubali na makafiri wanazikanusha. Na dalili ni Kauli ya Allâh (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ وَمِنْ ءَايَـٰتِهِ ٱلَّيْلُ وَٱلنَّهَارُ وَٱلشَّمْسُ وَٱلْقَمَرُ ۚ لَا تَسْجُدُوا۟ لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَٱسْجُدُوا۟ لِلَّهِ ٱلَّذِى خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿٣٧﴾ ﴾ [فصلت:٣٧]

{{Na katika alama Zake ni usiku na mchana, jua na mwezi; basi msilisujudie jua wala mwezi; bali msujudieni Allâh Aliyeviumba ikiwa nyinyi mnabuabudu Yeye}}. Na Kauli Yake (Subhaanahu wa Taala):

وقوله : ﴿ وَسَخَّرَ لَكُمُ ٱلْفُلْكَ لِتَجْرِىَ فِى ٱلْبَحْرِ بِأَمْرِهِۦ ۖ وَسَخَّرَ لَكُمُ ٱلْأَنْهَـٰرَ ﴿٣٢﴾ ﴾ [إبراهيم:٣٢]

{{Na (Allâh) Akafanya iwatumikieni majahazi yanayopita baharini kwa Amri Yake, na Akaifanya mito iwatumikie}}.

Na Kauli Yake Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿ وَءَاتَىٰكُم مِّن كُلِّ مَا سَأَلْتُمُوهُ ۚ وَإِن تَعُدُّوا۟ نِعْمَتَ ٱللَّهِ لَا تُحْصُوهَآ ۗ إِنَّ ٱلْإِنسَـٰنَ لَظَلُومٌ كَفَّارٌ ﴿٣٤﴾ ﴾ [إبراهيم:٣٤]

{{Na Akawapa kila mlichomuomba. Na mkihisabu neema za Allâh hamuwezi kuzidhibiti. Hakika mwanaadamu ni dhalimu mkubwa, mwenye kuzikufuru neema}}.

Allah (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

قال تعالى : ﴿ وَٱلشَّمْسُ تَجْرِى لِمُسْتَقَرٍّ لَّهَا ۚ ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ ٱلْعَزِيزِ ٱلْعَلِيمِ ﴿٣٨﴾ ﴾ [يس:٣٨]

{{Na jua linakwenda kwa kiwango chake. Hayo ni makadirio ya Mwenye nguvu, Mwenye kujua}}.

Allah (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

قال تعالى : ﴿ لَا ٱلشَّمْسُ يَنۢبَغِى لَهَآ أَن تُدْرِكَ ٱلْقَمَرَ وَلَا ٱلَّيْلُ سَابِقُ ٱلنَّهَارِ ۚ وَكُلٌّ فِى فَلَكٍ يَسْبَحُونَ ﴿٤٠﴾ ﴾ [يس:٤٠]

{{Haliwi jua kuufikia mwezi, wala usiku kuupita mchana. Na vyote vinaogelea

katika njia zao}}.

Abu Musa amesimulia: “Jua lilipatwa katika zama za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam), akasimama huku akiwa amefazaika isije ikawa Qiyama kimesimama, akaenda Msikitini akasimama akiswali Swala yenye kisimamo kirefu, rukuu na sijda ndefu mno ambapo sijamuonapo akifanya hivyo katika Swala yoyote ile. Kisha akasema: [Alama hizi zinazotumwa na Allâh, huwa haziwi ni kwa kufa yeyote wala kuwa hai, bali Allah Anazituma Akiwahofisha waja Wake. Mtakapoona alama yoyote katika hizo, kimbilieni kumtaja Allah (Subhaanahu wa Taala), kumuomba dua na kumuomba istighfari]. Imepokewa na Muslim.

Kupatwa jua ni onyo la Mola juu ya kuepuka Sharia Yake. Mifano ya kukhalifu mafundisho ya Uislamu.

Allâh (Subhaanahu wa Taala) Amesema:

قال تعالى : ﴿ولو يؤاخذ الله الناس بما كسبوا ما ترك على ظهرها من دابة ولكن يؤخرهم إلى أجل مسمى فإذا جاء أجلهم فإن الله كان بعباده بصيرا ﴿٤٥﴾﴾ [فاطر:٤٥]

{{Na lau Allâh Angeliwachukulia watu kwa waliyoyachuma, basi Asingelimuacha juu ya ardhi hata mnyama mmoja. Lakini Yeye Anawachukulia mpaka ufike muda maalumu. Basi ukifika muda wao basi hakika Allah ni Mwenye kuwaona waja Wake}}.

Jabir bin ’Abdullah Amehadithia: “Jua lilipatwa katika zama za Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) siku yenye joto kali, Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) akawaswalisha Maswahaba zake, akarefusha kisimamo mpaka wakawa wakianguka, kisha akarukuu kitambo kirefu, akaitadili kitambo kirefu, akarukuu (tena) kitambo kirefu, akaitadili kitambo kirefu kisha akasujudu sijida mbili, akasujudu sijida mbili, kisha akasimama, akafanya kama alivyofanya mara ya kwanza. Ilikuwa ni Swala yenye rukuu nne na sijda nne. Nimeonyeshwa kila mahala mtakapoingia. Nikaonyeshwa Pepo, hata lau kama ningalichukua kichala (cha matunda) ningaliweza kukichukua. Nikaonyeshwa moto, nikamuona mwanamke wa Kiisraeli akiadhibiwa kwa sababu ya kumfungia paka ambaye hakumlisha wala hakumuacha aende akale vijidudu vya ardhini. Nikamuona Abu Thumama akiziburuta chango zake (matumbo) motoni. Watu walikuwa wakisema kuwa jua na mwezi havipatwi la kwa sababu ya kufa mtu mkubwa. Lakini hizo ni alama mbili za Allah Anawaonyesha, vitakaposhikwa, swalini mpaka viachwe.” Muslim.

Enyi umati wa Muhammad! Hakuna mwenye ghera kuliko Allah (Subhaanahu wa Taala) kumuona mja wake akizini, au mjakazi wake akizini. Enyi umati wa Muhammad! Lau mngalijua ninachokijua, mngalicheka kidogo na mkalia sana. Naapa kwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), tangu niliposimama kuswali, niliona mutakayokutana nayo katika mambo ya dunia na Akhera yenu, hakuna ambacho sikukiona. Nimeyaona yote katika makamu yangu haya hata Pepo na moto. Nimeuona moto ukijitafuna wenyewe, sijaona mandhari ya kufazaisha kama leo. Nimemuona ’Amru bin Lahyi al-Khuzaiy akiburuta chango zake.

Nikamuona mwanamke akiadhibiwa kwa sababu ya paka, alimfungia wala hakumpa chakula wala hakumuacha aende akale vijidudu vya ardhini. Nimewaona jinsi mtakavyopewa mtihani makaburini mwenu, kama ule mtihani wa Dajjali atakapomjia mmoja wenu. Mtu ataulizwa: " Mtu huyu unamjua vipi?" Muumini au mwenye yakini atasema: " Ni Muhammad Mtume wa Allah, Alitujia na ubainifu na uongofu, tukamjibu, tukamuamini na tukamfuata." hapo ataambiwa: "Lala ukiwa mwema. Tulikuwa tukijua kuwa ulikuwa ni mwenye yakini. Ama mnafiki au mwenye shaka, atasema: Simjui, niliwasikia watu wakisema kitu na mimi nikakisema!.

KHUTBAH YA PILI

Sharia ya Swala ya kupatwa Jua au Mwezi

Kuongezea dalili zilizotangulia, nitatoa dalili ya Hadithi ya Hudhaifa, amesema: "Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alikuwa anapofazaishwa na jambo, huswali." Ibnu Jarir. Alqama amesema: "Mnapofazaishwa na vimondo vya mbinguni, kimbilieni kuswali". Ibnu Abi Shaibah.

Namna ya kuswali Swala ya Kupatwa Jua au Mwezi

Abdur-Rahman bin Samurah amehadithia: "Nilipokuwa nikirusha mishale yangu – katika zama za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) mara jua likapatwa, nikaitupa. Nikasema kuwa nitamtazama Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) atakavyofanya katika hali ya kupatwa jua leo. Nilipofika kwake nilimuona akiinua mikono yake, akipiga Takbira na akisema : [Laa ilaaha illallah] mpaka jua likaachwa, akasoma Sura mbili na akaswali rakaa mbili". Muslim. Abubakar amesema: "Jua lilipatwa katika zama za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam), akaswali rakaa mbili]. Bukhary.

Na Hadith ya 'Aisha amesema: [Jua lilipatwa wakati wa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). Mtume akasimama akawaswalisha watu. Akarefusha kisimamo, kisha akarukuu, akairefusha rukuu, halafu akasimama, akarefusha kisimamo – chini ya kisimamo cha kwanza - kisha akarukuu, akairefusha rukuu – chini ya rukuu ya kwanza – halafu akasujudu, akairefusha sijda. Kisha akafanya katika rakaa nyingine mfano wa alivyofanya katika rakaa ya kwanza. Halafu akamaliza na jua lilikuwa limeshaachwa (limeshadhihiri). Akaanza kuwahutubia watu. Akamshukuru Allâh na kumsifu, baadae akasema: "Hakika jua na mwezi ni alama miongoni mwa alama zenye kujulisha Uwezo na Umoja wa Allâh. Navyo havipatwi kwa kufariki yoyote wala uhai wa yoyote. Mtakapoona hivyo, muombeni Allah, mupige Takbira musali na mutoe sadaka. "Kisha akasema: "Enyi umati wa Muhammad! Naapa kwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), hakuna mwenye ghera kumshinda Allah, kwa hivyo Ame haramisha zina kwa waja Wake; mwanamume au mwanamke. Enyi umati wa Muhammad! Naapa kwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), lau mnayajua ninayoyajua, mngalicheka kidogo na mukalia sana!". Katika lafdhi nyingine imesema: " Akakamilisha rakaa nne na

sijda nne].

Mdugu Waislamu, mafundisho ya Mtume yako wazi kabisa kuhusu suala la kupatwa jua au mwezi. Jukumu letu ni kufuta sunna ya Mtume kwa kutekeleza swala ya kupatwa jua au mwezi. Na tuachani itikadi mbaya za kimila juu ya matukio kama haya.

Mwisho

Ndugu katika imani na kuusieni kurudi kwa Allah (Subhaanahu wa Taala), kuacha kutenda dhambi na kuwafanyia uadilifu raia. Amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ تُوبُوٓاْ إِلَى ٱللَّهِ تَوۡبَةٗ نَّصُوحًا عَسَىٰ رَبُّكُمۡ أَن يُكَفِّرَ عَنكُمۡ سَيِّـَٔاتِكُمۡ وَيُدۡخِلَكُمۡ جَنَّٰتٖ
تَجۡرِي مِن تَحۡتِهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ يَوۡمَ لَا يُخۡزِي ٱللَّهُ ٱلنَّبِيَّ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مَعَهُۥۖ نُورُهُمۡ يَسۡعَىٰ بَيۡنَ أَيۡدِيهِمۡ وَبِأَيۡمَٰنِهِمۡ يَقُولُونَ رَبَّنَآ أَتۡمِمۡ لَنَا
نُورَنَا وَٱغۡفِرۡ لَنَآۖ إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيۡءٖ قَدِيرٞ ٨﴾ [التحريم:٨]

{{Enyi mlioamini! Tubuni kwa Allah toba iliyo ya kweli! Asaa Mola wenu Mlezi Akawafutia maovu yenu na Akawaingiza katika Pepo ambazo inapita mito kati yake, siku ambayo Allah Hatamdhalilisha Nabii na walioamini pamoja naye. Nuru yao inakwenda mbele yao na pande zao za kulia, na huku wanasema: Mola wetu Mlezi! Tutimilizie nuru yetu, na utughufirie! Hakika Wewe ni Mwenye uweza juu ya kila kitu}}.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Atuhifadhi na Atuepushe na kila shida za ulimwengu na Atujalie miongoni mwa waja wake watakao ingia peponi pamoja na Mtume Muhammad.

[5] MNASABA WA MWAKA MPYA

Lengo La Khutbah:

1. Kuaga mwaka uliopita na kujiandaa kwa mwaka mpya
2. Kuzidisha mafungamano pamoja na Mwenyezi Mungu katika mambo yake yote katika mwaka unaokuja
3. Kuhimiza watu kufanya kazi

KHUTBA YA KWANZA

Utangulizi

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu, Swala na salamu zimfikie Mtume wetu Muhammad (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam). Inapaswa kwa kila mwanadamu kujiuliza maswala haya:-

- Nimekuja kutoka wapi?
- Naenda wapi?
- Ulimwengu huu ulioko pembezoni mwangu umekuja kutoka wapi?
- Kwa ajili gani nimeumbwa?

Matamanio ni sababu ya mtu kujisahau, na kumalizika mwaka kwa haraka, amesema Hassan Basri: Tahadharini na matamanio, kwani hapati mtu na tamanio kheri ya duniani na kesho akhera. Mafhumu Neno lake Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) :

قال الله تعالى ﴿أَوَلَا يَرَوْنَ أَنَّهُمْ يُفْتَنُونَ فِي كُلِّ عَامٍ مَّرَّةً أَوْ مَرَّتَيْنِ ثُمَّ لَا يَتُوبُونَ وَلَا هُمْ يَذَّكَّرُونَ ١٢٦﴾ [التوبة:١٢٦]

{{Je, Hawaoni ya kwamba wanatiwa mitihani kila mwaka mara moja au mara mbili au zaidi. Kisha hawatubu wala hawakumbuki}}. Amesema Mujaahid: wataonjwa kwa ukame na njaa. Amesema Qatada: wataonjwa kwa kupigana vita mara moja na mara mbili. Amesema Mujaahid: wataonjwa kwa ukame na shida. Amesema ‘Atwiyyah: Wataonjwa kwa maradhi na maumivu.

Maswali muhimu yanapaswa kwa mwanadamu kujibu. Maswali hayo baada ya kumalizika kwa mwaka. Kila mwanadamu anapaswa kujiuliza maswali haya:-

1. Swala ngapi hukuswali?
2. Umepuuza jumaa ngapi?
3. Saumu ngapi hukufunga?
4. Mali ngapi hukuyatolea zaka?
5. Hija ngapi zimekupita?
6. Umefanyia uvivu wema ngapi?
7. Uovu kiasi gani uliounyamazia?
8. Mambo mangapi ya haramu umeyaangalia?
9. Maneno mangapi machafu umeyazungumza?

10. Mara ngapi umewaudhi wazazi wako wawili na wala hukuwaridhisha?
11. Umewavisha madhaifu wangapi?
12. Wangapi umewadhulumu?

Umuhimu wa Wakati

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ ۖ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ خَبِيرٌۢ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٨﴾﴾ [الحشر:١٨]

{{Enyi mlioamini, Mcheni Mwenyezi Mungu; na kila mtu aangalie anayoyatanguliza kwa ajili ya kesho (Akhera); na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu Anazo habari za mnayoyatenda yote}}.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala):

قال تعالى : ﴿يَوْمَ تَجِدُ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ مِنْ خَيْرٍ مُّحْضَرًا وَمَا عَمِلَتْ مِن سُوٓءٍ تَوَدُّ لَوْ أَنَّ بَيْنَهَا وَبَيْنَهُۥٓ أَمَدًۢا بَعِيدًا ۗ﴾ [آل عمران:٣٠]

{{Siku ambayo kila nafsi itakuta mema iliyoyafanya yamehudhurishwa, na pia ubaya ilioufanya. Itapenda lau kungekuwa na masafa marefu baina ya ubaya huo na yeye}}. Amesema ‘Umar: ‘ Hesabuni nafsi zenu kabla hazijahisabiwa na pimeni nafsi zenu kabla hazijapimwa, kwani itakuwa ni wepesi kwenu nyinyi siku ya Qiyama ikiwa mtahesabu nafsi zenu.

Ndugu Waislamu, Je tumejiandaa kiasi gani kwenda kujibu maswali mbele ya Allah siku ya kiama?. Kila moja ajiulize suala hilo na aandae jibu la ukweli kabisa. Kwasababu kuokoka mwanadamu siku hiyo, ni kujibu swali atakalo ulizwa na Allah siku ya hesabu.

Mfano Mzuri wa Kuhesabu Nafsi

1. Abubakar alikuwa akiuzuia ulimi wake ukitoka nje, na akisema: kiungo hiki kimeniingiza katika maangamivu.
2. Amesema Ghunaym: tulikuwa tukijipatia mawaidha kwa mambo mane:
   - Fanya amali njema katika ujana wako kabla utu uzima
   - Unapokuwa na wakati kabla kuwa na shughuli
   - Unapokuwa na afya kbala kuwa mgonjwa
   - Unapokuwa hai kabla hujafa.

KHUTBA YA PILI

Daraja za kuhesabu nafsi:-

Ibnu Qayyim ameelezea njia za kuhesabu nafsi:

1. Kufanya mambo ya faradhi, fatiliza ukiona kuna upungufu
2. Ukifanya maasi, fuatiliza kwa toba na kumuomba Mwenyezi Mungu msamaha na kufanya amali njema.
3. Ukighafilika mtaje Mwenyezi Mungu
4. Kuhesabu nafsi viungo vyake, ni kujiuliza unataka nini? Na kwa njia gani umefanya?

Mambo Manne yenye Kunawirisha Moyo:

Amesema 'Uthman Bin Fuudy: mambo manne yenye kunawirisha moyo:

1. Kumcha Mwenyezi Mungu
2. Kusoma Qur'an.
3. Kusoma Hadithi za Mtume na sera zake.
4. Kujishughulisha na waja wema waliotangulia.

Amesema Ibrahim Nukhaiy: 'Ewe Mwenyezi Mungu, tuhifadhi na kitabu chako, na Sunnah ya Mtume wako, na tulinde kufuata matamanio, na njia iliyopotea na shubuhaat katika mambo, na dhulma na malumbano'.

Mwisho

Mwaka mpya ni neema kubwa kutoka kwa Allah (Subhaanahu wa Taala) na wakati huo huo neema hii inaweza ikabadilika na ikawa ni adhabu na mitihani mikubwa kwa mwanadamu. La msingi ni Muislamu kufuata maamrisho ya Allah (Subhaanahu wa Taala) na kushikamana na Sunnah ya Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam). Kufanya hivyo, ndio mwaka wako utakuwa ni mwaka wa neema nyingi. Kinyume na hayo, mwaka wako utakuwa ni adhabu na mitihani na misukosuko mbali mbali ya kilimwengu..

Tumuombe Mwenyezi Mungu Atusamehe madhambi yetu yaliopita na Atuwezeshe kufanya amali njema katika mwaka huu mpya, na Atuteremshie baraka na neema katika mwaka huu mpya.

MWISHO WA KITABU CHA KHUTBA ZA IJUMAA

Ewe mhutubiaji!

Umma wa Kiislamu ni amana kwenye mikono yako. Wewe hapo ulipo, popote pale, umesimama kwenye mwanya miongoni mwa mianya ya Uislamu, inachelewa usije Uislamu ukaingiliwa kupitia kwako.

Umeshajua kazi ya khutba ya Ijumaa inavyofanya katika ujenzi wa umma. Na

umeshapata maelezo kiasi kuhusu hukumu zake: masharti, nguzo na sunna. Na vishakufunukia vyombo vya utoaji khutba wenye kufurahisha na sifa za mhutubiaji aliyefaulu, matayarisho yake na zana zake. Na umetembea kwenye njia za utoaji khutba kama maelezo ya vitendo na mfano wa kutumiwa. Je, wajibu wako sasa ni nini?

Ni juu yako uingie uwanjani ukiwa na nguvu na ushujaa, na elimu na uvumilivu, na vitendo na ufuatiliaji. Uwanja ni wako na eneo ni lako. Na Amesema kweli Mwenyezi Mungu pale Aliposema: (Na sema: fanyeni! Kwani Mwenyezi Mungu Atayaona matendo yenu na Mtume Wake na Waumini. Na mtarudishwa kwa Mjuzi wa yasiyoonekana na yanayoonekana, Awape habari ya yale mliokuwa mkiyafanya.) {Taubah: 105}

Ujue kwamba kitabu hiki ni kiingilio cha uwanja huu, na ni tone la bahari, tumekuwekea mwanzo wa njia yake ya kuifuata. Basi usipitiwe na siku isipokuwa na wewe uko kwenye harakati za kuongeza utafutaji elimu, nayo ndiyo silaha ya jukumu tukufu sana. Uislamu huko nyuma ulienea kwenye nchi nyingi sana kwa maneno yao mazuri na miamala yao na watu. Kuna watu ambao mmoja wao analinganishwa na umma mzima. Mara ngapi historia ya umma ilibadilika huko nyuma kutokana na mtu mmoja aliyejua uzito wa jukumu lake akajitahidi kwa juhudi zake zote na akaondoa uvivu na ulegevu, akatoka kulingania watu mchana na usiku, kwa siri na kwa dhahiri, kila wakati na mahali. Ni mtu asiyekata tamaa, mpaka jicho lake linapotulia kwa kuuona Uislamu umetukuka, na jua lake limetokeza upya na kung’arisha miji na waja.

Namuomba Mwenyezi Mungu Akuzidishie, ewe ndugu yangu unayehutubu, uongofu na uchamungu, ujuzi na utendaji, na Atufanye sisi na wewe kuwa ni wenye utiifu Kwake. Na Atujaalie ni wastahiki wa kubeba amana iliyowekwa juu ya mabega yetu.

Faharasa ya yaliomo

[1] SEHEMU YA IMANI 17

[1] FADHILA YA KUDUMU KATIKA TAWHIDI (KUMPWEKESHA MWENYEZI MUNGU) 18

[2] MAJINA MAZURI YA MWENYEZI MUNGU NA UFAFANUZI WAKE 24

[3] ALAMA ZA KIAMA 30

[4] KUTAHADHARI NA UCHAWI NA UGANGA 36

[5] KUWAKUMBUSHA WATU DALILI ZA MWENYEZI MUNGU KATIKA VIUMBE 41

[6] KUMTEGEMEA MWENYEZI MUNGU (Subhaanahu wa Taala) 47

[7] MAPENZI YA MWENYEZI MUNGU (Subhaanahu wa Taala) NA MTUME WAKE (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) 51

[8] KUAMINI KADARI 54

[9] MAISHA YA AKHERA 58

[10] ATHARI YA MADHAMBI NA MAASI KATIKA MAISHA YA MWANADAMU 63

[11] UCHAJI MUNGU NA ATHARI ZAKE KATIKA MAISHA YA MUISLAMU 66

[12] KUOGOPA NA KUTARAJI 70

[13] IKHLAS (KUMTAKASIA NIA MWENYEZI MUNGU) 73

[14] NEEMA YA PEPO NA ADHABU YA MOTO 77

[15] BAADA YA KUFA 81

[2] SEHEMU YA IBADA 85

[1]UMUHIMU WA SWALA NA HEKIMA YA KUFANYA KUWA SHERIA 86

[2] SIKU YA IJUMAA NA HUKUMU ZAKE 90

[3] UMUHIMU WA DUA NA MASHARTI YAKE 94

[4] KUMI LA MWISHO LA MWEZI MTUKUFU WA RAMADHANI 98

[5] ZAKA ZA FITRI NA SWALA YA IDDI 101

[6] KUMTAJA MWENYEZI MUNGU (Subhaanahu wa Taala) 104

[7] KUUPOKEA MWEZI WA RAMADHANI 109

[8] ZAKA NA HIKMA ZAKE NA HUKUMU ZAKE 115

[9] MAFHUMU (Mtazamo) YA IBADA KATIKA UISLAMU 121

[10] KUJILAZIMISHA NA SUNNA YA MTUME (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) 127
[11] KUTAHADHARI NA UZUSHI KATIKA DINI 131
[12] FADHILA ZA SIKU KUMI ZA MWEZI WA MFUNGO TATU 136
[13] KUSOMA QUR’AN NA ADABU ZAKE 142
[14] MAANA YA HIJJA 148
[15] UTWAHARA WA MGONJWA 153
[3] SEHEMU YA MAADILI NA TABIA 159
[1] TAHDHARI NA KUTELEZA KWA ULIMI 160
[2] ATHARI YA KUSUHUBIANA NA RAFIKI MWEMA 164
[3] TAHADHARI NA FITNA ZA WANAWAKE 167
[4] UHIMIZAJI JUU YA SUBIRA 170
[5] UHIMIZAJI WA KUSEMA UKWELI NA UTAHADHARISHAJI WA KUSEMA UONGO 176
[6] TOBA BAADA YA KUFANYA MAASI 180
[7] REHEMA 185
[8] DHANA MBAYA 189
[9] HATARI YA MWANAMKE KUJIPAMBA NA KUDHIHIRISHA MWILI WAKE 192
[10] MADAWAYAKULEVYANAATHARIYAKEKATIKAKUMUANGAMIZA BAROBARO 196
[4] SEHEMU YA JAMII 202
[1] MIZANI NA NAMNA YA KUAMILIANA NA WATU 203
[2] UHIMIZAJI WA KUCHUMA HALALI NA KUJIEPUSHA NA HARAMU 207
[3] DINI YA KISLAMU IMEMTUKUZA MWANAMKE WA KIISLAMU 211
[4] KUWAFANYIA WEMA WAZAZI WAWILI NA TAHADHARI YA KUWAASI 215
[5] HAKI ZA JIRANI 219
[6] HAKI YA MUISLAMU JUU YA MUISLAMU MWENZAKE 222
[7] KUPEANA NASAHA NA KUTEKELEZA AMANA 226
[8] ZAKA NA MCHANGO WAKE KATIKA KUSHIKAMANISHA JAMII 230
[9] MAHIMIZO KATIKA KUUNGA JAMAA 235

[5] SEHEMU YA ULINGANIZI 238

[1] UMUHIMU WA KUAMRISHANA MEMA NA KUKATAZANA MABAYA 239

[2] VYOMBO VYA UTANGAZAJI NA ATHARI ZAKE KATIKA JAMII 243

[3] NJIA ZA KUZIVUTA NYOYO 249

[4] HIMIZO JUU YA KUTAFUTA ILIMU NA KUIFANYIA KAZI 253

[5] UKATI NA KATI (AL- WASWATWIYA) KATIKA QUR'AN NA SUNNAH 257

[6] MFUMO WA MITUME KATKA ULINGANIZI 261

[6] SEHEMU YA MISIMU NA MINASABA 265

[1] IDDI YA KUFUNGUA SAUMU 266

[2] IDDI YA KUCHINJA 269

[3] SWALA YA KUOMBA MVUA 272

[4] SWALA YA KUPATWA JUA AU MWEZI 276

[5] MNASABA WA MWAKA MPYA 280

العالمي
Global Minbar

Mradi wa Kimataifa wa Minbari

Ni kuandikwa kwa maelezo na mitazamo mbali mbali ya msingi kuhusu Uislamu na kuyafikisha na kuyatangaza kwa Umma kwa kutumia lugha mbali mbali hai zinazotumika na kusambaza katika jumla ya Khutbah 60 na kadhalika kutoa kwa matumizi ya Runinga (Television) na Radio na kuweka katika tovuti na vyombo vingine vya habari vya kisasa.

E_mail: info@global-minbar.com
Tele : 00966-537121504

فضاء القنوات
SPACE CHANNELS

Fikihi ya Ibada Pichani

Mradi wa mafunzo ya Kiislamu yaliyowepesishwa kwa njia ya picha zilizotua na zinazotembea kwa lugha mbali mbali ulimwenguni wa lengo la kufundisha Mafundisho ya Uislamu. Mradi huu una vipengele vifuatavyo:

SPACE CHANNELS

E_mail: info@global-minbar.com
Tele : 00966-537121504